# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

## Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 18 Aprili, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:-**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA – (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIAMWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:-**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu maoni ya kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU– KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 95

**Elimu kwa Watoto Wenye Mahitaji Maalum**

**MHE. SALMA R. KIKWETE** aliuliza:-

(a) Kwa kuwa elimu ni haki ya kila mtoto, je, Serikali inawasaidiaje watoto wenye usonji ili nao wapate elimu?

(b) Je, Walimu wanaofundisha watoto hao wanatosheleza kwa mujibu wa ikama?

(c) Kwa kuwa watoto hao wana mazingira tete, je, Walimu wao wana utaalam wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usonji ni ulemavu ambao huathiri mfumo wa mawasiliano katika ubongo, mahusiano na utambuzi. Wanafunzi wenye usonji wamekuwa wakifundishwa na Walimu watalaam wa ulemavu wa akili waliopatiwa mafunzo kazini. Hadi sasa tuna wanafunzi 1,416 wenye usonji na Walimu 157 walio katika shule 18 za msingi nchini. Walimu hao ni wachache na hawatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wapo Walimu waliopata taaluma hiyo kwenye Chuo cha Patandi, lakini hawako kwenye shule maalum, nasisitiza tena agizo langu nililolitoa kwenye Mkutano wa Kumi kwamba Halmashauri zote ziwahamishie Walimu hao kwenye shule zenye wanafunzi wenye ulemavu ikiwemo wenye usonji ifikapo mwezi wa Desemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa elimu maalum nchini kwa wanafunzi wenye ulemavu wasioona, viziwi, albino, usonji, viziwi–wasioona, walemavu wa akili, walemavu wa viungo, uoni hafifu, wenye vipawa na vipaji pekee pamoja na wenye matatizo ya ujifunzaji utaendelea kupewa kipaumbele. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo miundombinu, vifaa maalum kwa mahitaji maalum, kutoa mafunzo zaidi kwa Walimu pamoja na kugharamia kwa ujumla elimu msingi bila malipo kwa wanafunzi wote ikiwemo wenye mahitaji maalum.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salma Kikwete. 0713549173

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa

majibu yake mazuri. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Sheria Namba Tisa ya Mwaka 2010 inamzungumzia mtoto mwenye ulemavu kupata haki ya elimu pamoja na kulindwa. Watoto hawa wenye usonji, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi wana mazingira tete. Sasa je, nili lini, au je, upi ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba watoto hawa wanapata elimu toshelezi katika mazingira yao ya miundombinu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, watoto wenye usonji kwa kawaida wanatakiwa kila watoto watano wawe na Mwalimu mmoja. Sasa katika majibu ya msingi tunaambiwa watoto wapo 1,416 na Walimu wapo 157, maana yake watoto hawa wanatiwa wawe na Walimu wasiopungua 283. Sasa je, ni lini Walimu hawa watapewa elimu stahiki ili waweze kuwapa watoto wenye ulemavu, hasa usonji elimu inayostahiki? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, yeye ni mdau mkubwa wa elimu na kwa kweli hasa katika elimu maalum ametoa mchango mkubwa sana wa mawazo kuhusu kuendeleza watoto hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenye usonji mara nyingi huzaliwa kawaida na usonji huanza kuonekana baada ya mwaka mmoja na nusu hadi miaka miwili. Kwa hiyo, wazazi wengi wamekuwa wakipata shida ya kuwatambua vizuri kwamba huyu mtoto ana usonji, kwa hiyo, imekuwa vigumu hata kuwaratibu. Matokeo yake wengine wamekuwa labda wakiwapiga wanadhani ni watukutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mpango maalum wa kwanza kuwatambua watoto hao wote na kuwasajili ili hatimaye tuhakikishe kwamba wote wanapata elimu kama ilivyo haki ya kila mtoto Mtanzania kupata elimu. kwa hiyo, mkakati wetu tutaanza zoezi la kuwatambua na kuwasajili ili hatimaye wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, nakubaliana naye kwamba katika kila watoto watano wanatakiwa kuwa na Mwalimu mmoja lakini *standard* ambayo ni nzuri sana ya Kimataifa inatakiwa anapomfundisha amfundishe akiwa peke yake *(one to one),* hiyo ndiyo *standard* ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, upungufu wa walimu waliopo sasa hivi wanaofundisha shuleni ni mkubwa kama alivyoainisha. Hata hivyo, kwa kuwa tunao Walimu wengine ambao wameshapata mafunzo hayo kule Patandi halafu bado hawajahamishiwa kwenye hizo shule ambazo zinafundisha watoto hawa kwa sasa, ndiyo maana nimetoa agizo kwamba ifikapo Desemba wawe wamehamishiwa kwenye hizi shule ili kusudi watoto hawa waweze kupata haki yao ya msingi kabisa ya elimu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE. SUSAN A.LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba kuna tatizo kubwa la upungufu wa Walimu hawa, lakini nina taarifa kwamba tuna Walimu wengi sana waliosoma katika vyuo kwa mfano Chuo cha Tabora cha Viziwi, wamesomea kufundisha watoto hawa, lakini wapo mitaani na wana *resources.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa nini Serikali isiwachukue Walimu hawa ambao wamesomea kwa miaka mitatu *degree* zao na kuendelea kuchukua Walimu ambao wamepata kozi za juu juu tu za mafunzo kazini wakati tunajua tuna tatizo kubwa sana la Walimu kwa ajili ya watoto hawa

wenye ulemavu mbalimbali pamoja na viziwi na hawa wengine wa usonji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa sababu kwanza amekuwa ananiletea maswali mengi hata kwenye karatasi, vi-*note* na nimekuwa nikimpa maelezo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili namuahidi katika Walimu ambao tutawaajiri hivi karibuni, kipaumbele kitakuwa ni kwa hawa ambao wana taaluma ya elimu maalum ambao hawajaajiriwa ili waajiriwe haraka waweze kutusaidia katika shughuli zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum na linaulizwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 96

**Ujenzi wa Hospitali ya Tabora**

**MHE. MUNDE A. TAMBWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Manispaa ya Tabora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Manispaa ya Tabora hupata huduma za afya kupitia kwenye zahanati 22 zilizopo kwenye Wilaya hii. Kwa kuwa zahanati inatoa huduma za magonjwa madogo *(minor illness),* wananchi wa Manispaa ya Tabora hupata huduma kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kitete. Hata hivyo, Hospitali ya Mkoa kwa sasa imeelemewa na wagonjwa wengi, hivyo manispaa imeona ni vyema ianzishe ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ulianza mnamo tarehe 19/10/2015 kwa kuanza na jengo la *OPD* kwa gharama ya shilingi milioni 150 chini ya mkandarasi HERU *Construction Company Limited* ambapo hadi sasa sehemu ya msingi, nguzo, ngazi na slabu vimekamilika kwa asilimia 100, mkandarasi ameshalipwa jumla ya shilingi milioni 145.7 kwa fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Manispaa ya Tabora imetenga shilingi milioni sabini kwa ajili ya ujenzi wa jengo la *OPD* katika hospitali hiyo. Vilevile Ofisi ya Rais, TAMISEMI itahakikisha inatoa kipaumbele kwa Manispaa ya Tabora katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya mara fedha za awamu ya pili zitakapo patikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inasisitiza kuhakikisha fedha za miradi zinazopatikana zilenge katika ukamilishaji wa miradi iliyopo badala ya kuibua miradi mipya; kwa mfano fedha za *Local Government Capital Development Grand (LG- CDG)* milioni 483.5 kwa mwaka 2017/2018 ambazo zilitolewa maelekezo kwamba zitumike katika kukamilisha miradi iliyokwishaanzishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kutuletea pesa kwenye Wilaya ya Sikonge, Nzega na Uyui kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za wilaya, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza swali langu la kwanza la nyongeza. Ukizingatia *population* ya Wilaya ya Tabora Manispaa, ukizingatia Sera ya Serikali yetu kwamba mnatakiwa muanze ninyi wenyewe na Serikali iwa-*support* kitu ambacho wananchi wa Tabora Manispaa wameshakifanya. Kinachotushangaza zaidi ni pale Wilaya mpya zilizoanza mwaka jana zinavyopelekewa pesa ya kujenga Hospitali ya Wilaya na kuacha kupeleka katika Wilaya za zamani...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** zenye watu wengi na...

**MWENYEKITI:** Uliza swali.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** ...kuacha kupeleka kwenye Wilaya ya Tabora Manispaa. Je, Serikali inanipa *commitment* gani sasa ya kuleta pesa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Tabora Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Jimbo la Igalula halina hata zahanati moja wala kituo cha afya kimoja; hii inasababisha wananchi wote wa Jimbo hilo kwenda kwenye hospitali kubwa ya Mkoa wa Tabora ambayo ni Kitete na kuongeza msongamano mkubwa. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha inaleta pesa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya na kumalizia zahanati ambazo zilianzishwa na wananchi wa Jimbo la Igalula pamoja na Mbunge wao na mimi Mbunge wao wa Viti Maalum? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika tangu nimeingia Bunge hili na Mheshimiwa Munde akiwa ndani ya Bunge hili amekuwa ni mpiganaji kuhusiana na suala zima la afya kwa Mkoa wake wa Tabora, nampongeza sana kwa jitihada zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake mawili, swali la kwanza anauliza *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa hospitali ya Manispaa ya Tabora kwa maana ya hospitali ya wilaya. Katika jibu langu la msingi nimemweleza *commitment* ya Serikali kwamba katika awamu ya pili, fedha zitakazopatikana kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za wilaya hatutaisahau Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili anaongelea kuhusiana na Igalula ambayo hawana kituo cha afya na Hospitali ya Wilaya. Kwanza naomba niwaase na niwaombe wananchi wa Igalula, wao waanzishe ujenzi kama ambavyo Manispaa ya Tabora wamefanya na pesa ikipatikana awamu itakayofuata na sisi kama Serikali tutahakikisha kwamba tunaunga mkono juhudi za wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimemwona Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Miongoni wa vitu vya afya ambavyo vilipangiwa kupatiwa pesa Mkoani Ruvuma ni pamoja na Kituo cha Afya Namtumbo na Mkasali. Naishukuru Serikali vituo hivyo vimepata pesa. Hata hivyo, kipo Kituo cha Afya cha Matemanga ambacho kilipangiwa kupatiwa pesa kwa ajili ya ukarabati, lakini pesa ile mpaka sasa haijaenda. Ni nini kauli ya Serikali kuhusiana na hiyo pesa ya ukarabati wa vituo vya afya? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yale ya awali. Naomba kumpa *comfort* kwanza mtani wangu Mnyamwezi. Mheshimiwa Ntimizi wiki iliyopita alikuja ofisini kwetu pale kwa ajili ya vituo vya afya vitano vilivyoanzishwa

katika mchakato wa ujenzi wa na tumewapa *commitment* kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI itahakikisha kwamba ina-*support* ndani ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuhusu suala la Matemanga, tayari naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndani ya wiki hii tu-*cross-check accounts* zetu kule katika halmashauri yetu, tutakuwa tumeshaingiza hizo fedha tayari kwa ajili ya kuhakikisha kituo kile kinakamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Willy Qambalo na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kambi ya Simba Wilayani Karatu umekamilika kwa ufanisi mkubwa na kituo hicho sasa kiko tayari kuanza kutoa huduma. Hata hivyo, kituo hicho hakina gari la wagonjwa na ukizingatia Wilaya ya Karatu haina hospitali ya wilaya, je, ni lini Serikali italeta gari kwa ajili ya huduma ya wagonjwa kwenye kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, ni lini mtapeleka hiyo gari ya wagonjwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunashukuru kwa kazi nzuri ambayo mwenyewe ana-*recognise* kwamba kituo cha afya kimekamilika na kiko kwenye hali nzuri. Hatua inayofuata anaomba upatikanaji wa gari la *ambulance* ili kuweza kusaidia huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba uhitaji wa gari kwa ajili ya wagonjwa ni mkubwa sana. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kadri nafasi zitakavyopatikana, tulipata magari 50 na tumeweza kuyagawa, tukipata gari nyingine naamini na wao watakuwa miongoni mwa maeneo ambayo yatapata fursa ya kupata magari.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pia nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali yetu ya Wilaya iliyopo katika Manispaa ya Iringa ilifunguliwa ili kupunguza msongamano mkubwa uliyopo katika hospitali ya mkoa, lakini hospitali ile mpaka sasa hivi haina jengo la vipimo, haina wodi za wagonjwa wengine ina wodi za wazazi na hospitali ile imekuwa ikisaidia wagonjwa wanaotoka katika Wilaya ya Kilolo, *Iringa DC* na kwingineko; na Mheshimiwa Jafo tunamshukuru alifika; je, Serikali sasa inasaidiaje pamoja na kuwa imetoa pesa kwa ajili ya kujenga hospitali za wilaya nyingine wakati bado hazijajengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba ukienda Manispaa ya Iringa na kwa kuanzia hospitali ya mkoa ina wagonjwa wengi sana, ndiyo maana Serikali katika kuhakikisha kwamba tunapunguza mlundikano wa wananchi kwenda kutibiwa katika hospitali ya mkoa, ikawa ni wajibu kuhakikisha kwamba inajengwa hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama anavyotoa maelezo kwamba ile hospitali ya wilaya haijakamilika kwa kiwango ambacho kilitarajiwa, naomba nimhakikishie, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba hospitali zote za wilaya ambazo zinajengwa zinakuwa katika kiwango ambacho tunakitarajia ili mwananchi akipata rufaa kutoka kituo cha afya akienda kutibiwa kwenye hospitali ya wilaya apate matumaini kwamba nimefika katika hospitali ambayo hakika kwa majengo na huduma ataweza kupona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie, kwa kadri bajeti itakavyokuwa imeruhusu tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba suala la afya ni kipaumbele kama Serikali ilivyoelekeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa Sonia Juma Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, lakini linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Kiza Mayeye.

Na. 97

**Akinamama Wanaojifungua Kabla ya Muda wa Kustahili Likizo ya Uzazi**

**MHE. KIZA H. MAYEYE (K.n.y. MHE. SONIA J. MAGOGO)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia akinamama ambao wanajifungua kabla ya kipindi cha kuruhusiwa kupata tena miezi mitatu ya mapumziko ili waweze kuwahudumia (kuwanyonyesha) vichanga hao huku wakiendelea na majukumu yao ya kiofisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni namba H12 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, mtumishi wa umma anapojifungua hupewa likizo ya malipo ya siku 84. Hata hivyo, iwapo atajifungua zaidi ya mtoto mmoja (mapacha au zaidi), ataongezewa siku 14 na hivyo kuwa na likizo ya siku 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mtumishi wa umma atajifungua mtoto/watoto kabla ya kutimiza miaka mitatu atapewa likizo maalum ya wiki sita ili kuhudumia mtoto wake kwa mujibu wa Kanuni H12(6) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009. Baada ya hapo Serikali inaweza kumuongezea siku za kupumzika kulingana na ushauri wa daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, likizo ya uzazi hutolewa mara moja katika kipindi cha miaka mitatu kwa kuzingatia Sera ya Afya ya Mama na Mtoto inayosisitiza kulinda afya ya mama na mtoto na pia kuhimiza uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sera hii, msingi wa Serikali kuhimiza likizo ya uzazi kwa utaratibu huu ni kutoa fursa kwa watumishi wa umma kupata muda wa kutosha kutekeleza majukumu ya ajira yao na kuzingatia pia uzazi wa mpango.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni ukweli usiopingika kwamba suala la uzazi wa mpango ni makubaliano ya wanandoa kuhusu idadi ya watoto wanaowataka, lini wawazae na kwa wakati gani. Sasa, je, Serikali haioni sasa wakati umefika wa kuibadilisha hii sheria ili kuwawezesha wanandoa kupata watoto wanaowataka kutoka miaka mitatu hadi miwili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwa kuna tabia kwa sekta binafsi kuwa hawawapi nafasi ya likizo wafanyakazi wao kutokana na masharti mbalimbali. Sasa, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba hawa wafanyakazi wa Sekta Binafsi nao wenyewe wanapata likizo badala ya kunyimwa mshahara ili akapumzike au aamue apumzike akose mshahara; Serikali ina mpango gani kwa wafanyakazi hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Mkuchika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uzazi wa mpango sisi Watanzania tunaishi katika jamii, sisi ni wamoja. Sasa tumetafuta

utaratibu gani unaweza kutuweka sisi pamoja; mwingine anataka azae kila mwaka, mwingine anataka azae kila baada ya mwaka mmoja na nusu, mwingine anataka baada ya miaka minne, baada ya mjadala mrefu Bunge hili likaweka utaratibu kwamba miaka mitatu inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusisitiza; sheria hii kwanza inalinda afya ya mtoto mwenyewe kwamba unamwacha akue, lakini mhurumie na huyu unayemzalisha kila mwaka na yeye naye anahitaji kupumzika. Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba, hii sera Serikali imeweka kwa nia moja; kulinda afya ya mtoto apate kukomaa vizuri kabla hujamtafuta mwingine, lakini pia huyo mama naye anahitaji kupumzika, kumzalisha kila mwaka ukasema ni muafaka kati yetu sisi; hao wanandoa wanaishi katika jamii ambayo ina sheria, taratibu na kanuni na hiyo jamii inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sekta binafsi kwamba hawawapi nafasi; hizi *labour laws,* sheria za masuala ya kazi ni za nchi nzima. Kwa hiyo zinatakiwa ziheshimiwe na watu wote; binafsi na wale waliopo Serikalini na Mashirika ya Umma.  Pale inapotokea kwamba mtu kanyimwa likizo ya uzazi ati kwa sababu anafanya kwenye shirika binafsi, Waziri wa Utumishi ajulishwe na ntachukua hatua stahiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante.  Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLELL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini bado nina swali moja la nyongeza. Kwa wakati uliopo hivi sasa wanawake wengi wanazaa katika umri mkubwa, hasa kutokana na wengi wamekwenda shule au wakati mwingine pia uzazi kwa hivi sasa kwa wanawake wengi imekuwa ni shida, kwa hiyo utakuta wengi wanazaa…

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. AMINA S. MOLELL:** …Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo najenga hoja, tafadhali nakuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu ana miaka 40 ndipo anapata mtoto wa kwanza, mtu huyu anataka azae ndani ya miaka minne tayari awe na watoto wawili kwa sababu umri haumruhusu kwa wakati huo; hatuoni kwamba kwa sasa hivi sheria hii imepitwa na wakati na inabidi iletwe hapa ifanyiwe mabadiliko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema watu wanaozaa katika umri mkubwa tuwalegezee masharti waende wanavyotaka. Kwanza nataka niseme hii ni sheria, sheria katika nchi hufuatwa na watu wote, lakini pia mimi kwa ufahamu wangu na utu uzima wangu mama anayezaa akiwa mtu mzima ndiye haswa anatakiwa uangalizi mkubwa kuliko yule aliyewahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo miaka 40 anayoitaja kuanzia 40 kwenda juu, kwa ufahamu wangu, ni kipindi ambacho mama akijifungua anahitaji uangalizi wa hali ya juu. Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba hii sheria haijapitwa na wakati, hii sheria ni muafaka, inalinda afya ya mtoto na inajali uzazi wa mpango.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo na linaelekezwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 98

**Upotevu wa Nyara za Serikali**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za kulinda Nyara za Serikali:-

Je, vitalu vya uwindaji vinachangia kiasi gani katika upotevu wa Nyara za Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji wa kitalii ni sehemu ya matumizi endelevu ya wanyamapori na unafanyika kwa mujibu wa Sera ya Wanyamapori ya Mwaka 2007, Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori, Sura 283 na Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2015 zikisomwa kwa pamoja, pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017. Ili uwindaji uweze kufanyika, kampuni iliyopewa kitalu huomba na kupatiwa mgao wa wanyamapori *(quota)* watakaowindwa katika msimu husika. Mgao wa wanyamapori huandaliwa na Kamati ya Ushauri wa Mgao wa Wanyamapori *(Quota Allocation Advisory Committee).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vinavyotumika kutoa mgao ni pamoja na; moja, idadi ya wanyamapori *(population status)* kulingana na sensa; pili, taarifa kutoka kwa Maafisa Wanyamapori wa maeneo yanayohusika; tatu, mafanikio katika matumizi ya mgao wa wanyamapori *(offtake levels);* nne, ukubwa wa nyara zinazopatikana mwaka hadi mwaka *(trend of trophy size)* na tano, matakwa ya Mikataba ya Kimataifa kama vile *CITEs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeweka udhibiti wa kutosha ili kuzuia uwezekano wa kupotea nyara wakati wa uwindaji. Udhibiti huo unaanzia kwenye kutoa vibali ambavyo ni vya kielektroniki, usimamizi porini wakati wa uwindaji ili kuhakikisha aina na idadi ya wanyamapori wanaowindwa waliotolewa kwenye kibali inazingatiwa, umilikishwaji wa nyara zilizowindwa na ukaguzi wa nyara kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Aidha, pale inapotokea ukiukwaji wa sheria na kanuni wahusika hufikishwa mbele ya sheria na adhabu stahiki hutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kuongeza udhibiti katika usimamizi wa uwindaji wa kitalii kwa kutumia sheria na kanuni ambazo wanyamapori huwindwa kwa kuzingatia jinsi, umri na ukubwa wa nyara. Udhibiti huo umesaidia kupunguza uwezekano wa wanyamapori kupungua kutokana na kuwindwa na pia kumesaidia kupatikana kwa mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii. Hivyo basi, vitalu vya uwindaji husaidia katika kulinda na kuhifadhi nyara na kutoa mchango katika uchumi wa nchi, hasa kwa kuchangia fedha za kigeni, kutoa ajira kwa wananchi na kuchangia maendeleo ya jamii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbogo!

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika mapato yanayotokana na uwindaji katika hivi vitalu halmashauri zetu ambazo ziko na maeneo haya zinapata asilimia 25 ya mapato, lakini katika hiyo asilimia 25 ni baada ya kutoa zile gharama za uendeshaji. Sasa kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa haya makusanyo na kiwango hiki kinachotolewa bado ni kidogo na ukizingatia kwamba halmashauri ndizo ambazo zinasimamia kwa ukaribu maeneo haya. Sasa je, Serikali iko tayari kuongeza kiwango toka asilimia 25 mpaka 30 ili tuweze kukidhi gharama za operesheni katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika majibu ya Serikali wameeleza namna bora za kudhibiti hizi nyara za Serikali na tunatambua juhudi ambazo Wizara imefanya kwa kushirikisha vyombo vya ulinzi na usalama, kuboresha kanuni na kuvihusisha kwenye kulinda maliasili hizi za Serikali. Hata hivyo, kuna udhaifu waa kibinadamu, yaani watumishi katika hizi kampuni. Je, Serikali itafanya mkakati gani kuhakikisha kwamba watumishi wa hizi kampuni hawachangii katika udhaifu wa kupoteza nyara za Serikali?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu; mtaongeza kutoka 25% mpaka 30%?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Richard Mbogo kwa swali zuri na kwa jinsi ambavyo amekuwa akifanya kazi katika kutetea wananchi wake wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zinavyoelekeza ni kwamba 25% inayotokana na mapato yote ya uwindaji wa kitalii ndio yanakuwa-*calculated* na yanaenda kwenye halmashauri, si baada ya kutoa gharama. Hivi sasa tunafanya mapitio ya sheria zote zinazohusu uhifadhi na wanyamapori. Baada ya hizo sheria kukamilika kanuni husika pia zitapitiwa tutaangalia kama hilo walilopendekeza litawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu watumishi ambao wanajihusisha na upotevu wa nyara za Serikali; ni kwamba hivi sasa ofisi yangu tumeunda Kamati ndogo ambayo inapita katika maeneo mbalimbali kubaini makampuni pamoja na watumishi wa ofisi zetu, wale ambao wanakuwa wanahusika na upotevu wa nyara za Taifa. Baada ya Kamati hiyo kukamilisha na mapendekezo kuletwa, hatua stahiki zitachukuliwa kwa watumishi wote wa namna hiyo, kwa sababu tunataka mtumishi afanye kazi yake kwa weledi, kwa kuzingatia kanuni, sheria na maadili ya kazi yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Limechukua muda mrefu mno, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa Ibrahim Raza, Mbunge wa Kiembe Samaki, kwa niaba yake na Mheshimiwa Murad Saddiq.

Na. 99

**Kukiboresha Kituo cha Polisi Mazizini – Kiembe Samaki**

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ (K.n.y. MHE. IBRAHIM HASSANALI RAZA)** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Mazizini kilichopo Kiembe Samaki kipo katika hali mbaya na hakina vitendea kazi, jengo ni chakavu, hakina gari na mazingira yake hayaridhishi:-

Je, ni lini Serikali itaboresha kituo hicho kwa kutatua changamoto zilizopo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Raza, Mbunge wa Kiembe Samaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hali na mazingira ya Kituo cha Polisi Mazizini hairidhishi kutokana na uchakavu wa jengo pamoja na uhaba wa vitendea kazi kama ilivyo kwa baadhi ya vituo katika maeneo mbalimbali. Kituo cha Polisi Mazizini kina majengo mawili. Katika mwaka 2015 Serikali ilifanya ukarabati wa jengo moja la kituo hiki ambapo ukarabati ulikamilika na tayari jengo hilo linatumika kwa kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Jeshi la Polisi limependekeza kwa ajili ya maendeleo ya vituo kiasi cha shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya ukarabati na kuboresha miundombinu mbalimbali ya Jeshi la Polisi kote nchini ikiwemo ukarabati wa jengo la pili la Kituo cha Polisi Mazizini Jimboni Kiembe Samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya Jeshi la Polisi na kuongeza vitendea kazi kama vile magari awamu kwa awamu ili kutatua changamoto zinazokabili Jeshi la Polisi katika maeneo mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hebu subiri tu hapo hapo. Kwenye jibu nililonalo mbele yangu linasema hivi; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Jeshi la Polisi limetenga fedha, limetenga.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa-*edited,* nimependekeza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Murad Saddiq.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nasafi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na pamoja na bajeti ambayo wameipanga, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ambalo limeulizwa la polisi Mazizini linafafana kabisa na suala la Mvomero katika Kituo cha Polisi Turiani. Kituo cha Polisi Turiani kipo katika jengo la mabati na jengo lile lilijengwa tokea enzi ya mkoloni na hadi leo kituo kinatumika. Hata hivyo, wananchi na wadau mbalimbali tumeamua kujenga kituo cha polisi na sasa hivi kimefikia hatua ya *lenter* na ujenzi huo umefanyika zaidi ya miaka kumi iliyopita. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea Turiani na kuonesha nia yake kuweza kumalizia kituo cha polisi Turiani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Turiani ni sehemu ya Wilaya ya Mvomero migogoro ya wakulima na wafugaji ni mingi na jitihada kubwa zimefanyika. Je, yuko tayari kutusaidia gari kwa ajili ya Kituo cha Polisi Turiani?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mchemba.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Murad kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa karibu sana masuala ya wananchi wake wa Jimbo la Mvomero. Natambua Jimbo la Mvomero jiografia yake ni ya tofauti sana kwa sababu kuna baadhi ya tarafa ziko ukanda mwingine huku kama unaelekea barabara hii ya kwenda Mikumi na upande mwingine ndiko huko Turiani anakokusemea. Kwa hiyo nianze tu kwa kusema kwamba niko tayari na si mbali kutembea kituo hicho anachokisemea ili kuweza kujionea kazi nzuri ambayo wananchi wameshafanya kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tutaweka kipaumbele kwenye upande wa kuipatia wilaya yake vitendea kazi

ikiwemo gari kwa kuzingatia hali halisi ya migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza katika Wilaya ya Mvomero pamoja na Kilosa ambayo inahitaji sana vitendea kazi kama hivyo. Kwa hiyo tunazingatia punde tutakapokuwa tumepata magari kwa ajili ya kusaidia vituo vya polisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ali King na mwisho Mheshimiwa Jaku.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Waswahili wanasema usipoziba ufa utajenga ukuta na usipotibu utazika, swali langu dogo tu, namuuliza Mheshimiwa Waziri. Ni lini Serikali itakusanya mchango wa maafa kwa jengo bovu la Ziwani Polisi la Kilimanjaro pindi maafa hayo au jengo litakapoanguka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Nchemba, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limeletwa mara kadhaa. Niseme tu, kwa sababu tuna siku chache kabla hatujakwenda kwenye bajeti yetu tutapa fursa tuongee na Mheshimiwa Mbunge ili tukubaliane kuhusu ni lini kwa sababu swali lake ametaka tumtajie ni lini tutachukua hatua hiyo aliyoisema yeye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kuniona. Nina swali dogo sana la nyongeza. Swali la msingi linahusu vituo na nilikuwa nikipigia kelele huu mwaka wa tatu au wa nne kuna mjenzi wa kampuni ya Albatina na Mheshimiwa Waziri amekuwa akiahidi sana ndani ya jengo hili muhimu kwa wananchi. Kesho kutwa tarehe mosi mwezi wa Tano Mungu akijalia tunapitisha bajeti; na nilimwambia huyu mzee mpaka leo asubuhi tumezungumza, huyu mzee bado anaumwa anadai ng'ombe kama 30; na amekiri si mara ya kwanza si mara

mbili, si mara tatu, kesho kutwa sitakuja kuizuia shilingi Mungu akinijalia. Je, lini atalipwa mjenzi huyu karatasi zake na lini nimlete?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba Mheshimiwa Jaku amelifuatilia sana jambo hili Ofisi na hata kwenye masuala ya anapopata fursa ya kusemea hapa kwenye bajeti. Kama nilivyosema, tutaonana naye ili tuweze kukubaliana, kwa sababu kitu ambacho kimetuchelewesha hapa katikati ilikuwa ni kwamba lazima madeni yote yafanyiwe uhakiki kabla hayajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa yalikuwa yanafanyiwa uhakiki, nitaomba Mheshimiwa Jaku aridhie tuwe na kikao mimi pamoja na yeye na watendaji wangu ili tuweze kupata kwanza *status* ya upande wa uhakiki umefikia hatua gani. Tukishajua kwamba limeshahakikiwa liko tu kwenye hatua za kulipwa tutaweza kulifanyia uharaka kwa sababu kama anavyosema Meshimiwa Jaku mhusika anahitaji sana fedha kwa ajili ya matibabu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata ni linaulizwa na Mhehsimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia.

Na. 100

**Kutumika Ipasavyo kwa Wanazuoni Watafiti**

**MHE. DKT IMMACULATA S SEMESI** aliuliza:-

Kwa ujumla Serikali haiwatumii ipasavyo wanazuoni kama watafiti, hasa katika eneo la tafiti ya sayansi kwa kukuza sekta ya viwanda:-

Je, ni kwa nini vyuo vikuu vya Serikali havipati fungu kwa ajili ya tafiti ili kutoa suluhisho mbalimbali na miongozo ya kimaendeleo yenye misingi ya tafiti kisayansi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hutenga fedha kwa ajili ya tafiti kupitia Mfuko wa Taifa ya Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) unaoratibiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH).* Mfuko huu upo ili kuhakikisha maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yanapatikana ambayo ni pamoja na tafiti kufanyika kulingana na vipaumble vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kwa ajili ya tafiti kutoka kwenye Mfuko huu hutumiwa kwa utafiti wa ndani ya nchi wakiwemo wanazuoni kwa njia ya ushindani. Aidha pamoja na Wanazuoni kupata fedha za kufanya tafiti kupitia Mfuko wa MTUSATE, washirika wa maendeleo kama vile Serikali za Sweden na Norway hufadhili shule za utafiti kwa kupeleka fedha za utafiti moja kwa moja katika vyuo vikuu mbalimbali kama vile Chuo Kiuu cha Dar es Salam, Chuo cha Ardhi na Chuo cha Tiba ya Afya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa MTUSATE imefadhili miradi 102 ambayo ilitekelezwa na Taasisi mbalimbali za utafiti za vyuo vikuu vya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Kati ya miradi hiyo vyuo vikuu vilitekeleza jumla ya miradi 48 iliyofadhiliwa kwa njia ya ushindani ambayo imegharimu jumla ya shilingi bilioni 4.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya vyuo vikuu hivyo ni pamoja na Chuo Kiuu cha Kilimo cha Sokoine *(SUA),* Chuo

Kiuu cha Dar es Salam *(UDSM),* Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo Kikuu cha Zanzibar *(SUZA),* Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba, Taasisi ya Syansi na Teknolojia ya Nenson Mandela, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salam na chuo Kikuu Dodoma *(UDOM).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya tafiti zilizofanywa na Wanazuoni zimeonekana kuwa ni tafiti zenye tija katika maendeleo ya uchumi wa viwanda. Baadhi ya matokeo ya tafiti hizo ni pamoja na utengenezaji wa chanjo mseto ya kuku inayostahimili joto ya kukinga magonjwa matatu (mdondo, ndui na mafua) iliyofanywa na *SUA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kugunduliwa kwa mbinu bora za kuzalisha vifaranga vya kaa iliyofanya na *SUZA*, kugunduliwa kwa vifaa kusafishia maji kwa matumizi kwa matumizi majumbani iliyofanya na Taasisi ya Nenson Mandela; usindikaji wa ngozi na mazao ya mifugo ambayo imewezesha kuanzisha kwa mitaala ya astashahada na shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Sokoine iliyofanywa na *SUA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna udhibiti wa magonjwa yanayiharibu mazao ili kuleta uhakika wa chakula na kuondoa umaskini iliyofanyiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salam; pamoja na udhibiti wa uharibu wa mazao unaofanywa na panya kwa kutumia mkojo wa paka iliyofanyika na *SUA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wanazuoni wanafanya tafiti zenye tija Serikali imesaidia uazishwaji wa vituo mahiri *(African Center over Excellence*) vinne kupitia Benki ya Afrika ambapo takribani shilingi bilioni hamsini zimewekezwa kuendeleza utafiti katika Chuo Kiku cha Kilimo cha Sokoine na Taasisi ya Teknolojia ya Nelsoni Mandela.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa muuliza swali Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. DKT IMMACULATA S SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, nina maswali mawili ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa inafahamika kwamba vyuo vikuu ni chachu ya maendeleo kwa sababu wanazalisha hawa wataalam na wanavumbua au wanaleta suluhisho katika shughuli mbalimbali. Swali lilivyojibiwa kwa upande MTUSATE linaonesha kwamba MTUSATE wameshafadhili miradi 102, kati ya hiyo miradi 44 kutoka vyuo vikuu na shilingi bilioni 4.6 ndio zilizotumika. Hata hivyo, kwa bahati mbaya haiku-*indicate* ni muda gani. Je kipindi cha miaka 10, 20 au 30 kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya hizi ya elimu ya vyuo Vikuu na *issue* za tafiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni kuhusu utengaji wa fedha na upatikanaji wa fedha ambazo zinaelekezwa *COSTECH*. Mwaka wa fedha 2017/2018 zilitengwa bilioni 13.6, kati ya hizo bilioni bilioni tatu ni fedha za nje. Mwaka huu unaokuja wa fedha zimetengwa bilioni 9.5 kutoka kwenye mfuko wa ndani. Viwango hivi vya fedha ni vidogo sana lakini ningependa kujua kati ya hizi fedha zinazotengwa zinazowafikia *COSTECH* ni kiasi gani ili ziweze kushuka kwenye hivi vyuo vikuu husika kwa ajili ya tafiti? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi, majibu yalikuwa marefu.

**NAIBU WAZIRI ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo nimezungumzia kwamba tayari zimeshatolewa kwa ajili ya vyuo vikuu kwa ajili ya utafiti ni fedha ambazo zimetengwa kuanzia mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, kwamba ni kiasi gani ambacho kimeshatolea *COSTECH* ni suala la takwimu, naahaidi nitakapotoka hapa nitampatia takwimu sahihi Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi.

Na.101

**Kurudisha Chuo cha Ualimu Ndikwa**

**MHE. JEROME D BWANAUSI** aliuliza:-

Wakati Serikali inafanya juhudi za kuongeza idadi ya Walimu na kulipa stahiki zao:-

(a) Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kurudisha Chuo cha Ualimu Ndwika badala ya sekondari kama ilivyo sasa?

(b) Je, ni lini Serikali italipa madeni hayo?

**NAIBU WAZIRI ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1999, Serikali iliamua kuvibadilisha baadhi ya Vyuo Vya Ualimu kuwa shule za sekondari, Ndwika kikiwa kimojawapo. Uamuzi huo ulifikiwa baada ya utafiti uliofanyika kubaini kuwa vyuo hivi vilikuwa na uwezo mdogo wa kudahili wanachuo kiasi cha kutokuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uamuzi huo wa Serikali Chuo cha Ualimu Ndwika kilibadilishwa na kuwa na shule ya sekondari ya wasichana ya bweni kutokana na mahitaji makubwa ya shule za bweni kwa wasichana. Aidha, uamuzi huo ulitokana na changamoto mbalimbali yanayopata wanafunzi wa kike zikiwemo umbali mrefu wa kwenda shule na kurudi nyumbani, baadhi ya jamii ya

kutowapa fursa ya kwenda shule na pia vishawishi mbalimbali vinavyopelekea kupata mimba wakiwa masomoni. Hivyo, shule hii ina umuhimu mkubwa katika kumkomboa mwanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina jumla ya Vyuo vya Ualimu 35 ambavyo vimekuwa vikidahili wanachuo kutoka nchi nzima. Kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imefanyia upanuzi na ukarabati mkubwa vyuo 24; na katika mwaka wa fedha 2014/2019 vyuo vingine kumi vitapanuliwa kwa lengo la kuongeza nafasi za udahili hivyo kutosheleza mahitaji ya Walimu. Kwa hiyo Serikali itaendelea kuyatumia majengo ya kilichokuwa Chuo cha Ualimu Ndwika kutoa elimu ya sekondari kama ilivyo sasa.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI imelipa madeni ya Walimu 86,234 yenye jumla ya shilingi bilioni 33,804,082,905 katika kipindi cha mwaka wa 2015/2016 na 2017/2018. Serikali kwa sasa inahakikisha kuwa hakuna madeni yatakayolimbikizwa kwa kulipa stahiki za Walimu kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bwanausi.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini pia niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwajali Walimu na kuhakikisha kwamba inalipa malimbikizo yao, lakini nina maswali mawili ya nyongeza; kwanza sababu zilizotolewa na Serikali ya kukiondoa chuo hiki kuwa sekondari kwa sasa si sababu muhimu sana, kwa hiyo bado tunasisitiza Mheshimiwa Waziri kwamba. Je, hawaoni kwa kukiondoa Chuo kile cha Ualimu cha Ndwika kumefanya Kanda ya Kusini kuwa na vyuo vichache vya ualimu hivyo bado umuhimu wa chuo kile kurudi Serikali iutazame upya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, pamoja na kulipa malimbikizo ya Walimu lakini je, nini mikakati ya Serikali

kuhakikisha sasa malimbikizo haya ya Walimu hayarudii kama ilivyokuwa mwanzo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukanda wa Kusini, au niseme mkoa anaotoka Mheshimiwa Mbunge tayari una vyuo vingine vitatu vya ualimu. Mkoa wa Mtwara una Chuo cha Ualimu cha Kitangali kilichopo Newala, lakini vile vile kuna Chuo cha Ualimu cha Mtwara Ufundi pamoja na Mtwara Kawaida. Hata hivyo, ifahamike kwamba vyuo hivi vyote ni vyuo vya kitaifa na udahili wake unawachukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli huu kama Mheshimiwa Mbunge bado anafikiri kuna haja ya kurudisha shule hiyo ya sekondari kuwa chuo, nimshauri tu wajipange wakae katika halmashauri yao, walete mapendekezo wizarani na kwa vyovyote vile si msahafu, kama kuna haja za msingi bado Serikali inaweza kufikiria kurudi huko tulipotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, ni kweli kwamba kwa sasa Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba hakuna tena madeni ya Walimu ambayo yatajilimbikiza. Hatua mbalimbali tayari zimeshachukuliwa ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku sasa, kwa mfano kuhamisha Walimu kwa utaratibu wa kawaida bila kuwalipa stahiki zao. Vile vile kuhakikisha kwamba kila mwajiri anatenga fedha kwa ajili ya likizo za Walimu, lakini pia pale wanapostaafu kuhakikisha kwamba fedha za kusafiri zinakuwa zinatolewa. Kwa hiyo tunachofanya sasa ni kuhakikisha kwamba hakuna kulimbikiza tena madeni ya Walimu na inawezekana tu kufanya hivyo kama stahiki zao zote zitalipwa kwa wakati muafaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. HUSSEIN M.BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la elimu hapana mimi niliomba kuuliza swali la nyongeza kwenye swali namba 100.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali lanyongeza kutokana na swali namba 101 la Mheshimiwa bwana Jerome Bwanausi. Kwa muda mrefu pia Serikali imekuwa ikiwakopa wazabuni na kusababisha madeni makubwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Chuo cha Wauguzi Masasi, Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Masasi, Ndanda *High School* pamoja na Chidia Sekondari yanayotisha wazabuni hawa kufilisika lakini pia...

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

**MHE. CECII D. MWAMBE:** ...wanataka kusitisha kutoa huduma zao; sasa swali langu, ni lini Serikali kwa makusudi kabisa itaamua kuwalipa wazabuni wa ndani hasa wa vyakula katika hizi shule zetu za mabweni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba swali la Mheshimiwa Cecil Mwambe halina uhusiano wowote na swali la msingi, lakini nipende tu kusema kwamba kwa sasa Serikali imejidhatiti vilevile kuhakikisha kwamba inalipa madeni yote ikiwa ni pamoja na madeni ya wazabuni. Hata hivyo, ifahamike kwamba madeni yote yatalipwa tu baada ya uhakiki kufanyika, kwa sababu huko nyuma kuna madeni mengi yamelipwa lakini hayakustahili kulipwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuta ambalo linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano na linaulizwa na Mhehsimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo.

Na.102

**Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Mwezi Septemba 2015 Serikali ya Tanzania, China na Oman kwa pamoja zilisaini mkataba wa ujenzi wa Bandari mpya ya Bagamoyo:-

Je, ni lini ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo utaanza rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo utaanza rasmi mara tu Timu ya Wataalam wa Serikali *(Government Negotiation Team)* kukamilisha majadiliano na wawekezaji ambao ni Kampuni ya *China merchants port holdings company limited* ya China na *Oman State General Reserve Fund* na Serikali kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7 Desemba, 2016 Serikali ilifanya uamuzi kwamba mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo utekelezwe kwa ubia na sekta binafsi ili kuharakisha utekelezaji wa mradi huo. Kufuatia uamuzi huo tarehe 31 Machi, 2017 Serikali ya Tanzania ilipokea andiko la mapendekezo ya uwekezaji lililowasilishwa kwa pamoja kati ya Kampuni ya *China Merchants Port Holding Company Limited* ya China na *Oman State General Reserve Fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatarajiwa kuwa timu ya majadiliano ya Tanzania itakamilisha majadiliano hivi karibuni

na ujenzi kuanza mara tu baada ya mkataba wa uwekezaji wa mradi kusainiwa kati ya Serikali na wawekezaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dokta Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maijibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuzingatia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba *GNT* inatarajia kukamilisha majadiliano hivi karibuni. Sasa wananchi hawa watatakiwa bila shaka kuhama baada ya majadiliano kukamilika na ujenzi unaanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi 687 ambao walithibitika kuwa na mapunjo katika fidia zao na wakahakikiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Je, wananchi hawa lini watalipwa fidia zao ambazo tayari zimeshahakikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa fidia ya wananchi haijakamilika katika eneo hilo la Bandari, moja katika bilioni 57.7 imelipwa mpaka sasa bilioni 45 peke yake, lakini pia kuna hawana wananchi ambao walikuwa wana mapunjo katika fidia zao na wao hawajalipwa. Je, nini kauli ya Serikali kuhusu miundombinu ya Shule ya Msingi Pande, Shule ya Msingi Mlingotini na Zahanati Pande ambazo wananchi wanaendelea kuzitumia. Kwa vile watatakiwa kuondoka, nini kauli ya Serikali kuhusu kuihamisha miundombinu hiyo kuwapelekea mahali ambapo watakuja kuitumia?

**MWENYEKITI:** Ahsante. majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kawambwa kwamba anafuatilia sana upatikanaji au ujenzi

wa Bandari ya Bagamoyo na anafahamu kabisa kwamba Bandari hii itakapojengwa ni fursa kwa wakazi wa Bagamoyo. Kwa hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa kwa kutetea wananchi wake lakini pia amekuwa akifuatilia sana juu ya fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, kwamba Serikali inawajali wananchi ndiyo maana jumla ya shilingi bilioni 48 imelipwa kama fidia kati ya kiasi cha fedha cha bilioni 57 ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya kulipa fidia wananchi hawa. Eneo hili ni kubwa, lina ukubwa wa hekta 800 ni eneo kubwa sana, kwa hiyo changamoto zilikuwa nyingi, lakini Serikali imekamilisha kuwalipa wananchi. Wako wananchi wachache ambao walikuwa hawajalipwa pamoja na taasisi ikiwemo Taasisi hii ya Uvuvi Mbegani pamoja na hizi shule ambazo Mheshimiwa amezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu kwamba, kwa sababu Serikali iko *committed;* ni kwamba wananchi ambao walipunjwa uhakiki umekamilika, kwa hiyo wakati wowote kama ilivyofanya kwenye malipo yao ya awali watalipwa hawa wananchi. Kwa hiyo niwahakikishie wananchi wa Bagamoyo kwamba utaratibu unakamilishwa ili sasa hizi fedha ambazo zimekuwa ni za nyongeza; ni kiasi kidogo tu kama, Serikali imelipa bilioni arobaini na nane na bilioni zingine nane zipo; ni kwamba tupo *committed* kulipa hizi fidia. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi wananchi hawa watalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, anauliza juu ya hatima ya shule hii ya Pande. Ni dhahiri kwamba kati ya zile fedha bilioni nane zilizobaki ni hizi taasisi ambazo ziko chini ya Serikali ambazo ni pamoja na Shule ya Msingi ya Pande, Shule ya Msingi ya Mbegani, Zahanti ya Pande pamoja na Mbegani. Kwa hiyo hizi ndizo shilingi bilioni nane zilizobaki kwa ajili ya kulipa na kuhamisha hizi taasisi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi tumejipanga vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna uhakiki wa kuhamisha makaburi lakini pia tuliweza kupata thamani ya shilingi zaidi ya milioni mia tano ili kuweza kuhamisha makaburi pamoja na kuhamisha hizi shule. Kwa hiyo fedha zimeshapatikana na kibali kimeshatolewa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Bagamoyo wasiwe na wasiwasi, fedha hizi zilizobaki bilioni nane pamoja na hii milioni mia tano zipo, tutahamisha hizo shule ili wananchi wapate huduma na ujenzi uweze kuanza mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbaraka Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Tatizo la kutoanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo linafanana sana na tatizo la kutokuanza ujenzi wa Bandari ya Nyamisati katika Wilaya ya Kibiti. Bandari ya Nyamisati ni Bandari ambayo ni kiungo baina ya wananchi wa Mafia wanapokuja Dar es salaam. Mkandarasi ameshapatikana toka mwaka jana mpaka leo hajafika *site,* ni nini kauli ya Serikali kuhusu Mkandarasi huyu? Nakushuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua na Mheshimiwa Dau hapa amekuwa akipiga kelele kweli, uko ule utaratibu wa kujenga Bandari ya Nyamisati unaendelea. Nimwombe tu asiwahishe shughuli hata wakati wa bajeti ataona tumependekeza fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Bandari hii ya Nyamisati. Kwa hiyo kama atataka taarifa za ziada basi naomba tuonane ili angalau nimwoneshe mpango madhubuti uliopo kwa ajili ya kuokoa wananchi wa Mafia na Watanzania wengine ambao watakuwa wakisafiri kwenda Mafia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. ZITTO R. Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la changamoto za Bandari ya Bagamoyo, Bandari ya Nyamisati ni changamoto zinazofanana kabisa na miradi minne ya Bandari ya Kigoma. Uboreshaji wa Bandari ya Kigoma, Bandari kavu ya Katosho, Bandari ya Ujiji na Bandari ya Kibirizi; lakini tu ni kwamba fedha zimetengwa toka mwaka 2016/2017 na tayari Mamlaka ya Bandari imekwishaweka utaratibu wa manunuzi. Wizara imezuia Mamlaka ya Bandari kutangaza zabuni hizo za Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ilieleze Bunge hapa, ni kwa nini haijaidhinisha zabuni hizo kutangazwa ili wananchi wa Mkoa wa Kigoma waweze kupata faida ya uchumi wa jiografia kwa kuboresha Bandari ya Kigoma?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kwamba Serikali imezuia; unajua ujenzi una hatua zake, Mheshimiwa Zitto anafahamu. Ziko hatua, ndiyo maana tunaanza kwenye usanifu, tunaanza kuweka fedha na mijadala iko mingi kama kunajitokeza jambo ambalo linahitaji labda wakati mwingine kupata muda kuli-*clear* kwamba kama kuna *risk* inajitokeza lazima Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe wasiwasi na asubiri. Mheshimiwa Waziri wakati akijibu katika hotuba ya Waziri Mkuu alisema hapa Bungeni na alijaribu kusema kwa ufupi na akasema tusubiri wakati wa bajeti Mheshimiwa Zitto ataona namna tulivyojipanga ili kuhakikisha Bandari zote kwa upande wa Kigoma, kwa upande wa Ziwa Victoria, kwa upande wa Ziwa Nyasa na maeneo mengine. Kwa hiyo, niseme tu kwamba maeneo yote ambayo Mheshimiwa Zitto anataja kwa maana ya Katosho na Kibirizi tumeonesha vizuri katika mapendekezo ya bajeti ambayo ni Jumatatu tu tutaanza kuizungumza bajeti ya Wizara hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tumalizie swali letu la leo. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na.103

**Hitaji la Kiwanda cha Mbolea Mkoani Njombe**

**MHE. LUCIA M. MLOWE** aliuliza:-

Ardhi ya Njombe inahitaji mbolea kwa wingi zaidi kuliko mikoa mingine;

Je, Serikali ina mkakati gani wa uanzishaji wa Kiwanda cha Mbolea Mkoani Njombe?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya viwandani inatokana na malighafi za madini. Aina za mbolea hizo ni *nitrogen* inayotengenezwa kwa kutumia *ammonium* inayokana na gesi asilia, mbolea ya *phosphorous* na ile ya *phosphate.* Tanzania ina kiwanda kimoja kikubwa cha mbolea cha Minjingu Mkoani Manyara kinachotengeneza mbolea aina ya *phosphate* kutokana na malighafi husika kupatikana mkoani humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upatikanaji wa soko la mbolea Mkoani Njombe, tafiti za kijiolojia zinaonesha kuwa malighafi za *phosphate*, *phosphorous* na gesi asilia hazipatikani mkoani humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujenga viwanda vingine vya mbolea, majadiliano na wawekezaji wa kampuni za *HELM* na *FERROSTAAL* ya Ujerumani zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa viwanda viwili katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kutokana na upatikanaji wa gesi asilia. Hivyo ni vyema Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na mkoa na halmashauri kuhamasisha uwekezaji unaolenga zaidi kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya malighafi zinazopatikana kwa wingi katika mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo mkoa mmoja utakuwa soko la bidhaa za mkoa mwingine kama itakavyokuwa kwa mbolea kutoka Lindi na Mtwara wakati Mkoa wa Njombe ukitoa mazao ya chakula, matunda na mazao ya mbao. Serikali inaendelea kuvutia wawekezaji katika viwanda vya mbolea ili kutosheleza mahitaji ya nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlowe.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza; kwa kuwa kiwanda cha mbolea hakiwezi kujengwa Njombe kutokana na kutopatikana kwa malighafi; na kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Njombe wanalima mwaka mzima, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha mbolea inapatikana katika Mkoa wa Njombe kila wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Njombe mwaka jana wamelima kwa wingi mahindi ambayo yamekosa soko na hata mwaka huu bado wamelima mahindi kwa wingi yatakosa soko vile vile. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha inawatafutia soko la uhakika hawa wananchi wa Mkoa wa Njombe?

**MBUNGE FULANI:** Wale tu kama mbaazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa naomba tutulie tu tutapata majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali imekuwa ikifanya hivyo kuhakikisha kwamba mbolea inapatikana na si mara moja Waziri wa kilimo amekuwa akitoa taarifa juu ya upelekaji wa mbolea katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kuhusu suala la masoko ya mahindi; kimsingi nizidi tu kuwakumbusha, ni kwamba Serikali imekuwa ikiendelea kutafuta masoko. Pamoja na kutafuta masoko tunazidi kusisitiza kuhakikisha kwamba mbali ya kuuza mahindi yakiwa ghafi ni vyema kuhakikisha kwamba mahindi hayo kwanza yanatengenezwa kama unga au chakula cha mifugo au kuhakikisha kwamba yameongezwa thamani badala ya kuyasafirisha mahindi ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambayo inapenda kusafirisha mali zake zikiwa ghafi kwa kweli si nchi ambayo itaweza kupiga hatua kubwa katika uchumi hususani katika malengo ya nchi, haya ya uchumi huu wa viwanda.

**MWENYEKKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Niombe tu kuliarifu Bunge kwamba katika muda wa wiki moja ijayo tutafanya semina ya Bunge zima kuwaeleza mchakato mzima wa upatikanaji wa mbolea nchini. Tunatumaini kwamba katika semina hiyo Wabunge sasa tutakuwa tumekuwa na uelewa wa pamoja wa nini Serikali inafanya na kama zipo changamoto, basi hiyo itakuwa fursa nzuri ya kuzijadili ili tuweze kwenda kwa pamoja sawasawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Sisi Wabunge wa

Mkoa wa Njombe kwa ujumla wetu tumekuwa tukilalamika sana juu ya upatikanaji wa mbolea katika mkoa wetu; na wananchi wetu ni wakulima ambao hawatumwi na mtu kwenda kufanya kazi ya kilimo. Je, ni lini sasa *TFC* watakuwa na *godowns* za kutosha ili ku-*supply* mbolea katika Mkoa wa Njombe?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu kwa kifupi sana, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wa Njombe kwa jitihada kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa na kilimo kinachotosheleza katika ulishaji wa Taifa na kuweza kuuza nje. *TFC* imekuwa na maghala karibu katika kila Mkoa na hata sasa bado kuna mazungumzo yanayoendelea ya kuona kwamba pengine iweze kuwa moja kwa moja chini ya Wizara ya Kilimo ili sasa masuala hayo yaende vizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Martha Mlata atafuatiwa na Mheshimiwa Nape.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mkoa wa Singida unastawisha sana zao la alizeti na wananchi wa Mkoa wa Singida wameelewa sana dhana ya viwanda. Sasa tatizo linakuja kwenye zao la alizeti kwa sababu Serikali haijaweka msisitizo katika kuleta ruzuku ya mbegu ili zao lile lilimwe kwa wingi kukidhi viwanda vinavyojengwa Mkoani Singida. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mkakati mahsusi wa zao la alizeti ambao mkakati huo pamoja na mambo mengine umelenga kwanza kuongeza uzalishaji wa alizeti hapa nchini na usindikaji wa mazao yanayotokana na alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu kwa kuanzia umeanza kwanza na kuhakikisha kwamba upatikanaji wa mbegu bora za alizeti unakuwa na utoshelevu. Tumeshapata sasa aina nne za alizeti *variety* mpya ambayo tija *(productivity)* yake ni kubwa kuliko mbegu hizi ambazo au *variety* hizi ambazo tumekuwa tunatumia hapa nchini kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ni kweli kwamba kwa miaka ya nyuma mbegu ya alizeti ilikuwa haitoshi, mbegu yenye ubora lakini sasa mbegu inayoweza kutoa mafuta megi zaidi na katika kiwango kidogo imeshapatikana, ni *variety* hizo nne na zitaanza kusambazwa kwa wakulima hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Kilwa ni suala la Ilani ya Uchanguzi wa Chama cha Mapinduzi lakini pia ni ukombozi mkubwa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara na mapinduzi kwa kilimo chetu. Mwaka jana Serikali ilitoa ahadi kwamba mchakato unaendelea vizuri, nataka kujua mchakato huo umefikia wapi kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchakato umefika wapi wa Kiwanda cha Mbolea Lindi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati najibu swali la msingi kama Mheshimiwa Nape hakunisikiliza vizuri; ni kwamba nilisema tayari kuna wawekezaji ambao wameshaonesha nia wa Makampuni ya *HELM* na *FERROSTAAL* wa Ujerumani, kwa hiyo mchakato unaendelea katika mazingira hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi na mwisho Mheshimiwa Kasuku Bilago.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kilichokuwa Kiwanda cha Mbolea cha Tanga kimebinafsishwa na sasa zinaendelea shughuli nyingine pale ambazo hazihusiani na mbolea. Kwa mahitaji haya ambapo bado mbolea inahitajika nchini, je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa wa kukirejesha kiwanda kile ili kiweze kuzalisha mbolea?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru kwa jinsi ambavyo anafuatilia shughuli zetu za viwanda na kulifanya swali letu kuwa makini katika eneo husika. Niseme tu kwamba ni kweli eneo hilo ambalo lilikuwa Kiwanda cha Mbolea Tanga kimebadilishwa na sasa kinashughulika na shughuli za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba lengo la kubinafsisha ilikuwa si tu kwamba lazima kuendeleza kiwanda kile kilichopo hata kama mashine zilizopo zilikuwa hazifai. Kimsingi mashine zile zilikuwa zimezeeka sana na mwekezaji alitoa mapendekezo akaandika umuhimu wa kuwekeza katika mafuta kwa misingi ya kupokea mafuta, kuhifadhi na kusambaza na sasa hivi ana uwezo wa kusambaza mafuta kufikia lita za ujazo milioni 126.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli imekuwa ni mkombozi kwa wananchi na wafanyabiashara wote wa maeneo ya Tanga, Arusha na maeneo ya Kaskazini hata Kigoma. Kwa hiyo, binafsi nampongeza kwa uwekezaji huo kwa sababu lengo letu sisi ni kuongeza tija katika shughuli zote za kiuwekezaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Mtemi. Wilaya ya Kakonko mwaka jana ilipata shida

kubwa ya mbolea mpaka nikadiriki kumpigia Waziri wa Kilimo juu ya ukosefu wa mbolea katika Wilaya ya Kakonko. Tatizo hili lilitokana na wale *suppliers* ambao hawakuwa na uwezo kabisa wa kununua mbolea na kuiuza kwa bei elekezi kwa sababu ilikuwa inatoka mbali. Nataka Waziri, tena bila kumumunya maneno, anihakikishie kama wananchi wa Kakonko watapata mbolea mwaka huu bila usumbufu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa niaba ya Waziri Wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba tu nimhakikishie rafiki yangu Mheshimiwa Kasuku Bilago kwamba mfumo huu ambao tunataka kuwasiminisha Wabunge wote utampa huo uhakika anaoutaka. Naomba nimhakikishie kwamba mbolea itapatikana kwa wakati wote nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, kipindi chetu cha maswali ndiyo kimefikia tamati. Nina matangazo, nianze na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Katika Jukwaa la Spika tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni Mheshimiwa Sarah Cooke, Balozi wa Uingereza hapa nchini. Karibu sana Balozi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Cooke ameambatana na Mheshimiwa Matt Sutherland, Naibu Balozi wa Uingereza hapa nchini na Ndugu Andy Stephens, Mshauri wa Masuala ya Sheria Ubalozini na Ndugu Sean Hilhorst**,** Mshauri wa Masuala ya Rushwa. Karibuni sana Balozi na timu yako. *(Makofi)*

Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Sheria na Katiba ambao ni Profesa Sifuni Mchome - Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; Ndugu Amon Mpanju - Naibu Katibu Mkuu; Mheshimiwa Jaji Profesa Ibrahim Juma - Jaji Mkuu wa Tanzania,

sijamwona hapa; Mheshimiwa Jaji Ferdnand Wambali - Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu, karibu sana Mheshimiwa Jaji Kiongozi; tunaye pia Mtendaji Mkuu wa Mahakama Kuu - Ndugu Hussein Kattanga, karibu sana; Mheshimiwa Jaji Mwanaisha Kwariko - Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu, Kanda ya Dodoma, karibu sana Mheshimiwa Jaji na tunaye Msajili wa Mahakama Kuu, Ndugu Katarina Revokati, karibuni sana. Pia wapo viongozi na Watendaji Wakuu kutoka Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 26 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana.

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kutoka Chama cha Wanasheria Tanganyika wakiongozwa na Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika, Wakili Fatma Karume. Karibuni sana, hongera sana, hayupo yeye, simuoni hapo, hongereni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki ambao ni jamaa zake kutoka Zanzibar. Ndiyo Muungano huo. *(Makofi)*

Tuna wageni 29 wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma, wageni wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni wachezaji na viongozi wa timu ya mpira wa miguu ya wanawake *(Baobab Queens)* inayocheza Ligi Kuu ya Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wa timu hiyo Ndugu Innocensia Massawe. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tuna wageni 24 wa Mheshimiwa Richard Ndassa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Wilaya ya Kwimba, Mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Joel Makanyaga ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao wanafunzi 25 na Walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Shamsie iliyopo Dar es Salaam. Karibuni sana.

Tunao Wachungaji 150 kutoka Jumuiya Kuu ya Wabaptisti wa Tanzania kutoka mikoa mbalimbali nchini waliokuja Dodoma kwa ajili ya mkutano wa kitaifa. Wako wapi wageni wetu hawa, naona wako eneo lingine.

Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, kwa niaba ya Jumuiya ya St. Thomas Moore hapa Bungeni, wanatoa tangazo kwamba leo tarehe 18 Aprili, 2018 kutakuwa na ibada ya misa kwa Wakristo wa madhehebu ya Kikatoliki mara baada ya kuahirishwa Bunge saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wengine wote wanaopenda kushiriki ibada hiyo mnakaribishwa kwenye ibada hiyo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyoletewa hapa.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Nitaanzia huku, Mheshimiwa Mlinga, nichukue majina tu kwanza, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Haonga, wewe kila siku kwa nini, Mheshimiwa Julius Kalanga, nianze na Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 47 na naomba niisome kwa faida ya Bunge letu au kwa kuokoa muda siisomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwongozo wangu ni huu ufuatao. Nimeangalia katika taarifa ya habari ya *TBC* ikimwonesha Waziri Mpina akikagua Kiwanda cha Kuchinja Punda. Kiwanda hicho kwa siku kinachinja punda 30 - 60 na kiwanda hiki mwaka jana tulikizungumza hapa Bungeni kikiambiwa kinachinja punda lakini punda wale wanahifadhiwa hadi wakati mwingine wanakuwa wameoza. Wachina wanatumia sana ile methali ya Kimakonde inayosema, *chiumbele Mungu chonkumemeno*, kwamba kila kinachoumbwa na Mungu ni halali kuliwa. Nataka kujua, je, Serikali sasa imeruhusu punda wachinjwe na watumike kama kitoweo kwa matumizi ya binadamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo tukumbuke kwamba punda katika Mikoa ya Simanjiro, Kilimanjaro, Tanga na Arusha wanatumika kama wanyamakazi ama vitendea kazi kwa kulima, kubeba mizigo na hata kwenda kuchukulia maji. Je, hawa punda Wachina watakapowamaliza hawataingilia pundamilia kwenye hifadhi zetu za wanyama? Kubwa zaidi nataka kujua, kama Serikali imeruhusu kutumika kwa nyama ya punda kwa nini isitoe tamko humu Bungeni na wananchi wa Tanga na mikoa mingine tukaanza kutumia punda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wangu ndio huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mwongozo wako. Kuna jambo la hatari ambalo...

**MWENYEKITI:** Kanuni gani?

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Kanuni ya 68(7). Naomba mwongozo wako ikikupendeza jambo hili basi kwa sababu Serikali inasikia wakazi wa Mkoa wa Katavi tuweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna takribani siku 10 barabara ya kutoka Mpanda kuelekea Tabora imefungwa na wakazi wa Mkoa wa Katavi wanasafiri kwa kuzunguka kutoka Mpanda kuelekea Sumbawanga ili wafike Tabora na wengine wamekuwa wakizunguka kutoka Mpanda kwenda Mkoa wa Kigoma ili wafike Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufungwa kwa barabara hii imeleta usumbufu mkubwa kwa wakazi wa Mkoa wa Katavi kwani wamekuwa wakisafiri zaidi ya saa 14. Jana hakuna gari ambayo imeingia kutoka Kigoma kuja Mpanda, kwa hiyo, abiria wamelala njiani kwa saa 14. Kutokana na wakazi wa Mkoa wa Katavi kupata shida ya kusafiri saa nyingi pia gharama ya kuzunguka tofauti na kwamba wangeweza kusafiri kutoka Mpanda kwenda mpaka Tabora, wanatumia saa sita...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba jambo hili ...

**MWENYEKITI:** Ahsante, umeeleweka.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba mwongozo mara kadhaa na hatuna mashaka na watu wetu wa Usalama, lakini naomba mwongozo wako; watu wa Usalama wana vifaa ambavyo vinaweza vika-*sense* kuanzia kifuani mpaka miguu tunaambiwa tuvue viatu. Wakati huu mvua zimenyesha, ukipita pale kuna uchafu mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kama Bunge hili mmekubali tupate magojwa ambayo yanaweza yakapatikana kizembe tu. Kwa sababu kama kile kifaa kinaweza ku-*sense* kuanzia kichwani mpaka kifuani kwa nini kwenye miguu tunavua viatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, tuchukulie uzito jambo hili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kalanga Laizer.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa takribani sasa wiki nzima kumekuwa na tatizo la mafuriko katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ikiwepo Dar es Salaam na watu wemeendelea kufa, mawasiliano yamekatika, nyumba za watu zimejaa maji na hata katika Jimbo letu la Monduli kwa jana Mji wetu wa Mto wa Mbu umefurika na mwananchi mmoja katika eneo la Serela amefariki na mashamba ya wananchi yamezolewa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali jana ilisema inashughulikia jambo hili linahusu maisha ya wananchi wetu na akinamama wengi wanashindwa hata

kwenda hospitalini na watoto wengi wanashindwa kupata huduma lakini tumeendelea kupata majibu ya kirahisi kwamba Serikali itachukua hatua, lakini hakuna bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona jambo hili linahusu maisha ya wananchi wetu, linahusu afya ya Watanzania, linahusu makazi ya watu wetu, ni kwa nini Bunge lisijadili jambo hili kama jambo la dharura linaloathiri maisha ya watu wetu ili Serikali iji-*commit* na tupate namna ya dharura ya kusaidia wananchi ambao mvua hizi zinaendelea kunyesha na hatujui zinakatika lini. Hali ni tete, hakuna mawasiliano, hakuna namna ambavyo wananchi wetu wanaweza wakasaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ikikupendeza jambo hili lijadiliwe na Bunge na litoe maelekezo kwa Serikali ili lifike mwisho na wananchi wetu wasaidike. Naomba nitoe hoja ili Bunge lijadili jambo hili kama jambo la dharura. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama kumuunga mkono)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kaeni tu Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo lililotokea leo mapema hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kipindi cha maswali na majibu kinaendelea, swali namba 103 lililolenga Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji linalohusu kiwanda cha mbolea, nimejaribu kufuatilia majibu ya Serikali hata kupitia karatasi ambayo wamejibu kwenye ile aya ya pili kwamba pamoja na upatikanaji wa soko la mbolea Mkoani Njombe tafiti za kijiolojia zinaonesha kuwa malighafi za *phosphate, phosphorous* na gesi asilia hazipatikani mkoani humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako na najua kabisa kwamba lengo la Bunge pia ni kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali, leo Serikali hii ya Awamu ya Tano ina sera ya viwanda lakini ukiangalia kwenye uhalisia Serikali inaenda kinyume na sera yake. Tunanunua ndege ambazo ukiangalia siyo kipaumbele namba moja katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa mwongozo wako kwamba badala ya Serikali kununua ndege kwa nini sasa hizi fedha tusibadilishe tukajenge viwanda ili tuweze kusaidia wakulima wetu na ili tuweze kuendana na sera ya Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa hiyo, badala ya kununua ndege mimi nashauri tu kwamba tujenge viwanda vya mbolea tuweze kusaidia Watanzania wengi waliojiajiri kwenye kilimo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7), sitaisoma kwa sababu ya masuala ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati Mheshimiwa Spika anajibu na anatuhakikishia Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na masuala ya usalama wa Wabunge ndani ya Bunge pamoja na nje ya Bunge, tukikumbuka pia na tukio la Mheshimiwa Selasini alivyokuwa amelalamika kuhusu usalama wake kwamba kuna mwananchi mwenzetu Mtanzania anaitwa Musiba amekuwa akimfuatilia kila mara na mpaka leo hii ameonekana viwanja vya Bunge kiasi ambacho kinamfanya Mheshimiwa Selasini afikiri kwamba amekuja kuviziwa ili auawe kama ambavyo amesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyu huyu Musiba ameendelea kuongea kwenye vyombo vya habari akimchonganisha Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake akisema kwamba ana majina ya Watanzania viongozi wakubwa 1,800 ambao wamekuwa wakimfuatilia na kumpa

taarifa mbalimbali dada mmoja wa Taifa anaitwa Mange Kimambi. Viongozi wakubwa wa nchi hii tunaowafahamu ni watatu. Kwa hiyo, kama siyo Mheshimiwa Rais mwenyewe ataanza kuwafikiria Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu na Mawaziri kwamba wanampa taarifa mbalimbali Mange zinazofanya Serikali ipate uzito kwenye kuendesha mambo yake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kutokana na hili suala la usalama linaloendelea na tunajua kwamba hata Wabunge wengi wa Chama cha Mapinduzi hawako salama akiwemo Mheshimiwa Bashe na Mheshimwa Nape na wameshawahi kulalamika ndani ya Bunge hili na Musiba amekuwa akiendelea kuonekana ndani ya viwanja vya Bunge. Nataka mwongozo wako na utoe Kauli ya Serikali, kinachomleta humu ndani ni nini kama siyo kufuatilia usalama wa Wabunge hawa aliokuwa akiwataja kila mara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nami nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba kutokana na hali ya mvua inayoendelea huko kwenye mikoa yetu na kusababisha mafuriko makubwa na sehemu nyingi watoto wa shule hawaendi kwenye masomo yao kama kawaida kutokana na barabara kufurika maji. Tumeshuhudia hata mikoa mingine kama Dar es Salaam Walimu wameambiwa watoe likizo ya muda kwa sababu ya mafuriko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa nini Wizara ya Elimu isirudishe ule utaratibu wa zamani wa mihula mitatu yaani mwezi wa kwanza mpaka wa tatu, mwezi wa nne likizo kwa sababu huu mwezi wa nne ndiyo

mwezi wenye mafuriko mengi kwamba tuondoke kwenye mihula miwili turudi kwenye mihula mitatu ili kupisha haya mafuriko yanayotokea mwezi wa Nne na mwezi wa Desemba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) kutokana na swali la 100 na 101 la Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea suala la elimu msingi wake ni elimu ya msingi. Tunapoongelea elimu ya sekondari, elimu ya vyuo vikuu, msingi wake ni elimu ya msingi. Tunapoongelea elimu ya msingi, uti wa mgongo wa elimu ya msingi ni elimu ya darasa la nne na ndiyo maana tumeweka mitihani katika elimu ya darasa la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi ninavyoongea darasa la nne hawana mitaala wala hawana vitabu kwa maana hiyo hawasomi na Walimu wamekuwa wakiwafundisha kwa kupiga ramli kuwa hivi vitu vinaweza vikatoka. Kwa sababu wanafanya mtihani mwezi wa 11 lakini mpaka sasa hivi imebaki muda mfupi lakini hawana mitaala wala vitabu. Cha kusikitisha zaidi Waziri namwona humu ndani hatikisiki na Naibu Waziri hatikisiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako kwa kutumia mamlaka yako, kwa kuwa Bunge kazi yake ni kuisimamia Serikali na siyo kuiangalia Serikali, naomba kwa kutumia mamlaka yako chini ya Kanuni ya tano (5) nikuombe utoe maagizo Waziri wa Elimu na Naibu wake wasiingie humu ndani mpaka waje na majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba mwongozo wako. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru. Nimeona wakati Mheshimiwa Kalanga anaomba kutoa hoja ili Bunge lijadili jambo la dharura usingependa niende na njia hiyo, lakini hoja yangu iko hivi. Bunge hili ndiyo chombo cha wananchi ambacho kinapaswa kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa siku tatu au nne mfululizo kumekuwa na usumbufu mkubwa sana kwa Watanzania wanyonge wanaoishi Tarime. Mtu ana ng'ombe wake anataka kwenda kuuza mnadani huko anakokaa, mimi kuna vijiji kwa mfano Gibaso barabara haziendi kabisa kule yaani hakuna barabara, Nyanungu, Gibaso; mtu anataka kwenda kuuza ng'ombe mnada wa Mtana anakamatwa anaambiwa lazima ng'ombe wake apakie kwenye gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anauguliwa, ana mke yuko hospitali, amepeleka ng'ombe wake mnadani amekosa mtu wa kumuuzia kutokana na hali ya uchumi, anarudisha ng'ombe kijijini anaambiwa lazima awe amempakia kwenye gari. Hiyo hela ndiyo aliikosa akapeleka ng'ombe wake mnadani arudi aokoe maisha ya mtoto wake au mke wake au apeleke mtoto wake shuleni na barabara hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hao wametumwa kutoka Wizara a Mifugo na wananyanyasa watu, hawataki kuangalia hali halisi ya mazingira ili wa-*reason.* Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi ningeomba hili Bunge limwelekeze Waziri wa-*reason* au ndiyo kushughulikia wanyonge ambako Rais Magufuli alikosema ndiyo huku kweli? Watu maskini wanaonewa, wanaumizwa, wananyang'anywa pesa zao kwa nguvu na wanapigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba utoe mwongozo ili Serikali itoe kauli kusitisha hali hii inayoendelea ya kunyanyasa watu kule kijijini ili waweze kufanya kazi zao, tafadhali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosikia ninyi wenyewe, nimeombwa miongozo tisa hivi na mingine wanaomba tujadili suala la dharura. Mimi nitajikita zaidi kwenye Kanuni 68(7) maana sitachoka kuyasema haya. Hii ni nyumba ya Watanzania wote na inaongozwa na kanuni, sheria za nchi na sisi kama watunga sheria na wawekaji wa kanuni hizi lazima tuwe watu wa kwanza kuzifahamu lakini pia na matumizi yake.

Waheshimiwa Wabunge, lakini yapo mengine nadhani, nikichukua kama la Mheshimiwa Mlinga ameliweka kimatani matani haliangukii kwenye Kanuni ya 68, lakini nadhani Serikali muone namna gani mnavyoweza mkalitolea maelezo. Naamini mmemwelewa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Musukuma pia, hizi mvua wataalam wa masuala ya hewa na kwa vifaa hivi watakwambia na ninyi Wabunge angalieni tu mzunguko huu mtauona, kumbukeni mvua kubwa tena ilikuja lini hapa Tanzania. Mkishaelewa vipindi hivyo, wataalam hawa wanajua na ndiyo maana safari hii wataalam hawa walianza kulisema mapema sana. Wanapotoa taarifa ndiyo tujue tunajiandaa vipi katika kukabiliana na hayo yanayokuja.

Mheshimiwa Musukuma yeye ameomba mwongozo wangu kama Serikali inaweza ikaangalia uwezekano wa kurudi kwenye mihula tuliyokuwa nayo siku za nyuma. Hilo naiachia Serikali, mtaona wenyewe kama lina-*make sense.*

Mheshimiwa Kunchela, poleni sana wananchi wa Katavi, Tabora lakini siyo huko tu, hii mvua ni nchi nzima. Juzi Serikali ilisema maeneo ambapo barabara zimekatika na hakuna mawasiliano *TANROADS* kwa kushirikiana na *TARURA* wanajaribu kufanya kila lililo ndani yao kurejesha *passability* lakini siyo eneo moja. Sasa tukianza kuongelea dharura ya eneo moja kwa sababu gharama zimepanda kwa watu wanaosafiri kutoka Katavi, treni haziendi lakini tuone hali hii, ukiona Dar es Salaam kama tulivyosikia jana, mimi naongelea Tanzania nzima hata kule kwangu ni shida. Kwa hiyo, tukisema tuzungumze dharura Serikali tutaishauri ifanye kitu

gani? Ni haya ambayo tunasema maeneo ambayo tunaweza kuyakabili kwa mara moja Serikali inajitahidi kufanya kadri inavyoweza.

Kwa hiyo, mwongozo wangu kwa hilo, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu sana haya matukio ya mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi ya nchi yetu ni nini kifanyike kuweza kunusuru hali ya maisha ya watu wetu na mali zao lakini pia na usafiri wao. Watapima, kama barabara hazipitiki, je, reli upande huu inapitika? Wanaweza wakaona wafanye njia hiyo, lakini mimi hapa siwezi kutoa mwongozo lakini Serikali imesikia hayo ambayo yanahusiana na hali ya mvua hizi.

Waheshimiwa Wabunge, nije kwa Mheshimiwa Heche. Unafahamu ninyi kama Wabunge mna nafasi nzuri ya kuweza kuyasema hayo uliyoyasema ambayo yanawasibu wananchi wa Jimbo na Wilaya yako. Sihitaji kuwafundisha lakini ungeweza ukatumia nafasi hiyo vizuri siyo kuja kuomba mwongozo ambalo ni tukio ambalo halijatokea mapema hapa Bungeni tuone kama linaruhusiwa na Kanuni hizi au la.

Kanuni zinatoa mwanya, nenda ukakae uzisome vizuri, unaweza ukatumia nafasi hiyo ukaomba ukawa *slotted* ukalisema vizuri tu na Serikali ikakusikia inaweza ikakujibu pale pale au ikasema itakuja kukujibu siku nyingine. Kwa kufanya hivyo, utakuwa umepata *facts* za kutosha kuliko hii ya kusimama tu mara moja na kusema inaingia kwenye mwongozo.

Sasa mwongozo wangu ni huo, ukazisome vizuri Kanuni, ukitaka kuniona nje huko mimi naweza nika-*whisper* kwako namna ya kuweza kufanya kama una suala kama hilo.

Mheshimiwa Mwambe, umemtaja mtu mimi simfahamu na mimi sijamuona humu hata kwenye maeneo haya ya Bunge.

**WABUNGE FULANI:** Yupo.

**MWENYEKITI:** Mimi ningependa tu-*stick* kwenye Kanuni zetu za Bunge, je, ni tukio ambalo limetokea leo hapa, linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni zetu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mimi nisingependa tufike huko. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba nataka turejee ndani ya reli ya Kanuni zetu. Kama suala halikutokea mapema siku hiyo hapa hamna.

Mheshimiwa Aida Khenan, nimekuelewa. Hili suala alilitolea mwongozo Mheshimiwa Spika. Tunasubiri hayo maelekezo yatakayotoka kwa Spika. *Point* ya Mheshimiwa Aida ni kwamba kwa hali ya mvua hizi na *carpet* zetu tunapopita hapo na viatu tope zile, hujui umetokea wapi, unapovuliwa pale uko salama au vipi, ndiyo hoja yake hiyo. Mimi nalirejesha kwa maana ya kwamba uharaka wa maamuzi yale tuliyoomba lakini nimemwelewa. Huo ndiyo mwongozo wangu, vuta subira kidogo. *(Makofi)*

Narudia, Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Kalanga, hayo yamengukia katika yale niliyosema ya kidharura dharura ukiondoa la Musukuma ambalo nimesema nataka liangaliwe na upande wa Serikali.

Mheshimiwa Haonga, narudia maamuzi ya nyuma ya Kiti. Swali lililoulizwa limeulizwa na Mheshimiwa Lucy Mlowe. Aliyeuliza swali la msingi Serikali imejibu na Mheshimiwa muuliza swali la msingi akapewa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza, Serikali imemjibu vizuri tu, wewe pilipili usiyoila yakuwashia nini? *(Makofi)*

Uamuzi ni huo, wewe usidandie kwa swali la nyongeza la mwenzako ambaye ameridhika. Wewe kama unataka uliza sasa swali lako hilo. Huo ndiyo mwongozo wangu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa maeneo hayo tisa, huo ndiyo mwongozo wangu lakini ningependa kama Serikali

inaweza ikatoa majibu kwa upande wa eneo la elimu mtaona jinsi ambavyo mmejipanga kama mnaweza kusema sasa hivi, Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Napenda kujibu miongozo au masuala mawili ambayo yameibuliwa na Mheshimiwa Mlingwa na Mheshimiwa Musukuma. Mheshimiwa Mlingwa yeye...

**MWENYEKITI:** Mlinga.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mlinga, samahani. Yeye amehoji kwamba kwa nini mimi na Mheshimiwa Waziri hatutingishiki, sijui alikuwa na maana gani, lakini niseme tu kwamba madai yake kwamba wanafunzi au shule zetu hazina mitaala, kwa sasa hakuna mtaala wowote uliokosekana. Hata hivyo, Wizara inaendelea na taratibu za kuhaulisha na kuboresha mitaala iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu vitabu kwa sababu vilevile amezungumzia kuhusu suala la kukosekana vitabu. Vitabu ambavyo vilikuwa vimechelewa kwenda kwenye shule zetu ni vitabu vya darasa la nne. Naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba vile vitabu vya darasa la nne ambavyo vilichelewa kwa sasa vimeanza kugawiwa shuleni. Tunaamini ndani ya wiki nne vitakuwa vimesambaa nchi nzima. Tayari tumeshagawa katika Mkoa wa Pwani, Dar es Salaam na bado utaratibu wa kugawa unaendelea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Musukuma yeye alitaka tubadilishe utaratibu wa sasa wa kuwa na mihula miwili kuwa mitatu ili kukabiliana na hali inayoendelea ya mvua nyingi na mafuriko. Wazo lake sio kwamba halina msingi, lakini katika mazingira ya mabadiliko ya tabianchi ambayo moja kati ya sifa za mabadiliko ya tabianchi ni kwamba hali ya hewa haitabiriki, mvua haitabiriki, itakuwa

ni vigumu sana kubadilisha mihula yetu au muundo wetu wa namna tunavyoendesha elimu kwa sababu tu ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, hatuna uhakika mvua zinazonyesha kwa wingi mwezi wa nne mwakani zitanyesha hivyo. Kwa hiyo, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee tu na taratibu za kawaida za kukabiliana na majanga, lakini mfumo wetu wa mihula uendelee kama ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa, majibu ya miongozo ndiyo hayo. Katibu.

## NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Kauli ya Serikali kuhusu Kuibuka kwa Ugonjwa mpya kwenye zao la Korosho

**MWENYEKITI:** Kauli za Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu kuibuka kwa ugonjwa mpya kwenye zao la korosho, leo tarehe 18 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kanuni ya 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu tatizo la kuwepo kwa ugonjwa wa mnyauko fusari kwenye zao la korosho katika Mikoa ya Pwani, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho ni miongoni mwa mazao muhimu ya biashara yanayowanufaisha wakulima na kuchangia katika uchumi wa Taifa. Katika msimu wa mwaka 2017/2018 zao hili limeliingizia Taifa mapato

ya kiasi cha Sh.1,189,412,498,433. Zao la korosho linalimwa kwa wingi katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga. Mikoa mingine inayolima zao hili ni Morogoro, Iringa, Mbeya, Singida na Dodoma. Inakadiriwa kwamba zaidi ya kaya 500,000 zinajihusisha na kilimo cha korosho na kila kaya ina wastani wa hekta mbili za shamba la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia inakadiriwa kwamba Tanzania kuna mikorosho ipatayo milioni 50 yenye uwezo wa kutoa wastani wa kilo tano kwa mti. Uwezo huu wa uzalishaji ni mdogo ukilinganisha na miti ya mikorosho yenye matunzo bora ambayo inaweza kutoa wastani wa kilo 15 hadi 20 kwa mti mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa uzalishaji wa korosho umeonesha kuwa kuna kupanda na kushuka kwa uzalishaji kutoka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, msimu wa 2014/2015 uzalishaji ulikuwa tani 197,932.501 na msimu wa 2015/2016 tani 154,335, msimu wa 2016/2017 tani 265,237 na msimu wa 2017/2018 tani 313,053.7

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuibuka kwa ugonjwa. Pamoja na mafanikio haya, Wizara imepokea taarifa kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele kuhusu kuwepo kwa ugonjwa huo kwenye mikoa niliyoitaja. Taasisi ya Utafiti hii kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamefanya utafiti wa awali na kubaini kuwa ugonjwa huo wa mnyauko fusari unasababishwa na vimelea aina ya ukungu *(fungus)* viitwavyo *Fusarium oxysporum* ambavyo husababisha mti wa mkorosho kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ugonjwa huo husambaa kwenye udongo *(soil born disease)* na pia unaweza kusambazwa kwa njia ya vitendea kazi, vipando vya mikorosho vilivyoathirika na kuni za mikorosho zilizoambukizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili za huu ugonjwa. Dalili ya kwanza ni majani kuwa rangi ya njano na hatimaye

kahawia. Dalili ya pili ni uozo wa kikahawia kwenye kiini cha mti hatimaye mti kukauka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za ugonjwa huu. Athari ya kwanza ni kupungua kwa idadi ya mikorosho na hatimaye uzalishaji. Athari ya pili, ni mikorosho kufa. Athari ya tatu ni kupungua kwa pato la mkulima na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyoathirika na huu ugonjwa. Baadhi ya maeneo ambayo ugonjwa umeonekana ni pamoja na Magawa katika Wilaya ya Mkuranga, Nanganga katika Wilaya ya Masasi, Nakayaka na Mweru katika Wilaya ya Tandahimba, Mtawanya katika Wilaya ya Mtwara na Legezamwendo katika Wilaya ya Liwale, kama ilivyooneshwa kwenye jedwali. Kuna jedwali linaloonesha namna ugonjwa ulivyotawanyika katika wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa na serikali. Taasisi ya Utafiti Naliendele kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imeanza kufanya utafiti ambao unalenga kubaini viuatilifu na mbegu zenye ukinzani dhidi ya ugonjwa huo. Tafiti zimeanzishwa katika baadhi ya maeneo ambayo ugonjwa umeonekana kama nilivyoyataja. Tunachoomba ni kutoa taarifa kwa wadau uwepo wa ugonjwa huu katika Wilaya za Mikoa ya Pwani, Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kuendelea na utafiti ili kubaini viuatilifu;

(ii) Kufanya tafiti za kiikolojia;

(iii) Kufanya tafiti za kibaiolojia;

(iv) Kuendelea na utafiti wa kupata mbegu zenye ukinzani;

(v) Kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhusu utafiti wa namna ya kudhibiti ugonjwa huo;

(vi) Kuzishirikisha Taasisi au Maabara za Kimataifa *(CAB International, NRI)* na mashirika mengine;

(vii) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau jinsi ya kudhibiti ugonjwa huo; na

(viii) Kuendelea kutafuta taarifa za kuwepo kwa ugonjwa katika maeneo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kuzingatiwa na wakulima ili ugonjwa usienee. Baada ya kuona dalili kama nilivyoeleza hapo juu, tunawaomba wakulima kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kukata miti iliyoathirika kwa ugonjwa huo na kuichoma moto.

(ii) Kabla hawajakata au kupogolea matawi *(prooning)* ya mikorosho isiyoathirika na ugonjwa huo wahakikishe vitendea kazi walivyotumia katika mikorosho iliyoathirika vimebabuliwa na moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la pili ni muhimu sana kwa sababu panga lile litakalotumika kukata mti ulioathirika hata ukitokanalo huko Mtwara ukaendanalo Singida ukilitumia kukata mkorosho mwingine utakuwa umeuambukiza huo mkorosho wa Singida ugonjwa. Kwa hivyo, kama panga huwezi kulitupa basi ni bora ulibabue kwenye moto ili kuua hivyo vimelea visiende kuambukiza maeneo mengine.

(iii) Mabaki ya mikorosho iliyoathirika yasitumike kama kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; baada ya kusema hayo, napenda kusema kuwa, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuhakikisha kuwa uzalishaji na tija ya zao la korosho

unaimarishwa ikiwa ni pamoja na mazao mengine ya kimkakati. Aidha, tutaendelea kuchukua hatua stahiki za kuimarisha usimamizi wa uzalishaji wa mazao hayo ili yaweze kutoa mchango mkubwa katika kulipatia Taifa pato la kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inapenda kusisitiza kuwa wakulima wachukue tahadhari kuhusu ugonjwa huo kwa kuhakikisha kuwa wanazingatia ushauri tulioutoa na namna ya kudhibiti ugonjwa huu usisambae. Aidha, tutaendelea kusimamia utafiti unaondelea ili kupata ufumbuzi wa ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nikushukuru wewe mwenyewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Katiba na Sheria**

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa wingi wa rehema zake na kwa kuniruzuku uhai na kunipa afya njema iliyoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kipekee kabisa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini katika kuitumikia Serikali ya Awamu ya Tano katika nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi nitaendelea kuitumikia nafasi hiyo kwa uadilifu, uaminifu, unyenyekevu na namwomba Mwenyezi Mungu anijalie hekima na busara niweze kutimiza wajibu wangu kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majonzi makubwa nikupe pole wewe, Bunge lako Tukufu, familia na wananchi wote wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini kupitia Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu, napenda kumpongeza Spika kwa uongozi wake mahiri wa kuliongoza na kulisimamia Bunge letu Tukufu katika jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali. Nawapongeza pia Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu na kwa kuzingatia katiba, sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nimshukuru Spika kwa uamuzi wake wa kuunda Kamati Teule za Bunge za kushughulikia masuala ya uchimbaji na biashara ya madini ya *Tanzanite* na Almasi zilizokuwa chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Doto Biteko, Mbunge wa Bukombe na Naibu Waziri wa Madini sasa na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imeweka msingi na mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, naomba niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa kuchaguliwa tena kuziongoza Kamati hizo katika kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2018/2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wabunge wenzangu waliochaguliwa hivi karibuni kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha, Mheshimiwa Justine Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini na Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa, Mbunge wa Longido. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Adelardus Lubango Kilangi, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Dkt.

Evaristo Emmanuel Longopa kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Dkt. Julius Clement Mashamba kwa kuteuliwa na Rais kuwa Wakili Mkuu wa Serikali *(Solicitor General);* Bwana Edson Athanas Makallo kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka *(Deputy Director of Public Prosecution);* na Dkt. Ally Possi kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali *(Deputy Solicitor General)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani na matumaini yangu kwamba uzoefu, weledi na umahiri wao katika masuala ya sheria utasaidia sana katika kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya sheria na Taifa kwa ujumla. Vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Majaji 12 walioteuliwa na Rais hivi karibuni kuwa Majaji wa Mahakama Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, niwashukuru Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Bwana Gerson John Mdemu na Bwana Paul John Ngwembe kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wakitumikia nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Niwatakie wao na wengine walioteuliwa na Rais kuwa Majaji wa Mahakama Kuu kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya katika Mhimili wa Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu dira na dhima ya Wizara hii yapo ukurasa wa saba (7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo na majukumu ya Wizara. Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha:-

Mahakama ya Tanzania; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Tume ya Utumishi wa Mahakama; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini; Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania; na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni taasisi mpya za Wizara zilizoanzishwa kufuatia marekebisho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13 Februari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo halali vya maamuzi. Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu kwa Mawaziri, kupitia Tangazo la Serikali Na.144A la tarehe 22 Aprili, 2016. Majukumu hayo yameainishwa katika hotuba ya bajeti ukurasa wa nane (8) na wa tisa (9).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya mpango na bajeti kwa mwaka wa 2017/2018. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu ilipanga na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo mahsusi ya vipaumbele kama msingi wa kutekeleza dhima ya Wizara na Taasisi zake. Baadhi ya maeneo ya vipaumbele yalikuwa yafuatayo:-

(i) Kukamilisha uhamishaji wa Makao Makuu ya Wizara kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma;

(ii) Kuratibu masuala ya kisera katika Wizara na Taasisi;

(iii) Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini;

(iv) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya Katiba na Sheria;

(v) Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba;

(vi) Kuharakisha usikilizaji wa mashauri;

(vii) Kukuza na kutetea haki za binadamu hususan haki za makundi yenye mahitaji maalum;

(viii) Kuboresha utoaji huduma za Mahakama kwa kuongeza idadi ya watumishi wa Mahakama wenye weledi na sifa stahiki;

(ix) Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu;

(x) Kuendesha programu za mafunzo kwa wasaidizi wa sheria;

(xi) Kuimarisha na kuendelea kutoa mafunzo endelevu ya kimahakama pamoja na mafunzo kazini kwa watumishi wa mahakama na wengine wa sekta ya sheria kwa ujumla;

(xii) Kukamilisha utafiti kuhusu mfumo wa sheria za usimamizi wa haki jinai; na

(xiii) Kujenga na kukarabati miundombinu ya Wizara na taasisi zake katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi kuhusu vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 umetolewa katika Kiambatisho A cha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, Wizara iliandaa na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu mpango na makadirio ya bajeti ambayo yalipitishwa kwa ajili ya utekelezaji. Hivyo, kwa ridhaa yako naomba sasa niwasilishe mbele ya Bunge hili taarifa kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, mafanikio yaliyopatikana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamishia Makao Makuu ya Wizara Dodoma. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria, kupitia Fungu 41, imetekeleza

kikamilifu azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhamishia shughuli za Serikali Mjini Dodoma. Aidha, Mahakama ya Tanzania imeanza kutekeleza mpango wa kuhamia Dodoma ikiwa tayari imepata eneo lenye ukubwa wa takriban hekta 19 kwa ajili ya kuanza kujenga makao yake makuu katika mwaka huu wa fedha 2017/2018. Nipende tu kusisitiza kuwa, zoezi la kuhamia Mkoani Dodoma ni endelevu na linaendelea kuratibiwa vyema na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera na masuala ya sheria. Katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara iliendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu ya Sera ya Taifa ya Sheria. Maandalizi ya sera hiyo yamechukua muda mrefu kutokana na ukweli kuwa masuala ya sheria ni mtambuka na wadau wake ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu bado inaendelea kuratibu upatikanaji wa maoni ya wadau na kuyachambua kwa minajili ya kuboresha rasimu hiyo ili kuwa na Sera inayokidhi mahitaji halisi ya sekta ya sheria na kuakisi mahitaji ya jamii kwa ujumla. Ni matarajio ya Wizara yangu kuwa ifikapo mwezi Septemba, 2018 tutakuwa na sera kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya msingi ya Wizara ni kusimamia mfumo wa sheria nchini ikiwemo kutathmini hali ya utekelezaji wa sheria zilizopo na kutoa ushauri juu ya sheria mpya zinazotungwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, imeendelea kufanya tathmini ya hali ya utekelezaji wa sheria nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinawezesha kutekelezwa kwa mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kufanikisha azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, sheria zinazohusu masuala ya jinai, ardhi na mazingira ziliendelea kufanyiwa tathmini na taarifa yake itatolewa katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa. Hatua zilizochukuliwa zinahusu Ibara ya 27 inayoweka wajibu wa kulinda maliasili za nchi na Ibara ya 9(c) inayohusu utajiri wa Taifa kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo, Wizara iliandaa na kuwasilisha Bungeni Miswada ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi ya mwaka 2017. Miswada hiyo ilipitishwa na Bunge kuwa Sheria mwezi Julai, 2017 na kuanza kutumika mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuwa na mkakati unganishi wa utekelezaji wa sheria hizo kwa kushirikiana na wadau wote muhimu, kazi inayotarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha 2017/2018. Umuhimu wa Mkakati huu hauko tu katika kutekeleza masharti ya Katiba bali pia katika kuhakikisha kuwa utajiri na rasilimali asilia za nchi yetu zinatumika ipasavyo katika kufanikisha mipango ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi imara na kuinua hali ya maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utekelezaji wa masharti ya Ibara ya 18(d) ya Katiba kuhusu haki ya kupata taarifa, Wizara yangu katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 iliandaa na kuchapisha katika Gazeti la Serikali Kanuni za Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa kupitia Tangazo la Serikali Na. 507 la tarehe 29 Desemba, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hizo pamoja na Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa ya mwaka 2016 zinaakisi nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Kanuni

hizo zimeainisha utaratibu wa wananchi kutumia haki ya kikatiba ya kupata taarifa kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha, shughuli zao na masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki na mfumo wa utoaji haki. Kwa muda mrefu suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani limekuwa ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki kwa wakati. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Mahakama imeamua jumla ya mashauri 141,107 katika ngazi zote za Mahakama, hadi kufikia Machi 2018, sawa na asilimia 98 ya mashauri yaliyosajiliwa katika kipindi hicho na asilimia 67 ya mashauri yote yaliyokuwepo mahakamani kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza mlundikano wa mashauri, Serikali kupitia Mahakama ya Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya na za Hakimu Mkazi. Mafanikio haya ni matunda ya utaratibu waliojiwekea Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wa kuweka ukomo wa chini wa idadi ya mashauri anayotakiwa kuamua Jaji au Hakimu. Ukurasa wa 17 na 18 na Kiambatisho B cha hotuba yangu kinaainisha hali ya usikilizaji wa mashauri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekaji wa mifumo imara wa ujenzi wa miundombinu ya utoaji huduma umekuwa ni moja ya vipaumbele vya maboresho ya sekta ya sheria. Katika kutekeleza kipaumbele hicho, Mahakama ya Tanzania, katika mwaka wa fedha 2017/2018, kupitia Mpango wa Maboresho ya Mahakama kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020, ilikamilisha ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Ilala, Kigamboni na Mkuranga na kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, Mahakama inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi katika Mikoa ya Geita, Njombe, Katavi, Simiyu na Lindi; Mahakama

za Wilaya 16 na kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo nane, kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho C cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifahamishe Bunge lako Tukufu na wananchi wote kuwa, Serikali kupitia Mpango wa Maboresho ya Mahakama, imeazimia kuwa na Mahakama Kuu kila mkoa, Mahakama za Hakimu Mkazi kwenye mikoa yote na Mahakama za Wilaya katika wilaya zote za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha nidhamu na weledi wa Madalali wa Mahakama katika utekelezaji wa majukumu yao ya utekelezaji wa hukumu, mwaka wa fedha 2017/2018, kanuni zinazosimamia uteuzi na usimamizi wa nidhamu za madalali zimetungwa upya. Chini ya Kanuni hizo, dalali atatakiwa kuwa na walau elimu ya kidato cha nne na uthibitisho wa cheti kuwa amesoma na kuzifahamu sheria na kanuni za utekelezaji wa hukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika juhudi za kuimarisha usimamizi wa nidhamu ya Mawakili, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetunga kanuni za kusimamia nidhamu ya Mawakili na kanuni za kuratibu malalamiko dhidi yao. Kanuni hizi kwa ujumla wake zinalenga kuboresha utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ya Nidhamu ya Mawakili ilipokea malalamiko 18 na kufanya jumla ya malalamiko yaliyokuwa mbele ya Kamati hiyo kufikia malalamiko 48. Katika kipindi hicho, malalamiko 22 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi ambapo Mawakili sita wamesimamishwa kufanya kazi ya uwakili kwa muda kati ya miezi sita hadi miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Mawakili wote nchini kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wakitambua kuwa wao ni Maofisa wa Mahakama wenye dhamana kubwa ya kufanikisha utoaji wa haki kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imeendelea kuboresha huduma zake kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Tanzania kuanzisha kanzidata ya Mawakili inayowawezesha Mawakili kufanya usajili na kuhuisha leseni za uwakili bila kulazimika kufika Ofisi za Mahakama Kuu, Dar es Salaam. Kanzidata hii, pamoja na mambo mengine, itasaidia kudhibiti watu wanaojifanya kuwa Mawakili na kuwatapeli wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kufuta ada ya nakala za hukumu na pia kuweka nakala hizo kwenye tovuti kama njia moja ya kuwarahisishia wadaawa kuzipata kwa urahisi. Aidha, Mahakama ya Tanzania imeingia mkataba na Shirika la Posta ambapo kupitia Shirika hilo nakala za hukumu zitapelekwa hadi milangoni mwa wadaawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usogezaji wa huduma za sheria karibu na wananchi utakuwa wa manufaa zaidi endapo utafanyika sanjari na uwekaji wa mifumo madhubuti ya utoaji haki. Katika kutekeleza hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia marekebisho hayo, Rais alianzisha Ofisi huru ya Taifa ya Mashtaka yaani *National Prosecution Services* kuchukua nafasi ya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Rais alianzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaani *Solicitor General* kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai yakiwemo ya kikatiba ambayo Serikali ni mdaawa ambayo awali yalikuwa yakishughulikiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho hayo yanakusudia kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashtaka ya jinai nchini hususani utekelezaji wa azma ya Serikali ya

kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka. Kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaani *Solicitor General* kunalenga kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na pia kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuimarika katika weledi na ubobezi wa kitaalamu katika kuishauri Serikali na kuandika Miswada ya Sheria kwa kuzingatia mabadiliko makubwa katika tasnia ya sheria kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho hayo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaratibu na kusimamia Mawakili wa Serikali walio katika Ofisi hiyo na Wanasheria wote katika Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali ambao sasa watakuwa ni Mawakili wa Serikali. Aidha, Mawakili wa Serikali walio katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali watakuwa chini ya uratibu na usimamizi wa Mkurugenzi wa Mashtaka na Wakili Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandishi wa sheria. Nimeeleza hapo awali kwamba moja ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali kuhusu maendeleo katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2018, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliandaa Miswada 15 ya Sheria ambayo iliwasilishwa Bungeni na kupitishwa kuwa sheria za nchi. Hali kadhalika, iliandaa Sheria Ndogo na matamko mbalimbali ya Serikali 398 ambayo yalichapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa mashtaka. Katika kulinda misingi ya utawala wa sheria ambayo ni nguzo muhimu ya kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendelea

kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, kufungua na kuendesha mashauri ya jinai mahakamani. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya mashauri ya jinai 17,339 yalifunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, jumla ya mashauri ya jinai 444 yalifunguliwa katika Mahakama ya Rufani ambapo mashauri 226 yalihitimishwa. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kipindi hicho iliendelea kuendesha mashauri ya jinai 13,832 yaliyofunguliwa katika Mahakama za chini. Kati ya hayo, jumla ya mashauri 6,951 yalihitimishwa kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashauri ya jinai yanayoshughulikiwa ni pamoja na yanayohusu wanyamapori, dawa za kulevya, uhujumu wa uchumi, rushwa na mauaji. Pia, kulikuwa na mashauri sita yaliyohusu vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ualbino yaliyoshughulikiwa. Kati ya hayo, mashauri manne yalikamilika kwa watuhumiwa kutiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu ya kifungo cha kati ya miaka minne hadi ishirini na mashauri mawili yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pia ilipokea jumla ya majalada 683 ya tuhuma za rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kati ya hayo majalada 288 yaliandaliwa hati ya mashtaka na 275 yalirudishwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi. Majalada 115 yako katika hatua mbalimbali yakifanyiwa kazi na mengine matano (5) yalifungwa. Takwimu zaidi za uendeshaji wa mashtaka zinapatikana katika ukurasa wa 24 hadi 26 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, washtakiwa waliotiwa hatiani walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini na mali zao kutaifishwa ambapo jumla ya shilingi za Kitanzania 2,484,445,706 zilitozwa kama faini kutoka kwa washtakiwa. Mali zilizotaifishwa ni pamoja na kilogramu 24.5 za dhahabu zenye thamani ya Sh.2,012,357,164 na fedha za kigeni kutoka mataifa 15 zenye thamani ya Sh.908,091,979.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali nyingine zilizotaifishwa ni pamoja na magari matano ya kifahari aina ya *Range Rover Vogue* na moja aina ya *Audi* yaliyokamatwa katika bandari ya Dar es Salaam yakisafirishwa kama nguo za mitumba, pikipiki 34, mafuta, mashine za kuhesabia pesa na basi la abiria lililokuwa likitumika kusafirishia meno ya tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mali zilizotaifishwa kwa ujumla wake zinakadiriwa kuwa na thamani ya Sh.5,685,086,465. Pia, katika kipindi hicho mali za Vyama vya Ushirika vya Mwanza *(Nyanza Cooperative Union)* na Shinyanga *(SHIRECU)* zikiwemo nyumba, viwanja na viwanda vilirejeshwa Serikalini kutoka mikononi mwa watu ambao walizichukua bila kufuata utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha shughuli za uendeshaji wa mashtaka ya jinai, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliandaa mwongozo wa wapelelezi na waendesha mashtaka katika makosa yanayohusu wanyamapori na mazao ya misitu. Mwongozo huo uliozinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ulianza kutumika tarehe 1 Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendesha mafunzo ya utekelezaji wa mwongozo huo katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kuhusisha jumla ya watumishi 450 wakiwemo Mawakili wa Serikali, Maafisa Wanyamapori na Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa na Wilaya toka Jeshi la Polisi. Lengo la mwongozo huo ni kuongeza ufanisi wa kazi kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka na kuondokana na dosari za kiutendaji wakati wa kushughulikia makosa ya jinai katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuendelea kubadilika kwa mbinu za uhalifu ikiwemo kuongezeka kwa matukio ya uhalifu wa kimataifa, Wizara katika mwaka wa 2017/2018 iliendelea kutilia mkazo suala la ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kushughulikia uhalifu na masuala mengine ya kisheria. Juhudi hizo na ushiriki wetu katika vikao

mbalimbali vya taasisi za kikanda na kimataifa zinazoshughulikia haki za jinai kumeiwezesha Tanzania kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Urejeshaji wa Mali Zinazohusiana na Uhalifu Kusini mwa Bara la Afrika kuanzia Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na nafasi hiyo, vikao vya mkutano mkuu wa mwaka kwa miaka miwili mfululizo kuanzia Juni, 2018 vitafanyika hapa nchini na kutoa fursa kwa watumishi wengi ndani ya taasisi zetu kushiriki na nchi yetu kujitangaza zaidi kimataifa. Aidha, Tanzania ni mjumbe kwenye Kamati Tendaji ya Umoja wa Taasisi za Uendeshaji Mashtaka ya Jinai na ni Makamu wa Rais wa Chama cha Waendesha Mashtaka katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mashirikiano haya yameendelea kuwa ya manufaa kwa nchi yetu katika kubadilishana taarifa na uzoefu katika kushughulikia mashauri ya jinai kwa ufanisi zaidi na kuharakisha utoaji wa kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 219(5) na (6) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20, kinampa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria mamlaka ya kuwaachia watu waliotenda makosa mbalimbali ya jinai yakiwemo ya mauaji ambayo kutokana na kuwa na maradhi ya akili wakati wa kutenda makosa hayo Mahakama haikuwatia hatiani na badala yake iliamuru wahifadhiwe katika hospitali ya maradhi ya akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mamlaka hayo na kwa kuzingatia ushauri wa Bodi ya Ushauri iliyoundwa chini ya Sheria ya Afya ya Akili, Sura ya 98, katika mwaka wa fedha 2017/2018, nilisaini Amri ya kuachiwa huru kwa watu 55 waliokuwa na maradhi ya akili wakati walipotenda makosa ambao kati yao 37 ni wanaume na 18 ni wanawake ili waungane na familia zao na kuendelea na matibabu wakiwa nje ya Taasisi ya Isanga walipokuwa wamehifadhiwa wakipata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu wagonjwa hao walikuwa wakihifadhiwa kwenye Taasisi hiyo wakisubiri

kuimarika kwa afya zao za akili. Kupitia Bunge lako Tukufu nitoe wito kwa jamii, ndugu na jamaa za watu hao kuwapokea katika jamii na familia zao na kuishi nao kwa amani na upendo na kuhakikisha kuwa wanaendelea na matibabu kama ilivyoagizwa kwenye Amri ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa mashauri ya madai, Katiba na haki za binadamu. Wizara yangu, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliendelea kushughulikia mashauri ya madai, Katiba na haki za binadamu ambayo Serikali ni mdaawa ambapo katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 kulikuwa na jumla ya mashauri ya madai 3,767. Kati ya hayo, mashauri 216 yamehitimishwa na mashauri 3,551 yanaendelea kusikilizwa. Hali kadhalika, kulikuwa na mashauri 31 ya usuluhishi, ambapo shauri moja (1) limehitimishwa na mashauri 30 yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 kulikuwa na jumla ya mashauri 48 ya kikatiba yaliyofunguliwa katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Kati ya hayo, mashauri 30 yamehitimishwa na mengine 18 yanaendelea kusikilizwa. Vilevile, kulikuwa na mashauri 90 ya haki za binadamu kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hayo, mashauri manne (4) yamehitimishwa na mengine 86 yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kulikuwa na mashauri 10 kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki. Kati ya hayo, mashauri mawili (2) yamehitimishwa na mashauri nane (8) yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwenye mikataba na makubaliano mbalimbali yaliyofanywa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, Ofisi hii ilifanya uhakiki na kutoa ushauri kwa mikataba 1,068 yenye thamani ya Sh.2,366,478,349,257.40 na Dola za Marekani 6,424,707,221.33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mikataba inayohusu ununuzi, ukarabati na majengo, utoaji wa huduma za jamii na ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara. Hali kadhalika, ilitoa ushauri kwa Serikali katika masuala ya sheria zinazohusu sekta mbalimbali kupitia mikutano ya kikanda na kimataifa hususan mikataba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Haki za binadamu na msaada wa kisheria. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliendelea kuimarisha na kusimamia haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za nchi. Katika kipindi hicho, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliratibu maandalizi ya Rasimu ya Taarifa ya Nchi ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2009 na pia kutoa mafunzo kwa maafisa wa Serikali wakiwemo Mawakili wa Serikali kuhusu masuala ya haki za binadamu na biashara yaliyofanyika Bagamoyo, Pwani mwezi Agosti, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi na kufuatilia na kutoa ushauri kwa Serikali na taasisi zake kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Kutokana na juhudi hizo za pamoja (kati ya Serikali na Tume), Tume imefanikiwa kupata Daraja la “A” baada ya kufanyika Tathmini na Mtandao wa Tume za Haki za Binadamu Duniani. Mafanikio hayo ni kielelezo cha dhahiri kuwa nchi yetu inaheshimu na kuzingatia haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Tume imeendelea kufuatilia haki za binadamu kwa watu walio katika makundi yenye mahitaji maalum, mahabusu na wafungwa na kufanya uchunguzi wa malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2018, Tume ilifanya ukaguzi katika magereza 28 na vituo vya polisi 21 katika Mikoa ya

Ruvuma, Njombe, Geita, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Morogoro na Dodoma. Pia, ilikagua Taasisi ya Isanga inayohifadhi wagonjwa wa maradhi ya akili ambao awali walishtakiwa kwa kutenda makosa ya jinai na kutotiwa hatiani kutokana na kutenda makosa hayo wakiwa na maradhi ya akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume pia ilishughulikia malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukaji wa misingi ya utawala bora ambapo kufikia Machi, 2018 ilipokea malalamiko mapya 431 na kufanya jumla ya malalamiko kuwa 7,055. Kati ya malalamiko hayo, 412 yamefanyiwa uchunguzi na kuhitimishwa. Malalamiko mengine 6,610 yanaendelea kuchunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Tume ilifanya uchunguzi wa hadhara wa migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na wananchi na wawekezaji katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Singida na Manyara na kuwasilisha mapendekezo yake kwa taasisi zinazohusika na migogoro hiyo. Hali kadhalika, Tume ilikamilisha taarifa ya mwaka 2015/2016 na kuwasilishwa kwa Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya haki za binadamu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kuratibu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2017. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu maandalizi ya Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2022 ambao unalenga kukuza na kuimarisha usimamizi wa haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika mwaka wa fedha 2017/2018, iliendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini. Katika kipindi hicho, Wizara iliandaa Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria zilizotangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 44 la tarehe 9 Februari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia iliandaa Kanuni za Maadili kwa Watoa Msaada wa Kisheria ambazo zimeanza kutumika tarehe 10 Februari, 2018. Aidha, Wizara ilifanya uteuzi wa Msajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa mujibu wa kifungu cha tisa (9) cha Sheria ya Msaada wa Kisheria ambaye ana wajibu wa kuwasajili, kuwasimamia na kuwaratibu watoa huduma ya msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekamilisha uteuzi wa Wasajili Wasaidizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria ngazi ya mikoa na wilaya Tanzania Bara. Mafunzo kwa ajili ya Wasajili hao yameanza kutolewa mwezi huu Aprili, 2018 ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya mtaala mpya wa mafunzo ya wasaidizi wa kisheria. Hivyo, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, pamoja na kuandaa vitini vya kufundishia, itaanza kutoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria matarajali. Mafunzo haya yanatarajiwa kuongeza idadi ya wasaidizi wa kisheria nchini ambao ni nguzo muhimu ya utoaji wa msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya sheria. Wizara inatambua umuhimu wa marekebisho ya sheria katika maendeleo ya sekta ya sheria ili kuwa na mfumo madhubuti wa sheria nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania iliendelea kufanya utafiti na mapitio ya mfumo wa sheria zinazosimamia haki jinai, mfumo wa sheria za ushahidi na mfumo wa sheria za usuluhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2018 Tume ilikamilisha kuandaa taarifa ya utafiti wa mfumo wa sheria za usuluhishi ambayo imewezesha

Wizara kuanza mchakato wa mapendekezo ya kutungwa upya Sheria ya Usuluhishi. Pia, Tume imekamilisha taarifa za mwisho kuhusu sheria ya huduma ya ustawi wa jamii na mfumo wa sheria unaosimamia haki jinai. Aidha, utafiti kuhusu mfumo wa sheria za ufilisi ambao ni muhimu katika kujenga mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara nchini na mfumo wa sheria za ushahidi bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume imeendelea kutoa elimu ya sheria kwa umma ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018, vipindi 32 vya redio vilirushwa kuhusu majukumu ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na maudhui ya Sheria ya Mtoto, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu na Sheria za Serikali za Mitaa kuhusiana na wajibu wa viongozi wa kuchaguliwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano wa kimataifa kuhusu makosa ya jinai. Wizara yangu iliendelea kushughulikia masuala ya urejeshwaji wa wahalifu na kushirikiana na Mataifa mengine katika kukabiliana na uhalifu hususani ule unaovuka mipaka ambapo katika mwaka 2017/2018, ilipokea jumla ya maombi 14 ya kurejesha watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya jinai waliopo nchini kutoka nchi za Rwanda, Zambia, Kenya, Malawi, Marekani na Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi hayo yalishughulikiwa na Wizara kwa mujibu wa sheria za nchi. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara iliwasilisha maombi manne ya kurejeshwa nchini Tanzania kwa watuhumiwa wanaokabiliwa na makosa mbalimbali waliopo katika nchi za Rwanda, Uganda, Zambia na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ambayo Wizara ilipokea au kutuma nje ya nchi yalihusu makosa ya usafirishaji wa dawa za kulevya, mauaji ya kimbali, wizi, mauaji, makosa ya kimtandao na ubakaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kukabiliana na uhalifu unaovuka mipaka kwa kuzingatia sheria zetu na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imesaini na kuridhia. Pia Tanzania iliendeleza ushirikiano wa pamoja na mataifa mengine katika kushughulikia masuala ya jinai ikiwa ni pamoja na kuomba kukusanya ushahidi na vielelezo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara imeandaa rasimu ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria inayosimamia ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya jinai ili kuweza kunufaika zaidi na ushirikiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usajili wa matukio muhimu ya binadamu, ufilisi na udhamini. Mwaka wa fedha 2017/2018 Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)* uliendelea na usajili wa matukio muhimu ya binadamu ya vizazi, vifo, ndoa, talaka na hati za uasili wa watoto. Katika kipindi hicho jumla ya vizazi 1,593,313, vifo 46,914 na ndoa 15,866, talaka 91 na hati 44 za watoto wa kuasili zimesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni ongezeko la usajili wa watu 201,110, vifo 900,038, hati za watoto wa kusajili 10 na talaka 69 ikilinganishwa na matukio yaliyosajiliwa katika kipindi hicho kwa mwaka wa fedha 2016/2017 isipokuwa ambayo ni pungufu ya ndoa 1,907.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la usajili wa matukio ya vizazi na vifo ni kielelezo tosha kuwa wakala umejiimarisha katika kusajili matukio muhimu ya binadamu na kuhamasika kwa wananchi kutoa taarifa na matukio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya vizazi 1,593,313 vilivyosajiliwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Machi 2018, vizazi 929,938 vilisajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia mpango wa usajili wa watoto walio chini ya miaka mitano na kufanya kiwango cha usajili wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa Tanzania Bara kuongezeka kutoka asilimia 13 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 28 mwaka 2017,

sawa sawa na ongezeko la vizazi 2,673,406. Pia vizazi 63,550 vimesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia mpango wa usajili wa watoto walio shuleni katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwonekano wa *dashboard* ya kanzidata ya usajili wa vizazi vya chini ya miaka mitano umeambatanishwa katika kiambatanisho D cha hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *RITA* iliendelea na utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu *(CRVS)* ambao unalenga kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu na upatikanaji wa takwimu muhimu kwa maendeleo ya nchi. Kupitia mkakati wa *CRVS* Wizara imedhamiria kukuza na kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika usajli wa vizazi na vifo ambapo tayari imezindua mfumo wa kielekitroniki wa usajili wa vizazi na vifo kwa kuzingatia mahitaji ambayo ulianza kufanya kazi rasmi mwenzi Novemba mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya majaribio ya mfumo huo, jumla ya vizazi 12,688 na vifo 533 vilisajiliwa katika vituo 60 vilivyopo katika Mikoa ya Shinyanga, Geita na Dar es Salaam kufikia mwezi Machi 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi huu, wananchi wanapata huduma ya usajili wa vizazi na vifo kupitia Ofisi za Kata, vituo vya afya na hospitali ambapo kwa kawaida vipo karibu na wananchi walio wengi na vyeti vya kuzaliwa na kifo vinatolewa papo hapo. Orodha kamili ya vituo hivyo imeambatanishwa katika hotuba hii kama kiambatisho E.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia mfumo huu, *RITA* imeweza kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya usajili kama Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kuziwezesha taasisi hizo kufanya maamuzi sahihi kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hatua za *RITA* kubuni mikakati mbalimbali ya kusajili matukio muhimu ya binadamu,

bado mfumo wa usajili, utambuzi na uwekaji wa kumbukumbu umekuwa na changamoto kadhaa kutokana na mifumo ya sheria iliyopo. Matukio mengi hutokea katika ngazi ya Vijiji, Vitongoji, Mitaa na Kata ambapo watendaji na viongozi wa mamlaka husika wanatambua matukio yote yanayotokea katika maeneo hayo. Hata hivyo, Sheria ya Serikali za Mitaa haiwapi jukumu la kusajili na kutunza takwimu za matukio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia Taarifa ya Utafiti ya Mfumo wa Sheria ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu iliyoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kwa kushirikiana na *RITA,* Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu. Kutungwa kwa Sheria hiyo kutawezesha matukio mengi zaidi kusajiliwa kwa kuwa usajili wa matukio muhimu ya binadamu utaanzia ngazi ya vijiji, vitongoji na kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imefanya maandalizi ya awali ya kufanyia utafiti mfumo wa kisheria wa ufilisi nchini. Madhumuni ya utafiti huo ni kuweka msingi wa kutungwa upya kwa mfumo wa kisheria wa kusimamia masuala ya ufilisi katika juhudi za kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara iliendelea na usimamizi wa Bodi za Udhamini za taasisi mbalimbali ambapo kufikia mwezi Machi, 2018, Wakala ulisajili hati za miunganisho ya wadhamini 145, kufuatilia kwa karibu uendeshaji wa Bodi za Wadhamini wa taasisi na kutatua migogoro inayojitokeza katika usimamizi wa mali zilizo chini ya bodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za mafunzo, katika kuhakikisha watumishi wa sekta ya sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha, Wizara yangu kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kutoa mafunzo ya astashahada na stashahada kwa watumishi wa Mahakama na nje ya mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja na kuongeza uwezo wa chuo hicho kubuni na kuendesha programu mbalimbali za mafunzo na kukidhi mahitaji ya sekta ya sheria na Taifa. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, chuo kimeongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada kutoka 560 mwaka 2016/2017 hadi wanafunzi 702, sawa na ongezeko la asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa chuo kinaendelea na taratibu za kuhuisha ithibati yake kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE).* Pia, kutokana na ziara ya Jaji Mkuu wa Gambia, Mheshimiwa Hassan Bubacar Jallow, nchini Tanzania chuo kimeanza mazungumzo na Mahakama ya Gambia ili kuona uwezekano wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Mahakama ya nchi hiyo na mazungumzo hayo yapo katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Chuo kiliandaa mafunzo kwa wawezeshaji wa masuala ya haki na ulinzi wa mtoto wakiwemo Majaji, Mahakimu Wakazi, Maafisa Ustawi wa Jamii na Wahadhiri Wasaidizi. Vilevile, chuo kiliendesha mafunzo ya namna bora ya kuendesha mashauri ya watoto kwa washiriki 210 wakiwemo Mahakimu, Mawakili wa Serikali, Waendesha Mashtaka, Maafisa Ustawi wa Jamii na Mawakili wa Kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, chuo kimeendelea kutoa mafunzo endelevu kwa watumishi wa mahakama na wadau wengine wa sheria zaidi ya 500 wakiwemo Majaji, Mahakimu, Wasajili, watendaji na watumishi wa kada zote na pia mafunzo ya namna ya kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha Chuo kimeratibu mafunzo ya uendeshaji mashauri ya kikatiba na matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki kwa Majaji 61 wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Aidha, Chuo kimeratibu mafunzo ya uandishi wa hukumu kwa Mahakimu Wakazi wa

Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi 380 yaliyofanyika Mkoani Morogoro, Mwezi Februari na Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha chuo kimetengeneza Mtaala wa Kozi ya Madalali na Wapeleka amri za Mahakama yaani *Court Brokers and Court Process Servers* kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa madalali na Wapeleka Amri za Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni katika kutimiza matakwa ya kanuni zinazosimamia madalali na wapeleka amri za mahakama, *The Court Brokers and Process Serves (Appointment, Remuneration and Disciplinary) Rules*, *GN* 358 *of 2017).* Chuo pia kimeunda Kikosi Kazi cha kufanyia kazi wazo la kuanzishwa kwa kozi mpya ikiwemo Kozi ya Uongozi wa Mahakama. Kikosi Kazi hicho kimeshaanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Chuo kipo katika hatua za mwisho za kutengeneza mtaala wa mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya wa kada ya sheria. Chuo kwa kushirikiana na Wizara na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora wanaandaa Kikosi Kazi cha Kuandaa Mtaala wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria, kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, imeendelea kuchukua hatua za kuliwezesha Taifa kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi, weledi na utayari wa kushindana katika soko la ajira kwa wanasheria. Aidha, jumla ya wanafunzi 907 walifaulu mafunzo yao na kupata sifa ya kuandikishwa kuwa Mawakili Binafsi au kuajiriwa katika sehemu mbalimbali. Idadi hii inafanya wanafunzi waliohitimu mafunzo hayo kufikia 4,429 kati ya 8,130 katika makundi 26 waliosajiliwa tangu 2008 taasisi ilipoanza mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi 602 wa kundi la 24 wanasubiri matokeo yao ambayo yatatoka muda si mrefu.

Wanafunzi 501 wa kundi la 25 wapo katika mafunzo ya vitendo sehemu za kazi na wanafunzi 635 wa kundi la 26 wanaendelea na mafunzo ya *Semister* ya kwanza. Hali kadhalika, Taasisi imeandaa toleo la pili la jarida lijulikanalo kama *LST LAW REVIEW* na inategemea kutoa Toleo la Kwanza la Jarida lijulikanalo kama *Clinical Law Journal.* Majarida haya yanatarajiwa kukuza mwamko wa utafiti wa kisheria na uchambuzi maalum kwenye masuala mbalimbali ya sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya rasilimali watu katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara imeendelea kusimamia watumishi wake kwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na kwa kuzingatia weledi. Katika kipindi hicho, Wizara ilichukua hatua mbalimbali za kuendeleza watumishi wake ikiwemo kuajiri watumishi wapya, kugharamia masomo ya kujiendeleza ya watumishi na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi waliokiuka maadili ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiambatisho F cha Hotuba hii kinaainisha hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara katika kushughulikia maendeleo ya rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha utendaji wa Mahakama, katika kipindi hicho jumla ya watumishi wapya wa Mahakama 439 waliajiriwa. Vilevile, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilimshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu na kwa ushauri huo, Rais amefanya uteuzi wa Majaji wapya kumi na wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara, kupitia mradi wa *e-Justice*, ipo katika hatua za mwisho za kutengeneza kanzidata ya wanasheria wote walio katika utumishi wa umma. Kanzidata hiyo itakapokamilika uratibu wa wanasheria walio katika utumishi wa umma utarahisishwa na hatimaye kuwezesha wanasheria hao kutumika ipasavyo kulingana na sifa zao za kitaalam kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika kipindi hicho Wizara ilifanikiwa kuandaa mkutano wa wanasheria wote walio katika utumishi wa umma uliofanyika Mjini Dodoma. Kupitia mkutano huo, Wizara ilibaini changamoto kadhaa zinazowakabili wanasheria hao na tayari imeanza kuchukua hatua za kuondoa changamoto hizo mojawapo ikiwa kuwafanya wanasheria wote walio katika utumishi wa umma kuwa Mawakili wa Serikali, tofauti na awali ambapo wanasheria walio katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pekee ndio walikuwa wakitambulika kama Mawakili wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na miradi ya maendeleo, katika kuwa na uhakika wa upatikanaji wa rasilimali muhimu na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria nchini, Wizara yangu imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jitihada hizo, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ukiwemo Mradi wa *Strengthening Access to Justice and Human Rights Protection in* Tanzania unaohisaniwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa wenye madhumuni ya kuimarisha upatikanaji wa haki na ulinzi wa haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo pia Mradi wa Maboresho ya Haki Jinai unaohisaniwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza ukiwa na madhumuni ya kufanya maboresho katika mfumo wa haki jinai nchini. Katika kipindi hicho, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* lilishirikiana na wadau wengine katika kusaidia mradi wa usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kupitia Mkakati wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu *(CRVS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, *RITA* kwa ushirikiano na Benki ya Dunia imeanza kutekeleza Mfumo wa Usajili wa kizazi na kifo toleo la nne *(Birth Registration System 4$^{th}$ Generation- BRS 4G)* wenye lengo la kuboresha usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia mfumo wa TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine iliyoendelea kutekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na Mpango wa Maboresho ya Mahakama unaotekelezwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mradi wa *e-Justice* unaotekelezwa kwa fedha za ndani, Wizara yangu itaendelea na jitihada za kubaini maeneo mapya ya maboresho na kukaribisha wadau zaidi ili kufikia azma ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za kisheria na pia kuwa na mfumo madhubuti wa sheria nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara, hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha wa 2017/2018 ni kama vifuatavyo:-

Wizara kukamilisha mpango wa kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma kwa muda uliowekwa; kuimarika kwa usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya kisera kimuundo kutokana na kuhuishwa kwa miundo ya kitaasisi na kuanzishwa kwa taasisi mpya; wananchi kupata haki zao kwa wakati kutokana na kupungua kwa mlundikano wa mashauri katika Mahakama ya Tanzania kufikia chini ya asilimia kumi; huduma za mahakama kutolewa karibu zaidi na wananchi kwa kujengwa kwa mahakama mpya kama zilivyotajwa katika hotuba hii; kuimarika kwa mifumo ya ulinzi na matumizi ya utajiri na rasilimali za nchi kutokana na kuwekewa miongozo ya kisheria; watumishi kuendelezwa kitaaluma na kimaadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuendelea kuimarika kwa viwango vya usajili wa vizazi kitaifa hususan kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano; kuimarika kwa uwezo wa taasisi za mafunzo ya sheria katika kudahili wanafunzi zaidi na ubunifu wa programu mpya za mafunzo; kurejeshwa na kuokolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha na mali kutokana na uendeshaji wa mashauri ya jinai na madai mahakamani na mabaraza ya usuluhishi; kuimarika na kukua kwa mifumo ya upatikanaji wa haki za kisheria na haki za binadamu nchini; kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu haki zao, namna ya kudai haki zao na uwezo wa Serikali katika

kuwahudumia kupitia huduma ya msaada wa kisheria na mahakama;na Kuimarika kwa shughuli za utafiti na mapitio ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mafanikio haya, ni dhahiri kwamba sekta ya sheria imetoa mchango mkubwa katika ustawi na maendeleo ya Tanzania kwa kuimarisha amani, utulivu na utangamano nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mafanikio makubwa ambayo Wizara inajivunia, bado yapo maeneo yanayohitaji jitihada zaidi ili kutimiza malengo na matarajio ya Watanzania. Hivyo, Wizara yangu itahakikisha kuwa utekelezaji wa vipaumbele vya mwaka huu wa fedha vinakamilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 imekuwa ni moja ya miongozo mikuu kwa Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Wizara yangu imekuwa ikiwajibika vilivyo katika kuhakikisha kuwa inatekeleza ahadi zote za Ilani zinazoambatana na matarajio ya wananchi kutoka kwenye sekta ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi hizo ni nyingi lakini naomba uniruhusu nitaje walau chache kati ya hizo; kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala wa sheria katika ngazi zote za uongozi na kuimarisha mfumo wa utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza vipaumbele hivyo vya Ilani, Wizara ya Katiba na Sheria imeendelea kutumia mikakati mbalimbali ikiwemo ya muda mfupi na muda wa kati ikiwa ni pamoja na;

(a) Kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma. Hapa tumeanzisha Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ya Mahakama

Kuu. Divisheni hii ilianza kazi rasmi mwezi Julai, 2016, baada ya maandalizi yote muhimu kukamilika;

(b) Kutunga na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali, kupitia mkakati huu, Serikali imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi ya mwaka 2017,

(c) Kurekebisha Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 na kuandaa mapendekezo ya kutunga upya Sheria ya Usuluhishi, Sheria ya Urejeshwaji wa Mali Zinazohusiana na Uhalifu na Sheria ya Ushirikiano wa Pamoja Miongoni mwa Mataifa katika Masuala ya Jinai. Katika eneo hili Wizara yangu inakadiria kufikia asilimia 90 na jitihada za kukamilisha masuala yaliyosalia zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala wa sheria katika ngazi zote za uongozi. Hapa ni kutunga sheria mpya, kanuni na kufanya marekebisho ya sheria. Kupitia mkakati huu, Serikali imetunga Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria, Kanuni za Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa na kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya utafiti kuhusu mfumo wa sheria zinazolinda haki za wazee, sheria zinazolinda haki za walaji, sheria zinazosimamia mfumo wa haki jinai, mfumo unaosimamia usajili wa matukio muhimu ya binadamu, sheria za usuluhishi na mfumo wa sheria unaosimamia huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kutoa elimu kwa umma kuhusiana na masuala ya kisheria na kikatiba yanayohusu haki za binadamu ikiwemo haki ya kutambuliwa kupitia usajili wa vizazi, lakini pia kupokea na kufanyia uchunguzi malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora,

ikiwemo uchunguzi wa hadhara na kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu. Katika eneo hili Wizara yangu inakadiria kufikia asilimia 85 ya jitihada za kuboresha eneo hili zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha mfumo wa utoaji haki; hapa kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kama taasisi huru inayojitegemea; kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali *(Solicitor General)* kama taasisi inayojitegemea; kuanzishwa Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa mahakama za ngazi zote ili kutoa huduma bora za kimahakama karibu na wananchi walio wengi; kuanzisha matumizi ya mifumo ya teknolojia ya habari katika kusikiliza mashauri na kutunza kumbukumbu; kuanzishwa kwa Awamu ya Pili ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na kuanzishwa kwa mahakama zinazotembea na mashauri madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kufuta ada za kupata nakala za hukumu,tozo na amri mbalimbali za Mahakama na kuanzishwa kwa mfumo wa kusambaza nakala za hukumu, tozo na amri mbalimbali za mahakama kwa kutumia huduma ya Posta Mlangoni. Katika eneo hili Wizara yangu inakadiria kufikia asilimia 90 na jitihada za kuboresha eneo hili zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtiririko wa mapato na maduhuli ya Serikali. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge jumla ya Sh.166,479,908,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, Sh.76,441,279,000 ni za mishahara, Sh.66,801,799,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh.23,236,830,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za Maendeleo za ndani ni Sh.18,000,000,000 na fedha za nje ni Sh.5,236,830,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilipokea jumla ya Sh.146,148,048,788 sawa na asilimia 88 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo

Sh.69,546,409,422 ni mishahara na Sh.66,123,083,366 ni matumizi mengineyo, sawa na asilimia 99 ya fedha zilizoidhinishwa. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni Sh.10,478,556,000 zikiwemo fedha za ndani Sh.9,261,003,000 sawa na asilimia 51 ya fedha zilizoidhinishwa na fedha za nje Sh.1,217,553,000 ambazo ni sawa na asilimia 23 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Sh.24,087,507,200 kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilikusanya jumla ya Sh.15,318,449,410 kama maduhuli ya Serikali, sawa na asilimia 64 ya makusanyo yanayotarajiwa kukusanywa. Kiambatisho G cha hotuba yangu kinaainisha mchanganuo wa maduhuli ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na mikakati iliyopo; pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za kisheria, uchakavu wa miundombinu na uhaba wa vitendea kazi na matumizi hafifu ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na na changamoto hizo, Wizara yangu iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo na kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa kikatiba na kisheria muda wote ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha ushirikiano na wadau katika kulipatia ufumbuzi suala la upungufu wa watumishi pamoja na kuendeleza kitaaluma na kiujuzi watumishi waliopo;

(ii) Kuimarisha utafiti wa kisheria na kufanya mapitio ya sheria zilizopo;

(iii) Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya vipaumbele vya Wizara kuhusu mahitaji ya utoaji wa huduma za sheria;

(iv) Kubaini na kutumia vyanzo vipya vya mapato;

(v) Kushirikiana na wadau wa ndani na nje ili kukidhi mahitaji makubwa ya huduma za sheria;

(vi) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali zilizopo;

(vii) Kuimarisha uwezo wa Wizara wa kutumia fursa za TEHAMA katika utoaji huduma za sheria;

(viii) Kuimarisha taasisi za mafunzo zilizo chini ya Wizara; na

(ix) Kubaini na kutumia teknolojia ya gharama nafuu katika ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano thabiti uliopo baina ya Wizara na wadau wa maendeleo ni chachu ya mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hivyo, nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa:-

Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake, Jumuiya ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kushughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira, Shirika la Msaada la Watu wa Marekani, *PAMS Foundation, World Wildlife Fund,* Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ),* Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Udhibiti wa Usafirishaji Haramu wa Wanyapori na Misitu *(TRAFFIC),* Taasisi ya *Bloomberg Data for Health Initiative, Legal Services Facility,* Kampuni ya Simu ya Tigo na wadau wengine wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wao katika kuboresha Sekta ya Sheria nchini. Nawashukuru wadau wote wa nje na ndani kwa michango yao. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau hawa na wengine kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuimarisha Sekta ya Sheria nchini ili iweze kuwahudumia Watanzania na watu wengine kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umoja ni nguvu. Mafanikio yaliyopatikana yametokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata ndani ya Wizara yangu. Hivyo, kipekee nawashukuru viongozi na watendaji wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu katika Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Sifuni Ernest Mchome; Naibu Katibu Mkuu, Amon Anastas Mpanju; Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma; Jaji Kiongozi, Mheshimiwa Wambali; Msajili Mkuu wa Mahakama, Mheshimiwa Katarina Revokati; Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Hussein Kattanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Adelardus Lubango Kilangi; Mkurugenzi wa Mashtaka, Biswalo Eutropius Kachele Mganga; Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA)*, Bi. Emmy Hudson; Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria bwana Casmir Sumba Kyuki; Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu, Bi. Mary Crescent Massay; Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Mheshimiwa Jaji Dkt. Paul Faustine Kihwelo; na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, Dkt. Zakayo Ndobir Lukumay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2018/2019; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara yangu itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria kwa umma ili kuendana na dhima ya Wizara. Ili kufikia azma hiyo, Wizara yangu imeainisha maeneo ya kipaumbele

na kuyawekea mikakati mahususi ya kufanikisha utekelezaji wake. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria;

(i) kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa ajili ya mambo ya kisheria na utekelezaji wake. Sera hii ni muhimu katika kuupatia nguvu mfumo wa sheria nchini ya kuwezesha utekelezaji wa maboresho ya sekta ya sheria na vipaumbele mbalimbali vya maendeleo ya Taifa kwa wakati;

(ii) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria;

(iii) Kufanya mapitio na maboresho ya sheria mbalimbali ili ziweze kwenda na wakati kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na ahadi mbalimbali za Serikali;

(iv) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya maboresho katika mfumo wa utoaji haki nchini;

(v) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa kutenganisha mashtaka na upelelezi na maboresho mengine yanayoendelea katika mfumo wa mashtaka nchini na pia matokeo yanayopatikana kutokana na uendeshaji wa kesi za jinai;

(vi) Kuweka mfumo wa kimkakati wa kusimamia masuala ya utajiri na rasilimali asilia, kuratibu mapitio ya mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe;

(vii) Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu chini ya Wizara;

(viii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za taasisi, mipango na miradi mbalimbali chini ya Wizara; na

(ix) Kushiriki katika masuala mbalimbali ya kikanda na kimataifa yanayoihusu Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Tanzania:-

(i) Kuanza ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania Jijini Dodoma ili kuhamishia rasmi shughuli zake Makao Makuu ya nchi kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Serikali;

(ii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria kwa kufunga mfumo wa kielektroniki wa utunzaji wa kumbukumbu, usikilizaji wa mashauri, ukusanyaji wa takwimu za mashauri na kutoa taarifa mbalimbali;

(iii) Kushirikiana na Wizara katika kushughulikia mradi wa kujenga mfumo wa kieletroniki wa utoaji haki *(e-justice)* ili kuharakisha usikilizaji wa mashauri na hivyo kupunguza msongamano wa mahabusu magerezani;

(iv) Kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa Kamati za Maadili ya Mawakili wa Kujitegemea, udhibiti na kuwaondoa kwenye orodha Mawakili, wote wanaokiuka maadili pamoja na kujihusisha na vitendo vya kushawishi na kutoa rushwa bila kujali hadhi yao katika jamii;

(v) Kuendelea na ujenzi wa Mahakama nchini kote zikiwemo Mahakama Kuu mbili zinazoendelea kujengwa Mikoani Kigoma na Mara na kuanza kujenga nyingine katika Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Dodoma na Singida. Pia Mahakama kujenga Mahakama za Wilaya 32 na Mahakama za Mwanzo 20; na

(vi) Kuwajengea uwezo watumishi ili kuendeleza vipaji vya ubunifu, kuimarisha weledi na kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali:-

(i) Kuimarisha mfumo wa uandishi na urekebu wa sheria;

(ii) Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba; na

(iii) Kuwajengea ubobevu watumishi katika maeneo mbalimbali ya sheria ili kuweza kutoa ushauri stahiki kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka:-

(i) kuimarisha huduma za mashtaka kwa kuhakikisha kuwa ofisi ina vitendea kazi vya kutosha na rasilimali watu;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na uratibu katika utoaji wa haki kwa kushirikiana na wadau wengine katika utoaji wa haki kama vile Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi; na

(iii) Kufungua ofisi katika Mkoa wa Songwe na Wilaya za Kinondoni (Kawe) na Ilala (Kinyerezi) na Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali *(Solicitor General):-*

(i) kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashauri ya madai ndani na nje ya nchi ambayo Serikali ina maslahi;

(ii) Kuimarisha uwezo wa Wanasheria wa Serikali katika kushughulia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai; na

(iii) Kuandaa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

(i) Kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(iii) Kukagua sehemu wanazoshikiliwa watu kama vile magereza, vituo vya polisi na sehemu nyinginezo kwa kushirikiana na mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora inazingatiwa; na

(iv) Kuratibu na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania:-

(i) Kufanya mapitio ya Mfumo wa Sheria zinazohusu Masoko ya Mazao ya Kilimo *(Review of Legal Framework Governing Marketing for Agricultural Produce in Tanzania)*;

(ii) Kufanya mapitio ya Mfumo wa Sheria unaosimamia Ujenzi wa Nyumba Tanzania *(Review of Legal Framework Governing Buildings Construction in Tanzania)*;

(iii) Kufanya mapitio ya Mfumo wa Sheria unaosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa *( Review of Legal Framework Governing Local Government Election)*; na

(iv) Kufanya marejeo ya Taarifa ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania Kuhusu Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Utumishi wa Mahakama:-

(i) Kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya kwa kuandaa mwongozo wa uendeshaji wa Kamati hizo; na

(ii) Kufanya ukaguzi wa utendaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya kuona endapo zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini:-

(i) Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu *(CRVS)*;

(ii) Kuboresha mazingira wezeshi ya biashara...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ya muda naomba sasa uombe pesa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nenda kwenye Ibara ya 72.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara na taasisi zilizopo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.48,907,243,000. Kati ya fedha hizo, Sh.40,113,746,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.8,793,497,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila kifungu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 12, Tume ya Utumishi wa Mahakama; matumizi ya mishahara ni Sh.276,836,000 na matumizi mengineyo ni Sh.820,507,000, jumla ni Sh.1,097,343,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 16, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; matumizi ya mishahara ni Sh.3,345,651,000, matumizi mengineyo ni Sh.3,618,731,000, matumizi ya maendeleo (ndani) ni Sh.2,000,000,000, jumla ni Sh.8,964,382,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 19, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; matumizi ya mishahara ni Sh.1,624,217,000, matumizi mengineyo ni Sh.2,298,637,000, matumizi ya maendeleo (nje) ni Sh.248,363,000, jumla ni Sh.4,171,217,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 35**,** Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; matumizi ya mishahara ni Sh.9,404,840,000, matumizi mengineyo ni Sh.6,023,265,000, matumizi ya maendeleo (nje) ni Sh.527,000,000, jumla ni Sh.15,955,105,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 41, Wizara ya Katiba na Sheria; matumizi ya mishahara ni Sh.4,618,692,000, matumizi mengineyo ni Sh.2,265,859,000, matumizi ya maendeleo (ndani) ni Sh.1,000,000,000, matumizi ya maendeleo (nje) ni Sh.3,221,196,000, jumla ni Sh.11,105,747,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 55, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; matumizi ya mishahara ni Sh.2,273,852,000, matumizi mengineyo ni Sh.1,566,080,000, matumizi ya maendeleo (nje) ni Sh.1,796,938,000, jumla ni Sh.5,636,870,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 59, Tume ya Kurekebisha Sheria; matumizi ya mishahara ni Sh. 999,570,000, matumizi mengineyo ni Sh.979,009,000, jumla ni Sh.1,978,579,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh.141,584,739,000 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama. Kati ya fedha hizo, Sh.105,611,017,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.35,973,722,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa Mfuko wa Mahakama ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 40, Mfuko wa Mahakama; matumizi ya mishahara ni Sh.54,629,635,000, matumizi mengineyo ni Sh.50,981,382,000, matumizi ya maendeleo (ndani) ni Sh.15,000,000,000, matumizi ya maendeleo (nje) ni Sh.20,973,722,000, jumla ni Sh.141,584,739,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Sh.27,097,646,862 ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kutokana na vyanzo vya mapato vinavyoainishwa na taasisi mbalimbali kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini, yaani Fungu 12 hakuna; Fungu 16, Sh.3,002,000; Fungu 35, Sh.13,002,000; Fungu 40, Sh.12,328,200,862; Fungu 41, Sh.14,753,292,000; Fungu 55, hakuna; na Fungu 59, Sh.150,000; jumla ni Sh.27,097,646,862.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (MB), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

---

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja

kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa wingi wa rehema zake na kwa kuniruzuku uhai na kunipa afya njema iliyoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini katika kuitumikia Serikali ya Awamu ya Tano katika nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi nitaendelea kuitumikia nafasi hiyo kwa uadilifu, uaminifu, unyenyekevu na namwomba Mwenyezi Mungu anijalie hekima na busara niweze kutimiza wajibu wangu kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi wote.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa majonzi makubwa nikupe pole wewe, Bunge lako tukufu, familia na wananchi wote wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuondokewa na mwenzetu Mhe. Leonidas Tutubert Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, kupitia Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa moyo mkunjufu napenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri wa kuliongoza na kulisimamia Bunge letu tukufu katika jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali. Nawapongeza pia Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu na kwa kuzingatia Katiba, sheria , kanuni na taratibu.

5. **Mheshimiwa Spika,** kipekee nikushukuru kwa uamuzi wako wa kuunda Kamati Teule za Bunge za kushughulikia

masuala ya uchimbaji na biashara ya madini ya Tanzanite na Almasi zilizokuwa chini ya uenyekiti wa Mhe. Doto Biteko, Mbunge wa Bukombe na Mhe. Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala. Uamuzi wako wa kihistoria umechangia kuleta mabadiliko chanya katika usimamizi wa uchimbaji na biashara ya madini hayo muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Niwapongeze pia Mhe. Biteko na Mhe. Zungu pamoja na wajumbe wa Kamati zao kwa uzalendo na uaminifu waliouonyesha kwa Taifa.

6. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imeweka msingi wa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako tukufu.

7. **Mheshimiwa Spika**, kwa ridhaa yako naomba niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kwa kuchaguliwa tena kuziongoza Kamati hizo katika kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge hili. Wizara yangu inayo imani kubwa kwao na itaendelea kuwapatia ushirikiano wa kutosha katika kipindi cha uongozi wao. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inawezesha kupatikana kwa maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, mazingira na teknolojia.

8. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wabunge wenzangu waliochaguliwa hivi karibuni

kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Mbunge wa Songea Mjini, Mhe. Maulid Mtulia, Mbunge wa Kinondoni; Mhe. Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha, Mhe. Justine Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini na Mhe. Dkt. Stephen Kiruswa, Mbunge wa Longido. Binafsi nawatakia kila la heri na baraka tele katika kutekeleza majukumu yao ya Ubunge.

9. **Mheshimiwa Spika,** naomba kumpongeza Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi, Mbunge kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Dkt. Evaristo Emmanuel Longopa kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Dkt. Julius Clement Mashamba kwa kuteuliwa na Rais kuwa Wakili Mkuu wa Serikali; Bwana Edson Athanas Makallo kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka; na Dkt. Ally Possi kwa kuteuliwa na Rais kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Ni imani na matumaini yangu kwamba uzoefu, weledi na umahiri wao katika masuala ya sheria utasaidia sana katika kuleta mabadiliko chanya katika Sekta ya Sheria na Taifa kwa ujumla. Vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Majaji 12 walioteuliwa na Rais hivi karibuni kuwa Majaji wa Mahakama Kuu. Kipekee, niwashukuru Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Bwana Gerson John Mdemu na Bwana Paul John Ngwembe kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wakitumikia nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Niwatakie wao na wengine walioteuliwa na Rais kuwa Majaji wa Mahakama Kuu kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya katika Mhimili wa Mahakama.

## B. DIRA NA DHIMA

10. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Wizara ya Katiba na Sheria ni **"Katiba na sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa"**. Hii ni Dira inayolenga kuweka mazingira rafiki ya kisera na ya kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano

wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu kwa mstakabali wa Taifa letu. Aidha, Dhima ya Wizara ni **"Kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria katika kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa"**. Dhima hii inahimiza kufanya kazi kwa weledi na ubunifu katika kujenga mazingira wezeshi kwa wananchi kupata haki na huduma muhimu za kisheria.

## C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

**11.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni taasisi mpya za Wizara zilizoanzishwa kufuatia marekebisho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13 Februari, 2018.

**12.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na vyombo halali vya maamuzi, Wizara yangu imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu kwa Mawaziri, kupitia Tangazo la Serikali Na. 144A la tarehe 22 Aprili, 2016. Majukumu hayo ni:-

i. Kuweka Sera kwa ajili ya masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;
ii. Kushughulikia masuala ya kikatiba;
iii. Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;
iv. Uandishi wa Sheria;
v. Kuendesha mashtaka ya jinai;
vi. Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na mikataba mbalimbali inayoihusu Serikali na uratibu wa sheria za kimataifa;

vii. Kushughulikia masuala ya haki za binadamu na msaada wa kisheria;
viii. Kurekebisha sheria;
ix. Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa mataifa kwenye makosa ya jinai;
x. Kusajili matukio muhimu ya binadamu (vizazi, vifo, ndoa, talaka na uasili), ufilisi na udhamini;
xi. Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na
xii. Kuratibu shughuli za taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara.

## D. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/ 2018

13. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Wizara yangu ilipanga na kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo mahsusi ya vipaumbele kama msingi wa kutekeleza Dhima ya Wizara na Taasisi zake. Baadhi ya maeneo ya vipaumbele yalikuwa yafuatayo:-
i. Kukamilisha uhamishaji wa Makao Makuu ya Wizara kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma;
ii. Kuratibu masuala ya kisera katika Wizara na Taasisi;
iii. Kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini;
iv. Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya Katiba na Sheria;
v. Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba;
vi. Kuharakisha usikilizaji wa mashauri;
vii. Kukuza na kutetea haki za binadamu hususan haki za makundi yenye mahitaji maalum;
viii. Kuboresha utoaji huduma za Mahakama kwa kuongeza idadi ya watumishi wa Mahakama wenye weledi na sifa stahiki;
ix. Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu;
x. Kuendesha programu za mafunzo kwa wasaidizi wa sheria;

xi. Kuimarisha na kuendelea kutoa mafunzo endelevu ya kimahakama pamoja na mafunzo kazini kwa watumishi wa mahakama na wengine wa sekta ya sheria kwa ujumla;

xii. Kukamilisha utafiti kuhusu mfumo wa sheria za usimamizi wa haki jinai; na

xiii. Kujenga na kukarabati miundombinu ya Wizara na taasisi zake katika ngazi mbalimbali.

Ufafanuzi zaidi kuhusu vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umetolewa katika **Kiambatisho A** cha Hotuba hii.

**14.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia vipaumbele hivyo, Wizara iliandaa na kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Mpango na Makadirio ya Bajeti ambayo yalipitishwa kwa ajili ya utekelezaji. Hivyo, kwa ridhaa yako naomba sasa niwasilishe mbele ya Bunge hili taarifa kuhusu hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kutekeleza Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, mafanikio yaliyopatikana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji kama ifuatavyo:-.

## I. Kuhamishia Makao Makuu ya Wizara Dodoma

**15.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Wizara ya Katiba na Sheria, kupitia Fungu 41, imetekeleza kikamilifu azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhamishia shughuli za Serikali mjini Dodoma. Hadi kufikia mwezi Novemba, 2017 Wizara ilikuwa imehamishia shughuli na watumishi wake wote mjini Dodoma. Aidha, Mahakama ya Tanzania imeanza kutekeleza mpango wa kuhamia Dodoma ikiwa tayari imepata eneo lenye ukubwa wa takriban hekta 19 kwa ajili ya kuanza kujenga makao yake makuu katika mwaka huu wa fedha 2017/2018. Pia, Idara ya Uandishi wa Sheria iliyopo chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imehamia Dodoma. Nipende tu kusisitiza kwamba zoezi la kuhamia mkoani Dodoma ni endelevu na linaendelea kuratibiwa vyema na Ofisi ya Waziri Mkuu.

## II. Sera na Masuala ya Sheria

**16. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Wizara iliendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa kupokea maoni ya wadau kuhusu Rasimu ya Sera ya Taifa ya Sheria. Maandalizi ya Sera hiyo yamechukua muda mrefu kutokana na ukweli kuwa masuala ya Sheria ni mtambuka na wadau wake ni wengi. Hivyo, Wizara yangu bado inaendelea kuratibu upatikanaji wa maoni ya wadau na kuyachambua kwa minajili ya kuboresha Rasimu hiyo ili kuwa na Sera inayokidhi mahitaji halisi ya Sekta ya Sheria na kuakisi mahitaji ya jamii kwa ujumla. Kukamilika kwa Sera hii kutaupatia nguvu mfumo wa sheria ya kuwezesha utekelezaji wa maboresho ya sekta ya sheria na vipaumbele mbalimbali vya maendeleo ya Taifa. Ni matarajio ya Wizara yangu kuwa ifikapo mwezi Septemba, 2018 tutakuwa na Sera kamili.

**17. Mheshimiwa Spika,** moja ya majukumu ya msingi ya Wizara ni kusimamia mfumo wa sheria nchini ikiwemo kutathmini hali ya utekelezaji wa sheria zilizopo na kutoa ushauri juu ya sheria mpya zinazotungwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 imeendelea kufanya tathmini ya hali ya utekelezaji wa sheria nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinawezesha kutekelezwa kwa mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika kufanikisha azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda. Katika kipindi hicho, sheria zinazohusu masuala ya jinai, ardhi na mazingira ziliendelea kufanyiwa tathmini na taarifa yake itatolewa katika Mwaka wa Fedha ujao.

**18. Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa. Hatua zilizochukuliwa zinahusu Ibara ya 27 inayoweka wajibu wa kulinda maliasilia za nchi na Ibara ya 9(c) inayohusu utajiri wa Taifa kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote. Katika muktadha huo, Wizara iliandaa na

kuwasilisha Bungeni Miswada ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi ya mwaka 2017. Miswada hiyo ilipitishwa na Bunge kuwa Sheria mwezi Julai, 2017 na kuanza kutumika mara moja. Kimsingi, Sheria hizo zinalenga kuhakikisha matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi hususani kwenye kuondoa umaskini, ujinga na maradhi; na maliasilia za nchi, mali za mamlaka za nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi zinalindwa. Hivi sasa, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuwa na mkakati unganishi wa utekelezaji wa sheria hizo kwa kushirikiana na wadau wote muhimu, kazi inayotarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Umuhimu wa Mkakati huu hauko tu katika kutekeleza masharti ya Katiba pia katika kuhakikisha kuwa utajiri na rasilimali asilia za nchi yetu zinatumika ipasavyo katika kufanikisha mipango ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi imara na kuinua hali ya maisha ya wananchi wetu.

**19.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utekelezaji wa masharti ya Ibara ya 18(d) ya Katiba kuhusu haki ya kupata taarifa, Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliandaa na kuchapisha katika Gazeti la Serikali Kanuni za Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa kupitia Tangazo la Serikali Na. 507 la tarehe 29 Desemba, 2017. Kanuni hizo pamoja na Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa ya mwaka 2016 zinaakisi nia ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Kanuni hizo zimeainisha utaratibu wa wananchi kutumia haki ya kikatiba ya kupata taarifa kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha, shughuli zao na masuala muhimu kwa jamii.

## III. Haki na Mfumo wa Utoaji Haki

**20.** **Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu suala la kupunguza mlundikano wa mashauri mahakamani limekuwa ni moja ya vipaumbele muhimu vya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata haki kwa wakati. Katika

Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mahakama imeamua jumla ya mashauri 141,107 katika ngazi zote za Mahakama, hadi kufikia Machi 2018, sawa na asilimia 98 ya mashauri yaliyosajiliwa katika kipindi hicho, na asilimia 67 ya mashauri yote yaliyokuwepo mahakamani kwa kipindi hicho. Katika kupunguza mlundikano wa mashauri, Serikali kupitia Mahakama ya Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika Mahakama za Mwanzo, Wilaya na za Hakimu Mkazi. Mafanikio haya ni matunda ya utaratibu waliojiwekea Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wa kuweka ukomo wa chini wa idadi ya mashauri anayotakiwa kuamua Jaji au Hakimu. Ukurasa wa 17 hadi 18 na **Kiambatisho B** cha Hotuba yangu kinaainisha hali ya usikilizaji wa mashauri nchini**.**

**21.** **Mheshimiwa Spika,** uwekaji wa mifumo imara na ujenzi wa miundombinu ya utoaji huduma umekuwa ni moja ya vipaumbele vya maboresho ya sekta ya sheria. Katika kutekeleza kipaumbele hicho, Mahakama ya Tanzania, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, kupitia Mpango wa Maboresho ya Mahakama kwa kipindi cha 2015/16 hadi 2019/20, ilikamilisha ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Ilala, Kigamboni na Mkuranga na kuanza ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Kigoma na Mara. Kadhalika, Mahakama inaendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi katika mikoa ya Geita, Njombe, Katavi, Simiyu na Lindi; Mahakama za Wilaya 16 na kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo nane, kama zinavyoainishwa katika **Kiambatisho C** cha Hotuba yangu. Nilifahamishe Bunge lako tukufu na wananchi wote kuwa Serikali, kupitia Mpango wa Maboresho ya Mahakama, imeazimia kuwa na Mahakama Kuu kila mkoa, Mahakama za Hakimu Mkazi kwenye mikoa yote na Mahakama za Wilaya katika wilaya zote za Tanzania Bara. Ni imani ya Serikali kuwa kukamilika kwa miradi yote hiyo kutawezesha kupatikana kwa huduma muhimu na hivyo kuwezesha wananchi kupata haki kwa wakati.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha nidhamu na weledi wa madalali wa Mahakama katika utekelezaji wa majukumu yao ya utekelezaji wa hukumu, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, kanuni zinazosimamia uteuzi na usimamizi

wa nidhamu za madalali zimetungwa upya. Chini ya Kanuni hizo dalali atatakiwa kuwa na walau elimu ya kidato cha nne na uthibitisho wa cheti kuwa amesoma na kuzifahamu sheria na kanuni za utekelezaji wa hukumu. Aidha, katika juhudi za kuimarisha usimamizi wa nidhamu ya mawakili, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Serikali imetunga kanuni za kusimamia nidhamu ya mawakili na kanuni za kuratibu malalamiko dhidi yao. Kanuni hizi kwa ujumla wake zinalenga kuboresha utoaji haki nchini.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ya Nidhamu ya Mawakili ilipokea malalamiko 18 na kufanya jumla ya malalamiko yaliyokuwa mbele ya Kamati hiyo kufikia malalamiko 48. Katika kipindi hicho, malalamiko 22 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi ambapo Mawakili 6 wamesimamishwa kufanya kazi ya uwakili kwa muda kati ya miezi 6 hadi miaka mitano. Nitoe wito kwa mawakili wote nchini kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wakitambua kuwa wao ni Maofisa wa Mahakama wenye dhamana kubwa ya kufanikisha utoaji wa haki kwa wakati.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara imeendelea kuboresha huduma zake kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Tanzania kuanzisha kanzidata ya mawakili inayowawezesha mawakili kufanya usajili na kuhuisha leseni za uwakili bila kulazimika kufika ofisi za Mahakama Kuu, Dar es Salaam. Kanzidata hii, pamoja na mambo mengine, itasaidia kudhibiti watu wanaojifanya kuwa mawakili na kuwatapeli wananchi. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni kufuta ada ya nakala za hukumu na pia kuweka nakala hizo kwenye tovuti kama njia moja ya kuwarahisishia wadaawa kuzipata kwa urahisi. Aidha, Mahakama ya Tanzania imeingia mkataba na Shirika la Posta ambapo kupitia Shirika hilo nakala za hukumu zitapelekwa hadi milangoni mwa wadaawa.

25. **Mheshimiwa Spika,** usogezaji wa huduma za sheria karibu na wananchi utakuwa wa manufaa zaidi endapo utafanyika sanjari na uwekaji wa mifumo madhubuti ya utoaji

haki. Katika kutekeleza hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya marekebisho ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Matangazo ya Serikali Na.48, 49 na 50 ya tarehe 13 Februari, 2018. Kupitia marekebisho hayo, Rais alianzisha Ofisi huru ya Taifa ya Mashtaka kuchukua nafasi ya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, Rais alianzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai yakiwemo ya kikatiba ambayo Serikali ni mdaawa ambayo awali yalikuwa yakishughulikiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Marekebisho hayo yanakusudia kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashtaka ya jinai nchini hususani utekelezaji wa azma ya Serikali ya kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji wa mashtaka. Kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kunalenga kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na pia kuiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuimarika katika weledi na ubobezi wa kitaalamu katika kuishauri Serikali na kuandika Miswada ya Sheria kwa kuzingatia mabadiliko makubwa katika tasnia ya sheria kitaifa, kikanda na kimataifa. Kutokana na marekebisho hayo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaratibu na kusimamia Mawakili wa Serikali walio katika Ofisi hiyo na wanasheria wote katika wizara, mamlaka za serikali za mitaa na taasisi za Serikali ambao sasa watakuwa ni Mawakili wa Serikali. Aidha, Mawakili wa Serikali walio katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali watakuwa chini ya uratibu na usimamizi wa Mkurugenzi wa Mashtaka na Wakili Mkuu wa Serikali.

## IV. Uandishi wa Sheria

**26. Mheshimiwa Spika,** nimeeleza hapo awali kwamba moja ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuhakikisha kuwa sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi sera na vipaumbele vya Serikali kuhusu maendeleo katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, mazingira na teknolojia. Hivyo, katika kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2018, Wizara, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliandaa miswada 15 ya sheria ambayo iliwasilishwa Bungeni

na kupitishwa kuwa sheria za nchi. Hali kadhalika, iliandaa Sheria ndogo na matamko mbalimbali ya Serikali 398 ambayo yalichapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

## V. Uendeshaji wa Mashtaka

**27. Mheshimiwa Spika,** katika kulinda misingi ya utawala wa sheria ambayo ni nguzo muhimu ya kudumisha amani, utulivu na umoja wa kitaifa, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliendelea kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai, kufungua na kuendesha mashauri ya jinai mahakamani. Hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya mashauri ya jinai 17,339 yalifunguliwa. Vilevile, jumla ya mashauri ya jinai 444 yalifunguliwa katika Mahakama ya Rufani ambapo mashauri 226 yalihitimishwa. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kipindi hicho iliendelea kuendesha mashauri ya jinai 13,832 yaliyofunguliwa katika mahakama za chini. Kati ya hayo, jumla ya mashauri 6,951 yalihitimishwa, kimahakama.

**28. Mheshimiwa Spika**, mashauri ya jinai yaliyoshughulikiwa ni pamoja na yanayohusu wanyamapori, dawa za kulevya, uhujumu uchumi, rushwa na mauaji. Pia, kulikuwa na mashauri sita yaliyohusu vitendo vya ukatili dhidi ya watu wenye ualbino yaliyoshughulikiwa. Kati ya hayo, mashauri manne yalikamilika kwa watuhumiwa kutiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu ya kifungo cha kati ya miaka minne hadi ishirini na mashauri mawili yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pia ilipokea jumla ya majalada 683 ya tuhuma za rushwa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kati ya hayo majalada 288 yaliandaliwa hati ya mashtaka na 275 yalirudishwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi. Majalada 115 yako katika hatua mbalimbali yakifanyiwa kazi na mengine matano yalifungwa. **Takwimu zaidi za uendeshaji wa mashataka zinapatikana katika ukurasa wa 24 hadi 26 wa hotuba yangu.**

**29. Mheshimiwa Spika**, washtakiwa waliotiwa hatiani walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini na mali zao kutaifishwa ambapo jumla ya shilingi za kitanzania 2,484,445,706/- zilitozwa kama faini kutoka kwa washtakiwa.

mali zilizotaifishwa ni pamoja na kilogramu 24.5 za dhahabu yenye thamani ya Shilingi 2,012,357,164 na fedha za kigeni kutoka mataifa 15 zenye thamani ya shilingi 908,091,979. Mali nyingine zilizotaifishwa ni pamoja na magari matano ya kifahari aina ya Range Rover Vogue na moja aina ya Audi yaliyokamatwa katika bandari ya Dar es Salaam yakisafirishwa kama nguo za mitumba, pikipiki 34, mafuta, mashine za kuhesabia pesa na basi la abiria lililokuwa likitumika kusafirishia meno ya tembo. Mali zilizotaifishwa kwa ujumla wake zinakadiriwa kuwa na thamani ya shilingi 5,685,086,465/-. Pia, katika kipindi hicho mali za vyama vya ushirika vya Mwanza (Nyanza Cooperative Union) na Shinyanga (SHIRECU) zikiwemo nyumba, viwanja na viwanda vilirejeshwa Serikalini kutoka mikononi mwa watu ambao walizichukua bila kufuata utaratibu wa kisheria. Nitumie fursa hii kuwataka wananchi na watu wengine kutojihusisha na vitendo vya uhalifu na badala yake kufanya shughuli halali za kujiingizia kipato kwani uhalifu haulipi.

**30.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha shughuli za uendeshaji wa mashtaka ya jinai, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka iliandaa mwongozo wa wapelelezi na waendesha mashtaka katika makosa yanayohusu wanyamapori na mazao ya misitu. Mwongozo huo uliozinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulianza kutumika tarehe 1 Januari, 2018. Pia, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendesha mafunzo ya utekelezaji wa mwongozo huo katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kuhusisha jumla ya watumishi 450 wakiwemo mawakili wa serikali, maafisa wanyamapori na wakuu wa upelelezi wa mikoa na wilaya toka Jeshi la Polisi. Lengo la mwongozo huo ni kuongeza ufanisi wa kazi kwa wapelelezi na waendesha mashtaka na kuondokana na dosari za kiutendaji wakati wa kushughulikia makosa ya jinai katika eneo hilo.

**31.** **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuendelea kubadilika kwa mbinu za uhalifu ikiwemo kuongezeka kwa matukio ya uhalifu wa kimataifa, Wizara katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliendelea kutilia mkazo suala la ushirikiano

wa kikanda na kimataifa katika kushughulikia uhalifu na masuala mengine ya kisheria. Juhudi hizo na ushiriki wetu katika vikao mbalimbali vya taasisi za kikanda na kimataifa zinazoshughulikia haki jinai kumeiwezesha Tanzania kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Urejeshaji wa Mali Zinazohusiana na Uhalifu Kusini mwa Bara la Afrika kuanzia Mwezi Machi, 2018. Wanachama wengine wa Umoja huo ni Angola, Botswana, Lesotho, Malawi, Mauritius, Namibia, Afrika Kusini, Madagascar, Msumbiji, Swaziland, Zambia, Zimbabwe, Shelisheli na Uganda. Kutokana na nafasi hiyo, vikao vya Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa miaka miwili mfululizo kuanzia Juni, 2018 vitafanyika hapa nchini na kutoa fursa kwa watumishi wengi ndani ya taasisi zetu kushiriki na nchi yetu kujitangaza zaidi kimataifa. Aidha, Tanzania ni mjumbe kwenye Kamati Tendaji ya Umoja wa Taasisi za Uendeshaji Mashtaka ya Jinai na ni Makamu wa Rais wa Chama cha Waendesha Mashtaka katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mashirikiano haya yameendelea kuwa ya manufaa kwa nchi yetu katika kubadilishana taarifa na uzoefu katika kushughulikia mashauri ya jinai kwa ufanisi zaidi na kuharakisha utoaji haki.

**32. Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 219(5) na (6) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20, kinampatia Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria mamlaka ya kuwaachia huru watu waliotenda makosa mbalimbali ya jinai yakiwemo ya mauaji ambao kutokana na kuwa na maradhi ya akili wakati wa kutenda makosa hayo Mahakama haikuwatia hatiani na badala yake iliamuru wahifadhiwe katika hospitali ya maradhi ya akili. Kutokana na mamlaka hayo na kwa kuzingatia ushauri wa Bodi ya Ushauri iliyoundwa chini ya Sheria ya Afya ya Akili, Sura ya 98, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, nilisaini Amri ya kuachiliwa huru watu 55 waliokuwa na maradhi ya akili wakati walipotenda makosa ambao kati yao 37 ni wanaume na 18 ni wanawake ili waungane na familia zao na kuendelea na matibabu wakiwa nje ya Taasisi ya Isanga walipokuwa wamehifadhiwa wakipata matibabu. Kwa muda mrefu wagonjwa hao walikuwa wakihifadhiwa kwenye Taasisi hiyo wakisubiri kuimarika kwa afya zao za akili. Kupitia Bunge lako

tukufu nitoe wito kwa jamii, ndugu na jamaa za watu hao kuwapokea katika jamii na familia zao na kuishi nao kwa amani na upendo na kuhakikisha kuwa wanaendelea na matibabu kama ilivyoagizwa kwenye Amri ya Waziri.

## VI. Uendeshaji wa Mashauri ya Madai, Katiba na Haki za Binadamu

**33. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu, kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliendelea kushughulikia mashauri ya madai, Katiba na haki za binadamu ambayo Serikali ni mdaawa ambapo katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 kulikuwa na jumla ya mashauri ya madai 3,767. Kati ya hayo, mashauri 216 yamehitimishwa na mashauri 3,551 yanaendelea kusikilizwa.. Hali kadhalika, kulikuwa na mashauri 31 ya usuluhishi, ambapo shauri 1 limehitimishwa na mashauri 30 yanaendelea kusikilizwa.

**34. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2018 kulikuwa na jumla ya mashauri 48 ya kikatiba yaliyofunguliwa katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Kati ya hayo, mashauri 30 yamehitimishwa na mengine 18 yanaendelea kusikilizwa. Vilevile, kulikuwa na mashauri 90 ya haki za binadamu kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu. Kati ya hayo mashauri 4 yamehitimishwa na mengine 86 yanaendelea kusikilizwa. Aidha, kulikuwa na mashauri 10 kwenye Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki. Kati ya hayo, mashauri 2 yamehitimishwa na mashauri 8 yanaendelea kusikilizwa.

**35. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwenye mikataba na makubaliano mbalimbali yanayofanywa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Hadi kufikia mwezi Machi 2018 Ofisi hii ilifanya uhakikii na kutoa ushauri wa mikataba **1,068** yenye thamani ya Shilingi **2,366,478,349,257.40** na Dola za Marekani **6,424,707,222.33**. Hii ni mikataba iliyohusu ununuzi, ukarabati wa majengo, utoaji wa huduma za jamii na ujenzi wa miundombinu

ikiwemo barabara. Hali kadhalika, ilitoa ushauri kwa Serikali katika masuala ya sheria zinazohusu sekta mbalimbali kupitia mikutano ya kikanda na kimataifa hususan mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa.

## VII. Haki za Binadamu na Msaada wa Kisheria

**36. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara iliendelea kuimarisha na kusimamia haki za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria za nchi. Katika kipindi hicho, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliratibu maandalizi ya Rasimu ya Taarifa ya Nchi ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wa Mwaka 2009 na pia kutoa mafunzo kwa maafisa wa Serikali wakiwemo Mawakili wa Serikali kuhusu masuala ya haki za binadamu na biashara yaliyofanyika Bagamoyo, Pwani mwezi Agosti, 2017.

**37. Mheshimiwa Spika,** Serikali iliendelea kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili iweze kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kufuatilia na kutoa ushauri kwa Serikali na taasisi zake kuhusu utekelezaji wa Haki za Binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Kutokana na juhudi hizo za pamoja (kati ya Serikali na Tume), Tume imefanikiwa kupata Daraja la “A” baada ya kufanyiwa Tathmini na Mtandao wa Tume za Haki za Binadamu Duniani. Mafanikio hayo ni kielelezo dhahiri kuwa nchi yetu inaheshimu na kuzingatia haki za binadamu. Aidha, Tume imeendelea kufuatilia haki za binadamu kwa watu walio katika makundi yenye mahitaji maalum, mahabusu na wafungwa; na kufanya uchunguzi wa malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Katika kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2018, Tume ilifanya ukaguzi katika magereza 28 na vituo vya polisi 21 katika mikoa ya Ruvuma, Njombe, Geita, Kagera, Simiyu, Shinyanga, Morogoro na Dodoma. Pia, ilikagua Taasisi ya Isanga inayohifadhi wagonjwa wa maradhi ya akili ambao awali

walishtakiwa kwa kutenda makosa ya jinai na kutotiwa hatiani kutokana na kutenda makosa hayo wakiwa na maradhi ya akili.

**38. Mheshimiwa Spika,** Tume pia ilishughulikia malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ambapo kufikia Machi, 2018 ilipokea malalamiko mapya 431 na kufanya jumla ya malalamiko kuwa 7,055. Kati ya malalamiko hayo, 412 yamefanyiwa uchunguzi na kuhitimishwa. Malalamiko mengine 6,610 yanaendelea kuchunguzwa. Vilevile, Tume ilifanya uchunguzi wa hadhara wa migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji; na wananchi na wawekezaji katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Singida na Manyara na kuwasilisha mapendekezo yake kwa taasisi zinazohusika na migogoro hiyo. Hali kadhalika, Tume ilikamilisha taarifa ya mwaka 2015/16 na kuwasilishwa kwa Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya haki za binadamu Tanzania Bara na Zanzibar.

**39. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu iliendelea kuratibu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu kwa kipindi cha mwaka 2013 hadi 2017. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu maandalizi ya Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu kwa kipindi cha mwaka 2018 hadi 2022 ambao unalenga kukuza na kuimarisha usimamizi wa haki za binadamu nchini.

**40. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria nchini. Katika kipindi hicho, Wizara iliandaa Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria zilizotangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 44 la tarehe 9 Februari, 2018. Wizara pia iliandaa Kanuni za Maadili kwa Watoa Msaada wa Kisheria ambazo zimeanza kutumika tarehe 10 Februari, 2018. Aidha, Wizara ilifanya uteuzi wa Msajili wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Sheria ya Msaada wa Kisheria ambaye ana wajibu wa kuwasajili, kuwasimamia na kuwaratibu watoa huduma ya msaada wa kisheria. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekamilisha uteuzi wa

Wasajili Wasaidizi wa watoa huduma ya msaada wa kisheria ngazi ya mikoa na wilaya Tanzania Bara. Mafunzo kwa ajili ya Wasajili hao yameanza kutolewa mwezi Aprili, 2018 ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**41. Mheshimiwa Spika**, ninayo furaha kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya mtaala mpya wa mafunzo ya wasaidizi wa kisheria. Hivyo, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania, pamoja na kuandaa vitini vya kufundishia, itaanza kutoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria matarajali. Mafunzo haya yanatarajiwa kuongeza idadi ya wasaidizi wa kisheria nchini ambao ni nguzo muhimu ya utoaji wa msaada wa kisheria.

## VIII. Marekebisho ya Sheria

**42. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua umuhimu wa marekebisho ya sheria katika maendeleo ya sekta ya sheria ili kuwa na mfumo madhubuti wa sheria nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, iliendelea kufanya utafiti na mapitio ya mfumo wa sheria zinazosimamia haki jinai, mfumo wa sheria za ushahidi na mfumo wa sheria za usuluhishi. Katika kipindi cha kuishia mwezi Machi, 2018 Tume ilikamilisha kuandaa taarifa ya utafiti wa mfumo wa sheria za usuluhishi ambayo imewezesha Wizara kuanza mchakato wa mapendekezo ya kutungwa upya Sheria ya Usuluhishi. Pia, Tume imekamilisha taarifa za mwisho kuhusu sheria ya huduma ya ustawi wa jamii na na mfumo wa sheria unaosimamia haki jinai. Aidha, utafiti kuhusu mfumo wa sheria za ufilisi ambao ni muhimu katika kujenga mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara nchini na mfumo wa sheria za ushahidi bado unaendelea.

**43. Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kutoa elimu ya sheria kwa umma ambapo katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018, vipindi 32 vya radio vilirushwa kuhusu majukumu ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania na maudhui ya Sheria ya Mtoto, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria ya Watu

Wenye Ulemavu na Sheria za Serikali za Mitaa kuhusiana na wajibu wa viongozi wa kuchaguliwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

## IX. Urejeshwaji wa Wahalifu na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Makosa ya Jinai

**44.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kushughulikia masuala ya urejeshwaji wa wahalifu na kushirikiana na mataifa mengine katika kukabiliana na uhalifu hususan ule unaovuka mipaka ambapo katika mwaka 2017/ 2018, ilipokea jumla ya maombi 14 ya kurejesha watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya jinai waliopo nchini kutoka nchi za Rwanda, Zambia, Kenya, Malawi, Marekani na Uingereza. Maombi hayo yalishughulikiwa na Wizara kwa mujibu wa Sheria za nchi. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara iliwasilisha maombi manne ya kurejeshwa nchini kwa watuhumiwa wanaokabiliwa na makosa mbalimbali waliopo katika nchi za Rwanda, Uganda, Zambia na Afrika Kusini. Maombi ambayo Wizara ilipokea au kutuma nje ya nchi yalihusu makosa ya usafirishaji wa dawa za kulevya, mauaji ya kimbari, wizi, mauaji, makosa ya kimtandao na ubakaji. Wizara itaendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kukabiliana na uhalifu unaovuka mipaka kwa kuzingatia sheria zetu na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imesaini na kuridhia. Pia, Tanzania iliendeleza ushirikiano wa pamoja na mataifa mengine katika kushughulikia masuala ya jinai ikiwa ni pamoja na kuomba kukusanya ushahidi na vielelezo nje ya nchi. Pia, Wizara imeandaa rasimu ya mapendekezo ya marekebisho ya sheria inayosimamia ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya jinai ili kuweza kunufaika zaidi na ushirikiano huo.

## X. Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu, Ufilisi na Udhamini

**45.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) uliendelea na usajili wa matukio muhimu ya binadamu ya vizazi, vifo, ndoa, talaka na hati za uasili wa watoto. Katika kipindi hicho,

jumla ya vizazi 1,593,313, vifo 46,914, ndoa 15,866, talaka 91 na hati 44 za watoto wa kuasili zimesajiliwa. Hii ni ongezeko la usajili wa vizazi 201,110, vifo 9,038, hati za watoto wa kuasili 10 na talaka 69 ikilinganishwa na matukio yaliyosajiliwa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 isipokuwa ndoa ambayo ni pungufu ya ndoa 1,907. Ongezeko la usajili wa matukio ya vizazi na vifo ni kielelezo tosha kuwa Wakala umejiimarisha katika kusajili matukio muhimu ya binadamu na kuhamasika kwa wananchi kutoa taarifa za matukio hayo. Nitoe wito kwa wananchi kutoa taarifa za matukio ya vizazi, vifo, ndoa na talaka ili kuiwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za matukio hayo.

**46.** **Mheshimiwa Spika**, kati ya vizazi 1,593,313 vilivyosajiliwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Machi 2018, vizazi 929,938 vilisajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia Mpango wa Usajili wa Watoto walio Chini ya Miaka Mitano na kufanya kiwango cha usajili kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa Tanzania Bara kuongezeka kutoka asilimia 13 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 28 mwaka 2017 sawa na ongezeko la vizazi 2,673,806. Pia, vizazi 63,550 vimesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia Mpango wa usajili wa watoto walio shuleni katika Mkoa wa Njombe. Mwonekano wa Dashibodi ya Kanzidata ya usajili wa vizazi chini ya miaka mitano umeambatishwa kama **Kiambatisho D** cha Hotuba hii.

**47.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia RITA iliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu (CRVS) ambao unalenga kuimarisha shughuli za usajili wa matukio muhimu na upatikanaji wa takwimu muhimu kwa maendeleo ya nchi. Kupitia Mkakati wa CRVS Wizara imedhamiria kukuza na kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika usajili wa vizazi na vifo ambapo tayari imezindua mfumo wa kielektroniki wa usajili wa vizazi na vifo kwa kuzingatia mahitaji ambao ulianza kufanya kazi rasmi mwezi Novemba, 2017. Katika hatua ya majaribio ya mfumo huo, jumla ya vizazi 12,688 na vifo 533 vilisajiliwa katika vituo 60 vilivyopo katika mikoa ya Shinyanga, Geita na Dar es Salaam, kufikia mwezi Machi, 2018. Kupitia Mradi huu

wananchi wanapata huduma za usajili wa vizazi na vifo kupitia ofisi za kata, vituo vya afya na hospitali, ambazo kwa kawaida zipo karibu na wananchi walio wengi, na vyeti vya kuzaliwa na kifo vinatolewa papo hapo. Orodha Kamili ya vituo hivyo imeambatishwa katika Hotuba hii kama **Kiambatisho E**. Pia, kupitia mfumo huu RITA inaweza kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya usajili kama Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kuziwezesha taasisi hizo kufanya maamuzi sahihi, kwa wakati na kwa gharama nafuu.

**48.** **Mheshimiwa Spika**, licha ya hatua za RITA kubuni mikakati mbalimbali ya kusajili matukio muhimu ya binadamu, bado mfumo wa usajili, utambuzi na uwekaji wa kumbukumbu umekuwa na changamoto kadhaa kutokana na mifumo ya sheria iliyopo. Matukio mengi hutokea katika ngazi za vijiji, vitongoji, mitaa na kata ambapo watendaji na viongozi wa mamlaka husika wanatambua matukio yote yanayotokea katika maeneo yao. Hata hivyo, Sheria za Serikali za Mitaa haziwapi jukumu la kusajili na kutunza takwimu za matukio hayo. Kufuatia Taarifa ya Utafiti ya Mfumo wa Sheria ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu iliyoandaliwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kwa kushirikiana na RITA, Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu. Kutungwa kwa Sheria hiyo kutawezesha matukio mengi zaidi kusajiliwa kwa kuwa usajili wa matukio muhimu ya binadamu utaanzia ngazi ya vijiji, vitongoji na kata.

**49.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara, kupitia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, imefanya maandalizi ya awali ya kufanyia utafiti mfumo wa kisheria wa ufilisi nchini. Madhumuni ya utafiti huo ni kuweka msingi wa kutungwa upya kwa mfumo wa kisheria wa kusimamia masuala ya ufilisi katika juhudi za kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji nchini. Pia, Wizara iliendelea na usimamizi wa Bodi za Udhamini za taasisi mbalimbali ambapo kufikia mwezi Machi, 2018 Wakala

ulisajili hati za miunganisho ya wadhamini 145, kufuatilia kwa karibu uendeshaji wa bodi za wadhamini wa taasisi na kutatua migogoro inayojitokeza katika usimamizi wa mali zilizo chini ya bodi hizo.

## XI. Taasisi za Mafunzo

**50. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha watumishi wa sekta ya sheria wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutosha, Wizara yangu kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kutoa mafunzo ya astashahada na stashahada kwa watumishi wa Mahakama na nje ya mahakama. Hii ni pamoja na kuongeza uwezo wa Chuo kubuni na kuendesha programu mbalimbali za mafunzo na kukidhi mahitaji ya sekta ya sheria na Taifa. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Chuo kimeongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada kutoka 560 mwaka 2016/17 hadi wanafunzi 702, sawa na ongezeko la asilimia 12. Hivi sasa Chuo kinaendelea na taratibu za kuhuisha ithibati yake kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Pia, kutokana na ziara ya Jaji Mkuu wa Gambia, Mheshimiwa Hassan Bubacar Jallow, nchini Tanzania Chuo kimeanza mazungumzo na Mahakama ya Gambia ili kuona uwezekano wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Mahakama ya nchi hiyo na mazungumzo hayo yapo katika hatua nzuri.

**51. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Chuo kiliandaa mafunzo kwa wawezeshaji wa masuala ya haki na ulinzi wa mtoto wakiwemo majaji, mahakimu wakazi, maafisa ustawi wa jamii na wahadhiri wasaidizi. Vilevile, Chuo kiliendesha mafunzo ya namna bora ya kuendesha mashauri ya watoto kwa washiriki 210 wakiwemo mahakimu, mawakili wa serikali, waendesha mashtaka, maafisa ustawi wa jamii na mawakili wa kujitegemea. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo endelevu kwa watumishi wa mahakama na wadau wengine wa sheria zaidi ya 500 wakiwemo majaji, mahakimu, wasajili, watendaji na watumishi wa kada zote na pia mafunzo ya namna ya kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi kwa wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji.

52. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka huu wa fedha Chuo kimeratibu mafunzo ya uendeshaji mashauri ya kikatiba na matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki kwa Majaji 61 wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Aidha, Chuo kimeratibu mafunzo ya uandishi wa hukumu kwa Mahakimu Wakazi wa Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi 380 yaliyofanyika mkoani Morogoro Mwezi Februari na Machi, 2018.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka huu wa fedha Chuo kimetengeneza Mtaala wa Kozi ya Madalali na Wapeleka Amri za Mahakama yaani *Court Brokers and Court Process Servers* kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Madalali na Wapeleka Amri za Mahakama. Hii ni katika kutimiza matakwa ya kanuni zinazosimamia madalali na wapeleka amri za mahakama, *the Court Brokers and Process Serves (Appointment, Remuneration and Disciplinary) Rules*, GN 358 of 2017). Chuo pia kimeunda Kikosi Kazi cha kufanyia kazi wazo la kuanzishwa kwa kozi mpya ikiwemo Kozi ya Uongozi wa Mahakama. Kikosi Kazi hicho kimeshaanza kazi.

54. **Mheshimiwa Spika,** hivi sasa Chuo kipo katika hatua za mwisho za kutengeneza mtaala wa mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya wa kada ya sheria. Chuo kwa kushirikiana na Wizara na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora wanaandaa Kikosi Kazi cha Kuandaa Mtaala wa mafunzo hayo.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria, kupitia Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, imeendelea kuchukua hatua za kuliwezesha Taifa kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi, weledi na utayari wa kushindana katika soko la ajira kwa wanasheria. Aidha, jumla ya wanafunzi 907 walifaulu mafunzo yao na kupata sifa ya kuandikishwa kuwa mawakili binafsi au kuajiriwa katika sehemu mbalimbali. Idadi hii inafanya wanafunzi waliohitimu mafunzo hayo kufikia 4,429 kati ya 8,130 katika makundi 26 waliosajiliwa tangu 2008 Taasisi ilipoanza mafunzo. Wanafunzi 602 wa kundi la 24 wanasubiri matokeo yao ambayo yatatoka muda si mrefu. Wanafunzi 501 wa

kundi la 25 wapo katika mafunzo ya vitendo sehemu za kazi na wanafunzi 635 wa kundi la 26 wanaendelea na mafunzo ya Semesta ya kwanza. Hali kadhalika, Taasisi imeandaa toleo la pili la jarida lijulikanalo kama *LST LAW REVIEW* na inategemea kutoa Toleo la Kwanza la Jarida lijulikanalo kama *Clinical Law Journal.* Majarida haya yanatarajiwa kukuza mwamko wa utafiti wa kisheria na uchambuzi maalumu kwenye masuala mbalimbali ya sheria hapa nchini.

## XII. Maendeleo ya Rasilimali Watu

**56. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara imeendelea kusimamia watumishi wake kwa kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na kwa kuzingatia weledi. Katika kipindi hicho, Wizara ilichukua hatua mbalimbali za kuendeleza watumishi wake ikiwemo kuajiri watumishi wapya, kugharamia masomo ya kujiendeleza ya watumishi na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi waliokiuka maadili ya utumishi. **Kiambatisho F** cha Hotuba hii kinaainisha hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Wizara katika kushughulikia maendeleo ya rasilimali watu.

**57. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha utendaji wa Mahakama, katika kipindi hicho jumla ya watumishi wapya wa Mahakama 439 waliajiriwa. Vile vile, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilimshauri Rais kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu na kwa ushauri huo, Rais amefanya uteuzi wa Majaji wapya kumi na wawili.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara, kupitia mradi wa e-Justice, ipo katika hatua za mwisho za kutengeneza kanzi data ya wanasheria wote walio katika utumishi wa umma. Kanzi data hiyo itakapokamilika uratibu wa wanasheria walio katika utumishi wa umma utarahisishwa na hatimaye kuwezesha wanasheria hao kutumika ipasavyo kulingana na sifa zao za kitaalamu kwa manufaa ya Taifa. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara ilifanikiwa kuandaa Mkutano wa wanasheria wote walio katika utumishi wa umma uliofanyika mjini Dodoma. Kupitia

Mkutano huo, Wizara ilibaini changamoto kadhaa zinazowakabili wanasheria hao na tayari imeanza kuchukua hatua za kuondoa changamoto hizo mojawapo ikiwa kuwafanya wanasheria wote walio katika utumishi wa umma kuwa Mawakili wa Serikali, tofauti na awali ambapo wanasheria walio katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pekee ndio walikuwa wakitambulika kama Mawakili wa Serikali.

**XIII. Mipango na Miradi ya Maendeleo**

**59.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuwa na uhakika wa upatikanaji wa rasilimali muhimu na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kisheria nchini, Wizara yangu imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo. Kutokana na jitihada hizo, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ukiwemo Mradi wa *Strengthening Access to Justice and Human Rights Protection in Tanzania* unaohisaniwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa wenye madhumuni ya kuimarisha upatikanaji haki na ulinzi wa haki za binadamu nchini. Upo pia Mradi wa Maboresho ya Haki Jinai unaohisaniwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza ukiwa na madhumuni ya kufanya maboresho katika mfumo wa haki jinai nchini. Katika kipindi hicho, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) lilishirikiana na wadau wengine katika kusaidia mradi wa usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kupitia Mkakati wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu (CRVS). Vilevile, RITA kwa ushirikiano na Benki ya Dunia imeanza kutekeleza Mfumo wa Usajili wa kizazi na kifo toleo la nne (Birth Registration System 4$^{th}$ Generation- BRS4G) wenye lengo la kuboresha usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia mfumo wa TEHAMA. Miradi mingine iliyoendelea kutekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na Mpango wa Maboresho ya Mahakama unaotekelezwa na Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia; na Mradi wa e-Justice unaotekelezwa kwa fedha za ndani. Wizara yangu itaendelea na jitihada za kubaini maeneo mapya ya maboresho na kukaribisha wadau zaidi ili kufikia azma ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za kisheria na pia kuwa na mfumo madhubuti wa sheria nchini.

## E. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

60. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/18 ni:

i. Wizara kukamilisha mpango wa kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma kwa muda uliowekwa;
ii. Kuimarika kwa usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya kisera kimuundo kutokana na kuhuishwa kwa miundo ya kitaasisi na kuanzishwa kwa taasisi nyingine mpya;
iii. Wananchi kupata haki zao kwa wakati kutokana na kupungua kwa mlundikano wa mashauri katika Mahakama ya Tanzania kufikia chini ya asilimia kumi;
iv. Huduma za mahakama kutolewa karibu zaidi na wananchi kwa kujengwa kwa mahakama mpya kama zilivyotajwa katika Hotuba hii;
v. Kuimarika kwa mifumo ya ulinzi na matumizi ya utajiri na rasilimali za nchi kutokana na kuwekewa miongozo ya kisheria;
vi. Watumishi kuendelezwa kitaaluma na kimaadili;
vii. Kuendelea kuimarika kwa viwango vya usajili wa vizazi kitaifa hususan kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano;
viii. Kuimarika kwa uwezo wa taasisi za mafunzo ya sheria katika kudahili wanafunzi zaidi na ubunifu wa programu mpya za mafunzo;
ix. Kurejeshwa na kuokolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha na mali kutokana na uendeshaji wa mashauri ya jinai na madai mahakamani na mabaraza ya usuluhishi;
x. Kuimarika na kukua kwa mifumo ya upatikanaji wa haki za kisheria na haki za binadamu nchini;
xi. Kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu haki zao, namna ya kudai haki zao na uwezo wa Serikali katika kuwahudumia kupitia huduma ya msaada wa kisheria na mahakama; na
xii. Kuimarika kwa shughuli za utafiti na mapitio ya sheria.

Kwa mafanikio haya, ni dhahiri kwamba Sekta ya Sheria imetoa mchango mkubwa katika ustawi na maendeleo ya

Tanzania kwa kuimarisha amani, utulivu na utangamano nchini. Kutokana na hali hiyo, wananchi wameweza kuendelea na shughuli zao za kujenga uchumi na kuleta maendeleo kwa ajili ya Taifa.

**61. Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio makubwa ambayo Wizara inajivunia, bado yapo maeneo yanayohitaji jitihada zaidi ili kutimiza malengo na matarajio ya Watanzania. Hivyo, Wizara yangu itahakikisha kuwa utekelezaji wa vipaumbele vya mwaka huu wa fedha vinakamilishwa kwa wakati.

## F. MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015

**62. Mheshimiwa Spika**, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 imekuwa ni moja ya miongozo mikuu kwa Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Wizara yangu imekuwa ikiwajibika vilivyo katika kuhakikisha kuwa inatekeleza ahadi zote za Ilani zinazoambatana na matarajio ya wananchi kutoka kwenye sekta ya sheria. Ahadi hizo ni nyingi lakini naomba uniruhusu nitaje walao chache kati ya hizo; kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala wa sheria katika ngazi zote za uongozi na kuimarisha mfumo wa utoaji haki.

**63. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza vipaumbele hiyo vya Ilani ,Wizara ya Katiba na Sheria imeendelea kutumia mikakati mbalimbali ikiwemo ya muda mfupi na muda wa kati ikiwa ni pamoja na:

### a) Kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma

(i) Kuanzisha Divisheni ya makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ya Mahakama Kuu. Divisheni hii ilianza kazi rasmi mwezi Julai, 2016 baada ya maandalizi yote muhimu kukamilika. Hatua hii inaenda sambamba na kuratibu upelelezi wa makosa ya jinai, kufungua na kuendesha mashauri mahakamani;

(ii) Kutunga na kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali. Kupitia mkakati huu, Serikali imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili za Nchi ya mwaka 2017; kurekebisha Sheria ya Makosa ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200; na kuandaa mapendekezo ya kutunga upya sheria ya usuluhishi, sheria ya urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu; na sheria ya ushirikiano wa pamoja miongoni mwa mataifa katika masuala ya jinai.
Katika eneo hili Wizara yangu inakadiria kufikia alama 90 na jitihada za kukamilisha masuala yaliyosalia zinaendelea;

**b) Kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na utawala wa sheria katika ngazi zote za uongozi:**

(i) Kutunga sheria mpya, kanuni na kufanya marekebisho ya sheria. Kupitia mkakati huu, Serikali imetunga Kanuni za Sheria ya Msaada wa Kisheria; Kanuni za Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa; na kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya kisheria. Aidha, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania imefanya utafiti kuhusu mfumo wa sheria zinazolinda haki za wazee; sheria zinazolinda haki za walaji; sheria zinazosimamia mfumo wa haki jinai; mfumo unaosimamia usajili wa matukio muhimu ya binadamu; sheria za usuluhishi; na mfumo wa sheria unaosimamia huduma za jamii;
(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusiana na masuala ya kisheria na kikatiba yanayohusu haki za binadamu ikiwemo haki ya kutambuliwa kupitia usajili wa vizazi;
(iii) Kupokea na kufanyia uchunguzi malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, ikiwemo uchunguzi wa hadhara; na
(iv) Kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu. Mkakati huu unalenga kuhamasisha ushiriki wa wadau, kukuza uelewa wa wananchi kuhusu haki ya kusajiliwa na pia kuinua viwango vya Taifa vya usajili.
Katika eneo hili Wizara yangu inakadiria kufikia alama 85 na jitihada za kuboresha eneo hili zinaendelea;

**c) Kuimarisha mfumo wa utoaji haki:**

(i) Kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kama taasisi huru inayojitegemea;

(ii) Kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kama taasisi inayojitegemea;

(iii) Kuanzisha Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi;

(iv) Kuendelea na ujenzi na na ukarabati wa mahakama za ngazi zote ili kutoa huduma bora za kimahakama karibu na wananchi walio wengi;

(v) Kuanzisha matumizi ya mifumo ya teknolojia ya habari katika kusikiliza mashauri na kutunza kumbukumbu za mashauri;

(vi) Kuanzishwa kwa Awamu ya Pili ya Maboresho ya Sekta ya Sheria;

(vii) kuanzishwa kwa mahakama zinazotembea (mobile courts) zitakazokuwa zikiendesha shughuli zake kupitia magari maalum hususan katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma ya mahakama) na mahakama za madai madogo madogo (small claims courts) ili kuharakisha usikilizaji wa mashauri;

(viii) kufuta ada za kupata nakala za hukumu,tozo na amri mbalimbali za
Mahakama; na

(ix) Kuanzishwa kwa mfumo wa kusambaza nakala za hukumu, tozo na amri mbalimbali za mahakama kwa kutumia huduma ya Posta Mlangoni.

Katika eneo hili Wizara yangu inakadiria kufikia alama 90 na jitihada za kuboresha eneo hili zinaendelea

## G. MTIRIRIKO WA MAPATO NA MADUHULI YA SERIKALI

**64. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi 166,479,908,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi 76,441,279,000 ni za mishahara, Shilingi 66,801,799,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 23,236,830,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za Maendeleo za ndani ni Shilingi 18,000,000,000 na fedha za nje ni Shilingi 5,236,830,000.

65. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 146,148,048,788 sawa na asilimia 88 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi 69,546,409,422 ni mishahara na Shilingi 66,123,083,366 ni matumizi mengineyo, sawa na asilimia 99 ya fedha zilizoidhinishwa. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni Shilingi 10,478,556,000 zikiwemo fedha za ndani Shilingi 9,261,003,000 sawa na asilimia 51 ya fedha zilizoidhinishwa na fedha za nje shilingi 1,217,553,000 ambazo ni sawa na asilimia 23 ya fedha ziliidhinishwa.

66. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi 24,087,507,200 kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi 15,318,449,410 kama maduhuli ya Serikali, sawa na asilimia 64 ya makusanyo yanayotarajiwa kukusanywa. **Kiambatisho G** cha Hotuba yangu kinaainisha mchanganuo wa maduhuli ya Wizara.

## H. CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO

67. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/18, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na; kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za kisheria, uchakavu wa miundombinu na uhaba wa vitendea kazi, na matumizi hafifu ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria.

68. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na na changamoto hizo, Wizara yangu iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo na kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa kikatiba na kisheria muda wote ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na:

a) Kuimarisha ushirikiano na wadau katika kulipatia ufumbuzi suala upungufu wa watumishi pamoja na kuendeleza kitaaluma na kiujuzi watumishi waliopo;

b) Kuimarisha utafiti wa kisheria na kufanya mapitio ya sheria zilizopo;
c) Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya vipaumbele vya Wizara kuhusu mahitaji ya utoaji wa huduma za sheria;
d) Kubaini na kutumia vyanzo vipya vya mapato;
e) Kushirikiana na wadau wa ndani na nje ili kukidhi mahitaji makubwa ya huduma za sheria;
f) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali zilizopo;
g) Kuimarisha uwezo wa Wizara wa kutumia fursa za TEHAMA katika utoaji huduma za sheria;
h) Kuimarisha taasisi za mafunzo zilizo chini ya Wizara; na
i) Kubaini na kutumia teknolojia ya gharama nafuu katika ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**69.** **Mheshimiwa Spika**, ushirikiano thabiti uliopo baina ya Wizara na wadau wa maendeleo ni chachu ya mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Hivyo, nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Benki ya Dunia (WB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN Women), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DfID), Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kushughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), Shirika la Msaada la Watu wa Marekani (USAID), PAMS Foundation, World Wildlife Fund (WWF), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Udhibiti wa Usafirishaji Haramu wa Wanyapori na Misitu (TRAFFIC), Taasisi ya Bloomberg Data for Health Initiative, Legal Services Facility (LSF), Kampuni ya simu ya TIGO na wadau wengine wa maendeleo. Niwahakikishie kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wao katika kuboresha sekta ya sheria nchini. Nawashukuru wadau wote wa nje na ndani kwa michango yao. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau hawa na wengine kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuimarisha Sekta ya Sheria nchini ili iweze kuwahudumia Watanzania na watu wengine kwa ufanisi na tija zaidi.

**70. Mheshimiwa Spika, umoja ni nguvu.** Mafanikio yaliyopatikana yametokana na ushirikiano mkubwa ninaoupata ndani ya Wizara yangu. Hivyo, kipekee ninawashukuru viongozi na watendaji wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu wakiongozwa na Katibu Mkuu, Prof. Sifuni Ernest Mchome, Naibu Katibu Mkuu, Amon Anastas Mpanju, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamisi Juma, Jaji Kiongozi, Mhe. Ferdinand Wambali, Msajili Mkuu wa Mahakama, Mhe. Katarina Revokati; Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Hussein Kattanga, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Adelardus Lubango Kilangi, Mbunge, Mkurugenzi wa Mashtaka, Bw. Biswalo Eutropius Kachele Mganga, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Bi.Emmy Kalomba Hudson, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Bw. Casmir Sumba Kyuki, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bi. Mary Crescent Massay, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Mhe. Jaji Dkt. Paul Faustine Kihwelo na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania Dkt. Zakayo Ndobir Lukumay.

## 7I. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2018/ 2019

**71. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/ 2019 Wizara yangu itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za kisheria kwa umma ili kuendana na Dhima ya **kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na kisheria katika kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa”**. Ili kufikia azma hiyo, Wizara yangu imeainisha maeneo ya kipaumbele na kuyawekea mikakati mahsusi ya kufanikisha utekelezaji wake. Maeneo hayo ni yafuatayo:-

***(a) Wizara ya Katiba na Sheria***

i. Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria kwa ajili ya mambo ya kisheria na utekelezaji wake. Sera hii ni muhimu katika kuupatia nguvu mfumo wa sheria nchini ya kuwezesha utekelezaji wa maboresho ya sekta ya sheria na vipaumbele mbalimbali vya maendeleo ya Taifa kwa wakati;

ii. Kukamilisha na kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (LSRPII);
iii. Kufanya mapitio na maboresho ya sheria mbalimbali ili ziweze kwenda na wakati kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ahadi mbalimbali za Serikali;
iv. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya maboresho katika mfumo wa utoaji haki nchini;
v. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mpango wa kutenganisha mashtaka na upelelezi na maboresho mengine yanayoendelea katika mfumo wa mashtaka nchini; na pia matokeo yanayopatikana kutokana na uendeshaji wa kesi za jinai;
vi. Kuweka mfumo wa kimkakati wa kusimamia masuala ya utajiri na rasilimali asilia, kuratibu mapitio ya mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe;
vii. Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu chini ya Wizara;
viii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za taasisi, mipango na miradi mbalimbali chini ya Wizara; na
ix. Kushiriki katika masuala mbalimbali ya kikanda na kimataifa yanayoihusu Wizara.

***(b) Mahakama ya Tanzania***

i. Kuanza ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania mjini Dodoma ili kuhamishia rasmi shughuli zake Makao Makuu ya nchi kama ilivyo kwa taasisi nyingine za Serikali;
ii. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria kwa kufunga mfumo wa kielektroniki wa utunzaji wa kumbukumbu, usikilizaji wa mashauri, ukusanyaji wa takwimu za mashauri na kutoa taarifa mbalimbali za kimahakama;
iii. Kushirikiana na Wizara katika kushughulikia mradi wa kujenga mfumo wa kieletroniki wa utoaji haki (e-justice) ili kuharakisha usikilizaji wa mashauri na hivyo kupunguza msongamano wa mahabusu magerezani;
iv. Kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa kamati za maadili ya mawakili wa

kujitegemea, udhibiti na kuwaondoa kwenye orodha Mawakili, wote wanaokiuka maadili pamoja na kujihusisha na vitendo vya kushawishi na kutoa rushwa bila kujali hadhi yao katika jamii;

v. Kuendelea na ujenzi wa mahakama nchini kote zikiwemo Mahakama Kuu mbili (2) zinazoendelea kujengwa mkoani Kigoma na Mara na kuanza kujenga nyingine katika mikoa ya Morogoro, Mwanza, Dodoma na Singida. Pia Mahakama kujenga Mahakama za Wilaya 32 na Mahakama za Mwanzo 20; na

vi. Kuwajengea uwezo watumishi ili kuendeleza vipaji vya ubunifu, kuimarisha weledi na kuongeza tija.

***(c) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali***

i. Kuimarisha mfumo wa uandishi na urekebu wa sheria;

ii. Kuimarisha usimamizi wa masuala ya mikataba; na

iii. Kuwajengea ubobevu watumishi katika maeneo mbalimbali ya sheria ili kuweza kutoa ushauri stahiki kwa Serikali.

***(d) Ofisi ya Taifa ya Mashtaka***

i. Kuimarisha huduma za mashtaka kwa kuhakikisha kuwa Ofisi ina vitendea kazi vya kutosha na rasilimali watu;

ii. Kuimarisha ushirikiano na uratibu katika utoaji wa haki kwa kushirikiana na wadau wengine katika utoaji wa haki kama vile Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi; na

iii. Kufungua Ofisi katika Mkoa wa Songwe na wilaya za Kinondoni (Kawe) na Ilala (Kinyerezi) na Kigamboni.

***(e) Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali***

i. Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashauri ya madai ndani na nje ya nchi ambayo Serikali ina maslahi;

ii. Kuimarisha uwezo wa wanasheria wa Serikali katika kushughulia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai; na

iii. Kuanda Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

***(f) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora***

i. Kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini;
ii. Kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora;
iii. Kukagua sehemu wanazoshikiliwa watu kama vile magereza, vituo vya polisi na sehemu nyinginezo kwa kushirikiana na mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora inazingatiwa; na
iv. Kuratibu na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu nchini.

***(g) Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania***

i. Kufanya mapitio ya mfumo wa Sheria zinazohusu Masoko ya Mazao ya Kilimo (Review of Legal Framework Governing Marketing for Agricultural Produce in Tanzania);
ii. Kufanya mapitio ya mfumo wa Sheria unaosimamia Ujenzi wa Nyumba Tanzania (Review of Legal Framework Governing Buildings Construction in Tanzania);
iii. Kufanya mapitio ya mfumo wa Sheria unaosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania ( Review of Legal Framework Governing Local Government Election); na
iv. Kufanya marejeo ya Taarifa ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania Kuhusu Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

***(h) Tume ya Utumishi wa Mahakama***

i. Kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya kwa kuandaa mwongozo wa uendeshaji wa Kamati hizo; na
ii. Kufanya ukaguzi wa utendaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya kuona endapo zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu.

***(i) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini***

i. Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu (CRVS);
ii. Kuboresha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa kuratibu upatikanaji wa Sheria mahsusi ya Ufilisi;

iii. Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika kuboresha utoaji wa huduma za usajili na usimamizi wa ukusanyaji mapato; na
iv. Kuimarisha mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini.

***(j) Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania***

i. Kuongeza udahili wa wanafunzi ili kuongeza idadi ya wataalam wa sheria nchini;
ii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mawakili na wadau wengine katika maeneo mapya yanayojitokeza katika taaluma ya sheria;
iii. Kuendesha programu za mafunzo kwa wasaidizi wa sheria (paralegals); na
iv. Kuimarisha miundombinu ya Taasisi.

***(k) Chuo cha Uongozi wa Mahakama-Lushoto***

i. Kuimarisha Kurugenzi ya Mafunzo Endelevu ya Kimahakama;
ii. Kuboresha mitaala ya Stashahada na Astashahada ya sheria Chuoni;
iii. Kumalizia ujenzi wa Hostel ya wanachuo wa kiume;
iv. Kuimarisha mfumo wa barabara za ndani ya Chuo;
v. Kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Sheria; na
vi. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA iliyopo na kujenga mifumo mingine mipya Chuoni.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara na Taasisi zilizopo chini yake inaliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **Bilioni Arobaini na Nane, Milioni Mia Tisa na Saba, Mia Mbili Arobaini na Tatu Elfu (Shilingi 48,907,243,000)**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja Kumi na Tatu, Mia Saba Arobaini na Sita Elfu (40,113,746,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **Bilioni Nane, Milioni Mia Saba Tisini na Tatu, Mia Nne Tisini na Saba Elfu (Shilingi 8,793,497,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.276,836,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.820,507,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.1,097,343,000** |

**(ii) Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.3,345,651,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.3,618,731,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - | Sh.2,000,000,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.8,964,382,000** |

**(iii) Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.1,624,217,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.2,298,637,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - | Sh.248,363,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.4,171,217,000** |

**(iv) Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.9,404,840,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.6,023,265,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - | Sh.527,000,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.15,955,105,000** |

**(v) Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.4,618,692,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.2,265,859,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - | Sh.1,000,000,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - | Sh.3,221,196,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.11,105,747,000** |

**(vi) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.2,273,852,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.1,566,080,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - | Sh.1,796,938,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.5,636,870,000** |

**(vii) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.999,570,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.979,009,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.1,978,579,000** |

**73.** **Mheshimiwa Spika**, vilevile, naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **Bilioni Mia Moja Arobaini na Moja, Milioni Mia Tano Themanini na Nne, Mia Saba Thelathini na Tisa Elfu (Shilingi 141, 584,739,000)** kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Mia Moja na Tano, Milioni Mia Sita Kumi na Moja, Kumi na Saba Elfu (Shilingi 105,611,017,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **Bilioni Thelathini na Tano, Milioni Mia Tisa Sabini na Tatu, Mia Saba Ishirini na Mbili Elfu (Shilingi 35,973,722,000)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa kila Mfuko wa Mahakama ni kama ifuatavyo:-

**Fungu 40: Mfuko wa Mahakama**

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | - | Sh.54,629,635,000 |
| Matumizi Mengineyo | - | Sh.50,981,382,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | - | Sh.15,000,000,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (Nje) | - | Sh.20,973,722,000 |
| **Jumla** | **-** | **Sh.141,584,739,000** |

**74.** **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/ 2019 Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **27,097,646,862** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kutokana na vyanzo vya mapato vinavyosimamiwa na taasisi mbalimbali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

| | | |
|---|---|---|
| Fungu 12 | - | Sh.0 |
| Fungu 16 | - | Sh.3,002,000 |
| Fungu 35 | - | Sh.13,002,000 |
| Fungu 40 | - | Sh.12,328,200,862 |
| Fungu 41 | - | Sh.14,753,292,000 |
| Fungu 55 | - | Sh.0 |
| Fungu 59 | - | Sh.150,000 |
| **JUMLA** | **-** | **Sh.27,097,646,862** |

**75.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, anayefuata ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria iliyofanya uchambuzi, karibu Mheshimiwa Mchengerwa, karibu sana.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Chama cha Mawakili Tanganyika ni nguzo muhimu kwa Kamati yangu ya Katiba na Sheria, hususani nyakati za marekebisho ya sheria, nitambue uwepo wa Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika ambaye wakati wa utambulisho wako alikuwa hajafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu nikiwa mmoja wa Wabunge pekee au muhimu waliowahi kuhudumu katika mihimili miwili ya Serikali; mhimili wa Bunge na mhimili wa Mahakama ambao nimefanya kazi huko kwa takribani miaka 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uteuzi wa Waheshimiwa Majaji na baadhi ya watendaji wakuu kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji haki nchini na kuongeza ufanisi wa taasisi husika. Pia tunawapongeza wateule hao na kuwatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 6(2)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria. Aidha, Kanuni ya 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuanzia tarehe 14 hadi 18, Machi, 2018. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa kibajeti za Wizara na taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 23 hadi 29, Machi, 2018 ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria ina Mafungu nane ya bajeti kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama;
(ii) Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(iii) Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;
(iv) Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;
(v) Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama;
(vi) Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria;
(vii) Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na
(vii) Fungu 59 –Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na;

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; maelezo ya miradi ya maendeleo iliyokaguliwa. Katika kutekeleza Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita na Wilayani Chato, kuanzia tarehe 14 hadi 18, Machi, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini inayosimamiwa na Wizara ya Katiba kupitia Mahakama. Taarifa kuhusu yatokanayo na ukaguzi wa miradi pamoja na ushauri wa Kamati kwa kila mradi ni kama inavyoainishwa katika Jedwali Namba moja (I).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukaguzi wa Miradi husika hapo juu, pia Kamati ilipokea taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa chini ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo imetengwa katika makundi manne. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi Na. 6310;
(ii) Mradi Na. 6312;
(iii) Mradi Na. 6314 pamoja; na
(iv) Mradi Na. 6391.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ni ile ambayo imekwenda kufanya ukarabati na ujenzi wa Mahakama za

Wilaya katika maeneo mbalimbali nchini kwenye Wilaya za Geita, Kigamboni, Ruangwa na maeneo mengine lakini pia ni ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama za Mwanzo Kawe, Karatu na maeneo mengine pamoja na ujenzi wa ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu pamoja na ukarabati wa Mahakama Kuu Sumbawanga pamoja na ujenzi wa ukarabati wa nyumba za Majaji na ukarabati wa nyumba ya Mheshimiwa Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria ya tarehe 19 Machi, 2018, Mahakama imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa majengo matano kwa ujenzi wa kutumia teknolojia ya gharama nafuu (moladi) ambazo ni Mahakama za Wilaya za Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Kinyerezi na Mahakama za Mwanzo Kawe. Aidha, Mahakama imekamilisha miradi mingine nane ambayo ilikuwa imekwama katika hatua mbalimbali katika kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni kama Mahakama ya Mwanzo Karatu (Arusha), Loliondo (Ngorongoro), Robanda (Serengeti) na Totowe (Songwe). Ujenzi ulioko katika hatua za mwisho ni Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara, Mahakama za Mwanzo za Magoma, Korogwe na Itinje Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika majengo ya mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inashauri Mahakama kurudia kuezeka paa la Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga kutokana na kubainika kuwa na dosari zinazosababisha kuvuja kwa baadhi ya sehemu za paa hilo wakati bado jengo hilo ni jipya na hivyo kuhitaji ukarabati wa haraka. Hatua hiyo itekelezwe haraka ili kuokoa athari zinazoweza kujitokeza kwa jengo ambalo limegharimu mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zake kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati mnamo tarehe 29 na 30 Machi, 2017ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya Tatu ya Mwaka huu wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti na Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi, 2018 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili, 2017. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi na katika kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018; katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya Sh.24,087,507,200/=. Hadi kufikia Februari, 2018 kiasi cha maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni Sh.12, 967,841, 164 sawa na asilimia 54 ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina; katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mafungu yaliyosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa Sh.143,243,078,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018 Wizara na Taasisi zake zilipokea Sh.86,977,028,083/= sawa na asilimia 52% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu unaonesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa iendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimamizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Hatua hii, Kamati inaipongeza sana Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria na

Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha Sh.23,236,830,000/= ambapo kiasi cha Sh.18,000,000,000/=, sawa na asilimia 77.46% ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za ndani na Sh.5,236,830,000/=, sawa na asilimia 22.54% ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Februari, 2018, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni Sh.10,478,556,000/= sawa na asilimia 45% ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni Sh. 9,261,003,000/=, sawa na asilimia 51% ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi; Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za ndani na fedha hizo zimepatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia ya *MOLADI* ni mfumo wa gharama nafuu na unakamilisha ujenzi kwa haraka.Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali nchini ya Wizara ya Katiba na Sheria hususan Miradi ya Ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango na makadilio na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zote zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 23 na 24 mwezi Machi, 2018. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti

uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/2021).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria; Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeainishwa maeneo zaidi ya Arobaini (40) ya vipaumbele vya Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, yakiwemo:-

(i) Kuanza Ujenzi wa Majengo ya Makao Makuu ya Mihimili wa Mahakama ya Tanzania Mjini Dodoma;

(ii) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sheria;

(iii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa kutenganisha mashtaka na Upelelezi;

(iv) Kuweka Mfumo wa kimkakati wa kusimamia masuala ya utajiri na rasilimali asilia, kuratibu mapitio ya Mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe na Utekelezaji wa Vipaumbele vingine kama ilivyohainishwa katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhishwa na vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake zote kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vipaumbele hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa taaluma ya sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha Sh.24,087,507,200/=. Kiasi hicho ni sawa na maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.2

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadilio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa Fedha 2018/2019; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wazara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya Sh.145, 726,763,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, Sh.75,298,137,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh.70,428,626,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchanganuo wa mapato na matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ni kama inavyoainishwa katika Jedwali Na.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, katika mwaka wa fedha Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa Sh.45,015,582,000/= kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi Sh.18,000,000,000/= ni fedha za ndani na Sh.27,015,582,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Fedha za Miradi ya Maendeleo imeongezeka zaidi ya Shilingi bilioni 21 ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 91% ya Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kubaini ongezeko la Bajeti ya Maendeleo hatua ambayo

imepongezwa, bado kiasi cha fedha za nje ni kikubwa ukilinganisha na bajeti ya ndani. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika kugharamia Miradi ya Maendeleo na kwa upatikanaji wake unaweza usiwe wa uhakika na hivyo unaweza kukwamisha utekelezaji wa Miradi husika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu la 12 ni Tume ya Utumishi wa Mahakama; Tume hii ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utawala wa Mahakama ya mwaka 2011, lakini pia ni kwa mujibu wa Katiba. Jukumu la chombo hicho cha kiutawala ni kusimamia Mahakama ya Tanzania kama mhimili wa Serikali ambao umekuwa ukitekeleza kazi zake kwa uhuru na haki bila kuingiliwa na chombo au taasisi nyingineyo ambavyo imetamkwa chini ya Ibara ya 107A na 107B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na malalamiko ya muda mrefu kuhusu changamoto mbalimbali katika usimamizi wa masuala mbalimbali ya kiutawala katika Mahakama, Serikali ilichukua hatua ya kufanya maboresho yaliyoanzisha Kada ya Watendaji wa Mahakama ambao wengi wao walikuwa Makatibu Tawala wa Wilaya na Mikoa, kwa lengo la kuisaidia Mahakama kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki kwa uhuru na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati imebaini kuwa Watendaji hao wa Mahakama wameshindwa kuisaidia Mahakama kutatua kero zake na kwa kuwa imebainika kuwa Watendaji hao wamekuwa wakitumia nafasi zao vibaya kwa kutumia hata lugha zisizoridhisha, kujiingiza kwenye maamuzi ya kesi wakati wao siyo Mahakimu wala Majaji, pia kuwanyanyasa Mahakimu na baadhi ya Majaji na hivyo kuathiri nia njema ya Serikali ya kuhakikisha Mahakama zinatumia rasilimali zilizopo katika kurahisisha utoaji haki kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa, Serikali ione uwezekano wa kuboresha Sheria ya Utawala wa Mahakama ili kuongeza udhibiti wa nidhamu za Watendaji hao hata ikibidi kuwarejesha kwenye nafasi zao za awali. Hatua hiyo italinda utambulisho wa msingi wa asili ya Mahakama inayozingatia miiko na maadili ya kimahakama *(Judicial Identity).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wakati wa ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilibainika kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu watumishi wengi wa Mahakama hususan Mahakimu kuhamishwa vituo vya kazi na kupandishwa vyeo bila kulipwa stahiki zao kwa wakati; Kamati inaishauri kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhakikisha inatatua changamoto hizo kwa kuwalipa Watumishi wake wote ambao hawajalipwa stahiki zao katika Mahakama mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kamati kuridhishwa na matumizi ya Teknolojia ya *MOLADI* katika ujenzi wa majengo ya Mahakama nchini, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa uwazi *(Transparent and Competitive Bidding Process)* na kwa kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya Wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha miradi ya ujenzi wa Mahakama nchini kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Mahakama kurudia kuezeka Paa la Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga kutokana na kubainika kuwa na dosari zinazosababisha kuvuja kwa baadhi ya sehemu za paa hilo wakati jengo la paa ni jipya. Hatua hiyo itekelezwe haraka ili kutoa athari zinazoweza kujitokeza kwa jengo ambalo limegharimu mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa mtiririko mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha mwaka uliopita wa (2017/2018) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2018/2019); Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Tume ya Utumishi wa Mahakama zihakikishe fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika *(Value for Money).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Kamati inaishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika sekta zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja na kuongeza idadi ya rasilimali watu wa taaluma mbalimbali na kuwajengea uwezo kwa njia ya uanagenzi katika kupitia wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kuongeza weledi na ufanisi wa watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali; kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati ina shauri ofisi hii iwe na rasilimali ya kutosha na iendelezwe ili kuimarisha uwezo wa Wanasheria wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 35, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; kwa kutambua umuhimu wa Ofisi hii, Kamati inashauri kuwepo kwa ushirikiano wa karibu katika kuratibu mfumo mzima wa utoaji haki nchini baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi. Hatua hii itarahisisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii pamoja na kuongeza wigo wa utoaji haki bila kuingilia uhuru wa vyombo vingine vya kiupelelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Ofisi hii ihakikishe inafungua ofisi zake katika mikoa na wilaya zilizoainishwa katika taarifa ya Bajeti kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji haki katika maeneo husika kwa kusogeza huduma stahiki karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 55, Tume za Haki Binadamu na Utawala Bora; kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa watu magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha; Kamati ina shauri Tume ifanye ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko hayo na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 59, Tume ya Kurekebisha Sheria; kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, limefanya maboresho makubwa ya Sheria mbalimbali nchini ikiwemo kutunga sheria mpya zenye kugusa rasilimali za nchi katika sekta mbalimbali nchini; Kamati inaishauri Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na mfumo wa sheria nchini unaozungumza lugha moja yaani *(Uniformity of Laws)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima *(unnecessary Conflict of Laws)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Namba 41, Wizara ya Katiba na Sheria; wakati wa kupokea taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Taasisi za Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, ilibainika kuwepo kwa upungufu wa idadi ya udahili wa wanafunzi wa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Utumishi wa Mahakama imebainisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa Mahakimu wa kutosha wenye kukidhi vigezo vya ajira katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya nchini. Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, kuhakikisha inaboresha Mfumo wa udahili wa wanafunzi ikiwemo kuona uwezekano wa kuanzisha matawi mbadala ya Taasisi hiyo na kuyaratibu kwa lengo la kuongeza wigo wa udahili, ili kupata Wanasheria wa kutosha watakaotosheleza soko la ajira nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, hatua hiyo ihakikishe misingi ya kitaaluma inazingatiwa katika kuhakikisha Taasisi inazalisha Wanasheria wenye sifa stahiki ambao watakuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa hekima na weledi mkubwa katika kuishauri Serikali na manufaa ya wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa weledi na umahiri wake katika kumsaidia Mheshimiwa Spika, kuongoza Bunge hili. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge na kwa kazi nzuri mnayofanya ya kumshauri Mheshimiwa Spika na kumsaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Palamagamba J.A.M Kabudi; Katibu Mkuu Profesa Sifuni Mchome; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu. Amon Mpanju; Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa bajeti hii. Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wa michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Naomba majina yao yote yaingie kama yalivyo katika taarifa rasmi ya Bunge (*hansard).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabisa napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda niwashukuru Wakurugenzi wa Kamati Ndugu. Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu. Angelina L. Sanga; Makatibu wote, Ndugu. Stanslaus Kagisa, Ndugu. Dunford Mpelumbe na Wasaidizi wetu wa Kamati Ndugu. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) Ndugu Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mwenyekiti kwa taarifa yako ya Kamati.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

---

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria.

Aidha, Kanuni ya 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo chini ya Wizara ya Katiba

na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi 2018. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti za Wizara na Taasisi inazozisimamia kuanzia tarehe 23 hadi 29 Machi, 2018 ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ina Mafungu 8 ya bajeti kama ifuatavyo;

i) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
iii) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
iv) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,
v) **Fungu 40** – Mfuko wa Mahakama,
vi) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,
vii) **Fungu 55**- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na
viii) **Fungu 59** –Tume ya Kurekebisha Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-
i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Maelezo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Geita na Wilayani Chato, kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi, 2018. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa

Mahakama nchini inayosimamiwa na Wizara ya Katiba kupitia Mahakama. Taarifa kuhusu yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi pamoja na Ushauri wa Kamati kwa kila mradi ni kama inavyoainishwa katika Jedwali lifuatalo (Jedwali Na.1).

## JEDWALI NA.1: REJESTA YA TAARIFA KUHUSU MIRADI YA UJENZI WA MAHAKAMA ILIYOKAGULIWA NA KAMATI

| Namba na Maelezo ya Mradi | Mamlaka inayotekeleza Mradi | Thamani ya Mradi | Mahali unapotekelezwa | Tarehe ya Kuanza Mradi (As per plan) na Muda tarajiwa wa Mradi | Kiasi cha Pesa kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 | Kiasi kilichotolewa mpaka kufikia wakati wa ziara | Hali ya Mradi wakati wa ziara | Maoni ya Kamati kuhusu hatua ya Mradi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mradi Na.6314** Ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga | Mahakama ya Tanzania **FUNGU 40** | **Bil.4.4** | Manispaa ya Shinyanga | Awamu tatu: 2006/2007, 2011/2012 na 2014-2017 | - | **Bil.4.4** | Ujenzi umekamilika | Utekelezaji wa Mradi ni wa kuridhisha |
| **Mradi Na.6310** Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Geita*(Resident Magistrate Court) kwa teknolojia ya ghrama nafuu ya Moladi* | Mahakama ya Tanzania **FUNGU** 40 | Mil.644.40 | Mkoani Geita | 2017/2018 | Mil.644.40 | Mil.120.04 | Ujenzi wa msingi upo katika hatua za Mwisho | Mkandarasi Asimamiwe ipasavyo ili mradi utekelezwe ndani ya muda uliopangwa |
| ***Mradi Na.6310*** *Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Simiyu(Resident Magistrate Court) kwa teknolojia ya gharama nafuu ya Moladi* | Mahakama ya Tanzania **FUNGU 40** | Mil.644.38 | Mjini Bariadi | 2017/2018 | Mil.644.38 | Mil.198.88 | Ujenzi wa Msingi umekamilika | Mkandarasi Asimamiwe ipasavyo ili mradi utekelezwe ndani ya muda uliopangwa |
| ***Mradi Na.6310*** *Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Chato kwa teknolojia ya gharama nafuu ya Moladi.* | Mahakama ya Tanzania (FUNGU 40 | Mil.644.38 | Wilayani Chato | 2017/2018 | Mil.644.38 | Mil.198.32 | Ujenzi wa Msingi umekamilika | Mkandarasi Asimamiwe ipasavyo ili mradi utekelezwe ndani ya muda uliopangwa |

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukaguzi wa Miradi husika hapo juu, pia Kamati ilipokea taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa chini ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo imetengwa katika makundi manne. Orodha ya Miradi hiyo ni kama ifuatavyo;-

i) **Mradi Na.6310** - Kujenga na Kukarabati Majengo ya Mahakama za Wilaya za Ngorongoro, Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Geita, Bariadi, Bukombe, Chato, Kondoa, Longido, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Lindi, Mpanda, Rungwe, Bunda, Kilindi, Kasulu na Sikonge.

ii) **Mradi Na.6312 -** Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo za Kawe, Karatu, Old Korogwe, Wasso - Loliondo, Totowe, Magoma - Korogwe, Robanda - Serengeti, Itinje - Meatu, Iguguno - Singida, Bareko - Kondoa na kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Mwazo Mvomero - Morogoro.

iii) **Mradi Na.6314**: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo za Mahakama Kuu Kigoma, Mara na kukarabati Mahakama Kuu Sumbawanga.

iv) **Mradi Na.6391:** Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Majaji nchini (Ukarabati wa Makazi ya Jaji Mkuu, Nyumba za kufikia Majaji za Mtwara, Kigoma na Musoma).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya tarehe 19 Machi, 2018, Mahakama imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Majengo Matano(5) kwa ujenzi wa kutumia teknolojia ya gharama nafuu (MOLADI) ambayo ni Mahakama za Wilaya ya Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni, Kinyerezi na Mahakama ya Mwanzo Kawe.

Aidha, Mahakama imekamilisha Miradi mingine Minane (8) ambayo ilikuwa imekwama katika hatua mbalimbali katika kipindi cha nyuma. Miradi hiyo ni Mahakama za Mwanzo Karatu (Arusha), Loliondo (Ngorongoro), Robanda (Serengeti) na Totowe

(Songwe).Ujenzi ulioko katika hatua za mwisho ni pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara na Mahakama za Mwanzo za Magoma (Korogwe) na Itinje (Simiyu).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki. Hata hivyo, Kamati inashauri Mahakama kurudia kuezeka Paa la Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga kutokana na kubainika kuwa na dosari zinazosababisha kuvuja kwa baadhi ya Sehemu za Paa hilo wakati bado Jengo ni jipya na hivyo kuhitaji ukarabati wa haraka. Hatua hiyo itekelezwe haraka ili kuokoa athari zinazoweza kujitokeza kwa Jengo ambalo limegharimu mabilioni ya fedha.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 tarehe 29 na 30 Machi, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Aprili 2017 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi Machi 2018 katika Robo ya

Tatu ya Mwaka huu wa Fedha 2017/2018. Uchambuzi huu pia ulitazama kiasi cha fedha kilichoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kiasi cha Fedha kilichopokelewa katika Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Mwezi Machi 2018. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwelekeo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ili kujua vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa hadi Machi 2018 na lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2017. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake kama kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Themanini na Saba, Laki Tano Saba Elfu na Mia Mbili (24,087,507,200/=).** Hadi kufikia Februari, 2018 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Tisa Sitini na Saba, Laki Nane Arobaini na Moja Elfu, Mia Moja Sitini na Nne (12, 967,841, 164)** sawa na **asilimia 54** ya lengo lililokusudiwa.

### 3.3 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa **Shilingi**

**Bilioni Mia Moja Arobaini na Tatu, Milioni Mia Mbili Arobaini na Tatu na Sabini na Nane Elfu (143, 243, 078,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari 2018 Wizara na Taasisi zake zilipokea **Shilingi Bilioni Themanini na Sita, Milioni Mia Tisa Sabini na Saba, Ishirini na Nane Elfu na Themanini na Tatu (86,977,028,083/=) sawa na asilimia 52%** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** maoni ya Kamati ni kwamba hali hii ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inatakiwa kuendelea na kuzingatiwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ili kurahisisha usimaimizi na Utekelezaji wa Shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi. Kwa hatua hii, Kamati inaipongeza Hazina na Serikali kwa Ujumla kwa kutoa Fedha kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge.

### 3.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018,

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Elfu (23, 236, 830,000/=)** ambapo kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** sawa na **Asilimia 77.46%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa Fedha za Ndani na **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Mbili Thelathini na Sita, Laki Nane Thelathini Elfu (5, 236, 830,000/=),** sawa na **Asilimia 22.54%** ya Bajeti ya Maendeleo zilikuwa fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2018 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Laki Tano Hamsini na Sita Elfu (10,478, 556,000/=) sawa na asilimia 45.%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, kati ya fedha hizo

zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Mbili Sitini na Moja na Tatu Elfu (9,261,003,000/=)** sawa na **asilimia 51%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani.

## 3.5 Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilitegemea kwa kiasi kikubwa fedha za Ndani na Fedha hizo zimepatikana kwa wakati. Aidha, Ujenzi wa Mahakama kwa kutumia teknolojia ya *MOLADI* ni mfumo wa gharama nafuu na unakamilisha ujenzi kwa haraka.

Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuendelea kutumia vyanzo vya ndani katika kutekeleza Miradi mbalimbali nchini ya Wizara ya Katiba na Sheria hususan Miradi ya ujenzi wa Mahakama badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi ambayo haina uhakika.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 tarehe 23 na 24 Machi 2018. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

## 4.1 Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha

2018/2019 umeainisha maeneo zaidi ya Arobaini (40) ya viapumbele kwa Taasisi zote zilizo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya kiwemo;

(v) Kuanza Ujenzi wa Majengo ya Makao Makuu ya Mhimili wa Mahakama ya Tanzania Mjini Dodoma,

(vi) Kukamilisha na kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sheria,

(vii) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa kutenganisha mashtaka na Upelelezi,

(viii) Kuweka Mfumo wa kimkakati wa kusimamia masuala ya utajiri na rasilimali asilia, kuratibu mapitio ya Mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe,

(ix) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Miradi mbalimbali chini ya Wizara na Taasisi zake,

(x) Kujenga na kuboresha Majengo ya Mahakama nchini,

(xi) Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria nchini,

(xii) Kuwajengea uwezo Watumishi kwa lengo la kuendeleza vipaji vyao, kuimarisha weledi na kuongeza tija,

(xiii) Kuimarisha Mfumo wa uandishi na urekebishaji wa Sheria,

(xiv) Kukamirisha na kuboresha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na kufungua Ofisi katika Mikoa na Wilaya zilizoainishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019,

(xv) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi

(xvi) Kuchunguza Malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za Binadamu na ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora nchini,

(xvii) Kufanya mapitio ya Mfumo wa Sheria za Masoko ya Mazao ya Kilimo, Mfumo wa Sheria unaosimamia Ujenzi wa Nyumba Tanzania na Mfumo unaosimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Tanzania

(xviii) Kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Wilaya na Mikoa nchini,

(xix) Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu,

(xx) Kuongeza udahili wa Wanafunzi katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo ili kuongeza idadi ya Wataalam wa Sheria nchini, na

(xxi)Kuimarisha kurugenzi ya Mafunzo Endelevu ya Kimahakama na kuboresha Mitaala ya Stashahada na Astashahada ya Sheria katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2018/2019. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa Taaluma ya Sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Themanini na Saba, Laki Tano Saba Elfu na Mia Mbili (24,087,507, 200/=).** Kiasi hicho ni sawa na Maduhuli yaliyopangwa kukusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Mafungu ambayo yamepanga kukusanya kiasi kikubwa cha Maduhuli kuliko Mafungu mengine, ni pamoja na **Fungu 40**(Mfuko wa Mahakama) ambao upo chini ya Kamati ya Bunge ya Bajeti na **Fungu 41**(Wizara ya Katiba na Sheria) ambayo imepanga kukusanya **Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Saba Hamsini na Tatu, Laki Mbili Tisini na Mbili Elfu (14, 753, 292,000/=)**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2**

**JEDWALI NA.2: Mpango wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 0 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,002,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 13,002,000 |
| 40 | Mfuko wa Mahakama | 12,328,200,862 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 14,753,292,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 0 |
| 59 | Tume ya Kurebisha Sheria | 150,000 |
| **JUMLA KUU** | | **24,087, 507, 200** |

4.3 **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Waziri Mkuu inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Moja Arobaini na Tano, Milioni Mia Saba Ishirini na Sita, Laki Saba Sitini na Tatu Elfu (145, 726,763,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Sabini na Tano, Milioni Mia Mbili Tisini na Nane, Laki Moja Thelathini na Saba Elfu (75,298,137,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Sabini, Milioni Mia Nne Ishirini na Nane, Laki Sita Ishirini na Sita Elfu(70,428,626,000/=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ni kama inavyoainishwa katika **Jedwali Na.3.**

**Jedwali Na.3: Kiasi cha Fedha kinachoombwa kwa Mafungu ya Bajeti yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MAOMBI YA FEDHA |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,097,343,000 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 8,964,382,000 |
| 19 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 4,171,217,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 15,955,105,000 |
| 40 | **Mfuko wa Mahakama (Kamati ya Bajeti)** | **141,584,739,000** |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 11,105,747,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 5,636,870,000 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 1,978,579,000 |
| **JUMLA KUU** | | **190,493,982,000** |

4.4 **Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zimeombewa **Shilingi Bilioni Arobaini na Tano, Milioni Kumi na Tano, Laki Tano Themanini na Mbili Elfu (45,015, 582,000/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Kumi na Nane (18,000,000,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Kumi na Tano, Laki Tano Themanini na Mbili Elfu(27,015,582,000/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Fedha za Miradi ya Maendeleo imeongezeka zaidi ya **Shilingi Bilioni 21** ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ongezeko ambalo ni sawa na **asilimia 91%** ya Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kubaini ongezeko la Bajeti ya Maendeleo hatua ambayo

inapongezwa, bado kiasi cha Fedha za Nje ni kikubwa ukilinganisha na bajeti ya ndani. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kupunguza utegemezi wa Fedha za Nje katika kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa kuwa upatikanaji wake unaweza usiwe wa uhakika na hivyo inaweza kukwamisha utekelezaji wa Miradi husika kwa wakati.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake. Aidha, Maoni na Ushauri wa Kamati umezingatia pia Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

### 5.1 FUNGU 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

i) **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Mahakama ni Chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Utawala wa Mahakama ya mwaka 2011. Jukumu la chombo hicho cha kiutawala ni kusimamia Mahakama ya Tanzania kama muhimili wa Serikali ambao umekuwa ukitekeleza kazi zake kwa uhuru na haki bila kuingiliwa na Chombo au taasisi nyingine yoyote kama ambavyo imetamkwa chini ya Ibara ya 107A na 107B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na malalamiko ya muda mrefu kuhusu changamoto mbalimbali katika usimamizi wa masuala mbalimbali ya kiutawala katika Mahakama, Serikali ilichukua hatua ya kufanya maboresho yaliyoanzisha Kada ya Watendaji wa Mahakama ambao wengi wao walikuwa Makatibu Tawala wa Wilaya na Mikoa, kwa lengo la kuisaidia Mahakama kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki kwa uhuru na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** kwakuwa Kamati imebaini kuwa Watendaji hao wa Mahakama wameshindwa kuisaidia

Mahakama kutatua kero zake, na kwakuwa imebainika kuwa Watendaji hao wamekuwa wakitumia nafasi zao vibaya kwa kutumia hata lugha zisizoridhisha, kujiingiza kwenye Maamuzi ya kesi wakati wao siyo Mahakimu wala Majaji, pia kuwanyanyasa Mahakimu na baadhi ya Majaji na hivyo kuathiri nia njema ya Serikali ya kuhakikisha Mahakama zinatumia rasilimali zilizopo katika kurahisisha utoaji haki kwa wakati,

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, Serikali ione uwezekano wa kuiboresha Sheria ya Utawala wa Mahakama ili kuongeza udhibiti wa nidhamu za Watendaji hao hata ikibidi kuwarejesha kwenye nafasi zao za awali. Hatua hiyo italinda utambulisho na misingi ya asili ya Mahakama inayozingatia miiko na maadili ya kimahakama *(Judicial Identity).*

ii) **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wakati wa ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilibainika kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu Watumishi wengi wa Mahakama hususan Mahakimu kuhamishwa vituo vya kazi na kupandishwa vyeo bila kulipwa stahiki zao kwa wakati, Kamati inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhakikisha inatatua changamoto hiyo kwa kuwalipa Watumishi wake wote ambao hawajalipwa stahiki zao katika Mahakama mbalimbali nchini.

iii) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na matumizi ya Teknolojia ya *MOLADI* katika ujenzi wa majengo ya Mahakama nchini, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Zabuni za ujenzi wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kwa uwazi *(Transparent and Competitive Bidding Process)* na kipaumbele kitolewe kwa Makampuni ya Ndani ya Wakandarasi yaliyokidhi vigezo na yenye uwezo wa kutekeleza na kukamilisha Miradi ya ujenzi wa Mahakama nchini kwa wakati na kwa mujibu wa Mikataba ya Miradi husika.

iv) **Mheshimiwa spika**, Kamati inashauri Mahakama kurudia kuezeka Paa la Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga

kutokana na kubainika kuwa na dosari zinazosababisha kuvuja kwa baadhi ya Sehemu za Paa hilo wakati Jengo hilo bado ni jipya. Hatua hiyo itekelezwe haraka ili kuokoa athari zinazoweza kujitokeza kwa Jengo ambalo limegharimu Mabilioni ya fedha.

v) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa mtiririko mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa Fedha za Miradi yote ya Maendeleo iliyotengewa fedha Mwaka uliopita wa (2017/2018) na ile iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha ujao (2018/2019), Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Tume ya Utumishi wa Mahakama zihakikishe fedha zote za Miradi ya Maendeleo zinatumika kwa tija na kwa kuzingatia Kanuni ya thamani ya fedha kwa miradi husika *(Value For Money).*

## 5.2 Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote nchini.

Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali na kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kupitia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi wa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

## 5.3 Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati ina shauri Ofisi hii iwe na rasilimali ya kutosha na iendelezwe ili kuimarisha uwezo wa Wanasheria wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai kwa maslai ya nchi.

5.4 **Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

i) **Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua umuhimu wa Ofisi hii, Kamati inashauri kuwepo kwa ushirikiano wa karibu katika kuratibu Mfumo mzima wa utoaji haki nchini baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi. Hatua hii itarahisisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii pamoja na kuongeza uwigo wa utoaji haki bila kuingilia uhuru wa vyombo vingine vya kiupelelezi.

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Ofisi hii ihakikishe inafungua Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya zilizoainishwa katika taarifa ya Bajeti kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji haki katika maeneo husika kwa kusogeza huduma stahiki karibu na Wananchi.

5.5 **FUNGU 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu, ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa Watu magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha, Kamati ina shauri Tume ifanye ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko hayo na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

5.6 **FUNGU 59 -Tume ya Kurekebisha Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 Serikali kupitia Bunge lako Tukufu, imefanya maboresho makubwa ya Sheria mbalimbali nchini ikiwemo kutunga Sheria mpya zenye kugusa rasilimali za nchi katika Sekta mbalimbali nchini, Kamati inaishauri Tume ya kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mfumo wa Sheria nchini unaozungumza lugha moja *(Uniformity of Law)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima *(unnecessary Conflict of Law)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji.

## 5.7 FUNGU 41-Wizara ya Katiba na Sheria

**Mheshmiwa Spika,** wakati wa kupokea taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, ilibainika kuwepo na upungufu wa idadi ya udahili wa Wanafunzi wa mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa ya Tume ya Utumishi wa Mahakama imebainisha kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa Mahakimu wa kutosha wenye kukidhi vigezo vya ajira katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya nchini. Kamati inashauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, kuhakikisha inaboresha Mfumo wa udahili wa Wanafunzi ikiwemo kuona uwezekano wa kuanzisha matawi mbadala ya Taasisi hiyo na kuyaratibu kwa lengo la kuongeza uwigo wa udahili, ili kupata Wanasheria wa kutosha watakao tosheleza Soko la Ajira nchini.

Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, hatua hiyo ihakikishe misingi ya kitaaluma inazingatiwa katika kuhakikisha Taasisi inazalisha Wanasheria wenye sifa stahiki ambao watakuwa na tija kwa Taifa.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria. Napenda nikupongeze pia kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa Hekima na Weledi Mkubwa katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Prof. Palamagamba J.A.M Kabudi, (Mb), Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano waliotoa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

**NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb – M**akamu /Mwenyekiti**
3. Mhe. George Simbachawene, Mb - Mjumbe;
4. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
5. Mhe. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
13. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
14. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
15. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;
16. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi,Mb-Mjumbe;
18. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;

22. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
23. Mhe. Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mb – Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina L. Sanga, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, Ndg. Dunford Mpelumbe na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) Ndg. Hanifa Masaninga na Watendaji wote wa Idara hiyo kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**
18 APRILI, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa niaba yake Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha pamoja na Wajumbe wangu kuja mbele hapa kusoma taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti wa Mfuko wa Mahakama wa Mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi; kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mfuko wa Mahakama mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji waBajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019. Mashauriano hayo yamefanyika kwa mujibu wa kifungu cha 75 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka 2017/2018; kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jukumu kubwa la Mahakama ni kusimamia utoaji wa haki. Katika kutekeleza jukumu hili Mahakama imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha kusikiliza mashauri 264,035 kati ya mashauri 329,699 yaliyokuwepo Mahakamani kwa mwaka 2017 na hivyo kubakiza mashauri 65,634;

(b) Kukamilisha ukarabati mkubwa wa Mahakama Kuu ya Mbeya na Ujenzi wa Mahakama tano za Wilaya ya Bagamoyo, Kigamboni, Mkuranga, Ilala na Mahakama ya Mwanzo Kawe;

(c) Imeendelea kuimarisha mfumo wa ukusanyaji maduhuli ya Serikali, hadi kufikia mwezi Februari imekusanya kiasi cha Shilingi bilioni 7.172, sawa na asilimia 115 ya lengo;

(d) Imekamilisha ujenzi wa majengo yaliyokwama ya Mahakama za Mwanzo za Karatu, Iguguno-Singida, Loliondo-Ngorongoro, Bereko-Kondoa, Totowe-Songwe, Old Korogwe-Korogwe, Magoma-Korogwe, Mvomero-Morogoro, Itinje-Simiyu na Robanda-Serengeti;

(e) Inategemea kuanza mradi wa ujenzi wa Mahakama Kuu saba katika Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Arusha, Dodoma, Singida, Temeke na Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Mahakama inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2017/2018:-

(i) Upungufu mkubwa wa watumishi hususan Majaji, Mahakimu, Makarani na Wachapaji;

(ii) Taasisi zinazosimamia upimaji na ugawaji wa ardhi kutotenga maeneo ya viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama katika wilaya na mikoa mbalimbali nchini;

(iii) Bajeti ndogo ya Mfuko wa Mahakama isiyolingana na mahitaji halisi;

(iv) Uchakavu wa miundombinu ya Mahakama hasa katika ngazi za Wilaya na Mahakama za Mwanzo;

(v) Uhaba wa vitendea kazi kama vile kompyuta na magari kwa ajili ya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018; Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mfuko wa Mahakama Fungu 40 uliidhinishiwa jumla ya kiasi cha Sh.125,117,029,000. Kati ya fedha hizo Sh.54,524,408,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama na Sh.1,953,228,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama-Lushoto, Sh.50,481,382,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.18,158,011,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari 2018 jumla ya Sh.57,801,439,123 zilipokelewa ambazo ni sawa na asilimia 62.18 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo Sh.33,295,185,549 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.33,629,895,549 ni kwa ajili ya mishahara na Sh.9,937,014,000 ni fedha za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 54.22 ya bajeti ya maendeleo iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa Sh.1,158,011,000 zilikuwa fedha za nje sawa na asilimia 100 iliyotengwa ya Bajeti na Sh.8,779,003,000 zilikuwa fedha za ndani sawa na asilimia 51.6 ya bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2017/2018, ulipanga kukusanya maduhuli ya Sh.9,318,061,200 na hadi kufikia mwezi Februari, 2018 kiasi kilichokuwa kimekusanywa kilifikia Sh.7,172,570,000 ikiwa sawa na asilimia 77 ya malengo ya mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa Matumizi ya Kawaida; Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya Sh.141,584,738,222. Kati ya fedha hizo; Sh.54,629,635,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Sh.50,481,382,000 ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo *yaani*

*OC* na Sh.35,973,721,700 ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho Sh.15,000,000,000 ni fedha za ndani na Sh.20,973,721,700 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha zinazoombwa mwaka 2018/2019 ikilinganishwa na zilizopitishwa mwaka 2017/2018, Matumizi Mengineyo yameongezeka kwa asilimia 1 tu na fedha za maendeleo zimeongezeka kwa asilimia 98 wakati bajeti ya mishahara imepungua kwa asilimia 3.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja ya kwamba Mfuko huu umepewa kiasi hiki cha fedha, Kamati inaona kuwa Ukomo wa Bajeti unaotolewa na Serikali kwa Mfuko wa Mahakama unaweza kusababisha baadhi ya majukumu ya msingi ya Mahakama kushindwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Mathalani, kushindwa kulipa posho za Wazee wa Baraza, gharama za mashahidi, kushindwa kulipa gharama za kuunganisha Mahakama zote za Mikoa na Wilaya kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pamoja na kushindwa kuanzishwa kwa Mahakama katika Wilaya zisizokuwa na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha Sh.12,328,200,862 ikiwa ni ongezeko la Sh.3,010,139,662 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.9,318,061,200 mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba kama ifuatavyo:-

(a) Kuendelea kutoa hukumu ya haki sawa kwa wote na kwa wakati;

(b) Kuendelea kusikiliza mashauri na kuondoa mlundikano wa kesi mbalimbali;

(c) Kulipa gharama za mashahidi, posho za Wazee wa Baraza, posho za Mahakimu na pango kwa ajili ya Majaji;

(d) Kuimarisha uongozi, utawala bora na uwajibikaji kwa Mahakama pamoja na kuongeza upatikanaji wa haraka wa huduma za Mahakama kwa wananchi;

(e) Kuimarisha ufanisi katika kazi za Mahakama kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano yaani TEHAMA pamoja na kukusanya maduhuli kwa njia ya kieletroniki;

(f) Kuongeza mahusiano baina ya wadau wa nje na ndani ya Mahakama. Yote hayo yako katika jedwali namba moja (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati, kwa kuwa bajeti iliyotolewa kwa mwaka 2017/2018 haikukidhi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama na kwa kuwa, ufinyu huo wa kibajeti umepelekea Mfuko huu kukabiliwa na madeni mbalimbali yakiwemo madeni ya gharama za mashahidi, posho za Wazee wa Baraza, malipo ya pango la nyumba za kuishi Majaji, uanzishwaji wa Mahakama katika Wilaya zisizokuwa na Mahakama pamoja na madai mbalimbali ya watumishi; hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza bajeti ya Mfuko huu kulingana na mahitaji yaliyopo pamoja na kupeleka kiasi cha fedha kilichobakia kwa matumizi mengineyo pamoja na fedha za miradi ya maendeleo ili Mfuko huu uweze kulipa baadhi ya madeni hayo pamoja na kuanza ujenzi wa Mahakama katika Wilaya zisizokuwa na Mahakama;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa, ukomo uliotolewa wa Mfuko kwa mwaka 2018/2019 umeonesha kutohakisi mahitaji halisi ya Mfuko wa Mahakama na kwa kuwa, Waziri ameahidi Kamati kuwa baada ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti kwa Nusu Mwaka *yaani mid-year review* ya mwaka 2018/2019 na ikibainika kuwa kuna upungufu wa fedha, basi itakuwa tayari kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Mahakama kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kuwa fedha za Mfuko wa Mahakama

zinatolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya Mfuko kwa kuzingatia maeneo yote ya vipaumbele vya Mfuko kama yalivyopendekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile na kwa kuwa, moja ya vipaumbele vya Mfuko wa Mahakama ni kukusanya maduhuli kwa urahisi na kwa ufanisi kwa kutumia njia ya kielektroniki na kwa kuwa, taratibu za kuwezesha mifumo husika bado haujakamilika; Kamati inashauri taratibu za ndani za Serikali zifanyike kwa ajili ya kuiwezesha Mahakama kuwa na vifaa vya kuwezesha ukusanyaji wa maduhuli kwa njia ya kielektroniki yaani *a point of sale machines (POS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Mfuko wa Mahakama unategemea kuanzishwa na kujenga Mahakama katika maeneo ya wilaya mpya sambamba na ujenzi wa Mahakama katika Wilaya zisizokuwa na mahakama hizo; Kamati inashauri ujenzi huu utaleta tija kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama ikiwa ni pamoja ya kuwasogezea wananchi huduma karibu. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali ukomo wa fedha unaotolewa na Hazina uwe unazingatia hali halisi ya mahitaji ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali hususani Majaji, Mahakimu, Makarani na Wachapaji na kwa kuwa, Mahakama bado inaendelea na ujenzi wa Mahakama katika maeneo mbalimbali ambapo baada ya ukamilishaji ni lazima kutakuwa na uhitaji mkubwa wa watumishi mbalimbali wakiwemo hawa wenye kada husika; hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwenye kada mbalimbali kama zilivyoainishwa kwa awamu ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mahakama. Hatua hii iende sambamba na utolewaji wa fedha kwa ajili ya stahiki za kuhudumia watumishi wapya;

Mheshimiwa Mwenyekti, Kamati pia inashauri Mfuko wa Mahakama unategemea kuongeza ukusanyaji wa maduhuli katika utekelezaji wa shughuli zake, hivyo,

makusanyo ya mapato haya yanapelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama Sheria inavyotaka. Basi, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ianzishe utaratibu wa kununua na kugawa kwa Mahakama vifaa vya kieletroniki ili kurahisisha ukusanyaji wa maduhuli kwa njia ya kieletroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna uchakavu na uhaba wa miundombinu katika ngazi za Mahakama za Mwanzo na Wilaya, pia kuna mahitaji ya ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa 12, Mahakama za Hakimu Mkazi Mikoa 13 na Mahakama za Wilaya katika Wilaya 99 na Mahakama za Mwanzo ambapo kwa sasa zipo 960 ikilinganishwa na idadi ya kata 4,420 zilizopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa, Mahakama zilizopo hazina vitendea kazi kama vile kompyuta na magari na kusababisha utendaji wa kazi kuwa changamoto; hivyo basi, Serikali ihakikishe inasimamia upatikanaji miundombinu kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Mahakama katika ngazi za Wilaya na Mwanzo pamoja na ununuzi wa kompyuta na magari kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, Serikali ihakikishe inatoa fedha kwa awamu kwa kuzingatia bajeti ilivyopitishwa hapa Bungeni na tutakavyopitisha makadirio ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, naomba nimshukuru kabisa kwanza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Pia namshukuru Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango; na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao mkubwa katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu

Bajeti ya Mfuko wa Mahakama na naomba wote watambuliwe na majina yao yaingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Lina Kitosi na Makatibu wa Kamati Ndg. Michael Kadebe, Ndugu Godfrey Godwin, Ndugu Emmanuel Rhobi, Ndugu Lilian Masabala na Ndugu Maombi Kakozi na Msaidizi wa Kamati Ndugu Imelda Ntimba kwa umakini wao kwa kuihudumia vema na kuipa ushauri wa kitaalam Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama, Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa taarifa yenu.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Sera, Bunge, kazi, Vijana, Ajira na Walemavu pamoja na Katibu wa Bunge na kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/19. Mashauriano haya yamefanyika kwa mujibu kifungu cha 71 (b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mapitio ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Bunge hadi kufikia Machi 15, 2018 ya mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi yanayojumuisha vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2018/ 2019.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 Mfuko wa Bunge –Fungu 42 uliidhinishiwa kiasi cha **Sh. 121,652,262,000.00**. Kati ya fedha hizo **Sh.24,454,715,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), **Sh.89,997,547,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo (OC) na **Sh. 7,200,000,000.00** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo **Sh.7,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh. 200,000,000.00** ni fedha za nje.

### *2.1 Matumizi ya Kawaida*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2017/2018 (Cash Flow and Action Plan), Mfuko wa Bunge ulipanga kutumia fedha za Matumizi ya Kawaida kiasi cha **Sh.80,317,810,250.00** hadi kufikia Machi 31, 2018. Kati ya fedha hizo kiasi cha **Sh.18,341,036,250** ni Mishahara na **Sh.61,976,774,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi kufikia Machi 15, 2018 Ofisi ya Bunge ilikuwa imepokea fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha **Sh.81,479,720,100.09.** Kati ya fedha hizo **Sh.64,739,612,000.09** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na

**Sh.16,740,080,100.00** kwa ajili ya Mishahara (PE). Hivyo, fedha za matumizi mengineyo (OC) iliyopokelewa ni sawa na **asilimia 104.4** wakati fedha za mishahara ni sawa na **asilimia 91.2** ya fedha zilizopangwa kutumika hadi Machi 31, 2018.

### *2.2 Matumizi ya Fedha za Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Mpango Kazi na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2017/18; Mfuko wa Bunge ulipanga kutumia fedha za Maendeleo kiasi cha **Sh.6,885,000,000** hadi kufikia Machi 31, 2018. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 15 Machi 2018, Mfuko umepokea kiasi cha **Sh.115,980,000** ambazo ni sawa na asilimia **2** ya fedha zote ziliyopangwa kutumika katika kipindi cha Robo ya Tatu. Aidha, fedha hizo za nje ni kwa ajili ya kutekelezaji wa shughuli za Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP). Mfuko haujapokea fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Bunge, usimikaji wa Studio ya Bunge, ujenzi wa lifti katika jengo la utawala na ununuzi za mtambo wa kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge.

### *2.3 Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, Mfuko wa Bunge ulipanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh.42,500,000** Makusanyo hayo yalipangwa kutokana na marejesho ya masurufu (Recovery of Public Money) na malipo ya kodi ya Pango. Hadi kufikia Machi 15, 2018, Ofisi ya Bunge ilikuwa imekusanya kiasi cha **Sh.15,720,000** ambacho ni sawa na asilimia **36.9** ya bajeti ya maduhuli iliyoidhinishwa.**3.0**

### UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Bunge kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa Mwaka huu wa Fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika mwaka huu wa Fedha 2017/18; Ofisi ya Bunge itajitahidi kufikia malengo yake kwa usahihi na kwa wakati. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Ofisi ya bunge ilitekeleza majukumu yafuatayo;

8.4 ***3.1 Uratibu wa shughuli za Kamati za Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018.***

Mfuko wa Bunge, Fungu 42, uligharamia uratibu wa shughuli za Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati za Kisekta kwa ajili ya kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha, 2017/2018;
(b) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati Mbili (2) za kusimamia matumizi ya fedha za Umma kwa ajili ya kufuatilia thamani halisi ya matumizi ya fedha za Umma katika Maeneo mbalimbali;
(c) Kuwezesha na kuratibu ziara za Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kufuatilia miradi ya uwekezaji inayotekelezwa kwa mitaji ya umma;
(d) Kuwezesha na kuratibu utayarishaji na uwasilishaji wa Taarifa za Mwaka za Shughuli za Kamati Kumi na Sita (16);
(e) Kuwezesha na kuratibu vikao vya wiki mbili (2) kabla ya Mkutano wa nane, Mkutano wa Tisa na Mkutano wa Kumi vya Kamati Kumi na Saba za Bunge;

Aidha, Mfuko wa Bunge uliwezesha Uratibu wa Shughuli za Kamati Maalum zifuatazo:-

(a) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi na Udhibiti wa Madini ya Tanzanite;
(b) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Uchimbaji, Usimamizi na Umiliki wa Udhibiti wa Madini ya Almasi Nchini;
(c) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu Mfumo wa Usimamizi na Udhibiti wa shughuli za Uvuvi katika Bahari Kuu; na
(d) Kamati Maalum ya Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na Mapato yatokanayo na Sekta Ndogo ya Gesi.

8.5 ***3.2 Uratibu wa Shughuli za Mikutano Midogo Mitatu ya Bunge hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018.***

Mfuko wa Bunge, Fungu – 42 umefanikisha Mikutano Midogo Mitatu ya Bunge kwa ufanisi ambapo mambo mbalimbali yamefanyika kama ifuatavyo:-

(a) Wabunge Kumi na Mbili (12) waliapa kiapo cha Uaminifu;
(b) Taarifa za Mwaka za Taasisi/Mashirika manne (4) ziliwasilishwa Bungeni;

(c) Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake Arobaini na Nne (44) yaliwasilishwa Bungeni;
(d) Maswali ya kawaida Mia Tatu Themanini na Tatu (383) yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali;
(e) Waziri Mkuu aliweza kujibu maswali kumi na sita (16) ya papo kwa papo kutoka kwa Wabunge katika kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu;
(f) Bunge lilikaa kama Kamati ya Mipango kwa ajili ya kupokea, kujadili na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na mwongozo wa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2018/2019;
(g) Miswada Kumi na Nne (14) ilipokelewa na Katibu wa Bunge ambapo yote ilisomwa kwa hatua zote na kupitishwa na Bunge;
(h) Maazimio manne (4) yaliridhiwa na Bunge;
(i) Kauli Moja (1) ya Waziri ilitolewa Bungeni;
(j) Hoja za Kamati za Bunge (15) zilijadiliwa na kupitishwa Bungeni;
(k) Mbunge mmoja (1) alitoa maelezo binafsi;
(l) Jumla ya machapisho 20,412 yalichapishwa ambapo kati ya hayo vitabu vya Taarifa Rasmi (426), Taarifa za Kamati za Bunge (10,000), Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (6,750), Sheria za Kusaini Mhe. Rais (84), Machapisho mbalimbali (2,827), Kamati Maalum ya Bunge ya Ushauri kuhusu mfumo wa Udhibiti wa Shughuli za Bahari Kuu Nchini (95), Taarifa Rasmi ya Kamati Maalum ya Bunge ya Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na mapato yatokanayo na sekta ndogo ya Gesi (80) na Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa za Kamati Kumi na Sita za Kudumu za Bunge (150).

### *3.3 Kuwezesha ushiriki wa Bunge katika Mikutano ya Kimataifa*

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Mfuko wa Bunge umewezesha Wabunge kushiriki kwenye michezo ya

michuano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Dar es Salaam. Aidha, Viongozi wa Bunge na Wabunge wanaoliwakilisha Bunge la Tanzania kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge letu ni mwanachama waliweza kushiriki kwenye mikutano hiyo kama ifuatayo
(a) Bunge la Afrika (PAP);
(b) Umoja wa Wabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA), Kanda ya Afrika, *CPA- International;*
*(c) Africa Caribbean Pacific and European Union (ACP/EU);*
(d) Jukwaa la Kibunge la Jumuiya ya Maedeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC- PF);
(e) Bunge la Afrika Mashariki na
(f) Umoja wa Mabunge Duniani ( IPU).
(g) Mkutano wa Shirikisho la Wabunge Duniani (Global Parliamentarian Conference) pamoja na Mkutano wa Mwaka wa Benki ya Dunia (World Bank) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)

### *3.4 Kutoa Elimu kwa Umma kuhusiana na masuala ya Kibunge*

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2018, Mfuko wa Bunge umeweza kutoa elimu kwa Umma kuhusu Bunge kwa njia ya:
(a) Kuelimisha wageni mbalimbali wanaolitembelea Bunge pamoja na kufanya ziara katika Mikoa ya Mbeya, Tanga na Mara; na
(b) Kushiriki kwenye maonesho ya Saba Saba na Nane Nane ya Kitaifa.

## 4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA BUNGE KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

### 4.1 Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2018/2019 Mfuko wa Bunge umepanga kutumia kiasi cha **Sh.125,521,100,000.00** Kati ya fedha hizo kiasi cha **Sh.24,441,023,000.00** ni fedha za Mishahara; **Sh.92,764,464,000.00** ni fedha za Matumizi mengineyo na **Sh.8,315,613,000.00** ni fedha za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika fedha za Maendeleo, kiasi cha **Sh.5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Sh.3,315,613,000.00** ni fedha za nje ambapo kiasi cha **Sh. 3,015,613,000.00** ni kwa ajili ya Mpango wa Kuliwezesha Bunge (*Legislative Support Program)* ambao umekuwa ukiwajengea uwezo Waheshimiwa Wabunge kupiti Semina na Mafunzo mbalimbali. Na kiasi cha **Sh. 300,000,000.00** kimetengwa kwa Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma (*Public Finance Reform Program)* kwa ajili ya kujenga mifumo bora ya takwimu zinazotumika na Bunge zinazohusu Bajeti na Uchumi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/19 Ofisi ya Bunge inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 61,000,000.00.**

**4.2 Shughuli zitakazotekelezwa Katika Mwaka wa Fedha 2018/19**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa Fedha 2018/ 19, fedha zilizokasimiwa zimetengwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linatekeleza majukumu yake ya Kikatiba. Baadhi ya majukumu ambayo yamepangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2018/19 ni kama yafuatayo:

(a) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mkutano wa Bajeti na Mikutano Midogo Mitatu (3) ya Bunge;
(b) Kuratibu na kusimamia shughuli za Mikutano Minne (4) ya Kamati za Kudumu za Bunge;
(c) Kuratibu na kuchapisha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard);
(d) Kutoa ushauri wa kisheria kwa Wabunge na uchambuzi wa miswada;
(e) Kutoa huduma za Utafiti "Information Research" kwa Wabunge;
(f) Kuwezesha Wabunge kushiriki kwenye Mikutano ya Kimataifa ambayo Bunge ni Mwanachama.
(g) Kuandaa vipindi vya Televisheni na kurusha matangazo ya Bunge;

(h) Kuratibu shughuli mbalimbali za utawala (huduma kwa Wabunge, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya maji, umeme na simu, usafi na ulinzi);
(i) Kuwajengea Wabunge uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kikatiba kupitia Mpango wa Kuliwezesha Bunge;
(j) Kuratibu na Kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

- Ukarabati na ununuzi wa mitambo ya usalama;
- Kusimika Kituo cha Matangazo ya Bunge *(Broadcasting Studio)* katika Ukumbi wa Bunge
- Ujenzi wa Makazi ya Viongozi wa Bunge - Dodoma; na
- Ukarabati wa Ukumbi wa Msekwa, Ukumbi wa Bunge pamoja na majengo ya Ofisi ya Bunge;

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**5.1** **Kwa kuwa**, mara kadhaa kumeibuka umuhimu wa kuteuliwa kwa Kamati Maalum ili kushughulikia mambo muhimu yenye maslahi ya Kitaifa, na kwa kuwa mara zote Kamati hizo Maalum huwa hazikutengewa Bajeti yake kwa mwaka wa fedha husika hivyo kuathiri Bajeti ya Ofisi;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inarejesha mapema fedha ambazo zitatumika kutoka katika Bajeti ya Mfuko wa Bunge endapo yataibuka masuala muhimu zikiwemo Kamati Maalumu ili kutoathiri Bajeti ya Mfuko kwa Mwaka husika.

## 7.0 HITIMISHO.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge,

Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu) kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Bunge. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2) Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb - Makamu Mwenyekiti
3) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
4) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
5) Mhe. Abdallah Majura Bulembo, Mb
6) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
7) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
8) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
9) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
10) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11) Mhe. Hasna Sadi Kalunda Mwilima, Mb
12) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
13) Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb
14) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
15) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
16) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
17) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
18) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
19) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
20) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
21) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
22) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha napenda kuipongeza na kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa ushauri wa kitaalamu ambao wamekuwa wakiipa Kamati ambao uwezesha kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Bunge – Fungu 42, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.



Hawa A. Ghasia, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**
04 APRILI, 2018

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda ndiyo huo, mkipenda nitoe hoja tuongeze muda, msipopenda turudi saa 11:00 lakini achangie mmoja kwa dakika tano. Mheshimiwa Mbarouk, hayupo. Mheshimiwa Kombo.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia dakika tano hizi na naomba niseme machache. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kupata muda huu wa dakika chache na nianze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 133 na Ibara ya 134, inazungumzia uwepo wa Tume ya Fedha ya Pamoja na Akaunti ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hii ilianzishwa mwaka 1996 na ilizinduliwa rasmi mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie je, Tume hii ipo na kama ipo inafanya

kazi gani? Naomba hili suala liwekwe sawa, kwa sababu uwepo wa Kamati ya Pamoja ya Fedha na Tume ya Pamoja ya Fedha au Akaunti ya Pamoja ya Fedha bila shaka ingetufanya sisi Watanzania tukawa na mgawanyo sahihi wa mapato ya Muungano na Tume hii ingetusaidia sisi kuondoa na ikawa ndiyo kimbilio la kuondoa changamoto zote zinazogusa maslahi ya pande mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu Tume hii haipo ingawa imezungumzwa kwenye Katiba, ni suala la Kikatiba, lakini kwa sababu haipo na haijaundwa tunaamini kwamba kero za Muungano ambazo tokea juzi zimekuwa zikitawala kwenye Wizara hizi mbili za Katiba na Sheria na Wizara inayoshughulikia mambo ya Muungano zitaendelea kuwepo na haziwezi kutatuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujui ni sababu zipi ambazo au kuna changamoto zipi ambazo zimepelekea Tume hii ya Pamoja ya Fedha mpaka leo iwe haipo na haijaanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo naomba nilizungumze ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya nne (4) ambayo imezungumzia mamlaka mbili za Serikali ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Katiba imezungumzia Mamlaka mbili za Mahakama; Mahakama ya Tanzania Bara au Mahakama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini imezungumzia Mahakama ya Zanzibar ambazo Taasisi hizi mbili zote zina mamlaka sawa ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatekeleza matakwa na masuala yanayohusu Muungano na Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatakiwa isimamie masuala yanayohusu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kumekua na mwingiliano mkubwa wa utekelezaji wa majukumu haya.

Mhesimiwa Mwenyekiti, ambacho nataka kukisema hapa kwamba tumekuwa tukizungumzia malalamiko mengi na masuala mengi yanayohusu utekelezwaji wa Mamlaka hizi mbili kwamba kumekuwa na mwingiliano na kumekuwa na kutokuaminiana katika utekelezaji wa majukumu. Tunachokizungumza hapa ni kwamba, Wizara ituweke wazi na akija Mheshimiwa Waziri atuweke wazi juu ya Mamlaka hizi mbili zinatendaje majukumu yake.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kubwa, Zanzibar imekuwa ikipigania mara nyingi kujiunga na Taasisi ambazo ingeruhusiwa kujiunga, lakini Mamlaka moja imekuwa ikichukua fursa ya kuiamuru Mamlaka nyingine kwamba hamna haki ya kujiunga na Taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishirikiana katika masuala pengine ya Zanzibar kujiunga na *FIFA,* Zanzibar kujiunga na *CAF,* lakini tumeambiwa au tunaelezwa kwamba tunashirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili Zanzibar ijiunge na vyombo .

Mheshimiwa Mwenyekiti, masikitiko makubwa ni pale Zanzibar ilipokuja kuruhusiwa kujiunga na *OIC* kwa nini iliambiwa ijitoe? Halafu leo tunajikomba tunakuja kusema kwamba tunaisaidia Zanzibar ili ijiunge na *FIFA*, ili ijiunge na *CAF* huu si uongo kweli? *Huu si unafiki kweli?* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunapigania kujiunga na vyombo hivi kwa nini leo tusiiruhusu Zanzibar kwa sababu ina uwezo wa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo nakuheshimu sana na mchango wako nauheshimu. Hebu nisaidie neno "unafiki" maana unalielekeza kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, nakuomba kabisa futa hiyo kauli yako, futa tu, halafu uchangie.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Nafuta.

**MWENYEKITI:** Ahsante, endelea.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naomba nizungumze, nalielekeza kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Kila siku tumekuwa tukilalamika kuna kesi zimechukua muda mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale Masheikh wa Uamsho na wale Masheikh waliokamatwa katika Mji wa Arusha, tunaomba kama Ofisi hii ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeshindwa kupeleka ushahidi wale ni Watanzania, wale ni Wazanzibari tunaumia na lazima tuwasemee kwa sababu hawana mtu wa kuwasemea, lazima tutasimama Bungeni, tutaendelea kusema, tutaendelea kupiga kelele. Kama Serikali kupitia Ofisi hii imeshindwa kuthibitisha kwamba wale watu wana hatia basi waachiwe huru waende kwenye familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na Tume ya Haki za Binadamu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako ndiyo huo nilitaka umalizie sentensi, si umemaliza, muda ndiyo huo dakika tano, ahsante.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni maana mlikataa hoja ya kuongeza muda. Nawajueni nyie, wapi, msibishane na mimi sasa. Watakaoanza na sisi mchana atakuwa ni Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafsi hii ili niweze kuchangia katika Wizara ya Katiba na Sheria. Katika kuchangia Wizara hii ya Katiba na Sheria, naomba kuchangia kuhusiana na masuala ya utoaji haki kwenye Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi yalianzishwa kwa sheria ya mwaka 2002 Sura ya 114, lakini Mabaraza haya ya Ardhi yalianzishwa ili kuweza kusaidia kutatua migogoro mingi ambayo inajitokeza katika umiliki wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza haya yamekuwa yakikumbwa na changamoto mbalimbali. Changamoto mojawapo ni kwamba Wenyeviti wa Mabaraza haya ya Ardhi hawana uelewa wa kutosha kwa upande wa kisheria na hivyo kushindwa kuitatua vizuri migogoro ya ardhi na kusababisha wananchi kukosa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia changamoto nyingine katika Mabaraza haya ya Ardhi ni kutokana na posho ambayo wanalipwa kwamba ni ndogo sana na wakati mwingine posho ambayo wanalipwa Wenyeviti hawa wa Mabaraza ya Ardhi inacheleweshwa. Kwa hiyo, inasababisha Wajumbe hawa wa Mabaraza ya Ardhi kukosa ari ya kufanya kazi vizuri na hivyo kusababisha kushindwa kutatua migogogro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kwamba ilete mabadiliko ya kisheria ili kuweza kufanya

mabaraza haya ya ardhi kutokufanya kazi zake kwa sababu wameshindwa kufanya kazi zao katika kutatua migogoro ya ardhi. Kwa sababu hapo kabla, migogoro ya ardhi ilikuwa inatatuliwa katika mfumo wa kimahakama. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iweze kufanya marekebisho ya sheria ili kurudisha kesi hizi za migogoro ya ardhi kufanyika katika mfumo wa kimahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu katika Mahakama, mawakili wetu hawa wanao uwezo mkubwa wa kisheria kuweza kutatua migogoro ya ardhi. Pia mawakili wanakuwa na maadili kiasi kwamba wana uwezo wa kutatua migogoro ya ardhi na hivyo kupunguza kabisa migogoro ya ardhi au kuimaliza kabisa katika nchi yetu ya Tanzania ambayo inaongoza pia katika Bara la Afrika katika akuwepo kwa migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la kesi la mirathi pamoja na kesi za ndoa. Wanawake wengi ndio wamekuwa waathirika katika kesi za mirathi pamoja na kesi za ndoa. Naishauri Serikali itusaidie kuleta sheria ya kuwa na Mahakama Maalum ambayo inaweza ikasikiliza kesi za mirathi pamoja na kesi za ndoa. Kwa sababu kutokana na jamii yetu sijui kubadilika au kupata uelewa mkubwa zaidi, sijui inakuwaje, migogoro ya mirathi na ndoa imekuwa ni mingi sana, imekuwa ikilundikana katika mahakama zetu. Tunafahamu kabisa tuna upungufu wa watumishi katika mahakama zetu na hivyo kufanya kesi kuludikana na kushindwa kufanyika vizuri. Kwa hiyo, naishauri Serikali kuleta sheria ili paweze kuanzishwa Mahakama Maalum ambayo itakuwa inasimamia kesi za mirathi pamoja na kesi za ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea suala la Uandishi wa Sheria kama inavyoonekana katika Kitabu cha Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa muda wa miaka miwili na nusu nimekuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo.

Katika uchambuzi wa sheria ndogo tumekuwa tukiona makosa mbalimbali yamekuwa yakifanyika katika uandishi wa sheria ndogo. Makosa hayo yalikuwa ni makosa

ya kiuandishi na makosa ya kikatiba. Cha kushangaza sana, tunao watendaji ambao ni wanasheria katika Halmashauri zetu ambao wanaziandika hizi sheria lakini bado makosa yamekuwa yakipatikana kwa takribani asilimia 60 katika sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, hiyo inasababisha watu kunyimwa haki zao. Kwa sababu unakuta kabisa kama sheria inakiuka Katiba, moja kwa moja mtu atakuja kukosa haki yake. Hivyo basi, ninashauri pawepo na semina mbalimbali. Pamoja na kwamba Serikali inafanya jitihada mbalimbali, lakini naomba semina ziweze kufanyika katika Halmashauri zetu kwa wale wanasheria ili wafahamu namna ya uandishi mzuri wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ipewe uwezo, watumishi waongezwe na pia watumie teknolojia mpya katika uandishi wa kisheria ili kuepuka makosa mbalimbali ambayo yanatokea hususan katika uandishi wa sheria ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijielekeze katika suala la kuomba mabadiliko ya sheria mbalimbali. Katika Bunge hili Waheshimiwa Wabunge, na mimi nikiwepo wa kwanza tumekuwa tukiomba mabadilko ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali, kuna siku nilisimama hapa tarehe 5 Mei,2016 nikiitaka Serikali kuleta mabadiliko ya Sheria ya Ndoa na Serikali ilitoa ahadi kwamba mwezi Septemba katika mwaka huo 2016 wataleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza sana, Serikali mpaka sasa imekaa kimya, ukiuliza kuhusiana na suala la sheria, wanaanza kusema mabadiliko ya Sheria ya Ndoa Serikali haina majibu sahihi, lakini hiyo illkuwa ni ahadi ya Serikali. Hivi tunataka kusema kwamba wananchi wasiiamini tena Serikali yao kwa sababu inatoa ahadi za uongo? Naomba tusifike huko, wananchi bado wanayo imani na

Serikali. Kwa hiyo, ninaitaka Serikali kutimiza ahadi yake ya kuleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria hii ya Ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoitaka Serikali, kuna sababu mbalimbali. Serikali baada ya kusema kwamba italeta huo Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Ndoa, hawakuleta. Matokeo yake, wanamitandao wametumia upenyo huu au wametumia mwanya huo kwenda kuishtaki Serikali mahakamani na hatimaye Serikali wakashindwa katika kesi hiyo. Mahakama ikatoa *ruling* kwamba kifungu cha 13 na 17 viondolewe kwa sababu vinaleta ubaguzi katika Sheria hii ya Ndoa. Serikali ikakata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kukata rufaa, mimi sitaki kuingilia muhimili wa Mahakama, mimi niko katika muhimili mwingine kabisa wa Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabisa Serikali sasa iangalia na ione kwamba umefika muda muafaka, Watanzania wote wanataka Sheria ya Ndoa iweze kufanyiwa marekebisho kwa sababu watoto wetu wanateseka sana. Ukiangalia sheria hiyo, inaenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 12 (1) ambayo inasema: "Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa." Vilevile (2) inasema, "Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa." Mtoto huyu wa kike naye anastahili kutambuliwa na kuheshimiwa na kupewa uhuru wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la usawa katika utaungwaji wa sheria, lakini sheria hii ya ndoa imetungwa kibaguzi, imeenda kinyume kabisa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania. Ibara ya 13 inasema, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki mbele ya sheria, lakini sheria hii inambagua mtoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 kifungu cha 16 inatafsiri maana ya ndoa.

Inasema, "Muungano lazima uwe wa hiari." Sasa muungano huu unafanywa na wazazi, ndio wanaotoa ridhaa ya mtoto wa kike kuolewa chini ya umri wa miaka 18. Kwa maana hiyo basi, sheria hii ya ndoa iko kinyume, yaani yenyewe inaji-*contradict* yenyewe kwa yenyewe. Kwa maana hiyo, ninaitaka Serikali kuangalia vifungu hivyo ambapo vina *contradiction* yenyewe kwa yenyewa na pia na Katiba iweze kufanyia marekebisho sheria hii ya ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hapa nchini Tanzania, pamoja na makubaliano ya Kimataifa ambayo tumekuwa tukiyasaini, tunaenda kinyume kwa sababu gani? Hizi ndoa ambazo zinafungwa za hawa watoto ambao wako chini ya umri wa miaka 18 zinaenda kinyume na hichi kifungu cha 16. Kwa maana hiyo, sheria hizo zote ni batili. Kwa hiyo, ninaitaka Serikali kutoa tamko na kusema kuwa watoto walioolewa chini ya miaka 18, ndoa hizo ni batili na waweze kurudi katika kazi zao, waende wakasome waweze kuwa kama sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mngenipata mimi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema. *(Makofi)*

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Awali ya yote namshukuru Mheshimiwa Waziri na Watendaji kwa taarifa nzuri ya bajeti ambayo wametuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Shule Kuu ya Sheria kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuchuja wanasheria na kada hii ya sheria ili tuwe na wanasheria wazuri. Pamoja na mambo

hayo yote, kuna changamoto nyingi ambazo zinaikabili Shule Kuu ya Sheria.

Kwanza, bajeti finyu. Kwenye bajeti ya matumizi mengineyo, tukumbuke kwamba Shule Kuu ya Sheria inahudumia takribani vyuo vikuu 17 ambavyo vinatoa wahitimu wa shahada ya kwanza ya sheria, lakini bajeti yake ni ndogo katika matumizi mengineyo na haifiki hata asilimia 22. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo la kisheria. Ukisoma kifungu cha 15 (1)(d) ya Sheria ya Shule Kuu ya Sheria Na. 18 ya 2007, imeanzisha *Governing Council* ambapo Wajumbe wake, mmoja kati ya Wajumbe ni Mkuu wa Kitivo cha Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema, kuna vyuo vikuu 17 vinavyotoa shahada ya kwanza ya sheria, ni kwa nini sheria hii imetoa upendeleo kwa chuo kikuu kimoja kupeleka Mkuu wake wa Kitivo katika *Governing Council* wakati tuna vyuo vikuu 17*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sheria hii inataungwa mwaka 2007, hivi vyuo vingi vilikuwepo. Kwa hiyo, ni mapendekezo yangu Mheshimiwa Waziri akiona inafaa, itendwe haki jinsi ya kupata mwakilishi wa Vitivo vya Sheria vya Vyuo Vikuu vyote Tanzania badala ya kupendelea chuo kikuu kimojan kwa sababu upendeleo huo ni ubaguzi ambao unapingwa kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 13(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili kwa Wizara hii ni suala la usajili wa vyeti vya kuzaliwa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ametueleza kwamba ni asilimia 28 tu ya watoto wote wanaozaliwa wanaandikishwa na kupata vyeti. Hivyo tuna upungufu wa asilimia 72. Upungufu huu ni mkubwa sana, tuna kila sababu ya kuwa-*address* upungufu huu kuhakikisha kwamba kila mtoto anayezaliwa anapata cheti cha usajili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zilizopo katika kiambatisho 'D' ukurasa wa 94 kinatupa mshtuko ambao inabidi Wizara na Serikali iangalie vizuri zaidi. Katika mikoa 26 takwimu zimeonesha kwamba ni mikoa 12 tu ndipo takwimu zake zimeonesha pale. Kuna mikoa 14 haijaonesha ule usajili wa *under five years* jinsi ulivyofanyika. Katika hiyo mikoa 14, upo Mkoa wa Ruvuma na Jimbo la Songea. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba watoto hawa wa *under five years* wanakosa haki zao za msingi katika kusajiliwa mara baada ya kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosa haki huko ni kukiuka Ibara ya 7 ya Tamko la Haki za Watoto Duniani la mwaka 1989, ni kukiuka Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia ni kukiuka kifungu cha 6(3) cha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Sura ya 13. Ni ushauri wangu kwa Serikali na kwa Wizara kwamba ni muhimu sana kuhakikisha kwamba suala la usajili wa *under five years* linafanyika nchi nzima ili kuhakikisha kwamba siyo tu tunapata takwimu, lakini pia tunatekeleza haki za watoto hao kama zilivyoelezwa katika nyaraka hizo za kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nieleze kuhusiana na ukosefu wa Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Kibiashara. Katika hotuba nzima aliyoelezea Mheshimiwa Waziri Profesa Kabudi, sijaona mahali ambapo ameelezea kuwepo au kuanzishwa kwa Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro *(International Commercial Arbitration).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba mikataba mingi ambayo tunaingia kama nchi, tunalazika kuweka *arbitration clause* ya kupeleka migogoro yetu ya kibiashara katika nchi mbalimbali duniani, nchi ambazo hatujui mambo yao ya kisheria yakoje, *systems* zao ni ngumu, matokeo yake tunakuja kupata maamuzi ambayo yanakuja kutuathiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hilo, ni ushauri wangu kwamba ni vizuri tuwe na Kituo cha Kimataifa

cha Utatuzi wa Migogoro hapa nchini ambacho kitasaidia sana kutatua migogoro mingi ya kibaishara na sisi tulazimishe. Nchi jirani kama Rwanda wameanzisha *Kigali International Arbitration Center* ambayo inakuja kwa juu sana. Tusipokuwa makini itachukua *districts* zote katika Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi tunapaswa kujipanga kuhakikisha kwamba tunaanzisha kituo hicho ambacho kina faida. Sheria nyingi ambazo tumezitunga za kulinda rasilimali za nchi hii ambazo ni nzuri sana, tunahitaji kuzilinda zaidi kuwa na mifumo ya utatuzi wa migogoro ambayo tunaiamini na inaeleweka. Hivyo, kuanzishwa kwa kituo kama hicho, hakuepukiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kama hicho kikianzishwa ni muhimu sana kwa kusaidia wataalam wa ndani kujenga uwezo wao katika utatuzi wa migogoro ya kibiashara ya Kimataifa. Kituo kama hicho kikiwepo hapa ndani kitatuokolea fedha nyingi sana ambazo tunatumia kwenda kutatua migogoro katika nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Hivyo basi, ni ushauri wangu Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima waone umuhimu wa kuanzisha kituo kama hicho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nina mambo ya msingi sana ambayo nataka niliambie Bunge. Taifa lolote duniani linaweza likaendelea kama utawala wa sheria na Katiba utazingatiwa. Kwa bahati mbaya, mambo ya kisheria na kikatiba yanayokosewa sasa watu wanafikiri ni *temporary* na wengine miongoni mwenu mnasema ngoja haya mambo yapite awamu hii tu, lakini baadae tutakuja kurudi kwenye *line* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kwamba kinachoendelea sasa ni tabia ambayo inaanza, wa-Spanish wanasema tabia inaanza kama utando wa buibui na mwisho wake unaishia kama lehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujadili masuala ya Katiba na Sheria bila kuwa na utawala unaoheshimu Katiba, bila kuwa na Bunge ambalo linaweza likasimamia Serikali Kikatiba na Kisheria, Taifa hili litaendelea kwenda mahali pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Polepole ametoa maelekezo kwenye vyombo vya habari kwamba Mheshimiwa Mbunge Zitto Kabwe akamatwe na polisi kwa sababu ya kuchambua hoja za *CAG.* Maana yake nini? Maana yake ni kwamba sasa Polepole hana maana amemwongelea Mheshimiwa Zitto, maana yake anaongelea Bunge hili lisiendelee na uchambuzi wa jambo lolote ambalo ni kinyume na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ilianza humu ndani, maoni yetu ya Kambi Rasmi ya Upinzani mnayafanyia *screening,* tumeacha kusoma. Sasa imefika mahali Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi anaonya na kutoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi limkamate Mbunge anayechambua ripoti ya *CAG.* Kama kuna wa kwanza kukamatwa, ni aliyepoteza shilingi trilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee, nina masuala muhimu sasa kuhusu matumizi mabaya ya sheria hasa Mahakamani na mara nyingi tukiongelea habari ya Mahakama, watu huwa wanakuja hapa wanasema mambo yaliyoko Mahakamani tusiyaongee. Kwa sababu Bunge ndiyo linatunga sheria na Mahakama inakwenda kutafsiri sheria, mambo yaliyoko Mahakamani yasiongelewe kwa kina gani, lazima tafsiri yake ipatikane, lakini uzembe na matumizi mabaya ya sheria Mahakamani, lazima tuyaongee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna kesi ya *money laundering.* Hizi kesi zinatumika kuonea na kutesa wafanyabiashara. Juzi *TLS* walipitisha azimio Arusha kwa ajili ya kumtetea Wakili Median Mwale. Mwale ana mwaka wa nane Magereza; *DPP* amesha-*enter nolle* zaidi ya mara tano. *Nolle* nyingine imekuwa *entered* mwaka huu. Huyu mtu mafaili yake yamekwenda mpaka *Court of Appeal,* vielelezo vimetupwa na *Court of Appeal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Jaji amemwachia na Ofisi ya *DPP* ikasema ukimwachia huyu mtu, hatutamkamata tena. Kwa miaka nane Ofisi ya *DPP* imeshindwa ku-*establish evidence* ya kumfunga mtu, bado yuko ndani kama mahabusu. Siyo yeye tu, ilipotokea ya Mwale, watu walifikiri ni Mwale peke yake. Leo kuna Dkt. Ringo Tenga, kuna Sioi, kuna akina Kitillya; hawa ni wale ambao magazeti yanawaandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekwenda Magereza nimekuta watu wana *money laundering* ya shilingi 800,000 M-pesa. Nimemkuta mtu yuko Magereza kwa *money laundering* ya dola 1,500. Ukishapelekwa kwenye Mahakama ya chini, wanasema hatuna mamlaka ya kusikiliza shauri hili. Mtu anakaa jela miaka nane. Suala hili nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri mara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natetea kwa sababu moja, najua mateso ya Magereza. Leo tuna kesi ya Mheshimiwa Mbowe, hii kesi kwenye *penal code* ikiwa watakutwa na hatia, watakwenda jela mwaka mzima. Hakimu anatoa masharti ya Waheshimiwa Wabunge kuripoti Kituo cha Polisi kila Ijumaa. Haya ni matumizi mabaya ya sheria, matumizi mabaya ya Hakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongea hivyo ninyi mnasema hivi, kama hamkuridhika na masharti haya, nendeni kwenye A*ppellate Court.* Kama *remedy* yetu itakuwa ni kwenda *Appellate Court,* lakini bila kuwakemea Mahakimu wanao-*abuse* sheria, wanao-*abuse power,* maana yake watu

wataanza kuiona Mahakama haitendi haki. Mahakama ikipoteza *trust,* nchi hii itaingia kwenye *civil war.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo una Wabunge ambao wana kesi ya mkusanyiko usio halali. Wakikutwa na hatia ni mwaka mmoja jela, unawapa masharti ya dhamana kila Ijumaa Waheshimiwa Wabunge waende Kituo cha Polisi Dar es Salaam. Leo Mheshimiwa Heche ni Mbunge wa Tarime, maana yake kuanzia Jumatano ya kila wiki, kesi ikichukua miaka miwili Jumatano ya kila wiki anaanza safari kutoka Tarime kuja Dar es Salaam. Mambo haya yanaleta maumivu makali sana kwetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema hivi, pamoja na kwamba ni kweli Mahakama ni mhimili mwingine, lazima kuwepo na *check and balance.* Hakimu alinipeleka Magereza mimi kwenye kesi ambayo nilikuwa nimeingia nasikiliza, anamwambia *State Attorney* usini-*mislead* kama mlivyoni-*mislead* kwenye kesi ya Lema. Nimekaa jela miezi minne kwa sababu ya makosa ya Hakimu. Mahakama ya Rufaa inakuja kuamua ndiyo, lakini mtu ameshaumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sugu, ameomba, huyu kesi yake akikutwa na hatia amefungwa miezi mitano. Alinyimwa dhamana kwenye kesi ambayo akikutwa na hatia anafungwa miezi mitano, Hakimu anasema huyu akae ndani kwa usalama wake. Huyu anamaliza kifungo kesho kutwa, rufaa yake haijasikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema Serikali inaingilia Mahakama, ni mikakati kama hii tunayoiona kwamba Mheshimiwa Sugu sasa rufaa yake ikisikilizwa mwezi unaokuja na anatoka tarehe 20, atakuwa amepata *remedy* gani katika kifungo ambacho alikuwa ametumikia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, mambo haya siyo ya CHADEMA, ni yetu wote. Utakapokuwa na Mahakama huru, Ofisi ya *DPP* huru, Ofisi ya *AG* huru haiwasaidii CHADEMA. Mimi naweza nikaamua leo nikaja

huko CCM, lakini haijalishi. Unapokuwa na Mahakama ambayo haiko huru, unakuwa na mazingira mabaya ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Polisi hawako huru; juzi mmemwona Makonda na sinema yake ya watoto. Leo wamemkamata yule dada waliyekuwa wamempa *deal* aseme ni mtoto wa Mheshimiwa Lowassa, anakamatwa tena kwa sababu alikanusha juzi. Haya matumizi mabaya ya sheria ambayo sasa yanaingia Mahakamani. Watu wanaozea jela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *money laundering,* Waheshimiwa Wabunge msipolileta humu Bungeni, Bunge liweze kuichambua na kutolea maelekezo mapya, hii kesi haitamwacha Mbunge yeyote salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimeona barua ya *TRA;* mtu kanunua nyumba ya shilingi milioni 80 Sinza. *TRA* wanaandika barua, wanakwambia badala ya ku-*claim capital gain,* wanaenda kuandika barua wanasema, tunataka uje utuambie na chanzo cha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siku nikifanya hivyo, mkatafuta chanzo cha fedha, Mheshimiwa Jenista Mhagama mimi nitasema umenihonga wewe ama Mheshimiwa Angellah Kairuki, sasa sijui hiyo kesi itaendeshwaje? *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo siyo tu yanaua uchumi, haya mambo yanaondoa *confidence* kwa wafanyabiashara. Mimi nawaambia, leo watu nchi hii wanahamisha fedha kwa sababu ya sheria za ajabu ajabu. Hakuna tena *transaction* zinazopita kwenye mabenki. Ukiweka shilingi milioni 20 kwenye akaunti; mimi nili-*transfer* hela kwenye akaunti yangu wanazuia, tueleze sababu ya ku-*transfer* hela. Napeleka hela kwa mke wangu unaniuliza sababu? Sababu inaweza ikawa *love.* Haya mambo yanafanya watu sasa wasiweke hela benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU, hizi *tax holdings* zilizoundwa ambazo ziko chini ya Kamati ya Ulinzi wa Mkoa huko zinafanya watu wanakuwa na hofu. *Transaction* hazipiti kwenye mabenki, benki wanakosa *deposits,* benki sasa zinaanza ku-*fail.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, Mheshimiwa Waziri, punguza uoga. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Musukuma. Ngoja niende kwa Mheshimiwa Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Sabreena ajiandae.

Hayupo, haya. Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, lakini naomba uniruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Profesa Kabudi kwa taarifa yake nzuri sana na mimi nitatoa ushauri, lakini pia nitakuwa na maombi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika watu ambao nawaamini sana ni pamoja na Profesa Kabudi ambaye ni mbobezi wa mambo ya sheria kama ulivyo wewe Mwenyekiti wetu Mtemi Andrew John Chenge na ndiyo maana wamekuweka leo makusudi ili utusaidie baadhi ya mambo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwenye maeneo mawili. Ushauri wangu wa kwanza, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aongeze pesa kwa ajili ya kugharamia mashahidi ili kusudi mashahidi hawa wanapokwenda kutoa ushahidi wao, waweze kuukamilisha mapema kwa sababu pesa hizi zinapochelewa au zinapokuwa kidogo, mashahidi hawaendi na kesi zinachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, naomba sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu *(AG)* iangalie namna nzuri zaidi ya kuwa na wataalam kwa maana ya makada ambao wataweza kusaidia hasa katika masuala ya kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, inaweza ikatokea kesi ya mambo ya fedha, lazima kuwe na mtaalam wa mambo ya fedha, lazima kuwe na mtaalam kwa kesi hizi, lazima kuwe na mtaalam wa mambo ya ujenzi, mambo ya benki lakini la lazima kuwa na mtaalamu wa mambo ya *IT.* Kwa sababu kwa kufanya hivyo, kesi hizi wakati mwingine zinachelewa kwa sababu wataalam kutoka Ofisi ya *AG* katika fani hizi ni wachache. Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu ili kesi hizi ziweze kwenda haraka daima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kama nilivyotangulia kusema kwamba namwamini sana Profesa Kabudi, naomba nilete ombi kwako Mheshimiwa Waziri. Wilaya ya Kwimba tunazo Mahakama za Mwanzo kumi. Tunayo Buyogo, Nyambiti, Nyamikoma, Ngula, Bungulwa, Malya, Nyamikoma na Kikubiti. Mahakama hizi hazina Mahakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mahakama za Mwanzo kumi zilizoko Wilaya ya Kwimba na jiografia ya Kwimba inajulikana, tuna Mahakimu wanne tu wa Mahakama za Mwanzo. Wanne tu kati ya Mahakama kumi. Sasa hili ni tatizo kubwa, kwa kufanya hivyo, hao Mahakimu hao huwa wanazunguka, lakini katika kuzunguka wakati mwingine wanachelewa kwa sababu hawana usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri ninayemwamini na ninazungumza kwa upole kabisa. Kwa sababu suala hili tumekuwa nalo kwa muda mrefu. Nakuomba sana Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mahakama kumi hizi bila kuwa na Mahakimu, ni kesi ngapi mnasema kwamba kesi ndani ya muda fulani ziwe zimeshapitiwa na kutolewa maamuzi, lakini Mahakimu wanne kwa Mahakama kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine namwomba Mheshimiwa Waziri, kulikuwa na ahadi ya muda mrefu sana, tangu enzi za Mheshimiwa Waziri Mwapachu, akaja Mheshimiwa Migiro, akaja Mheshimiwa Nagu, Marehemu Mheshimiwa Kombani, Mheshimiwa *Chikawe One* na *Chikawe Two,* leo upo wewe kuhusu ukarabati wa Mahakama za Mwanzo katika Mahakama ya Nyamikoma na Kikubiji. Mahakama hizi ni za siku nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na tumeshaandika kwa maandishi. Pia Mahakimu hawa, hawana hata karatasi kabisa za kuandikia. Pia pamoja na upungufu wa Mahakimu, makarani hawapo, waliopo ni wahudumu. Sasa angalia, Mahakimu hawapo, makarani hawapo, sasa hebu niambie maana ya kuwa na Mahakama pale ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa unyenyekevu mkubwa, sitaki kusema kwamba Mahakama hizo amezitelekeza kwa sababu siyo tabia yake. Sitaki kusema kwamba Mahakama hizo hazipendi au hazitaki, siyo tabia yake.

Namsihi sana mwana wa Singida, hebu Mahakama hizi sasa ambazo zilipangiwa kukarabatiwa muda mrefu kama ilivyoandikwa kwenye vitabu hivi, Mahakimu basi wapatikane, nyumba na majengo hayo yakarabatiwe na watu walioko kule ambao ni watumishi walioko chini yake, basi vifaa ambavyo wanavihitaji viweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Sabreena dakika tano.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Rais mpya wa *Tanganyika Law Society* kwa

ushindi huo mnono. Tuko pamoja naye sisi kama timu ya wanasheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa masikitiko yangu makubwa na kumpa pole Kamanda wetu na Waziri Kivuli wetu na Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Tundu Lissu kwa madhila yaliyomkuta hapa Dodoma. Suala hili limeshakuwa komavu, ni suala ambalo katika jamii yetu ya Watanzania limekomaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kugusia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *Article 14* inazungumzia *right to life.* Kila Mtanzania ana haki ya kuishi na wajibu wa kutoa roho ni kazi ambayo inafanywa na Mwenyezi Mungu, lakini pale inapotokea mtu ameuawa, basi hata kwenye *Islamic Sharia,* mimi ni msomi wa *Islamic Sharia,* tunasema kuna *option* tatu; moja kisasi; mbili kusamehe; tatu, yule aliyemuua mwenzake abebe gharama za kuhudumia familia ya yule mtu aliyoiacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la kutoa nafsi za Watanzania katika nchi yetu limekuwa ni *common.* Napenda niipongeze Serikali, mnajua kwamba kila mtu ana haki ya kuishi na ndiyo maana toka kipindi cha Mzee Mkapa, Mzee Kikwete na kuendelea, Serikali haijajaribu hata siku moja kuchukua jukumu la kunyonga, kwa sababu inajua kila mtu ana haki ya kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii tabia inayoendelea ya watu kunyongwa, watu kutupwa kwenye viroba, kupigwa risasi hadharani, inatutisha sana. Ni tabia ambayo sisi kama Taifa bila kuangalia vyama, sura na rangi lazima tuikemee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma uko pembezoni mwa nchi, lakini pia tuko karibu na nchi ambazo zimeingia kwenye vita. Tukiangalia sababu ambazo zilifanya watu wetu wengi wapigane huko nchi jirani ni mauaji ya kimya kimya ya watu wasiojulikana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama nchini watu wataendelea kufa, kuumia, tusipochukua hatua, sisi tunakaa jirani kule, walikuwa wanakuja wakimbizi, tunawauliza sababu ya vita ni nini? Wanatuambia, tulikaa usiku baba akavamiwa akauawa. Watoto wakiamka asubuhi wanajua ni nyumba fulani ndiyo iliyovamia; kinachofuatia ni kisasi; vikaanza vita vya wao kwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kama Taifa, tuungane, tuhakikishe kwamba tunazuia aina yoyote ya Mtanzania asiweze kuuawa bila sababu. Mambo haya yamekomaa. Juzi juzi tulisikia Mtwara kule mtu kapigwa risasi kwenye kichogo, juzi juzi tumesikia Mwandishi wa Habari katekwa, kaumizwa; Ndugu yetu Alphonce Mawazo, Mwenyekiti wa Geita alipigwa kule hadharani akafariki; Ben Saanane kapotea mpaka leo haonekani. Mambo haya tukiyakalia kimya kama Taifa kwa kweli naamini tutaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali ina moyo wa dhati ndiyo maana ikafuta adhabu ya kifo. Basi iendelee kusimamia haya mauaji ambayo yanafanywa na kuendelea kuchafua nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawakumbuka makamanda wetu waliopoteza maisha kule Kibiti. Ni dhahiri sasa, lazima Serikali isimame na Watanzania tusisikie tena vifo vinavyotokea bila sababu ya msingi ili kutii Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika Sheria yetu ya Ardhi, katika kifungu cha 167 kinachozungumzia uanzishaji wa Mabaraza ya Ardhi. Kaka yangu Mheshimiwa Cosato pale ameelezea vizuri sana kwamba Mabaraza haya yana upungufu, wengine wakapendekeza yaletwe yafutwe, wengine wakapendekeza hivi na hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza haya yameanzishwa kwa mujibu wa sheria. Ukiangalia kifungu cha

167(1) tunaona kabisa kwamba vyombo ambavyo vimepewa mamlaka ya kusimamia migogoro ya ardhi inaanza *Court of Appeal* inakuja *High Court of Tanzania,* inakuja *District, Land and Housing Tribunal,* inakuja *Ward Tribunal* na inakuja V*illage Land Council.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusikitika kwa kile kilichotokea kwa mwenzetu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu Paul Makonda, miezi miwili iliyopita kuamua kufuta Mabaraza ya Ardhi kinyume kabisa na sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo pekee chenye mamlaka ya kutunga sheria, chombo pekee chenye mamlaka ya kufuta sheria na chombo pekee chenye mamlaka ya kufanya *amendment* za sheria ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaomba Waziri wa Katiba na Sheria atueleze Mkuu wa Mkoa huyu mamlaka ya kufuta sheria za nchi hii anayatoa wapi? Mnataka nani aseme ili basi kila mtu...

**TAARIFA**

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Sabreena.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, taarifa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** *Mheshimiwa Sabreena, ukisema chombo chenye mamlaka ya kufuta sheria sijui na kufanya nini, Bunge hili sasa hivi linadharaulika, elewa hivyo Mheshimiwa Sabreena. (Makofi/Kicheko)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo naipokea. Bunge limewahi kumwita Paul...

**MWENYEKITI:** Hebu subiri kwanza. Mheshimiwa Heche, nakuomba ufute kauli yako. *(Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ungeniuliza akina nani wanalidharau ningekwambia.

**MWENYEKITI:** Nakuomba ufute tu kauli yako, twende vizuri tu.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufuta. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limewahi kumwita Paul Makonda na kumwonya juu ya uvunjaji wa taratibu na sheria za nchi hii na aliomba msamaha akasema kwamba itakuwa ni mwanzo na mwisho, lakini mara baada ya hapo, tunaona Mabaraza ya Kata ya Mkoa mzima wa Dar es Salaam sasa hivi yamesitishwa na hakuna shughuli zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ni mamlaka gani yanayompa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa huyu mamlaka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako ndiyo huo. Nina dakika tano tu muda wangu, Mheshimiwa Musukuma dakika tano tu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Sheria afikirie upya na kuendelea kufanya ziara hasa kwenye Majimbo yetu yaliyoko kule vijijini. Tuna shida kubwa sana ya Mahakama, namaanisha majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ni sehemu ambayo kila mtu anategemea akatendewe haki, lakini kweli

Mahakama nyingine hata huyo hakimu kwenye kutenda haki inamuwia vigumu kutokana na mazingira yenyewe ya kufanyia kazi. Huwezi ukafanya kazi ya kuhukumu watu halafu umekaa kwenye jengo limejaa popo, unakwepana na mavi ya popo, halafu ukatenda haki sawa sawa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kufanya ziara, aangalie hasa kule vijijini, tuna hali mbaya sana kuhusiana na majengo ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, Mheshimiwa Waziri, Mahakama nyingi zimejaa mahabusu ambao kimsingi wengine wako mle tu kwa makosa ambayo yanastahili hata ungeleta *amendment* tukabadilisha sheria wakapigwa hata makofi tu wakarudi nyumbani. Kwa mfano, Gereza letu la Geita, *capacity* yake ni watu 141, lakini mpaka jana watu 750 wako ndani. Hii ni hali mbaya sana. Ukiangalia watu wengi walioko humo, wana kesi ndogo ndogo kuingia kwa jinai. Mtu ameingia tu labda eneo la mgodi, amekutwa karibu na ziwa kwenye maeneo ya hifadhi huko Rubondo; wamerundikwa wako mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu jaribu kuangalia uwezekano, ikiwezekana hata kupanua Magereza, lakini ikiwezekana kujaribu kuleta tubadilishe hizo sheria makosa ambayo hayastahili mtu kuingia ndani, basi aachwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi za wenzetu zilizoendelea, nakumbuka siku moja nilikuwa China, nilifanya kosa Hong Kong, nilivyokamatwa, nilikuwa na kosa tu, tumebishana tukataka kupigana ngumi na mwenzangu, lakini nilivyoitiwa oolisi, walikuja wakaniomba kitambulisho changu peke yake. Nilivyowapa kitambulisho, wakaniachia na mwenzangu wakamwachia. Siku ambayo tunataka kutoka, tulitozwa faini ya dola 5,000 pale pale *immigration* wakati wa kugongewa *passport.* Lakini Tanzania unakuta mtu anamwambia tu huyu amenitukana, huyu amenidhulumu, hata hawajahakikisha, mtu amerundikwa Magereza. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa

ukaze buti, lakini nikuhakikishie Mheshimiwa Kabudi unaenda sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa najaribu kuangalia michango, hata rafiki yangu Mheshimiwa Lema mwenye uzoefu kule Magerezani, anakushauri tu, ni mambo madogo madogo, ujaribu kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sisi kama Waheshimiwa Wabunge ambao tunatunga hizi sheria, tuviache vyombo vifanye kazi. Haya mambo ya kuwa watu wanakuja humu wanasema nani kapotea, *Beni Saanane,* hata watu wa CCM wamechinjwa wengi tu. Kibiti wamechinjwa, hatujapiga kelele, tumevikabidhi vyombo vifanye kazi. Kwa hiyo, hata wale ambao mnasema wamepotea, polisi wanafanya kazi. Ukitaka kujua vizuri, acha kupiga kelele.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Ongeeni sasa, maana nawasikiliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona watu wanapiga kelele, tunaelekea kuzuri, kwa sababu kila siku tunaambiwa tufuate sheria bila shuruti, lakini watu wanajitokeza na viburi vyao.

Mhshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye kampeni ile ya Kinondoni. Tumepiga kampeni na hawa wenzangu, nani hajui kama mlikuwa mnasema watu waandamane mbebe majeneza 200? Ungekuwa wewe ni Serikali ungewaacha watu wanahamasisha watu wafe? Mimi nilikuwa nadhani tuviache vyombo vifanye kazi, nina hakika polisi na watu wengine wasitishwe na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi niliwekwa ndani, si nilikuwa na kosa, kuna shida gani? Ni vizuri hata Waheshimiwa Wabunge hawa wakorofi korofi wanapowekwa Magereza kule wanapewa fundisho.

Unamwona hata rafiki yangu Mheshimiwa Lema sasa hivi kidogo amekuwa binadamu! Tena nashukuru hata leo amenisalimia vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nimekuwa nikisikia mara nyingi sana wanapiga kelele kuhusiana na matamko ya Rais kwamba anavunja Katiba, lakini humu ndani kuna wasomi Wabunge, wanasahau kwamba Waheshimiwa Wabunge mnatunga sheria, lakini na tamko la Rais nalo ni sheria. Kwenye Katiba Ibara ya 37 inampa mamlaka Rais kusikia au kutokusikia ushauri. Sasa kama mnaona ni tatizo, leteni hoja humu ndani tubadilishe sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naelekea kwenye kumpata mtoa hoja. Mheshimiwa *AG,* dakika kumi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mezani. Nitaanza kwa kuchangia kwa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ambayo ilizungumza mambo mawili yanayohusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, Kamati imeshauri na kupendekeza kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inahitaji kuimarisha Mfumo wa Uandishi wa Sheria pamoja na usimamizi wa mikataba kwa namna ambayo itaweza kusaidia kulinda maliasili zetu za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba ushauri huo wa Kamati umepokelewa na kwamba hatua tayari zimeanza kuchukuliwa. Katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali sasa tunaanza kujenga uwezo mahsusi kuiwezesha ofisi hiyo iweze kushughulika na hii mikataba, kwa sababu hii mikataba ina mambo ambayo yako *a bit complex,* yanahitaji utaalam wa juu. Kuna sheria za mikataba huko ndani, kuna sheria za uwekezaji, kuna

sheria za Kimataifa, kuna sheria za aina mbalimbali ambazo zinahusika humo. Tumeligundua hilo na tunalifanyia kazi tuweze kuwa na wanasheria waliobobea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu, hata Mheshimiwa Rais amechukua hatua kadhaa za kuweza kuiboresha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kiasi kwamba sasa inaweza ikakabiliana na changamoto na *technicalities* zote zilizomo katika masuala ya mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imetoa ushauri kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iongezewe rasilimali ili iweze kufanya kazi zake vizuri. Naomba tu nikuhakikishie kwamba ombi hili limeshapokelewa tayari na Serikali, kwa maana ya kwamba bajeti ya mwaka huu nafikiri kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaongezeka kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michango kadhaa ya Waheshimiwa Wabunge na baadhi imeelekezwa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, labda nitaomba niizungumzie kidogo. Mheshimiwa Zuberi - Mbunge wa Liwale ambaye mchango wake pia umeongezewa nguvu na Mheshimiwa Richard Ndassa ambaye amezungumzia uwezo wa Wanasheria katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa kuingia mikataba kwamba pengine imeonekana mikataba hiyo haikuwa na tija na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, hatua zinachukuliwa. Mheshimiwa Rais ameanza kutusaidia kwa kuchukua hatua kuirekebisha na kuibadilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na sisi huko ndani tumejipangia mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndassa alisema ni vyema sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikawa na *specializations* kule ndani. Tunakubaliana naye kwa

asilimia mia moja. Yanapokuja masuala ya ujenzi, ni vema ukawa na mtaalam wa sheria za ujenzi; yakija mambo ya kodi, uwe na mtaalam wa sheria za kodi; yakija mambo ya mipaka, migogoro ya mipaka na kadhalika uwe na mtaalam wa sheria hizo na ndiyo ofisi nyingine za Wanasheria Wakuu duniani zinavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Ndassa kwamba tumeona hatuhitaji tu kuwa na wanasheria ambao wako *specialized,* lakini kuna baadhi ya maeneo tunahitaji tulete ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hata wataalam wasio wanasheria. Kwa mfano, una mambo ya *construction* ya ujenzi wa barabara, kwa kweli inafaa sana mkawa na *engineer* wa mambo ya barabara. Kuna mambo labda ya afya, ni vema mkawa na mtaalam wa mambo ya afya ambaye sio mwanasheria, atatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na michango mingine nitapenda nijielekeze kwa mchango wa Mheshimiwa Lema, amezungumza kwa kweli kwa hisia juu ya mwenendo wa kesi mbalimbali na ametaja kesi ya Mwale, Ringo Tenga, Kitillya na Sioi; ninafikiri kwa ujumla sekta ya sheria ina lengo moja la kuboresha utoaji wa haki. Hilo ndiyo lengo la sekta ya sheria. Nikisema sekta ya sheria ninachukua kwa ujumla wake Mahakama, Wizara, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni vema nikalisema hili kwa sababu mchango huo unazungumzia kwa kweli kusimamia utawala wa sheria na alikuwa akipata mashaka kidogo tunapozungumza kwamba kama kesi iko Mahakamani tusizungumzie hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukitaka kuweka msisitizo katika kusimamia utawala wa sheria, ukitoa hoja ambayo inapingana na *essence* ya utawala wa sheria, inaleta matatizo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine ni kwamba Mheshimiwa Mbunge nadhani alipenda kusema kwamba tusifungwe sana na taratibu zetu zinazosema tusilizungumzie suala linapokuwa liko Mahakamani. Hili liko katika Kanuni zetu za Kudumu za Bunge, kanuni ambazo Bunge lenyewe limetunga, Kanuni ya 64(1)(c) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016 inasema kwamba tusijadili jambo ambalo Mahakama haijalitolea uamuzi; ni kanuni zetu. Hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza wazi wazi kwamba Mahakama itafanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa wala kutiwa shinikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari ya kujadili mambo ambayo yako Mahakamani ni namna moja ya kuipa Mahakama shinikizo. Kwa hiyo, labda niseme tu kwamba wale wote tulioko katika sekta ya sheria, tunafanya kazi ya kuhakikisha kwamba mfumo wa sheria unakuwa bora zaidi. Mifumo yote duniani, hata ukienda Marekani, utakuta kuna matatizo yake. Watasema mfumo huu una shida na mfumo huu una shida. Siku zote kinachofanyika, ni kufanya juhudi ya kuuboresha. Basi tusipendekeze kuboresha mfumo wetu wa sheria kwa kuvunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, huo ndio mchango wangu na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Profesa Kabudi, una dakika zako 50.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* kwa kuniwezesha leo asubuhi kuwasilisha Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya pekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kushiriki na kuchangia hotuba ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nachukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba yangu na kwa umahiri wako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge na kwa kusimamia mjadala huu vizuri. Nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Adeladus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano ambao ananipa katika kutekeleza majukumu yangu na kipekee kwa kuungana na mimi katika kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa maoni na ushauri ambao wanaipatia Wizara na Taasisi zake katika kutekeleza majukumu yetu vizuri. Napenda nikuhakikishie wewe binafsi, Kamati yako na Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tumepokea kwa unyenyekevu na shukrani maoni, hoja na ushauri mliotupa wakati wa mjadala wa bajeti yetu. Kwa niaba ya Wizara tunaahidi kuyafanyia kazi masuala yote yaliyojitokeza katika mjadala huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wa hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu na katika mjadala wa hotuba ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine ziligusa Wizara yangu na Sekta ya Sheria kwa ujumla. Tumezipokea hoja zote zilizotolewa na tunaahidi kuzifanyia kazi na kuleta mrejesho wake Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi na kuichambua bajeti yetu kwa kina. Michango yenu ni nyenzo muhimu ya kuboresha utendaji kazi wa Wizara na taasisi zake ili sekta ya sheria ikidhi matarajio ya Watanzania na iwe na mchango chanya katika maendeleo yao ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla wa Wabunge 40 wamechangia hotuba yetu, ambapo Wabunge 34

wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge sita wamechangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa uniruhusu nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na nitoe indhari tu kwamba hoja zote nyingine ambazo sitazijibu zitajibiwa kwa maandishi. Nianze na hoja zilizotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusu uhaba wa watumishi wa Mahakama wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali. Napenda kusema kwamba upo uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali kama Mahakimu, Wasaidizi wa Kumbukumbu na Makatibu Mahsusi. Hata hivyo, kwa mwaka wa 2017/2018 vibali vilipatikana na ajira kutolewa. Mfano, Majaji 12 na Mahakimu 194 wameajiriwa; Wasaidizi wa Kumbukumbu 90 na Makatibu Mahsusi 30 wameajiriwa pia. Aidha, watumishi 298 wa idara nyingine waliajiriwa. Kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019 ajira 513 za kada mbalimbali zinategemewa kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ya Kamati ni kwamba Watendaji wanawanyanyasa Majaji na Mahakimu na kujiingiza kwenye maamuzi ya kesi, lakini pia sheria ya uendeshaji wa Mahakama iboreshwe kudhibiti nidhamu na ikiwezekana kuwarejesha kwenye nafasi zao za awali. Wizara, Tume ya Utumishi wa Mahakama na Mahakama tumefanya mikutano ya pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria mara kadhaa ikiwemo kupitia bajeti ya Wizara na taasisi zilizo chini yake. Kwa bahati mbaya hatukupata fursa ya kupewa hoja hii na kujadiliana na Kamati wala Mwenyekiti wala Kamati katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, suala hili lina historia ndefu kwa sisi tuliokuwepo na kushiriki kwenye maboresho ya Mahakama. Mapendekezo ya maboresho ya uendeshaji wa Mahakama na hatimaye kutungwa Sheria Na. 4 ya mwaka 2001 na muundo wake kupitishwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2014 yana historia ndefu ya

mapendekezo ya Tume za Mheshimiwa Msekwa, Mheshimiwa Jaji Bomani na Mheshimiwa Jaji Mroso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, takwimu na hata viashiria mbalimbali vinaonesha kuwa Mahakama kwenye nyanja karibu zote inapiga hatua kubwa ya maendeleo ya uendeshaji pamoja na kazi yake ya msingi ya utoaji haki. Tume ya Utumishi wa Mahakama chini ya Mheshimiwa Jaji Mkuu na hata Wizara ama mimi Waziri hatujapokea malalamiko yoyote juu ya kunyanyaswa ama kunyanyasana kuingilia shughuli za kazi nje ya majukumu yao ya kiutendaji kwa watendaji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo kuna tatizo la mtu mmoja mmoja kama binadamu, ni vyema litolewe taarifa husika na suala husika kwenye mamlaka husika za kikatiba na kisheria, yaani Tume ya Utumishi wa Mahakama na ama niletewe mimi kama Waziri ili yashughulikiwe kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo. Serikali kwa maana ya Wizara, tutaendelea kushirikiana na Tume ya Mahakama kwenye kusimamia na kuendeleza maboresho ya Mahakama kwa manufaa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa ni kuwahamisha watumishi bila kulipwa stahili zao kwa kuzingatia umuhimu wa kujaza nafasi mbalimbali hasa za madaraka *(duty post)* watumishi wamekuwa wakihamishwa na kulipwa sehemu ya stahili zao kabla ya kuhama na sehemu inayobaki inamaliziwa baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri wa Mahakama kurudia kuezeka paa la Mahakama Kuu ya Kanda ya Shinyanga, ningependa kusema kwamba mradi wa Mahakama Kuu ya Shinyanga ulikamilika mwaka 2016, mara baada ya kukamilika kulikuwa na tatizo la kuvuja kwa maeneo machache ya paa hilo. Kwa kuwa mradi ulikuwa bado kwenye kipindi cha matazamio *(defect liability period)* mkandarasi alirekebisha na sasa tatizo hilo halipo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zabuni za ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa Mahakama kwamba zitolewe kwa uwazi, kipaumbele kitolewe kwa makampuni ya ndani ya Wakandarasi yanayokidhi vigezo na uwezo wa kukamilisha mradi kwa wakati na kwa mujibu wa mikataba husika; napenda kusema kwamba Mahakama imekuwa ikitekeleza miradi yake kwa uwazi wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto kubwa ya ukosefu, uhaba na miundombinu ya Mahakama na kwa kuzingatia uchache wa rasilimali fedha, ukilinganisha na mahitaji halisi ya Mahakama na gharama kubwa za ujenzi, Mahakama ilifanya utafiti wa kubaini teknolojia ya ujenzi yenye gharama nafuu iitwayo moladi ambayo inapunguza gharama kwa takribani asilimia 40 mpaka 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa zabuni za miradi ya Mahakama za Wilaya na za Mwanzo iliyotangazwa mwaka 2016/2017 ilionesha kuwa waombaji wa zabuni waliokuwa na gharama za chini kabisa zilikuwa ni shilingi bilioni 1.2 kwa Mahakama za Wilaya na shilingi milioni 898 kwa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na gharama kubwa, Mahakama ilisitisha zabuni hizo na kutumia teknolojia mbadala ya moladi ambayo ni ya Watanzania japo ni teknolojia yenye asili ya Afrika ya Kusini na teknolojia hii imehuishwa na Chuo Kikuu cha Ardhi. Kanuni na taratibu zote za ununuzi wa umma zilizingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimefungua Mahakama Kigamboni ya utaratibu wa moladi, ni mahakama nzuri kwa gharama ambayo mtu hawezi kuamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa udahili katika Taasisi ya Mafunzo kwa Vitendo *(Law School of Tanzania),* ningependa nieleze kwamba hakuna upungufu wa wahitimu wa sheria katika vyuo vikuu nchini. Sasa hivi tuna vitivo vya sheria 17 nchini. Kwa hiyo, hakuna upungufu

wa wahitimu wa sheria. Suala la kwenda *Law School,* zipo sababu nyingi kwa nini baadhi ya wanafunzi hawaendi *Law School.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, wapo ambao wamesoma sheria lakini lengo lao siyo kuwa Wanasheria. Wamemaliza *degree* ya sheria na hawakutaka kuendelea na sheria, wamekwenda kufanya kazi nyingine. Na mimi namfahamu mwanafunzi mmoja ambaye amemaliza sheria, amemaliza na *Law School,* amekuwa *Advocate,* ameacha na sasa anajifunza u-*pilot* wa ndege. Aliniambia kazi ya sheria ilikuwa ya baba, Uwakili ulikuwa wa baba, nimemaliza ya baba, sasa nafanya mimi ninayotaka. Sasa hivi ninavyosema, anajifunza Urubani chini ya shirika fulani la ndege silitaji. Kwa hiyo, wapo ambao wakimaliza *degree* ya sheria hawana *interest* ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wapo wanaoangalia *perspective* ya soko. Ukiangalia katika *private sector* ya *practice* ya sheria, napenda niseme kwamba miongoni mwa maeneo ambayo watu hawatengi fedha kwa ajili ya huduma, ni sheria. Hakuna hata mtu mmoja humu ndani ya Bunge hili ambaye ana *Family Lawyer* ambaye amempangia bajeti kwa mwaka atam-*retain* amlipe kiasi fulani. Kwa hiyo, vijana wetu hawa nao ni mahiri na wajanja, wakiona kwamba huku hakuna maendeleo mazuri, basi wanakwenda kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kweli huko nyuma wanafunzi walikuwa napewa mikopo moja kwa moja, lakini sasa mikopo inatolewa kwa wale ambao wanastahili kwa kutumia *means test* na katika maeneo ya kipaumbele. Sheria siyo mojawapo ya eneo la kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuanzisha matawi mbadala ya taasisi ya sheria, napenda kusema kwamba jambo hilo tumekuwa tunalifikiria na kulitafakari kwa makini, lakini jitihada yetu kubwa kwanza ni kuimarisha ubora wa taasisi hii pale ilipo na baada ya kuimarisha ubora ndipo tutaweza kufikiria mambo ya kupanua kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufahamu kwamba sasa tuna vitivo 17 vya sheria. Mahali pekee ambapo wanasheria wote hawa wanakutana na kupikwa ni kwenye *Law School of Tanzania.* Kwa hiyo, kabla ya kuanza kufikiria kuanzisha matawi, ni lazima tufanye utafiti wa kutosha ili tuhakikishe wanasheria wote wana utamaduni, mila na desturi zinazofanana kwa sababu sasa wanatoka kwenye vyuo vingi tofauti na ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetushauri pia kuhusu Ofisi ya Taifa ya Mashitaka kwamba pawe na ushirikiano kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashitaka, Mahakama, Polisi na vyombo vingine vya upelelezi ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi pamoja na kuongeza wigo wa utoaji haki bila kuingilia uhuru wa vyombo vingine. Ushauri huu umepokelewa na utafanyiwa kazi. Ofisi ya Huduma ya Mashitaka itaendelea kuimarisha na kuboresha mahusiano na ushirikiano na taasisi na wadau wa haki jinai na ndiyo maana katika mabadiiko ya sheria ambayo tunategemea kuyaleta Bungeni, ni pamoja na kuanzisha *Criminal Justice Forum* ambayo itahusisha taasisi mbalimbali lakini pia kuwe na *Government Legal Team* ambayo itahusisha mambo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine wa Kamati ni kwamba Ofisi hii ya Taifa ya Mashitaka ihakikishe inafungua ofisi zake katika Mikoa na Wilaya zilizoainishwa katika taarifa ya bajeti kwa lengo la kuongeza wigo wa utoaji haki. Napenda kusema kwamba ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi. Ofisi imeainisha maeneo itakayofungua ofisi kuwa ni Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Kinondoni, Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Kigamboni na kwa kadri inavyowezekana, basi tutafungua katika Wilaya na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilizungumzia suala la Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwamba kuwepo kwa malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa watu Magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au

majibu yanayoridhisha. Kamati ilishauri Tume ifanye ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko hayo na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika. Ushauri umepokelewa na utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itatembelea sehemu zilizolalamikiwa zikiwemo Magereza na Vituo vya Polisi na taarifa itawasilishwa kwenye mamlaka husika kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati imetoa maoni kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania. Kamati imeshauri Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na mfumo wa sheria nchini unaozungumza lugha moja *(uniformity of law)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio na lazima *(unnecessary conflict of law)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji. Napenda niseme kwamba ushauri unapokelewa na utazingatiwa. Aidha, Tume katika kufanya mapitio ya mifumo ya sheria mbalimbali itahakikisha kutokuwepo kwa migongano baina ya sheria wakati wa kutoa mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ya Bajeti nayo ilikuwa na maoni yafuatayo; moja, bajeti iliyotolewa ya mwaka 2018/2019 haikidhi mahitaji ya msingi ya Mfuko wa Mahakama na kwamba Serikali ihakikishe inaongeza bajeti ya mfuko. Maoni ya Kamati yatazingatiwa, bajeti ya mfuko kwa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kutoka Serika itaongezwa kadri mapato ya Serikali yanavyoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ilitoa maoni kuwa kutokukamilika kwa utaratibu wa kuwezesha mifumo ya ukusanyaji maduhuli kielektroniki *(E-pos machine),* tunasema Serikali kupitia Mahakama tayari imeanza kutumia mfumo wa kielekroniki *(Pos machine)* ambapo Mahakama zote za Mkoa wa Dar es Salaam zinatumia mfumo huo. Utaratibu utafanyika pia mikoani kwa kuongeza mashine hizo

kama Kamati ilivyoshauri. Aidha, mawasiliano yanaendelea kufanyika kati ya Wizara na Wizara ya Fedha ili vifaa hivyo viweze kupatikana kwa bei nafuu na kwa wakati ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale waliochangia kwa mdomo, nianze na Mheshimiwa Kombo. Niseme kwamba suala la *Joint Finance Commission* na suala la *Joint Account* lilitolewa maelezo mazuri sana jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano) na majibu ya Serikali ni hayo hayo kwamba jambo hilo ni kama lilivyokuwa limeelezwa kwenye Wizara hiyo. Tume ipo na mchakato wa kuanzisha akaunti hiyo unaendelea kwa taratibu za kiserikali na hapo utakapokamilika, basi mambo hayo yatatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kutekeleza matakwa ya Katiba, lakini ni jambo ambalo utekelezaji wake unahitaji maandalizi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mwingiliano kati ya Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoshughulikia mambo yasikuwa ya Muungano ya Tanzania Bara na Mahakama Kuu ya Zanzibar, napenda kukubaliana nawe kwamba Mahakama zote hizo zina mamlaka sawa *(concurrent jurisdiction)* lakini pamoja na kuwa na *concurrent jurisdiction,* yapo mashauri ambayo yanaweza kuwa yamefanyika Tanzania Bara yakalazimika kujadiliwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar ikiwa yatakuwa na uhusiano na Mahakama Kuu ya Zanzibar na vivyo hivyo yapo ambayo yatafanyika Zanzibar, lakini yakasikilizwa na Mahakama Kuu ya Tanzania kutegemea ni wapi palipokuwa chanzo cha mgogoro au kesi hiyo, mtandao unaohusika na nyezo zilizotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na hizo mahakama kuwa na *concurrent jurisdiction,* lakini upo wakati ambapo moja inaweza ikasikiliza mashauri yaliyotoka upande mwingine kwa kutegemea muktadha na aina ya tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *OIC,* tarehe 4 Aprili, 2018 Wizara ya Mambo ya Ndani ilijibu na kutoa maelezo mazuri kuhusu suala la *OIC* na nadhani majibu hayo yanakidhi suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mashehe wale wa Uamsho na wale wa Zanzibar, suala hili lipo Mahakamani na Wizara iahidi tu kwamba itazidi kuhamasisha uchunguzi ukamilike ili kesi hiyo iendelee. Kesi za namna hii ni *very complex* na wakati mwingine ushahidi wake kuukusanya unahitaji muda na umahiri na wakati mwingine unahitaji ushirikiano na taasisi na vyombo vilivyo nje ya nchi ambako pia tunalazimika kuomba ushahidi kwa njia mbalimbali. Ni imani yangu kwamba jambo hili litapata muafaka na litapata suluhisho wakati uchunguzi utakapokuwa umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Kiteto kuhusu Mabaraza ya Ardhi; Tume ya Marekebisho ya Sheria ilifanya utafiti kuhusu Mabaraza ya Ardhi. Taarifa hiyo ilifikishwa kwa Waziri na nimetoa maelekezo, kuna maeneo ambayo nimeomba yafanyiwe utafiti zaidi. Kwa hiyo, mara baada ya maeneo hayo ya nyongeza ambayo nimewarudishia Tume ya Kurekebisha Sheria yatakapokamilika, basi Serikali itashauriwa ifanye nini kuhusu Mabaraza haya ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, Serikali ilitoa ahadi hiyo Septemba ya mwaka 2016, lakini baada ya kutafakari kwa makini suala la mabadiliko ya Sheria ya Ndoa linahitaji umakini mkubwa sana. Wewe unafahamu vyema ni sisi Tanzania peke yetu tuliofanikiwa mwaka 1971 kutunga Sheria ya Ndoa. Uganda ambao walikuwa wa kwanza kuanza mchakato huu mwaka 1966 chini ya Ripoti ya Kalema mpaka leo wameshindwa kuwa na sheria moja ya ndoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya ambao walianza juhudi za kuwa na sheria moja ndoa ya mwaka 1968 hawakufanikiwa mpaka baada ya mauaji yaliyotokea. Wametunga sheria, sheria imepita na baadhi ya mambo ambayo sheria imeyakataza, sasa watu wameanza kuyadai

na moja ya mambo ambayo sheria ya Kenya ya sasa ya ndoa inayakataza na sasa yameanza kudaiwa, tena wanaodai ni wanawake, ni kufuta talaka. Hii ni kwa sababu Sheria ya Ndoa ya Kenya imefuta talaka, lakini wote tumeona sasa jitihada kubwa tena ya hadharani na inaongozwa na wanawake kudai sheria ya kuwaruhusu talaka irejeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Mashauri ya ndoa, mirathi, mashauri yanayogusa mila na destruri, yanayogusa dini na itikadi, ni vyema kuyaendea kwa uangalifu mkubwa. Najua kabisa na niseme tu kwa unyenyekevu, somo hili la ndoa nimelifundisha kwa miaka 19, siyo eneo jepesi. Kuhusu kwa mfano, umri wa mtoto kuolewa mpaka ninavyozungumza sasa umri wa mtoto wa kike kuolewa Uingereza ni miaka 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zipo sababu kubwa na mukhtadha wake tuambiane, mwaka 1971 wakati sheria hii ya ndoa inapitishwa, elimu ya mwisho ya mtoto ilikuwa darasa la saba. Asipoendelea kwenda *form one,* ina maana amekaa nyumbani na turudi twende kwenye jamii na kila mmoja nyumbani kwake. Hivyo, mtoto wa kike aliyevunja ungo, kipi chema, aolewe azae katika ndoa au azuiwe kuolewa mpaka afike miaka 15 wakati huko kwingine hakujafungwa na anaweza akapata ujauzito? Atakapoupata ujauzito huo akazaa huyo mtoto, kama ni mkatoliki hatabatizwa mpaka aende akafanye maungamo na maungamo hayo ya kikatoliki ni ya yeye mama, sio baba aliyemzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ukiifumua leo, kuipitisha ndugu zangu ni ngumu. Yapo mambo matatu ndani ya hii Sheria ya Ndoa ambayo kwa Kanisa Katoliki hayakubaliki. Moja, hawakubali kubadili ndoa ingawa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu kubadili ndoa ya mke mmoja kuwa ndoa ya wake wengi. Baraza la Maaskofu Katoliki lilipinga, lakini Mwalimu ambaye alikuwa ni mkatoliki aliwaambia, situngi sheria ya wakatoliki, natunga sheria ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Sheria ya Ndoa ya sasa inaruhusu kubatilishwa na ndoa na Mahakama za kawaida. Kanisa Katoliki halikubali. Mimi sio Mkatoliki, lakini kwa Kanisa Katoliki ndoa inabatilishwa tu na Askofu baada ya kushauriwa na *Judicial Vicar.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapofungua hii, *we are opening a pandora box.* Ukiangalia tuna tafsiri tofauti ya ndoa. Zipo ndoa ambazo kwao ni sakramenti; wapo ambao ndoa kwao ni *covenant.* Kwa hiyo, unapokuwa na mchanganyiko huo mkubwa kiasi hicho ni vyema ukafanya mambo kwa tahadhari*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ndani ya sheria hii bado yana vikwazo kwa Waislam, ni *compromise.* Sheria yoyote iliyofikiwa kwa *compromise, be careful when you want to change it.* Sheria hii ni *very progressive* katika maeneo mengine. Ndiyo sheria ya kwanza duniani kuwaruhusu wanawake kuwa na nguvu hasa wanawake wasomi na watalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Sheria ya Ndoa ya Uingereza, *cohabitation* maana yake mke na mume waishi ndani ya nyumba moja muda wote. Ndiyo maana wanawake wa Kiingereza hawakuweza kupanda vyeo kwenda kufanya kazi nje ya maeneo ambayo waume zao wanafanya kazi. Mwaka 1971 Sheria ya Ndoa, *cohabitation* maana yake siyo kuishi ndani ya nyumba moja, mnaweza kuishi sehemu mbali lakini kwa makubaliano, kwa simu na kwa barua. Tafsiri hiyo ni *cohabitation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya hii Sheria ya Ndoa ya kwetu, malipo ni jukumu la mwanaume kuitunza familia *(the necessity of life).* Kwa hiyo, yapo maeneo mengi ambayo sisi tumepiga hatua ambayo nchi nyingine bado hawajapiga hatua. Hiyo haina maana tusiangalie yaliyopungua. Niliwaeleza hapa na ninarudia, mpaka leo Ulaya Wabunge wanawake wanapata mshahara mdogo kuliko Wabunge wanaume kwa sababu ni wanawake. Kwa hiyo, sihalalishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, kila nchi ina sababu ya kutokufanya mambo fulani na yanahitaji muda; na moja ni Sheria ya Ndoa. Tukiindea kwa haraka tutavuruga zaidi kuliko kujenga. Kwa hiyo, tujenge muafaka wa taratibu, kwa sababu Sheria ya Ndoa ni jamii sio mtu. Ndiyo maana Sheria ya Ndoa ya sasa kuhusu ugoni *(adultery)* niwaambie, ndani ya sheria ya sasa ya ndoa *adultery* inaweza kuwa *evidence; the marriage has broken down irreparably and therefore the Court can grant divorce.* Humo humo *adultery* kwa kutambua yako makabila hapa ambayo *adultery* siyo sababu ya kuvunja ndoa, sheria hii ya ndoa inatoa kibali cha *compensation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nayafahamu makabila mawili ambayo bila kumfumania mke wako ugoni, unaona hujaoa. Kwa hiyo, mambo haya yanahitaji umakini. Kwa hiyo, mtanifuata baadae nitawaambia. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuliendee kwa utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali imekata rufaa kuhusu Sheria ya Umri wa Mtoto Kuolewa, lakini tunapokata rufaa, hatukati rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa *on matters of facts.* Tunakata rufaa *on points of law.* Ule uamuzi bahati mbaya sana tunaangalia matokeo, hatuangalii hoja za uamuzi ule. Ukizifuata hoja za uamuzi ule, hakuna sababu ya kuwa na Viti Maalum.

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ndiyo. Ukifuata hoja ya uamuzi ule, hakuna sababu ya kuwa na Viti Maalum, kwa sababu huo pia ni upendeleo ambao hauruhusiwi na Katiba kwa Ibara ya 13. Maana yake nini? Ndiyo maana Katiba inaruhusu *positive discrimination, affirmative action.* Ni *affirmative action* inayoruhusu Viti Maalum. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa historia ya Tanzania, bila *affirmative action,* idadi ya Wabunge wanawake humu wengi watatoka Mtwara na Lindi, kwa sababu ni *matrilineal* na ndiyo wamekuwa wanaleta Wabunge wengi wa kuchaguliwa. Suala la Tarime, ni ajali kwa mila na desturi. Ninapenda niliweke vizuri, kwa mila na desturi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lengo kubwa la sheria hiyo…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu. Kaa kidogo tu Mheshimiwa Waziri. Ngoja, niambie Kanuni gani imevunjwa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1) ni Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani imevunjwa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1), *can i have my* Kanuni. Ni Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kanuni gani imevunjwa?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1), ni mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Naomba nisome lugha za kuudhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anayehitimisha hoja sio tu kwamba ameongea lugha za kuudhi kwangu mimi, lakini kuanzia mwanzo mwisho, kwanza amewadhihaki Viti Maalum, Wabunge Wanawake lakini zaidi naomba afute kauli yake dhidi yangu mimi kwa kuniambia kwamba nimekuja kwa ajali ilhali akitambua kwamba mimi Esther Nicholas Matiko, nimefanya kampeni kwa muda ambao ulitangazwa na Tume ya Uchaguzi, nikashinda kwa kishindo

kwenye kura za maoni ndani ya chama changu ambapo nilishindana na wanaume wengi, tulikuwa 12 mimi nikiwa mwanamke peke yangu, nikaja kwenye *pool* ya watu vyama vingine vingi ikiwemo CCM, nikawashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo afute kauli yake ya kunidhihaki kwamba nilikuja kwa bahati ilhali nilichaguliwa kwa kura nyingi zaidi ya mgombea wenu wa CCM. Na ukizingatia yeye amekuja kwa kuteuliwa na Rais, hakupigiwa kura. Nakuheshimu sana mzee wangu, *watch your words,* usitukwaze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu.

Mheshimiwa Esther Matiko amesimama kuhusu utaratibu, ametumia kifungu cha 68(1) kufika kwenye 64, kwa yale ambayo hayaruhusiwi humu Bungeni.

Mheshimiwa Mtoa Hoja katika kufafanua mila na desturi za baadhi ya makabila ya nchi yetu, amejaribu kujielezea katika mukhtadha wa sheria ya sasa ya ndoa ya mwaka 1971 kwamba ilikuwa ni *compromise* na katika hali ya kawaida. Ndivyo alivyokuwa analielezea...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Msibishane na mimi. *(Makofi)*

Katika hali ya kawaida, na ndiyo ukweli, hatuwezi kubadilisha ukweli kwa baadhi ya makabila ya nchi yetu. Na katika kila *rule* kuna *exception,* na ndiyo maana amelielezea hilo, tukienda kuangaliana kwa misingi ya mila na desturi ya maeneo tunakotoka utakuta wengi ni bahati, lakini *rule* inabaki palepale, *exception. (Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nasema hakuna haja ya Mheshimiwa Waziri kufuta kauli, amelielezea. Endelea Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ndiyo maana nasema kwamba lengo la Serikali kwenda Mahakama ya Rufaa ni kubakiza *principle* ya *positive discrimination, principle* ya *affirmative action* ili kwa kuangalia hali halisi ya Tanzania wanawake waendelee kupata nafasi katika vyombo vya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lengo lake sio suala la umri wa mtoto kuoa au kuolewa, someni *arguments* za yule Jaji ninayemheshimu sana kwa sababu tumesoma darasa moja, hoja ni ile ya *argument.* Ni sawasawa na hesabu, unaweza ukasema jibu ni nne, lakini mwalimu hasahihishi jibu, mwalimu mzuri wa hesabu anaangalia *method* uliyotumia, sasa kama *method* mbaya itavuruga. Ndilo ninalotaka kuwaambia, itavuruga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu ina maana wasichana watapungua idadi yao, si ni usawa tu, kila usawa una mipaka yake kwa hali halisi ya nchi yenyewe. Ndiyo maana mwanamke ni mwanamke na mwanaume ni mwanaume ingawa wote ni binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ameleta suala la bajeti ya *Law School of Tanzania,* suala hilo litaangaliwa. Kuhusu Mjumbe kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuwa ndio Mjumbe wa *Governing Council,* nakubali viko vyuo vingine 17 ambavyo pia naviheshimu sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu Bungeni.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kwa hiyo, jambo hilo ni jambo la kujadiliwa, lakini wakati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawekwa pale, ni kwa sababu ndicho ambacho kwa lugha ya Kilatini, *primus inter pares.* Huo ukweli pia hautafutika, kwamba Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika vitivo vyote vya sheria, siyo Tanzania tu, Afrika ya Mashariki ni *primus inter pares.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana na wewe unafahamu, umekwenda mara nyingi Kenya. Nikifika Kenya huwa lazima niwatambie, tumewapa Kenya Majaji Wakuu watatu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Jaji Chesoni, Jaji Gicheru na Jaji Mutunga. Tumewapa Uganda Jaji Mkuu Benjamin Odok; sasa hivi Jaji Mkuu wa Gambia Jalo ametoka Dar es Salaam. Kwa hiyo, kitabaki kuwa *primus inter pares,* kwa lugha ya kawaida *first among equals* (wa kwanza kwa walio sawa). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuvumilie tu, lakini hawazuiwi kubadili kama wakiona hawataki huyu wa kwanza kwa walio sawa aendelee kuwawakilisha. Ni hiari ya vituvo vya sheria. Na mimi kwa sababu pia nina *conflict of interest,* nitaacha jambo hilo liamuliwe na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uandikishaji wa watoto, Mkoa wa Ruvuma nao utafikiwa. Tulianza na *pilot,* sasa tutasambaza mikoa yote. Hii ilikuwa ni *pilot scheme* kuona ni jinsi gani itafanya kazi, lakini sasa itagusa watoto wa nchi yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Kibiashara, wazo hilo limechukuliwa linafanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria imeshakamilisha utafiti kuhusu Sheria mpya ya Usuluhishi, yaani Sheria mpya ya *Arbitration* na itakapoletwa tutashukuru sana kupata mchango wako ni jinsi gani ndani ya sheria hiyo tuwe na vifungu vya kuanzisha hii *International Commercial Arbitration.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mengi ya ndugu yangu, Mheshimiwa Lema, nimeyapokea. Amesema nisiwe muoga, inategemea nisiwe mwoga wa nini? Ninachoogopa ni kutenda dhambi na kuikosa pepo. Uoga huo wa kuogopa dhambi na kuikosa pepo, nitakuwa nao, lakini pia siwezi kuwa jasiri katika mambo ambayo hayahitaji ujasiri. Kwa hiyo, nimeyazingatia yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya Sheria ya *Money Laundering,* tutayafanyia kazi maoni haya yote aliyoyatoa. Kama kweli wako watu ambao wako ndani kwa *money laundering* ya dola 1,800 au kiasi fulani, basi ni suala la kupitia na kuona je, sheria ifanyiwe marekebisho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Lema amesema tumeongea, niseme katika kesi hiyo ya Mwale, wale wawili wengine ni ndugu zangu, lakini sasa mimi ni Waziri wa Katiba na Sheria, lazima niheshimu utaratibu. Sikupenda kulisema, lakini ni vyema niseme kwamba kati ya wale wawili walioshtakiwa na Mwale, wawili ni ndugu zangu. Sasa tuache sheria iende na ningependa jambo hilo lishughulikiwe kwa mkondo wa sheria ili baadaye haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndassa, masuala yako yamechukuliwa yote na yatazingatiwa kuhusu Mahakama hizo kumi na Mahakimu wanne tu, lakini pia ukarabati wa majengo ya Mahakama hizo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sabreena nakushukuru sana kwa uliyoyasema. Jambo lolote linaloondoa uhai wa binadamu linahitaji liangaliwe kwa umakini. Nchi yetu ilipita katika kipindi kigumu. Mauaji yale ya Rufiji na Kibiti hayakuwa ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wakati mwingine Watanzania ni vyema tukakumbushana, nchi moja ya Ulaya ilipokabiliwa na aina hiyo ya matukio ilitoa amri kwa askari wake *to shoot on sight,* sitaitaja humu ndani ya Bunge kwa sababu siyo vizuri kuitaja nchi nyingine, lakini Balozi wa nchi

hiyo alipokuja kuniona kwa mambo hayo nilimkumbusha, kwa sababu kipindi hicho nilikuwa naishi huko. Ilitoa amri ya ku-*shoot on sight* na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anajua. Sisi hatujafikia mahali, pamoja na matukio hayo ya idadi kubwa ya askari polisi kuuawa kutoa amri ya ku-*shoot on sight.* Kwa hiyo, nilimkumbusha Balozi yule kwamba hata ninyi mlipopita katika kipindi kigumu, mlifikia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tujitahidi kuyakabili mambo hayo, tuombe Mwenyezi Mungu atusaidie kuepuka hayo. Kwa sababu mwanadamu akiondolewa hekima, busara na kiasi, anakuwa hayawani. Usimwite mwanao hayawani, kwa sababu hayawani ni lahaja ya kimvita kwa maana ya mnyama. Mwanadamu akishakosa hiyo, anakuwa hayawani. Kwa hiyo, tumwombe Mwenyezi Mungu atuepushe kuingia katika uhayawani ili tusiuane hovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mabaraza ya Ardhi, nichukue tahadhari hiyo niliyosema, tumeshaiagiza Tume ya Kurekebisha Sheria ili ituletee mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea maoni mengi ya maandiko ambayo mengi tumeshayajibu na tutawapa Waheshimiwa Wabunge wahusika ili wapate majibu tuliyowapa na mengine yanafanana na haya ambayo yameletwa na Kamati, kwa hiyo, ili tuweze kuwatendea haki wale wote waliotuletea maoni yao kwa maandishi, wote tumehakikisha kuwa wanajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamehusu *Law School of Tanzania* ambayo tayari nimeshayaeleza, mengine yamehusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kuboresha utendaji wao ambayo tayari Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameyajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mengine yamehusu Tume ya Haki za Binadamu ambapo pia tumeeleza kwamba Tume ya Haki za Binadamu itatembelea sehemu zinazolalamikiwa yakiwemo Magereza na Vituo vya Polisi na taarifa itawasilishwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo ambao wameomba Mahakama za maeneo yao, nao pia tutahakikisha tunatekeleza kwa sababu tulitoa ahadi. Kwa mfano, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ambaye alikuwa ameomba ile Mahakama ya Mtae ambayo imejengwa mwaka 1926 ifanyiwe ukarabati. Tutahakikisha katika mwaka huu wa fedha Mahakama hiyo ya Mtae huko Mlalo ambayo ina umri wa miaka mingi inafanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir wa Viti Maalum CUF, naye amezungumzia kuhusu ukarabati wa majengo ya Mahakama, tutaendelea kuyafanyia kazi. Swali hilo hilo pia limeulizwa na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya kuhusu ukarabati wa Mahakama, tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuangalia maswali ya upande wa pili ili nihakikishe nimeyagusia pia. Mheshimiwa James Millya wa Simanjiro, Mbunge wa CHADEMA kuhusu Tume ya Utumishi wa Mahakama Tanzania kumshauri Mheshimiwa Rais kufanya teuzi kutoka ndani ya mfumo wa Mahakama kwamba kitendo cha kuteua Majaji kutoka nje ya mfumo wa Mahakama kutawakatisha tamaa watumishi walio ndani ya Mahakama kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumjibu Mheshimiwa Millya kwamba sifa za mtu anayefaa kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu zimeainishwa kwenye Ibara ya 109(7)(a) mpaka (c), hizo ndiyo sifa. Na mimi niseme toka Majaji waanze kuteuliwa kutoka katika sehemu mbalimbali, imeleta tija kubwa katika Mahakama. Kwa hiyo, hii *mixing* ya watu kutoka ndani na nje ya Mahakama kwenye *private practice* na kwenye taasisi nyingine ambayo haivunji Katiba ya nchi, maadamu inazingatia sifa na inazingatia *recommendations* za *Judicial Service Commission,* utaratibu huo ni vizuri ukaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA aliuliza kesi kuchukua muda mrefu Mahakamani. Napenda tu kumjibu

kwamba hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa ili kukamilisha kesi na kuhakikisha hazichukui muda mrefu. Hii ni pamoja na kesi katika kila ngazi ya Mahakama kuwekewa muda maalum wa kukaa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kila Hakimu na kila Jaji amepangiwa idadi maalum ya mashauri anayopaswa kumaliza kila mwaka na tatu, kila ngazi ya Mahakama iliyo na mashauri yasiyozidi umri uliowekwa katika ngazi inayoendeshwa, zoezi maalum la kuziondoa na kumaliza mlundikano, lakini pia kuendesha vikao vya *case flow management* na *Bench-Bar Meetings* zimesaidia sana kumaliza huo mlundikano wa kesi na kuupunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kesi ya Mwale ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA; Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA; Mheshimiwa Risala Saidi Kabongo, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA; na Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu CCM; majibu yameshatolewa. Kwa taarifa yenu, tarehe 20 Aprili, keshokutwa, Mahakama ya Rufaa itatoa uamuzi kuhusu *appeal* ya akina Mwale na hao jamaa wawili kuhusu suala zima la *nolle prosequi.* Kwa hiyo, tusubiri Mahakama ya Rufaa kesho kutwa itoe uamuzi kuhusu suala hilo ili tujue kesi hiyo inaendelea vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Serikali kuweka ukomo wa upelelezi wa kesi, swali ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, napenda kusema kwamba kesi zinatofautiana. Kuna kesi zinazohusisha maslahi ya umma na nyingine huhitaji ushahidi kutoka nje ya nchi na hivyo kuchukua muda mrefu. Hivyo, siyo rahisi kuweka ukomo wa upelelezi wa kesi kwa sababu inaweza kuwa na athari kwa mhanga mwenyewe na mhalifu. Ni muhimu kuwa na mizania kwa pande zote. Kwa hiyo, siyo rahisi kusema upelelezi ukome lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuchanganya watuhumiwa wa makosa madogo, swali lililoulizwa na

Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Viti Maalum, CHADEMA, niseme kwa kweli uhalifu wote ni sawa na *Penal Code* yetu ilikuwa *amended* kuondoa tofauti kati ya *felony* na *misdemeanor.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani palikuwa na tofauti ya *felony* na *misdemeanor,* lakini *Penal Code* Bunge hili hili liliondoa tofauti ya *felony* na *misdemeanor.* Kwa maana hiyo Tanzania leo hakuna kosa dogo wala kubwa, makosa yote yako sawa. Tukitaka turudi kwenye utaratibu wa *felony* na *misdemeanor* basi tubadili sheria hapa Bungeni ili tuwe na makosa ya *misdemeanor* ambayo ni makosa madogo na *felony* ambayo ni makosa makubwa. Bila kufanya hivyo, sasa Tanzania makosa yote yako sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mrundikano wa mahabusu Magerezani, hilo nalo limetolewa maelezo na litatolewa maelezo zaidi wakati wa Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati kuhusu vitendo vya ukatili kwa wanawake, Tume inajitahidi kuchukua hatua za kushughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lililoulizwa na Mheshimiwa Risala Saidi Kabongo, Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA, kuhusu Tume ina jukumu la kuchunguza uvunjwaji wa haki za binadamu na msingi wa utawala bora, mfano wananchi kukutwa kwenye viroba kando ya fukwe za bahari na kutekwa.

Napenda kusema kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Tume, Sura ya 391, taarifa zake za mwaka zinawasilishwa kwa Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya haki za binadamu na utawala bora Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Tume imekamilisha taarifa zake hadi mwaka 2015/2016 na zitawasilishwa Bungeni mwaka ujao wa fedha. Aidha, taarifa za mwaka 2016/2017 ziko tayari na zinasubiri Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema michango ya maandishi ni mingi na wote tumeijibu na tutahakikisha Wabunge wote wanapewa majibu yao kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kuhitimisha hoja yako. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, kwenye mshahara wa Waziri ambaye ndiyo Fungu la 41 Wizara ya Katiba na Sheria, majina nimepewa. Katibu.

Kif.1001- *Admin & Human Resources Mgt. Div.*......................................Sh. 5,316,735,000/=

**MWENYEKITI:** Wako wapi wahusika, Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ngoja tunawatambua tu kwanza, una haraka, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa wewe ni mrefu sana, Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Ryoba Chacha,

Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Waheshimiwa Wabunge muelewe uwiano wetu wa Vyama sina *control* nalo hilo, napokea maelekezo tu, tunaanza na Mheshimiwa Kombo.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu huu wa Tanganyika na Zanzibar tumeungana mwaka 1964, sasa tunaenda kuadhimisha miaka 54 ya Muungano wetu. Katika jambo ambalo lilikuwa ni muhimu na la kulifanyia kazi katia hatua za awali ni suala ambalo limo ndani ya Katiba ni utekelezwaji wa kikamilifu katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimesikiliza maelezo ya Waziri vizuri kuhusiana na kuanzishwa kwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha ambayo imo ndani ya Katiba, tena bahati nzuri kwa sababu ya umuhimu imezungumzwa katika sura nzima Sura ya Saba Ibara ya 133 na Ibara ndogo ambazo zipo hapo na Ibara ya 134 pamoja na Ibara zake nyingine, imezungumzwa kwa kina sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1996 ilianzishwa Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo ilitakiwa isimamie Akaunti ya Pamoja ya Fedha baina ya mapato ya Muungano, mapato yatakayolidhiwa na Tume hiyo kutoka Zanzibar na kutoka Tanzania Bara. Tume hii ndiyo ambayo ilipewa jukumu la kuchakachua au kupendekeza, kutoa mapendekezo ya mgawanyo, kutoa mapendekezo ya matumizi ya fedha za Muungano, hadi leo akaunti hii ya pamoja ya fedha haijaazishwa pamoja na umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana, sasa tumekuwa na vikao ambavyo havimo ndani ya Katiba, ambavyo haviongozwi na sheria yoyote ni vikao tu vya mapendekezo ni vikao tu vya kirafiki, ambavyo eti tuna maana kwamba hivi ndiyo vinaenda kutatua kero za Muungano. Ninataka *commitment* ya Serikali hapa leo, kwamba ni lini Akaunti hii ya Pamoja ya Fedha itaanzishwa ili ile Tume ambayo ilianzishwa mwaka 1996 iweze kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo huwezi kusema hapa eti unachagua kiongozi halafu majukumu yake unakuja kumpangia baada ya miaka 25. Naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri vizuri kama sikupata *commitment* basi intaondoka na shilingi ya Waziri. Nashukuru na ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ulipokuwa unasema kuchakachua ulikuwa na maana gani, una maana kukokotoa?

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuchakata.

**MWENYEKITI:** Kuchakata. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Makamba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Juma Kombo Hamad.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli jambo hili ni muhimu na lipo ndani ya Katiba, ni mahitaji ya Katiba. Kama alivyosema kwamba mwaka 1996 iliundwa ile Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission)* na ukisoma Katiba majukumu yake mle yameainishwa ikiwemo kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu masuala ya fedha na mgawanyo wa fedha kati ya pande zote mbili. Ilivyoanzishwa mwaka 1996 ikaanza kazi na ikafanya utafiti mkubwa sana, ikazunguza sehemu mbalimbali duniani na kutengeneza mapendekezo mahsusi kabisa kuhusu masuala ya vyanzo vya mapato ya kugharamia shughuli za Muungano, mgawanyo wa mapato ya Muungano na utaratibu mzima wa kifedha wa shughuli za Muungano. Kamati hiyo ikawasilisha ripoti yake Serikali mwaka 2006, miaka kumi baada ya kuanzishwa kwake. Kwa utaratibu wa Serikali ile ripoti ilikuwa lazima ishughulikiwe sasa ndani ya Serikali baada ya kuwasilishwa na ikashughulikiwa ukatengenezwa Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kupitisha mapendekezo ya ile Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo peke yake linaonesha tu dhamira ya Serikali ya kushughulikia mapendekezo ya *commission* ile ikiwemo kuanzisha mfuko a pamoja. Sasa vikao kadhaa vilivyopaswa kufanyika, bahati mbaya au bahati njema uwakilishi wa upande wa Zanzibar haukuwepo, kwa hiyo mjadala wa yale mapendekezo ukaahirishwa mara kadhaa. Kwa hiyo, ikaenda mpaka ikafika mahala mwaka 2011 hivi, ikaonekana kwamba yale mapendekezo yamechukua muda mrefu, kwa hiyo, inabidi zile takwimu na nini zipate mwamko mpya, kwa hiyo ikafanyiaka hivyo. Baadae ikaonekana kwamba badala ya kutengenezwa Waraka wa Baraza la Mawaziri na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili ujadiliwe kwenye Baraza la Mawaziri na kupitishwa basi uandaliwe Waraka mmoja ambao utamilikiwa na pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba yale mapendekezo yashughulikiwe na wataalam kwa pamoja, ikiwemo mapendekezo ya kuanzisha mfuko huo ili *paper* ile iwe moja ambayo inamilikiwa na pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndipo tulipoingia Serikali ya Awamu ya Tano ndicho ambacho tuliamua tufanye kwamba *paper* iwe inamilikiwa na pande zote mbili za Muungano. Kwa hiyo, zikaundwa timu za wataalam kutoka Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Fedha ya Zanzibar kazi ile sasa wameifanya na wanaileta sasa kwenye ngazi ya sisi wanasiasa kuamua ili hatimaye mapendekezo yale yaweze kupitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba maelezo niliyoyatoa kwanza yanaonesha dhamira ya Serikali ya kutimiza matakwa ya Katiba kwa kuchukua yale mapendekezo ya kuyafanyia kazi na tunaamini kwamba kikao ambacho kinafanyika tarehe 28 Aprili, hapa Dodoma cha wataalam na Mawaziri wa Wizara ya Fedha wa pande zote mbili hii ni moja ya ajenda ambayo itazungumziwa.

Kwa hiyo, naomba usichukue shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwenye mshahara wake kwa sababu Serikali hilo ni jambo ambalo inalishughulikia tayari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kombo baada ya maelezo hayo bado unahoji.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mwanzo tumeungana ni miaka 54 sasa tatizo kubwa la Muungano, changamoto kubwa la Muungano, ni mgawanyo wa fedha za Muungano ambazo wadau wote wa Muungano wa Tanzania Bara na wa Zanzibar hawajui wakahoji wapi suala la mgawanyo wa mapato ya Muungano hawajui! Siyo Mbunge, si Waziri si mtu wa kawaida hajui akahoji wapi mgawanyo wa Muungano unapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri January Makamba ameongea hapa kuanzia mwaka 2006 ripoti iliwasilishwa na wataalam, ripoti hizi zimewasilishwa nyingi na mapendekezo yametolewa mengi, nataka *commitment* ya Serikali lini mchakato huu utafikia maamuzi, lini? Nahitaji *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa jambo hili na kwa sababu ya nia njema tuliyonayo ya suala hili la Muungano wa Tanganyika na Zanzibar naomba uniruhusu tu nitoe hoja ili tulijadili kwa kina na naamini kwamba mwisho wa siku tutapata maafikiano na akaunti hii itapatikana na matatizo yote ya Muungano yataisha na tutaendeleza Muungano huu kwa amani, utulivu na mapenzi makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Umetoa hoja haijaungwa mkono.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mimi naanza kuwatambua, tutende haki Muungano wawili kwa wawili tu; Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Naibu Waziri wa Fedha Dkt. Kijaji, Mheshimiwa Ali Khamis na Mheshimiwa Lema.

Haya tunaanza na Mheshimiwa Ali Khamis.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaunga hoja ya Mheshimiwa Juma Kombo. Jambo hili ambalo limo katika Katiba nimepitishwa mwaka 1977. Kwa hiyo, mwaka 1977 limewekwa jambo hili kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka1996 ndiyo Tume imeundwa, miaka 20 kabla ya kuundwa kwa Tume. Baada ya kuundwa Tume mwaka 2003 ndiyo imetengenezewa sheria kufanya kazi, mwaka juzi hapa nilichangia hoja hii kumuuliza Waziri wa Fedha na majibu yake haya ambayo leo yametolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaunti hii sasa hivi toka imependekezwa kuundwa miaka 41 bado tu kuna mchakato miaka 41, mchakato gani huo, vikao gani hivyo ambavyo vinakaa haviishi? Leo Mheshimiwa Waziri wa Muungano anasema kwamba wana kikao tarehe 27 inaonekana wana ajenda nyingi kweli kwa sababu alivyojibu hoja hapa kuna kero chungu mzima za Muungano unakuja kuzikalia kikao na hili pia nalo limo kwenye kikao hicho inaonyesha hawa wana ajenda nyingi sana za kujadili masuala ya Muungano siku ya tarehe 27. Haiwezekani upande wa pili wa Muungano iwe namna kama hii ni sawa sawa na timu ambayo ishashinda sasa hivi wanapasiana wanapeka kule ili muda upotee haiwezekani! Ifike pahala lazima tukubaliane tuambiwe na Serikali kwamba akaunti hii lini inaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Muungano ni masuala *very serious,* hii biashara ya kuichukulia Zanzibar kama Jimbo ama kama Mkoa ni jambo ambalo linawatia hasira sana wenzetu. Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 133 imesema suala la Akaunti ya Pamoja, wewe ni sehemu ya watunzi na marekebisho ya Katiba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hayati Karume na Hayati Nyerere walitumia siku sita kuunganisha Tanganyika na Zanzibar; ninyi mnatumia zaidi ya miaka 20 kufungua akaunti. Mjipime kama ninyi ni wanafunzi wa Mwalimu Nyerere ama ninyi ni wananfunzi sijui wa Rais gani. Kwa sababu haiwezekani suala la akaunti ambalo liko Kikatiba likachua miaka zaidi 20 na Muungano wa nchi zenyewe mbili ukachukua chini ya siku saba. Tulipombana Waziri wa Fedha hapa alitoa *commitment* ya jambo hili mwaka jana mpaka leo bado mnadanadana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashauri wenzetu wa upande wa Zanzibar kuweni *serious,* haki haiombwi lazimisheni hii haki ya msingi kwa sasa, kwa sababu Serikali haina majibu na ingekuwa na majibu ingekuwa ni utii wa Katiba na kwa sababu mmeshindwa kutii Katiba kwenye mambo mengi ya msingi sasa mnaanza kuvunja kila kipengele, mwisho wake sasa hata huyu mnayemsaidia kuvunja Katiba naye mtakuja kumvunjavunja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumjibu mtoa hoja kwamba

siyo kweli kwamba tangu miaka yote ya Muungano hakuna jambo lililofanyika. Niwaambie tu kwamba, kwa utaratibu ulikuwa unatumika Serikalini kuna *items* nyingi sana ambazo zinaruhusu Serikali ama mambo ya nchi yaweze kufanyika yamefanyika, mengi ya kisera, kikodi, kifedha pamoja na kuruhusu shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi kuweza kufanyika. Ningeweza kutaja vingi lakini kwa ajili ya muda niwaambie tu kwamba awe na kumbukumbu kwamba tulipofika mwaka 2014/2015 kama Taifa tulikuwa na jambo kubwa ambalo lilikuwa linakwenda kumaliza sheria zingine zote zinazokinzana ambayo ilikuwa ni jambo la Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Katiba iliyopendekezwa yeye mwenyewe ni shahidi anakumbuka kwamba moja ya vipengele tulivyotumia muda mwingi sana kujadili vilikuwa vinahusiana na vile ambavyo vinaleta kero kwenye Muungano. Tangu tupite mwaka 2015 mpaka sasa ndiyo ambayo tulielezea jana wakati tunapitisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Tumeshaenda kwenye vipengele vingi sana, hiki ambacho kimesalia ambacho ni cha mwisho tu ambacho kimsingi siyo akaunti ambayo inagombaniwa, kinachojadiliwa kwenye mijadala mingi ni nini kinachotakiwa kuwa kwenye akaunti na hivyo ndivyo ambavyo tumeshavimaliza, tumeshakubaliana katika mafungu mengi, kwa hiyo yanayotakiwa haya mengine ni ya *procedure* tu, kwa sababu *issue* ya akaunti siyo jina la akaunti, ni nini kinachotakiwa kuwa kwenye akaunti na hao yote tumeshayaongelea na jana tumeongea wakati tunapitisha bajeti ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu hii ni hoja ya msingi kwa maana ni jambo ambalo linatakiwa likamilike, basi uridhike kwamba kwa kuwa tumeshakamilisha hivi na tunavyoenda na Makamu wa Rais analisukuma kwa nguvu kubwa sna na Mheshimiwa Waziri anaratibu kwa nguvu kubwa sana, wewe ruhusu na kama unadhani kwenye yale ambayo yanafanyika kuna hoja zingine za ziada ambazo unatakiwa uchangie toa maoni kwenye ile timu ambayo inashiriki kwenye vikao hivyo ili tuweze kuboresha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia hii fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumuomba mtoa hoja aachie tu shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimeshtuka nilipomuona Mheshimiwa amesimama kwa hoja hii kwa sababu jana Mheshimiwa Makamba ameisema vizuri sana, sasa kuona tunarudia jambo lile lile yaani jana tu, leo tumesahau tunalirudia tena, napata wasiwasi kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba sana ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira na Muungano amesema vizuri hatua tuliyofika ni nzuri sana, kilichosalia ni kitu kidogo tu na chenyewe siyo mjadala ni kikao ndiyo kimebaki na kikao chenyewe ni tarehe 28 Aprili, kwa hiyo ni siku chache, wiki moja na nusu iliyobaki leo tunashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri mimi siamini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge sana tu tumeshakaa na mimi vya kutosha, tumeongea mengi kuhusu jambo hili na wewe unafahamu, tumeshamaliza hatua kubwa ambayo ilikuwa inafanyiwa kazi na wewe kama unavyokiri ni jambo la msingi sana, ni jambo nyeti ambalo lilihitaji vikao vingi, vikao ambavyo vinahitaji majadiliano na makubaliano na sasa Serikali imesema jana leo tunasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana mtoa hoja kwamba akubaliane na hoja iliyoko mezani kwamba jambo hili linaenelekea kufika mwisho na uzuri bajeti ya Wizara ya Fedha inakuja, Bajeti Kuu ya Serikali inakuja hapa. Kwa hili la leo amuachie Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili tuweze kulimalizia jambo hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Bado tu unaendeleza? Haya funga hoja yako tumalize.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** *Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kawaida ya mtu laghai kuwa na lugha nyepesi na ya ukarimu sana.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba Waheshimiwa Wabunge tafadhali nakuomba sana futa kauli yako ya ulaghai.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuta. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kawaida hata wanaume wakati tunapokwenda kuposa mke, hata kama ni wavuta bangi, hata kama ni walevi wa kuanguka, hata kama *whatever* tutakavyokuwa kwa muda huo tunaweza tukavaa kanzu nzuri, tukazungumza maneno laini, maneno ya busara, tunaweza tukapiga hata koti lakini siku ukipewa mtoto wa watu, wala huoni hasara kumtwanga makofi, kumpiga ngumi, kumnyima chakula, kumnyima nguo na kumfanyia kila aina ya kitendo kibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili na umuhimu wake kwa sababu sikupata *commitment* ya Serikali ni lini suala hili la akaunti ya pamoja, suala la kukaa vikao miaka 13 hili haliwezekani, tupige kura kukamilisha hii hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa tutapiga kura ndiyo, lakini Waheshimia Wabunge hizi kauli nasema anayepigwa konzi hapa ni nani? Mwanamke hapa ni nani? Tafadhali sana naomba tuheshimiane humu. Ongeeni lugha, unaweza ukachangia hoja yako kwa lugha ya Kibunge tu, lakini lugha za kihuni nasema haziruhusiwi humu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ninawahoji sasa.

*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na kesi nyingi ndogo ndogo na kusababisha gharama kubwa kwa watuhumiwa wa kesi hizo kwa kusafiri hasa wale wanaokaa mbali na Mahakama, lakini kwa kubeba mashahidi kwa gharama zao kupeleka kwenye Mahakama hizo za mbali, bila kujua kwamba mtuhumiwa anaweza akaendelea kuwa mtuhimiwa au akawa siyo mtuhumiwa baada ya kesi kuhukumiwa.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha Mahakama za kutembea *(Mobile Courts)* ili kupunguza mrundikano wa kesi Mahakamani, kupunguza mrundikano wa mahabusu kwenye Magereza yetu, kupunguza gharama za kuwalisha mahabusu hao na kupunguza gharama za kuwatibu mahabusu hao wanapopata maradhi wakiwa Gerezani.

Naomba jibu zuri kwa Mheshimiwa Waziri ambaye namheshimu sana vinginevyo nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kukubalian na Mhesimiwa Munde kwamba ni vizuri tukawa na mfumo wa kutoa haki ambao unawafikia wananchi wengi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ni kubwa sana kwa mfano, tumepanga kuwa na Mahakama Kuu katika kila Mkoa, lakini mpaka sasa tunazo Mahakama Kuu 14 tu, tumepanga kuwa na Mahakama za Mwanzo katika kila Kata na tuna Kata 3,963 lakini mpaka sasa tuna Mahakama za Mwanzo 960 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia yapo maeneo ambayo yana changamoto kubwa ya kijiografia. Wilaya ya Simanjiro, Wilaya ya Kilombero, Wilaya ya Manyoni ni Wilaya kubwa na mtawanyiko wa watu ni mkubwa na ni kweli kabisa hilo limechangia sana katika kuchelewesha haki kutendeka kwa watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, Mahakama ya Tanzania katika mpango wake mkakati wa mwaka 2015/2020 kwa kupata uhisani wa Benki ya Dunia mkopo, imeanza mradi wa kuanzisha Mahakama zinazotembea yaani *mobile court* lakini pia Mahakama za madai madogo madogo *(small claims court)*. Lengo la Mahakama hizo ambazo wengine wanaziita *justice on wheel program* yaani Mahakama ambazo zinatembea, Serikali imechukua hatua na ndiyo manaa sikulisema kwa kirefu ndani ya hotuba kwamba katika Bunge hili, katika mabadiliko ya sheria *(miscellaneous amendments)* ambazo tunapanga kuzileta, moja itakuwa ni ya kuyafanyia *amendments, The Magistrate Court Act* ili kuanzisha hizi *mobile court* na pia kuanzisha zile *small claims court* ili kama alivyoeleza kuhakikisha mashauri mengi yanatatuliwa na wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo hili siyo la leo lilianza wakati wa Jaji Mkuu, Philip Terrifor Georges lakini kwa sababu ya uwezo na matatizo mbalimbali halikutekelezwa. Kwa hiyo, tunategemea kwamba mara baada ya sheria kuwa imefanyiwa mabadiliko katika Bunge lijalo la mwezi Septemba basi tutaanza na *pilot* ya hizi *Mobile Court* na ambazo kwa sasa zitaanza katika Jiji la Dar es Salaam na Jiji la Mwanza. Katika maeneo ya vijijini tutaanza na Wilaya ya Ngorongoro na Wilaya ya Handeni na kama nilivyosema hiyo ni kufanya majaribio ya awali ili kuweza kujiridhisha na kuboresha zaidi; baada ya hapo sasa maeneo mengi ya Tanzania ambayo yanahitaji aina hiyo ya Mahakama yatapelekwa ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Ukerewe. Lengo baadae kwa Wilaya ya Ukerewe ni kununua boti ambayo pia itazunguka katika visiwa mbalimbali ili kuhakikisha wananchi katika vile visiwa pia wanapata haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imekwishafanya utaratibu, mkopo umeshapatikana Benki ya Dunia na Mwezi Septemba naamini Bunge lako litapitisha sheria ya uwepo wa Mahakama hizi *mobile court* na hizo *small claims court.* Naamini kwa maelezo hayo Mheshimiwa Mbunge Munde atakuwa ameridhika na hivyo atairejesha shilingi kwa mimi ndugu yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Munde baada ya maelezo hayo mazuri ya Mheshimiwa Waziri unesemaje?

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuunga mkono kabisa Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake mazuri na ambayo nina imani Watanzania wengi watakuwa wamefurahi kutokana na majibu mazuri aliyoyajibu hapa na ninamrudishia shilingi yake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ulikuwa hujaitoa, ulikua umekusudia. Tunaendelea Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba majibu ya Waziri anipe ufafanuzi kuhusiana na zoezi holela ambalo lilikuwa linafanywa na uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo kulikuwa na ukanyagwaji mkubwa wa Sheria na Katiba na uvunjaji mkubwa wa misingi ya Sheria na Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ilivunja Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kifungu cha158 ambacho kinazuia ku-*publish* picha za watoto. Wote mtakuwa mashahidi lile zoezi lilikuwa linaendeshwa kwa kamera. Pili, lilivunja Katiba ya nchi, Ibara ya 16 sina haja ya kuisoma Mheshimiwa Waziri anaifahamu ambayo inahusiana na faragha ya maisha ya mtu binafsi na familia yake. Tatu, zoezi halikushirikisha hata Wizara. Tulishuhudia Naibu Waziri aki-*tweet* kuwa hapendi jinsi zoezi linavyoendelea. Mwisho, Tume ya Haki za Binadamu haikuhusishwa kabisa. Hivyo, naomba ufafanuzi bila ya hivyo nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria maelezo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *paternity*, suala la nani ni baba wa mtoto ni muhimu kwa sababu mbalimbali. Moja ni suala la *identity*, mtu angependa kumfahamu baba yake ni nani na suala hilo la mtoto baba yake ni nani limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa nchi za Magharibi, kwa sababu nchi za Magharibi mtoto na mke ni *commodity.* Kwa jamii nyingi huku tulikuwa hatuhangaiki sana na suala la *biological father* kwa sababu *father would be social and not biological.* Kwa sababu dunia tunaingiliana ndiyo maana tumeanza sana kuhangaika na *biological father.* Kawaida *father would be social, most of us in this House and in Tanzania we are social fathers, we are fathers to our children because of socialization. Biologically, we are not 100 percent sure and we should not trouble ourself to know, whether we are biological father of the kids we are taking care of or not. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu jamii inabadilika na inaingiliana sana hilo limekuwa suala la msingi sasa na limekuja pia hata na suala la *DNA* na sitaki kuingia huko, humu wako watalaam wa *medicine* wanafahamu hata *DNA* inategemea umetumia aina gani ya mashine na aina gani ya zile kemikali *(re-agency)* na zile maabara zinatofautiana ziko zile za *reference*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kweli kabisa kumekuwa na wimbi hilo la kutaka kujua *biological father* kwa minajili ya wengine ya *identity* lakini pia kwa minajili ya chini ya sheria ili yule mtoto aweze kutunzwa na jukumu la watoto ambalo watu wengi hawafahamu, watoto *essentially* ni mali ya Taifa, Taifa lina jukumu la kuhakikisha watoto wanalelewa vizuri. Kwa hiyo, zoezi zima ambalo lilikuwa linaendelea na limekuwa linaendelea katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa maoni yangu mimi limekuwa na msukumo

huo, katika msukumo huo wa aina yoyote ile ya kampeni inayofanyika katika jambo, linakuwa na udharura na kazi ya wale ambao wamepewa majukumu ya kusimamia sheria hiyo yenye kutoa tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nnampongeza sana Waziri wa Afya alilizungumza mbele ya Makamu wa Rais kwamba jambo hili linahitaji faragha na nvyombo vya habari vilieleza na nimshukuru sana Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Ndugulile na yeye ali-*tweet* kulieleza. Lengo zima lilikuwa ni kuhakikisha kwamba zoezi hilo la kampeni ambalo ningewashauri Watanzania tusipende sana kuiga mila na desturi za Magharibi za kung'ang'ania kutaka kujua *whether you are biological father* badala yake tukubali kuwa *social fathers* ili *pressure* hiyo ipungue, lakini tukiendelea kutaka *biological fathers* na kuendelea na kampeni za aina hii zina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema tu kama mzaha ziko jamii ambazo ukifanya jambo hilo watakushangaa, kwa sababu jamii nyingi za Kiafrika hakuna mwanaume ambae alikuwa anakuwa *impotent* na familia ikijua ni *impotent* itamuolea mke, binamu yake ili siri ibaki ndani na mara nyingi atapewa kazi ya kusafiri sana ili ndugu zake wamsaidie. Watoto watakaozaliwa ni watoto wa ile familia na ile jamii. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, pamoja na maelezo haya yote najua kabisa Maafisa wa Ustawi wa Jamii walikuwepo na kadhalika, ni vizuri tumekuwa na kampeni lakini ningewahamasisha Watanzania tusihangaike sana kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi kama mshauri wa ndoa huko ninakoabudu nimekuwa ninawazuia watu kufanya *DNA.* Hebu fikiria umefanya *DNA* na yule mtoto ametambulika ni wako, hivyo atakutazamaje baada ya hapo? Kwamba baba alimuona mama yangu ni kahaba, siyo mwaminifu kwa sababu majibu siyo lazima yaje siyo wako, sasa yamekuja ni mtoto wako na yeye amejua wewe baba hukunipenda mimi, hukudhani i ni mwanao na mara

nyingi niseme tu Mwenyezi Mungu hata katika vitabu, Suleiman katika Biblia alikuwa mtoto wa nje ya ndoa na ndiyo Mungu alimbariki, mara nyingi watoto wa aina hiyo ndiyo Mungu huwapa baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningemuomba Mheshimiwa Mlinga anirejeshee shilingi yangu na tutahakikisha kwamba kampeni hizi kwa kadri tunavyoweza kwa indhari iliyotolewa na Waziri wa Afya na indhari iliyotolewa na Naibu Waziri wa Afya yafanyike kwa faragha na kwa ukarimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga baada ya maelezo hayo.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametoa majibu mazuri, lakini naomba niseme kitu kimoja, kwanza naomba ni-*declare interest* sijapelekwa kwa Makonda siko kwenye *list* ile kwa hiyo naomba mnielewe.

Naomba niseme kitu kimoja, Makonda binafsi ni rafiki yangu tumeshamuita huku Bungeni, *damage* ya hili kwanza hii Sheria ya Mtoto kifungu cha158 (d) ukii-*violate* faini yake ni milioni tatu hadi milioni 15. Wamama waliokwenda pale ni 17,000. Watu 17,000 mara milioni 15 ni zaidi ya bilioni 225, sasa kwa mfano wakaenda mahakamani Serikali itapata hasara kiasi gani? Hapo hatujapata *Bombadier* tatu? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni udhalilishaji wa mihimili mingine ya Serikali. Kwa mfano, pale wametajwa Wabunge 47 wakati aliyefanya Mlinga na Mlinga wakati anafanya pale hakufanya kwa koti la Ubunge, nilifanya mambo yangu mimi mwenyewe binafsi, lakini wametajwa Wabunge kwa hiyo ni udhalilishaji wa mihimili mingine, hii itakoma lini nataka *commitment* ya Serikali, pia lile zoezi lilileta hamaki katika Taifa letu hata humu Bungeni kuna watu

hawakukaa sawa hadi ilipotajwa lile zoezi litakoma lini, nataka *commitment* ya Serikali sina haja, lini itakoma natoa hoja Bunge lijadili sawa Serikali iji-*commit* lini tabia hii itakoma? *(Makofi)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lakini mbona mmemuhamasisha kutoa hoja? Alikuwa amekubali maelezo ya Serikali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka *commitment* ya Serikali tabia hii itakoma lini? Ndiyo maana nimetoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza. Mheshimiwa Mlinga, Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tuwe *fair,* wawili tu kwa hoja hii. Mheshimiwa Mlinga ni mtoa hoja, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Kasuku.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Wanawake mbona huwapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msabaha, wametosha.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mussa Mbarouk.

**MWENYEKITI:** Haya tunaanza, Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ni nyeti sana, kwanza nataka nianze wale wanawake waliokwenda kule waliolewa na nani? Halafu wanawake hawa wamekwenda kule wakasema wamezaa watoto wengine ni watoto wa wakubwa tukaona viongozi ambao wametumikia Serikali hii wanadhalilishwa kwa kuambiwa wale ni watoto wao, halafu baadae wanawake wale wale wakarudi kuja kukataa kwamba wao hawakusema na wakaomba radhi, sasa kitu kama hiki wale viongozi wanaume ambao walidhalilishwa je, nyuso zao wataziweka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake hawa kama kweli wana haki madhubuti ya kutetea kama mtoto unamtetea mtoto leo nilikwenda pale kwa Mheshimiwa Makonda ukienda ukasema mtoto huyu kanizalisha fulani ile ni starehe yao wawili walivyofanya huko kitandani ilikuwa vipi mpaka wewe unaenda kule? Hawa wanawake na huyu Mkuu wa Mkoa wanachukuliwa hatua gani kwa kudhalilisha wanawake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja kuwa Mheshimiwa Makonda achukuliwe hatua kwa sababu ni udhalilishaji wa kinjinsia kwa watoto na kwa akina mama kwa sababu kuna Wizara ambayo inahusika na mambo hayo na ni kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mambo haya ya kuwaita watu Dar es Salaam na kufanya *DNA* kwa watoto ni kuwaponza hawa watoto. Kwa mfano, leo katika Vyombo vya Habari wametangaza kwamba Bukoba kuna baba amewachinja watoto wawili mapacha wa miaka minne na mitano. Kwa mwanaume kuambiwa watoto siyo wake au ametelekeza watoto inakuwa ni aibu. Hili jambo la kuwaita akina mama waende na watoto wengine

walikwenda pale wakijua wanakwenda kufanya *deal* labda watapata fedha watalipwa fidia na kadhalika sasa hili Mheshimiwa Makonda lazima aangalie kwamba analofanya ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapa Mlinga kwamba Sheria ya Mtoto imekiukwa, naitaka Serikali ikataze jambo hili mara moja na Mheshimiwa Makonda aonywe na achukuliwe hatua za kisheria juu ya jambo hili likome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wasidhalilishwe na asilete fitna kati ya baba na watoto, kwa sababu mtoto anapozaliwa kama anaishi vizuri na mama yake ataoneshwa tu baba yakea na atamjua au anaweza kumtafuta hata mwenyewe baba yake ni nani, lakini siyo kuwaita watu katika mazingira yale, ule ni udhalilishaji mkubwa.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

**MHE. MWANNE J. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naitetea hoja hii, kwa sababu mpaka hivi leo wanaume 602 wamekubali. Sasa hivi sheria yetu ya mwaka 1971 inamruhusu mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa kulipwa shilingi 100, kwa hiyo, akina mama wengi wamekwenda kwa uchungu wanazalishwa wanaachwa, labda alichokosea ni kutoa hadharani, lakini mimi nasema kama mwanamke acha nichukiwe lakini hana haki ya kufanya hivyo, namuunga mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mlinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa najiuliza mara nyingi sana huyu Makonda anapata wapi huu ujasiri, haya yanayofanyika ndani ya Taifa hili, ambayo hayajawahi

kutokea tangu nchi hii imeumbwa yanafanywa na Makonda na watu wanashangilia, tutakuja kuleta matatizo hapa nchini. Imefikia hatua tunapigiwa simu huko ndoa zinataka kuvunjika umetajwa na wewe umo, haya mambo gani tunayofanyiana na Makonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Makonda achukuliwe hatua na Bunge hili amelidhalilisha anataja Wabunge kama ana watu wake anawatafuta aendelee kuwatafuta kimya kimya, sasa baada ya Dar es Salaam mnakwenda kutafuta watoto hao mkoa gani mwingine mmepanga? Hii biashara ni hatari sana watu waanze kuishi kwa hofu tupu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwalimu Bilago ahsante. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru mimi naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nyingi inazofanya nzuri kabisa kwa asilimia mia moja, lakini naona tunakoelekea tunaenda kutokuwa kabisa na Wakuu wa Mikoa kwa sababu Serikali ina Mawaziri na Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu wanafanya kazi nzuri mpaka mikoani mpaka inapelekea na Wakuu wa Mikoa wanakosa kazi wanaanza kushughulika na hizi kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua tu ni suala la uelewa kwamba wako watu tunawafahamu hawajapata bahati ya kupata watoto, yaani baba na mama imeshindikana kupata mtoto, wakaenda kupandikizwa, watoto ikashindikana kwa sababu pia pengine mayai yanafanana, mnisikilize vizuri. Baada ya kushindikana ikabidi mmoja kati yao ambaye ni mama akanunue mayai yanayouzwa hospitali, akapandikizwa akabeba mimba, sasa huyu mtoto atakapozaliwa naye ataitwa pale ili baba yake aje amtunze? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kuwa, zoezi ambalo limeendeleshwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kama alivyosema Waziri wa Katiba na Sheria lilikuwa ni zoezi halali, kwa sababu Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 inatoa mamlaka kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii kusimamia masuala yote ya matunzo na malezi ya mtoto, lakini sheria imekasimu madaraka kwa Maafisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri na Mikoa ambao wako ndani ya Mkoa wa Mheshimiwa *RC Makonda.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wito zoezi lile liliendeshwa na Maafisa Ustawi wa Jamii kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupo kwenye Kamati.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Waziri wa Katiba na Sheria, kasoro iliyojitokeza ilikuwa ni suala la faragha hasa kulinda haki ya mtoto.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize, nisikilizeni! Naomba Waheshimiwa Wabunge wanisikilize.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge!

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa tahadhari ile, sasa hivi tumeona zoezi lile likiendeshwa bila kuwa-*expose* watoto tumeona mpaka magazeti wakifunga

sura za watoto, kwa hiyo kwa kiasi fulani zoezi lile ni halali, lakini tunataka kukiri kwamba wananchi bado wana changamoto ya uelewa wa kupeleka mashauri ya matunzo ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa mujibu wa sheria ya mtoto wanatakiwa kwenda kwa Maafisa Ustawi wa Jamii, alichofanya Mheshimiwa Makonda kama alivyosema Waziri ni kampeni ya kuwahamasisha wanawake waende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba mwanangu Mheshimiwa Mlinga arudishe shilingi kwa sababu zoezi lile limefanyiwa marekebisho baada ya Wizara kutoa maoni na ushauri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichofurahi Wabunge wamelijadili na Serikali imeona kwa namna gani Waheshimiwa Wabunge ambao ni watetezi wananchi wamelipokea lile zoezi, kwa hiyo mimi narudisha shilingi yangu, lakini *message* imefika na naomba *commitment* ya Serikali masuala haya yasirudie tena katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo ya kina kuhusiana na vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya akina

mama na watoto, kwa sababu vitendo hivi sasa hivi vimekithiri sana hapa nchini kiasi kwamba pamoja na kuwa hapa Bungeni tulipitisha ile sheria ya msaada ya huduma za kisheria, lakini bado matendo haya yamekuwa yakiwatesa sana watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala kwanza kabisa vitendo hivi vimekuwa vikihatarisha hata maisha ya watoto wetu, watoto wengi wamepata vifo, watoto wengi wamepata hata maambukizi ya UKIMWI, watoto wengi wamepata hata ulemavu wa kudumu kutokana vitendo hivi vya kubakwa na kulawitiwa, lakini bado Serikali haijaweza kuchukua hatua zinazotakiwa pamoja na kuwa zipo haki za binadamu haya matendo yanapokwenda Mahakamani bado hayajapewa kipaumbele, kesi zinachukua muda mrefu sana na nyingine kwa sababu wale watuhumiwa wanatumia wanasheria kwa hiyo unakuta wale wanaotuhumu hizi kesi wamekuwa hawapati haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano halisi katika Mkoa wangu wa Iringa kwamba mtu alituhumiwa akaenda Mahakamani na kule Mahakamani akapewa dhamana lakini alikuja kuhukumiwa miaka 30 yule mtuhumiwa hayuko Mahakamani, unaona jinsi gani ambavyo kesi hizi za ubakaji na ulawiti zimekuwa zikiathiri sana watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo lilikuja swali hapa Bungeni, Wabunge wengi sana walijadili lile swali kwa mfano Mheshimiwa Faida aliweza hata kulia kabisa hapa hadharani, kwa hiyo, ninaomba Serikali ituambie sasa mkakati halisi wa kumaliza hizi kesi kwa sababu kwenye Mkoa wetu wa Iringa hivi vitendo vimeathiri kwa kiasi kikubwa sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kwa mamlaka niliyonayo naongeza muda usiozidi dakika 30 ili tumalize shughuli iliyo mbele yetu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Ritta

Kabati. Ni kweli mambo haya yamekuwa akiyafuatilia sana yanapotokea hata katika kushauri tu namna nzuri ya kwenda na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni tatizo la kijamii ambalo kushughulikiwa kwake siyo kwa upande mmoja kwa maana ya siyo kwa utaratibu wa kisheria tu; kwanza Serikali imechukua hatua kubwa ya kuiweka sheria kali sana punde mtu anapothibitika amefanya vitu vya aina hii, tatizo tunalokutana nalo ni jinsi ambavyo sisi kwenye jamii tumekuwa watu wa kuficha matendo haya yanapotokea, hilo ndilo ambalo limekuwa tatizo kubwa pale Serikali ambapo imeweka sheria kali taratibu zipo, lakini inalotokea watu wanamaliza kifamilia na wakati mwingine wengine wanajificha kwenda kutoa ushahidi, wakati mwingine wanaficha matukio yanapokuwa yametokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu ni vema kama Wawakilishi wa Wananchi kwanza tulifanyie kampeni kubwa sana kwa wananchi kule, kwamba inapotokea tatizo hili watoe taarifa mapema lakini pia mtuhumiwa anapokuwa ameshakamatwa tuache utaratibu wa kuelewana kwa ngazi za kifamilia au kijamii ili sheria iweze kuchukua mkondo wake na Serikali kama ambavyo imeshatunga sheria kali hukumu ziweze kutolewa na hao watu waweze kupata mafunzo na kuacha kufanya vitu hivyo ambavyo ni vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nimtaarifu tu Mheshimiwa Zungu kuwa timu ya Yanga imefuzu yeye aendelee kushangilia Njombe kule. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini bado hili jambo siyo dogo kwa kiasi hicho kwa sababu jambo hili limekuwa likiwaathiri watoto wetu kisaikolojia hata na wazazi pia jambo nimetolea mfano kwamba kwenye haya Mahakama zetu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nenda moja kwa moja unachotaka sasa, maana wakati huo sasa ni kutoa shilingi kama unataka kutoa shilingi.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha kwa mbwembwe kubwa sana hapa Bungeni Sheria ya Msaada wa Kisheria lakini bado haujawekwa mkakati jinsi gani hawa watu wanaweza wakasaidiwa, kwa sababu unaona kwa mfao Iringa kule vijijini hata *NGO* zenyewe haziwasaidii kisheria wale watu wanaofanyiwa hivi vitendo, sasa tunataka mkakati na *commitment* ya Serikali kuhusiana na msaada wa kisheria kwa watu wanaofanyiwa hivi vitendo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea Waziri *respond* tu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa hoja hii muhimu sana inayopambana na ukatili kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana nae kwamba tatizo hili limekuwa ni kubwa na linaongezeka na kwa kuzingatia hilo Wizara yangu kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuja na mpango wa kitaifa wa kukomesha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto *(National Plan of Action to end Violence Against Women and Children in Tanzania 2017/2018 to 2021/2022),* na katika kutekeleza mpango huu ili kukomesha vitendo vya ukatili wa jinsia Tume imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, imepokea jumla ya malalamiko 16 yaliyohusu vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupitia dawati la wanawake na watoto lililoanza mwaka 2006. Malalamiko yote 16 yamefanyiwa kazi na walalamikaji wamepata haki zao. Pia kupitia Mradi wa *Enhance Access to Justice and Realization of Human Rights to all in Particular Women* unaofadhiliwa na asasi ya kiraia ya *Legal Service Facility,* Tume imetoa elimu kwenye Manispaa na Halmashauri za Miji na Mikoa mitano

ya Manyara, Mara, Mtwara, Mbeya na Shinyanga. Maadam sasa tumefahamu kwamba Mkoa wa Iringa nao una matatizo katika awamu inayofuata pia elimu hiyo itatolewa pia kwa Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu msaada wa kisheria, ningependa kutoa taarifa tu kwamba tayari tumekwisha zipitisha Kanuni za msaada wa sheria pamoja na kuwateua wasajili kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ili kuhakikisha sasa tunakuwa na mfumo wa kupambana na mambo kama haya. Kwa hiyo, tayari mpango upo, mafunzo yameanza kutolewa na pia tutaona jinsi ya kwenda Iringa ambako pia nako kuna matatizo hayo ambayo yameongezeka ili tuweze kuyatatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo namuomba Mheshimiwa Ritta Kabati basi airejeshe shilingi akiwa ameridhika na maelezo haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla sijaendelea niseme kama sikupata maelezo kwenye hoja yangu hii nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria, kanuni na taratibu. Sisi sote, mimi Ryoba na wewe Mwenyekiti na Wabunge wote tuliapa kulinda Katiba hii. Sasa niruhusu tu niisome Katiba hii *article 3(1)* inasema; *"The United Republic is a democratic circular and socialist state which adheres to multiparty democracy."* Kwa hiyo, nchi yetu ni nchi inayofuata mfumo wa vyama vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu *principles of multiparty democracy* na tuna Sheria ya Vyama vya Siasa. Nitaomba nisome kifungu cha 11(1) kinasema: *"Every party which has been provisionally or fully registered shall be entitled; (a) to hold and address public*

*meeting in any area in the United Republic after giving notification to the Police Officer In Charge of the area concerned for purpose of publicizing itself and soliciting for membership."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano ya Vyama vya Siasa imezuiliwa kwa sheria ipi? Kwa hiyo, ninamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge kwamba ni sheria ipi ambayo Serikali imeitumia kuzuia mikutano ya vyama vya siasa. Ninahitaji majibu, bila kupata majibu ya kueleweka nitatoa shilingi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye jambo hili tusikilizane vizuri sana, kwa sababu ni jambo *sensitive* ambalo tumezoea kulifanya kwa mazoea na linapofanyika kwa utaratibu watu tunakuwa na tafsiri tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano ya vyama vya siasa haijazuiwa, imewekewa utaratibu. Kungekuwa na mikutano ya vyama vya siasa imezuiwa basi tunapokuwa na uchaguzi hakuna chama cha siasa kingefanya mkutano wa hadhara. Lakini tumefanya mkutano ya hadhara nchi nzima, hata nchi za wenzetu hivi ndivyo wanavyofanya. Wanafanya mikutano ya hadhara panapokuwepo na utaratibu wa kuwa na jambo ambalo linahitaji mikutano ya hadhara. Hata waliotuletea hizi siasa za vyama vingi hivi ndivyo wanavyofanya. Hakuna nchi ambayo itasema kwamba yenyewe ina demokrasia kubwa zaidi kuliko hao walioanzisha na inafanya mikutano *fulltime*. Wana utaratibu ambao wanatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachoweza kusema ni kipi, panapokuwa hakuna uchaguzi nenda Marekani, nenda Uingereza, wanafanya siasa kufuatana na vyombo ambavyo vimechaguliwa kuwawakilisha wananchi ndivyo inavyokuwa. Wanafanya ujenzi wa vyama vyao kwa kutumia

mikutano ya ujenzi wa vyama vyao ambayo hata hapa imeruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge ni kwa sababu tu jambo hili tunalitafsiri kwa jazba, lakini utaratibu uliopo tena unawalinda sana Wabunge. Mimi binafsi niko kinyume sana na utaratibu wa Mbunge aliyechaguliwa, amepewa kura na Watanzania wote katika eneo lake, halafu anaenda mtu mwingine tu kwa kigezo cha chama cha siasa anaenda kutukana mtu aliyechaguliwa na akapewa haki hiyo na Katiba. Huo ndiyo utaratibu ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge ambao pia wanatokana na vyama hata ninyi hapa wewe mwenyewe Mheshimiwa Heche ni Kiongozi wa Kanda yako, una eneo kwako unafanya mikutano. Sasa tunachosema...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Waruhusu waje wafanye.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Hamna cha taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe kwa yule ambaye atakuja kusema Tanzania tunafanya kitu cha tofauti aniambie hizo nchi ambazo zilianzisha vyama vingi ambao wao *fulltime* hawatumii utaratibu huu, ambao wanatumia vitu ambavyo ni rasmi vinavyoweza kuongoza mikutano hiyo.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwanza niweke sawa kwamba mikutano haijazuiwa ila imewekewa utaratibu na kila nchi ina utaratibu wake wa kuendesha mambo yake katika Taifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ngoja niwaambie Waheshimiwa Wabunge, endeleeni kujifunza tu. Tuko kwenye Kamati, hakuna cha utaratibu hapa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anadanganya, anaongea uongo.

**MWENYEKITI:** Hakuna cha utaratibu!

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anadanganya, anaongea uongo.

**MWENYEKITI:** Nasema hivi, wewe utapata nafasi baadae. Bunge litarejea tu. Kama siyo leo, kesho, kesho kutwa, lipo Bunge utaendeleza hoja yako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anaongea uongo unatetea.

**MWENYEKITI:** Hapana, hujaelewa kwamba katika hatua huwezi ukasimama *on a point of order,* hapana. Lakini siyo kwamba uliyonayo eti yamefutika. Tunaendelea Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema mikutano haijazuiwa ila imeandaliwa utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kusoma Katiba nikasoma *Political Party Act* na nina Kanuni za Vyama vya Siasa na nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni ndivyo nilivyotumia. Mimi ninataka majibu ya kisheria, kikanuni. Naomba kutoa hoja, Wabunge waniunge mkono tujadili hoja hii. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Haya, hoja imetolewa, hivi imeungwa mkono? Ndiyo, imeungwa mkono.

Haya tunaanza na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Lameck Mwigulu.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani.

**MWENYEKITI:** Ngoja tuje huku basi, msijisemee. Ngoja tuelewane, Mheshimiwa Abdallah Mtolea bado mmoja, Mheshimiwa James Millya.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Waziri Kivuli Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Hii ni Wizara ya Katiba na Sheria, siyo *Home Affairs.* Mheshimiwa Aida Khenani. Tunaanza na Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mimi ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ryoba kwamba kweli kuna ukiukwaji mkubwa wa Katiba na Sheria ambazo tumejiwekea. Nimesikiliza maelezo ya Serikali wakijaribu ku-*copy* mifano mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tuna-*copy* mifano mingine pale ambapo sheria zetu zinakuwa hazijitoshelezi lakini kwa hili sheria yetu iliyopo sasa inajitosheleza kwamba vyama vya siasa vinatakiwa kufanya mikutano, vijitanue, vitengeneze mtandao mkubwa ili baadae na wao waweze kuleta upinzani kwenye uchaguzi. Hatuzungumzii vyama ambavyo leo vina Wabunge, vina Madiwani, kuna vyama havina hata Mwenyekiti wa Serikali wa Mtaa lakini ni haki yao kufanya siasa ili na wenyewe waweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yamekatazwa bila kuambiwa kwamba yamekatazwa kwa sheria ipi. Hao wanaotekeleza huko wanakwenda mbali zaidi. Mimi Mbunge wa Jimbo niliandaa mkutano wa kwangu, siku ya mkutano polisi wanakuja kuzuia kwamba tuna taarifa zitatokea fujo, kwa hiyo huu mkutano usifanyike. *(Makofi)*

Sasa mimi Mbunge wa Jimbo, niko Jimboni kwangu unaniambia umepata taarifa za kwamba kutakuwa na fujo, nilitegemea ndiyo unilinde muongeze ulinzi ili mkutano wangu uishe vizuri lakini yote haya tunakatazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mkituambia kwamba mna-*copy* mifano kutoka nje mazingira yetu yanatofautiana na sheria zetu zinajitosheleza. Ni vizuri tukaheshimu sheria na ndiyo maana tunayasema haya tukiwa tunajadili bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu tunaamini tunayemuambia ni muumini mzuri wa haya, alikuwa akihubiri mambo haya ya demokrasia na kufuata utaratibu huu. Hatuamini kama leo anaweza akatukwepa eti kwa sababu amekuwa Waziri. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja na ninaunga mkono hoja kwa sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili chama cha siasa kisajiliwe kinahitaji kuwa na wanachama. Leo ukizuia mikutano ya hadhara unategemea hicho chama kitoe wanachama wapi? Wakakutane *bar* au sokoni? Wanaposema Wabunge na Madiwani wanaruhusiwa kufanya mikutano, kuna vyama havina Wabunge na Madiwani. Tafsiri yake ni kwamba mnakwenda kuzuia vyama visifanye shughuli zake za kisiasa na ukisema kuna muda ambao wanatakiwa wafanye ni kwa nini hivi vyama vinaendelea kuwepo visubiri kipindi cha uchaguzi, wakati huo huo mkumbuke na mimi nataka nimweleze Mheshimiwa Mwigulu kwamba Mheshimiwa Magufuli ni Mwenyekiti kama alivyo Mheshimiwa Freeman

Mbowe, kama alivyo Mheshimiwa Dovutwa na yule anafanya mikutano na kuna sehemu anakwenda na anapokea wanachama wa CCM kwa hiyo ile mikutano inakuwa siyo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme Serikali inajua na hapa tunazungumza kwa sababu leo ni Katiba na Sheria. Katiba ndiyo sheria mama na ndiyo dira ya nchi yetu. Mnapokwenda kinyume na Katiba ina maana mnaikanyaga wenyewe na tunaposema mnavunja Katiba mnakuja juu! Muache uoga, tuacheni tuingie kwenye *game* tutakutana huko. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Millya.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Kabudi ni mtu ambaye ninamheshimu sana na ataingia kwenye historia ya nchi hii kutomshauri vizuri Rais iwapo Serikali hii itaendelea kuvunja haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuangalia Mwenezi wa Taifa wa CCM Ndugu Humphrey Polepole anaenda Kigoma, anazunguka nchi hii anafanya mikutano ya hadhara na yeye anaruhusiwa, lakini hoja ya msingi ya Mheshimiwa Marwa ni kwamba kwa nini vyama vya siasa vingine visiruhusiwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo amefanya Profesa Kabudi, Ibara ya 14 ya Katiba yetu haki ya kuishi, leo amesema ametoa mfano wa nchi fulani, mtu fulani kaja kutembelea Tanzania anasema *shoot on sight,* Profesa Kabudi unapotosha nchi kwamba tunaruhusiwa kupiga watu risasi. Hiyo ni *wrong!*

**MWENYEKITI:** Hajasema hivyo.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Aah, hajamalizia, ninaomba atoe ufafanuzi wa hiyo *shoot on sight* maana yake ni nini, kwa sababu mimi nilivyomuelewa kwa mwanasheria mbobezi kama yeye *I feel pity*, najisikia vibaya eti mtu

anaweza aka-*justify* eti *shoot on sight* mambo yaliyotokea Kibiti na yaliyotokea Kusini mwa nchi yetu. Ninaomba, kwenye hoja ni kwamba Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano inavunja sheria kama ambavyo mnahamisha pesa shilingi trilioni 1.5 bila kupangiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni jambo ambalo mmelizoea, kuvunja sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Mimi naanza tofauti kidogo. Naunga mkono tamko la Serikali la kutofanya mikutano ya hadhara, lakini kwa sababu humu ndani tuna wasomi wa sheria na tunawaheshimu sana, hili Bunge linatunga *acts,* nitaongea kizungu leo ili tuelewane vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Bunge linatunga *acts,* lakini mtambue kuna kitu kinaitwa *Presidential Decree,* alichokifanya Rais ni sahihi. Kwa sababu Rais ndiyo ametoa ile kauli, mimi nadhani kama wapinzani wanaona yanayoendelea siyo sawa wana haki ya kwenda Mahakamani. Wafungue kesi Mahakamani basi Mahakama ndiyo chombo cha mwisho tuone kama ninyi mnasahau kwamba *decree* ya Rais ni sheria. Ninyi ni wasomi mtusaidie kwamba kama mnaikataa *decree* ya Rais siyo sheria, hata *acts* nayo siyo sheria. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi hoja ya Mheshimiwa Ryoba kwa sababu moja, Wabunge na Madiwani wameruhusiwa kufanya mikutano kwenye majimbo ya, tena kitu cha ajabu kwa ushahidi ninao dada yangu Aida Khenani alikuja mpaka Namanyere kidogo apigwe kwa sababu Jimbo siyo lake, anakuja kudanganya wananchi, kuja kudanganya

na Serikali haina Askari wa kutosha kuwalinda. Kwa hiyo, wanawasiaida, fanyeni mikutano kwenye majimbo yenu. Serikali haijawakataza kufanya mikutano kwenye majimbo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmepewa miaka 20 wanachama wanapungua siku hadi siku, hawajaongezeka, kwa hiyo nawaomba ndugu zangu acheni kupiga kelele, fanyeni kazi na ikiwezekana chama anzeni kuhama mmoja baada ya mmoja kabla ya 2020, kwa sababu wanachama wanapungua siku hadi siku. Kila siku unasikia kwenye magazeti, kwenye redio wanakabidhi kadi sasa mikutano mnaenda kuwafanyia akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi siungi hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Huna adabu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kama nilivyosema mwanzoni kwamba ni vema sana kwenye jambo hili tukaelewana vizuri. Moja, kitu nilichokuwa nasema ni kwamba kila nchi ina utaratibu wake na mimi ninatamani sana kuishi kwenye nchi ambayo ina utaratibu, nchi ambayo inafuata sheria. Tanzania haiwezi ikawa nchi ya kampeni miaka yote mitano. Tuna kazi ya kufanya, tuna Ilani tunatekeleza. Mwaka kesho tuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kila kijiji, kila Tawi, kila Kitongoji patakuwepo na kampeni na kila chama kitaruhusiwa kushiriki na kufanya taratibu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwalimu wangu, babu yangu Mbunge wa Serengeti wakati anataja zile sheria kataja zile alizozitaja hakutaja ya Jeshi la Polisi wala hakutaja sheria zingine ambazo ziko katika nchi husika. Kwa maana hiyo la msingi ambalo Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa wazingatie ambalo ni jambo jema kwa nchi hii ni yetu sote lazima twende

kwa utaratibu na mikutano ya hadhara tusiendelee kutumia kauli za kuna ambao wanatuambia mikutano ya hadhara imezuiwa, lakini hata kwao wao hawafanyi hivyo wanafanya kama tunavyofanya sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kama hiki tunachofanya ndivyo ambavyo utaratibu ulivyo na ndiyo sheria inavyotaka, twende tukubaliane kwamba panapokuwepo na jambo ambalo ni mahsusi tushughulikie jambo lililo mahsusi, lakini si kwenye yale ambayo kwa ujumla wake yamewekewa utaratibu na tukafanya kama kupotesha au kuweka utaratibu.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kwa hiyo, sikubaliani naye nakubaliana na utaratibu uliowekwa na ni vema tukafanya vitu kwa utaratibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba niseme kwamba tunazungumza Katiba, lakini tunazungumza sheria na kanuni ambazo tumejiwekea, hivyo vyote vinatuongoza katika kufanya jambo lolote katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudie kusema tunapozungumzia uhuru wa vyama kufanya shughuli za siasa, tunazungumzia masuala ambayo yameainishwa kwa mujibu wa sheria ili kukuza demokrasia ndani ya nchi yetu ya Tanzania, kama tunazungumza hivyo ni lazima tukubaliane kwamba kila aina ya demokrasia mahali popote lazima ifuate sheria, kanuni lakini ifuate na taratibu zilizowekwa katika kutekeleza demokrasia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi baada ya uchaguzi kukamilika, kila eneo la uchaguzi aliyechaguliwa ndiye mwenye kupewa...

**MBUNGE FULANI:** Mwongo huyu! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchaguzi kama ni Mbunge ameshinda kwenye Jimbo lake la uchaguzi huyo ni kiongozi halali katika eneo lake la uchaguzi. Kama ni Diwani ameshinda kwenye eneo lake la uchaguzi huyo ni kiongozi halali kwenye eneo la uchaguzi, na kama hivyo ndivyo ilivyo...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hebu muacheni achangie, siyo lazima ukubaliane naye. Ngoja bwana, hebu muacheni achangie hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wangekuwa wavumilivu tu wakasubiri nimalize. Ninaendelea kusisitiza baada ya uchaguzi wa mwaka 2015 aliyechaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Dkt. John Pombe Magufuli na wananchi wamempa imani ya kuwa Rais, Wabunge ambao wako ndani ya Bunge hili ndiyo waliochaguliwa kuwawakilisha wananchi wao katika maeneo wanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama uchaguzi umeshakamilika, mwananchi anategemea mwakilishi wake aliyeshinda kwenye eneo husika ana wajibu wa kukutana na wananchi wake na kufanya mikutano inayohusika. Niendelee kusema hakuna Mbunge, hakuna Diwani hata kwenye nafasi ya Rais kila aliyeshinda ameshinda akitokea kwenye chama cha siasa, kwa hiyo anapokwenda kufanya mkutano katika eneo lake la uchaguzi ina maana anakwenda kueneza siasa katika eneo lake la uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja ya Serikali kwamba uchaguzi umepita na hivyo kila Mwakilishi akafanye kazi kwenye eneo lake la uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, mwenye hoja…

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza vizuri wachangiaji wote.

**MWENYEKITI:** Nitawataja, nawasikia mpaka hapa.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianza kwa kunukuu kifungu cha Katiba kinachohusu *Multi-Party Democracy* na profesa anajua *principles of multi-party democrary* na nchi yetu inaongozwa kwa utaratibu wa kutumia Katiba hii, Sheria ya Vyama vya Siasa ipo.

**MWENYEKITI:** Unayarudia hayo hayo tunataka tuamue hoja hii.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya ku-*justify* kwamba Wabunge na Madiwani ndiyo wanaruhusiwa kufanya mikutano na kwamba Sheria ya Uchaguzi imesema hivyo ni jambo la kupotosha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wote hakuna mwenye *legal ground* ambayo inalishawishi Bunge na Taifa zima kwamba kilichofanywa kuzuia mikutano ya kisiasa ni cha kisheria.

**MWENYEKITI:** Unataka nimnyanyue? *Attorney General*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mtoa hoja amejikita katika Katiba, Sheria na Kanuni naomba sasa Bunge lifuate Katiba, Sheria na Kanuni. Ibara ya 30(3) ya Katiba inasema: "Mtu yeyote anayedai kuwa sharti lolote katika Sehemu hii ya Sura hii ya Katiba au katika sheria yoyote inayohusu haki yake au wajibu wake imevunjwa, inavunjwa au inaelekea kuvunjwa anaweza kufungua shauri hilo Mahakamani." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafuata sheria sasa. Kuna shauri limefunguliwa Mahakamani; *Miscellaneous Civil Case* Na. 4 ya 2018, imefunguliwa na Francis Galatwa na wenzake

dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa Kanuni hizo zinasema katika Kanuni za Bunge ya 64(1) (c) Bunge halipaswi kujadili jambo ambalo liko Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema hata Katiba Ibara ya 107(b) inazuia hivyo kulinda uhuru wa Mahakama. Ninashauri mjadala huu usiendelee.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nilisema nimnyanyue.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge...

**MWENYEKITI:** Sasa tuamue, hitimisha tu hoja yako.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha. Kazi ya Bunge ni kuishauri Serikali ifanye nini. Sasa kwa kuwa Serikali imeamua kuvunja Katiba makusudi na Sheria ya Vyama vya Siasa makusudi na kanuni zilizotungwa na Bunge hili, naomba tupige kura ipo siku ninyi yatawarudia.

*(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Sasa tunaingia kwenye *guillotine.*

**Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 – *Adm & HR Mgt Div*..................Sh. 5,316,735,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh.163,735,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*.......Sh. 389,917,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*...................Sh. 104,274,000/=
Kif. 1005 – *Govt. Comm. Unit*......................Sh. 74,400,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Mgt. Unit*................Sh. 55,664,000/=
Kif. 1007 – *Info. & Comm. Tech. Unit*..........Sh. 134,114,000/=
Kif. 2004 – *Public Legal Services division*.......Sh. 299,837,000/=
Kif. 4001 – *Constitutional & Justice Monitoring Div*...........................Sh. 345,875,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kif. 1001 – *Admin. & HR Mgt*…………………Sh. 906,193,800/=
Kif. 1002 – *Finance & Accounts*………………Sh. 24,295,000/=
Kif. 1003 – *Procurement Mgt Unit*……………Sh. 15,675,800/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*…………………Sh.10,000,000/=
Kif. 1005 – *Recruitment, Appointment & Confirmation*……Sh. 121,088,400/=
Kif. 1006 – *Ethics and Discipline Section*……..Sh. 20,090,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 16 -Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 – *Adm & HR Mgt*…………………Sh. 2,001,811,000/=
Kif. 1002 – *Finance & Accounts Unit*………..Sh. 421,474,000/=
Kif. 1003 – *Planning Division*…………………Sh. 705,725,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*………………Sh. 252,201,000/=
Kif. 1005 – *Gov. Comm. Unit*…………………Sh. 86,630,000/=
Kif. 1006 – *Legal Registry Unit*…………………………………Sh. 0
Kif. 1007 – *Procurement Mgt. Unit*…………..Sh. 223,123,000/=
Kif. 1008 – *Research & Library Service Unit*……Sh. 84,171,000/=
Kif. 1009 – *Info. & Comm. Tech, unit*………..Sh. 216,955,000/=
Kif. 2001 – *Coordination & Advisory Services*..Sh. 562,196,000/=
Kif. 2003 – *Legislative Drafting*………………Sh.1,260,017,000/=
Kif. 3001 – *Civil Litigation & Arbitration Div.*………………Sh. 0
Kif. 3002 – *Treaties & Contracts Div.*……….Sh.1,150,079,000/=
Kif. 4001 – *Constitutional Affairs & Human Rights*…………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

Kif. 2001 – *Monitoring of Civil Litigation & Arbitration*…………Sh. 744,001,000/=
Kif. 2002 – *Arbitration Division*………………..Sh. 926,072,000/=
Kif. 2003 – *Litigation Division*…………………..Sh.970,872,000/=
Kif. 1001 – *Admin. & Finance Div.*……………Sh. 826,426,000/=

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*…………………Sh.136,469,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mg. Unit*……………Sh.157,198,000/=
Kif. 1006 – *ICT & Information Unit*……………Sh.161,789,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 -Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kif. 3001 – *Fraud, Money Laundering & Corruption Offence*……………Sh. 213,191,000/=
Kif. 3002 – *Assets Forfeiture Transnational & Specialized Crimes*……………Sh. 232,741,000/=
Kif. 3003 – *Case Mgt. Coordination of Criminal Cases*……………Sh. 209,961,000/=
Kif. 1001 – *Administration & Finance*……..Sh. 3,193,314,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*…………………Sh.100,556,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit*……………Sh.127,071,000/=
Kif. 1006 – *ICT & Information Unit*……………Sh.148,817,000/=
Kif. 2002 – *Civilanization & Prosecutions*…….Sh. 384,844,000/=
Kif. 2004 – *Zonal Office Arusha*………………Sh. 833,280,00/=
Kif. 2005 – *Zonal Office Dodoma*……………Sh. 436,922,000/=
Kif. 2006 – *Zonal Office Dar es Salaam*…….Sh. 2,009,950,000/=
Kif. 2007 – *Zonal Office Iringa*………………Sh. 377,368,000/=
Kif. 2008 – *Zonal Office Moshi*………………Sh. 439,732,000/=
Kif. 2009 – *Zonal Office Kagera*………………Sh. 326,884,000/=
Kif. 2010 – *Zonal Office Mbeya*………………Sh. 513,510,000/=
Kif. 2011 – *Zonal Office Mtwara*………………Sh. 368,006,000/=
Kif. 2012 – *Zonal Office Mwanza*……………Sh. 861,397,000/=
Kif. 2013 – *Zonal Office Ruvuma*……………Sh. 278,298,000/=
Kif. 2014 – *Zonal Office Sumbawanga*……….Sh. 294,994,000/=
Kif. 2015 – *Zonal Office Tabora*………………Sh. 510,242,000/=
Kif. 2016 – *Zonal Office Tanga*………………Sh. 438,945,000/=
Kif. 2017 – *Zonal Office Shinyanga*…………Sh. 359,676,000/=
Kif. 2018 – *Zonal Office Singida*………………Sh. 281,035,000/=
Kif. 2019 – *Zonal Office Lindi*…………………Sh. 217,039,000/=
Kif. 2020 – *Zonal Office Mara*…………………Sh. 262,205,000/=
Kif. 2021 – *Zonal Office Manyara*……………Sh.174,786,000/=
Kif. 2022 – *Zonal Office Kigoma*………………Sh. 237,244,000/=
Kif. 2023 – *Zonal Office Pwani*…………………Sh. 328,385,000/=

Kif. 2024 – *Zonal Office Njombe*………..…….Sh. 283,459,000/=
Kif. 2025 – *Zonal Office Morogoro*…………..Sh. 304,308,000/=
Kif. 2026 – *Zonal Office Geita*……...………...Sh. 218,918,000/=
Kif. 2027 – *Zonal Office Simiyu*……........……..Sh.184,493,000/=
Kif. 2028 – *Zonal Office Katavi*……….....……Sh.197,334,000/=
Kif. 2029 – *Zonal Office Songwe*……......……..Sh. 79,200,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 – *Administration & HR. Mgt*…….Sh. 73,378,668,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.…...…Sh.186,400,000/=
Kif. 1003 – *Planning & Monitoring Div.*………Sh. 574,950,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*………………..Sh. 242,744,000/=
Kif. 1005 – *Information, Comm. & Tech*..……Sh. 257,750,000/=
Kif. 1007 – *Procurement Mgt. Unit*……….….Sh. 340,995,000/=
Kif. 1008 – *Estates Mgt. Unit*………………….Sh. 254,506,500/=
Kif. 1009 – *Records Mgt. Unit*…………….......Sh.171,948,000/=
Kif. 1010 – *Library Services Unit*……………….Sh. 291,552,000/=
Kif. 1011 – *Legal Services Unit*………..……...Sh. 229,274,800/=
Kif. 2001 – *High Court Main Registry*………Sh. 1,898,840,400/=
Kif. 2002 – *Court of Appeal Dar es Salaam*.............................Sh.1,723,372,000/=
Kif. 2003 – *High Court Zone*………………..Sh. 6,572,216,200/=
Kif. 2004 – *High Court Division*……..………Sh. 4,331,555,500/=
Kif. 2005 – *Resident Magistrate Courts*…....Sh. 4,723,935,000/=
Kif. 2006 – *District Courts*……………..……Sh. 5,942,183,600/=
Kif. 2007 – *Primary Courts*…………………Sh. 3,888,501,000/=
Kif. 2008 – *Case Mgt. Division*………………..Sh.174,750,000/=
Kif. 2009 – *Judicial Services Inspection, Supervision & Ethics*…….........…..Sh.197,875,000/=
Kif. 2010 – *Judiciary Delivery Unit*……………Sh. 229,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 – *Administration and HR. Mgt*……Sh.1,514,850,498/=
Kif. 1002 – *Finance & Accounts*……………..….Sh.197,122,000/=
Kif. 1003 – *Internal Audit Unit*…………………Sh. 52,457,602/=
Kif. 1004 – *Legal Services Unit*………………..Sh. 256,345,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit*……………Sh. 32,950,000/=
Kif. 1006 – *Mgt. Information System Unit*…......Sh. 43,470,000/=
Kif. 2001 – *Administrative Justice*…….....……Sh. 640,558,000/=
Kif. 2002 – *Human Rights*………………..……Sh. 480,717,900/=
Kif. 2003 – *Research & Documentation*…..….Sh.161,762,000/=
Kif. 2004 – *Public Edu. & Training*……………..Sh.187,641,800/=
Kif. 3001 – *Zanzibar Office*……………………Sh.194,519,200/=
Kif. 3002 – *Mwanza Office*……………………..Sh. 41,738,000/=
Kif. 3003 – *Lindi Office*………………………...Sh. 35,800,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 – *Administration & HR Mgt*…………Sh. 908,175,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..…..Sh.195,093,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*……………..…..Sh. 98,415,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Mgt. Unit*…….......….Sh. 59,224,000/=
Kif. 1006 – *Public Legal Awareness Unit*…….Sh. 241,656,000/=
Kif. 1007 – *Law Review Unit*…………………..Sh. 229,680,000/=
Kif. 1008 – *Law Research Unit*………………..Sh. 246,336,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 1003 – *Planning Division* ………..…….Sh. 2,000,000,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

Kif. 2001 – *Monitoring of Civil Litigation & Arbitration*……..……...Sh. 248,363,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Kif. 3001 – *Fraud, Money Laundering & Corruption Offence*…….Sh. 527,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 - Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 – *Administration & HR Mgt*.............…….……....Sh. 0
Kif. 1003 – *Planning & Monitoring Division*..............................…….Sh.15,000,000,000/=
Kif. 1005 – *Information, Comm.& Tech*..........…………….Sh. 0
Kif. 1008 – *Estates Mgt. Unit*…………….......…….........….Sh. 0
Kif. 2001 – *High Court Main Registry*.........……………….Sh. 0
Kif. 2010 – *Judiciary Delivery Unit*………..Sh. 20,973,722,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1003 – *Policy & Planning Division*……..Sh. 4,221,196,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna hoja.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku naomba ukae chini.

**Fungu 55 - Tume ya Utawala Bora na Haki za Binadamu**

Kif. 1001 – *Administration& HR. Mgt*……......................Sh. 0
Kif. 1004 – *Legal Services Unit*………………Sh. 1,140,970,000/=
Kif. 2002 – *Human Rights*…………………… Sh. 655,968,000/=
Kif. 2003 – *Research & documentation*………...........………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2018/2019 - Wizara ya Katiba na Sheria yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha

2018/2019 sasa yamepitishwa rasmi na Bunge na isipokuwa kama itaamuliwa vingine kati ya mashauriano kati ya Serikali na Kamati ya Bajeti huu ndio uamuzi wa Bunge kuhusiana na mafungu yote yaliyopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na timu yenu yote pamoja na Jaji Kiongozi lakini nyuma yenu Wataalam wote wa upande wa utoaji haki lakini pia usimamizi wa Katiba, Sheria, Kanuni na miongozo iliyowekwa kwa mujibu wa sheria sasa mmepewa uwezo huu na Bunge kwa mwaka ujao wa fedha mkatumie hizi. Yapo mengi mmeanza vizuri yaendelezeni, mna nia njema mmeyasema vizuri na nchi imesikia mipango ipo mizuri inakuja Waheshimiwa.

Kwa hiyo, kama Bunge tumewawezesha mlichoomba, *In Shaa Allah* mwaka kesho tutakaporejea hapa mtatueleza yale mliyoyafanya kutokana na rasilimali fedha mliyopewa katika mwaka ujao wa fedha.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Alhamis, tarehe 19 Aprili, 2018 saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.16 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 19 Aprili, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*